

## **BUNGE LA TANZANIA**

---

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

#### **MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Arobaini – Tarehe 10 Juni, 2016**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### **D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA**, Tukae, Katibu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani Walitoka nje ya Ukumbi wa Bunge na kubakia Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango Mhe. David D. Silinde)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

#### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/2017 – 2020/2021 *(The National Five Year Development Plan, 2016/2017 -2020/2021).*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. DAVID D. SILINDE – NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI  
KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/17; pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA:** Maswali

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 334

**Wabunge wa Viti Maalum Kushiriki katika Kamati za  
Fedha na Mipango za Halmashauri**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kamati za Fedha za Mipango za Halmashauri za Wilaya ni Kamati muhimu sana kwa Wabunge wote kushiriki bila kujali ni wa Viti Maalum au wa Jimbo kwa sababu zinashughulika na masuala ya fedha, bajeti na mipango ya miradi ya maendeleo; na kwa muda mrefu sasa Wabunge wa Viti Maalum wamekuwa wakiomba kuondolewa kwa sheria kandamizi na ya kibaguzi ya kuwazuia kushiriki katika Kamati hizo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kusikiliza kilio cha Wabunge wa Viti Maalum ili kuwaruhusu kushiriki kwenye Kamati hizo?

(b) Je, Serikali iko tayari kufuta sheria hiyo kandamizi na yenye ubaguzi ambayo haina tija na hasa ikizingatiwa kuwa ilitungwa mwaka 1998 wakati ambao Ubunge wa Viti Maalum bado haujaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Halmashauri wametajwa katika kifungu cha 75(6) cha Sheria, Sura 287 ya Mamlaka za Serikali za Wilaya na kifungu cha 47(4) cha Sheria Sura 288 ya Mamlaka za Miji. Kwa mujibu wa sheria hizo mbili, Wajumbe wa Kamati hawatazidi theluthi moja (1/3) ya Madiwani wote isipokuwa Kamati ya Fedha na Mipango ambayo Wajumbe wake ni wale wanaoingia kwa nyadhifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango umefafanuliwa katika Kanuni za Kudumu za Uendeshaji wa kila Halmashauri ambapo Wajumbe wake ni Mwenyekiti au Meya wa Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Naibu Meya wa Halmashauri, Mbunge au Wabunge wa Majimbo wanaowakilisha majimbo katika eneo la Halmashauri, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Halmashauri na Wajumbe wengine wasiozidi wawili watakaopendekezwa na Mwenyekiti/Meya kisha kupigiwa kura na Baraza la Halmashauri mmoja kati yao awe mwanaume au mwanamke. Hivyo, ili Wabunge wa Viti Maalum waweze kushiriki kwenye Kamati za Fedha tutahitaji kubadili sheria kwanza ili pendekezo hilo liweze kutekelezeka.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika sehemu (a) ya jibu hili, Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango wataendelea kuwa ni wale waliotajwa katika Sheria na Kanuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi hapo sheria itakapofanyiwa marekebisho kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Umbulla swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zote za Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wananchi vijijini zinapita kwenye Halmashauri za Wilaya na katika vikao vya Halmashauri za Wilaya hasa Kamati hiyo ya Fedha na Mipango Wabunge wa Viti Maalum hawashiriki na ndiyo watu wenye dhamana na maendeleo ya wanawake.

Kwa kuwa sheria hiyo iliyotungwa ambayo inawakataza Wabunge wa Viti Maalum kuingia kwenye Kamati hizo ilitungwa zamani sana kabla hata utaratibu wa Ubunge wa Viti Maalum haujaanza bali kulikuwa na Wabunge wa Majimbo na Wabunge wa Kuteuliwa na Rais; na kwa kuwa mwaka jana kwenye Bunge la Kumi, Mheshimiwa Mwanri aliyekuwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali hapa Bungeni, alitueleza kwamba sheria hiyo ni kandamizi na tunahitaji kuileta hapa Bungeni ili tuirekebishe Wabunge wa Viti Maalum washiriki.

Je, Serikali italeta lini hiyo sheria ili Wabunge wa Viti Maalum waweze kushiriki katika Kamati hii muhimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Halmashauri zetu za Wilaya hasa kwa Mkoa wetu wa Manyara zinatenga asilimia kumi za fedha kwa ajili ya miradi ya wanawake. Utaratibu na mfumo wa utoaji wa fedha hizo kwa ajili ya miradi ya wanawake hauko vizuri na kuna upotevu mkubwa sana wa fedha hizo za Serikali.

Je, ni kwa nini Madiwani wa Viti Maalum wakisaidiana na Wabunge wao wasisimamie kikamilifu utoaji na urejeshaji wa fedha hizo ili ziweze kuwafikia walengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali kila kitu kipo kwa mujibu wa sheria na kanuni zake. Katika jibu langu la msingi katika eneo la pili nikasema mchakato unaweza ukaendeshwa kwa kuwashirikisha wadau. Hili la kuwashirikisha wadau kama nilivyosema lina umuhimu mkubwa sana. Katika maeneo mengine kwa mfano nikichukua Jimbo langu mimi la Kisarawe, Mbunge wangu wa Viti Maalum anaingia katika Kamati ya Fedha na sehemu zingine wanaingia katika Kamati hii, ina maana hivi sasa katika zile nafasi mbili Mwenyekiti anaweza akateua Mbunge wa Viti Maalum kuweza kuingia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kusimamia fedha ni wajibu wa Madiwani na Wabunge wahusika katika eneo hilo. Kwa upana wa jambo hili, ndiyo maana nimesema wadau lazima washirikishwe. Kuna baadhi ya Majimbo, mfano Jimbo la Ilala, lina Wabunge wa Majimbo watatu, lina Madiwani wa Viti Maalum wasiopungua watano, kwa hiyo ukiangalia hapo, ndiyo maana nasema lazima wadau washirikishwe kuona jambo hilo linakaajekaaje na kuangalia ni jinsi gani tutafanya Kamati ya Fedha iweze kufanya vizuri. Kwa mfano, kwa hali ya sasa hivi ukisema Jimbo la Ilala Wabunge wote wa Viti

Maalum waingie katika Kamati ya Fedha mtapata sura hapo, ndiyo maana nasema lazima sheria hiyo tuitazame kwa upana na wadau washiriki kila mmoja katika eneo lake kuangalia jinsi gani tutafanya, hilo ni jambo la msingi lakini kwa sasa hivi sheria inasimama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu asilimia tano ya akina mama na siyo ya akina mama peke yake, ni ya vijana na akina mama. Jambo hili nililisema katika vikao mbalimbali kwamba jukumu la Kamati ya Fedha ni kuhakikisha kwamba fedha zinazokusanywa kutoka *own source* ziweze kuyafikia yale makundi ya akina mama na vijana. Kwa bahati mbaya hata katika kaguzi mbalimbali zilizopita hili ni miongoni mwa eneo lenye changamoto kubwa na ndiyo maana tumetoa maelekezo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema agenda ya kuhakikisha akina mama na vijana wanapata fedha hii ni yetu sote. Ndiyo maana bajeti ya mwaka huu *criteria* tuliyotumia kuhakikisha Halmashauri zote zinatengewa bajeti ni kuhakikisha kwamba wanatenga asilimia tano ya vijana na akina mama na walemavu watakuwa katika mchakato huo. Kwa hiyo, hili ni agizo la jumla kwamba kwa vile bajeti tumeipitisha basi kila Halmashauri ihakikishe inasimamia asilimia tano za akina mama na tano za vijana ziweze kuwafikia walengwa. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tuendeleo Waheshimiwa na swali linalofuata.

Na. 335

### **Uwekaji wa Mipaka Upya - Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Kutoka Kijiji cha Mutelewele kwenda Makambako ni kilometa tano wakati kwenda Halmashauri ya Wanging'ombe ni kilometa 65; kutoka Kata ya Soja kuja Makambako Mjini ni kilometa 25 na kwenda Halmashauri yao ya Wanging'ombe ni kilometa 88 na kutoka Kijiji cha Nyigo kuja Makambako ni kilometa 8 wakati kwenda Halmashauri ya Mufindi ni kilometa 88 na huduma zote zikiwemo matibabu wanazipata Makambako; kutoka Kijiji cha Igongolo ni umbali wa kilometa 6 kwenda Makambako wakati kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni kilometa 54.

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kugawa mipaka upya ili wananchi wapate huduma karibu na Halmashauri yao ili iendane na kauli mbiu ya kusogeza huduma karibu na wananchi?

(b) Je, ni lini sasa Serikali itapima upya mipaka hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, Vijiji vya Mutewele na Saja viko katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe na Kijiji cha Nyigo kiko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Aidha, ni ukweli usioplingika kuwa vijiji hivyo kijiografia viko karibu na Halmashauri ya Mji wa Makambako kwa maana ya huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Mbunge ya kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi vipo vigezo na taratibu zinazozingatwa katika kusajili au kubadili mipaka ya vijiji. Mapendekezo haya yanapaswa kujadiliwa kwanza katika Mikutano Mkuu ya Vijiji, Kamati za Maendeleo ya Kata, Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri zote, Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) na Kamati za Ushauri za Mikoa. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mabadiliko ya mipaka hiyo yataathiri mipaka ya utawala ya Mikoa ya Iringa na Njombe ambapo lazima wadau wa pande zote wakubaliane kuhusu maamuzi hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoieleza katika sehemu (a) ya jibu hili, napendekeza haya yapitishwe kwanza kwenye vikao vilivyotajwa na endapo vitaridhiwa, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itayafanyia kazi mapendekezo hayo sambamba na maombi yaliyowasilishwa kutoka maeneo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini naomba niulize maswali ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu swali langu la msingi nimeelezea namna ambavyo wananchi wa Kata ya Saja, Kijiji cha Nyigo na Mtebelele namna wanavyopata tabu kwani huduma zote zinapatikana Makambako na kwenda kwenye Halmashauri yao kutoka Saja kwenda Wanging'ombe ni kilometa 88 na kwenda Makambako ni kilometa 20 na kutoka Mtebelele ni kilometa tano na Waziri amekiri ni kweli katika suala la upatikanaji wa huduma ni mbali. Kwa nini Waziri asiagize shughuli hii ya vikao ianze kufanyika? Siku za nyuma vilishafanyika na kupelekwa kwenye vikao vinavyohusika vya mkoa na

hivi juzi tu tulikaa kwenye kikao na mkoa tayari walianza kushughulikia. Niombe Waziri sasa ashughulikie suala hili na kuagiza kwamba waweze kukaa vikao ili wananchi hawa wapate huduma jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Kijiji cha Nyigo, GN ambayo iko katika Halmashauri ya Makambako inaonyesha Kijiji cha Ngigo mpaka wake mwisho ni barabara ya zamani ya Mgololo. Hata hivyo, uongozi wa Iringa umewahi kwenda pale na kutaka kupotosha ukweli. Niombe sasa Waziri asimamie na afuatane na mimi ili tukaone ile GN ambayo tulipewa Halmashauri ya Mji wa Makambako ili wananchi wale waweze kupata huduma jirani na Mji wa Makambako. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna suala zito kama linalohusu mipaka. Mimi namuelewa sana Mheshimiwa Sanga katika *concern* yake hiyo, wananchi wanahitaji kweli kwenda eneo hilo lakini kwa sababu maeneo ya mipaka yameshaainishwa itakuwa ni vigumu leo niagize kufanya jambo fulani. Isipokuwa nifanye jambo moja, endapo haya mahitaji yanaonekana ni ya msingi, kama nilivyosema katika jibu langu la awali, Mheshimiwa Deo Sanga najua una ushawishi mzuri sana katika maeneo yale na ukizingatia kwamba ulikuwa Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa kwa hiyo kauli yako inasikika vizuri sana, nadhani mchakato ukianza kama nilivyoeeleza katika vikao vyetu vya vijiji vya WDC, DCC na RCC jambo hili litaisha vizuri. Jambo hili linaenda hadi kubadilisha zile *coordinates* katika GN, ndiyo maana nasema lazima liwe shirikishi, watu wa maeneo hayo wakubaliane kwa pamoja ni jinsi gani tutafanya kama tunataka kubadilisha mipaka. Kwa mujibu wa Sheria Sura 287, kifungu cha 10 mpaka 11 vimempa mamlaka Waziri mwenye dhamana kubadilisha mipaka lakini ni endapo itaonekana ninyi mmemaliza mchakato huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kijiji cha Nyigo kwamba GN zimebadilishwa yaani haziko sawasawa, naomba niseme kwamba katika hilo niko radhi kutembelea kijiji hicho. Katika safari zangu za Nyanda ya Juu Kusini nitamshirikisha na nitamuomba tushirikiane kama tulivyoshirikiana katika ziara yangu iliyopita lengo kubwa likiwa ni kuleta mtengamano mzuri katika maeneo yetu. (Makofi)

**NABU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nishukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yaliyoko kwenye Jimbo la Makambako yanafanana sana na matatizo yaliyoko kwenye Jimbo la Nyamagana katika Kata za Kishiri na Igoma. Majibu ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri sana ila nilitaka tu kupata uhakika kutoka kwake na sisi ambao tuna matatizo ya kupata huduma kati ya Kata ya Kishiri na Igoma tukirudia mchakato huu upya kuanzia kwenye ngazi zote ambazo amezitaja tukaleta kwake tutapata *approval* ya kufanya marekebisho kwa wakati? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri Jafo, napenda niongezee kwenye swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Mabula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na migogoro mingi ya mipaka ambayo kimsingi si yote inaitwa migogoro. Wakati mwingine kulitokea makosa wakati wa kutafakari mipaka hiyo na kugawanya mamlaka za utawala lakini wakati mwingine inatokana tu na mabadiliko ya kijiografia na mahitaji yameelekea upande ambao pengine busara sasa inataka namna mpya itizamwe ili kuweza kurekebisha mipaka hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niwashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba michakato hii kwa mfumo wa kisheria na taratibu zake inaanzia huko huko chini. Kama ninyi huko chini mtatoa kwenye vikao vyote vya Wilaya na Mkoa mkawa mmekubaliana sisi huku kubadilisha hizi GN si tatizo kubwa. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mkazitaarifu mamlaka na vikao vinavyohusika viweze kufuata taratibu za kisheria kama zinavyotaka na kama walivyopendekeza mpaka tukafikia kuweka mipaka hiyo, wafanye hivyo hivyo katika kupendekeza kama wanataka kubadilisha mipaka hiyo na sisi Serikali hatutakuwa na pingamizi katika jambo hilo. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea.



Na. 336

### **Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mima na Mbori**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Serikali ilikwishaanza kujenga vituo vya afya katika vijiji vya Mima na Mbori na ujenzi huo umesimama kutokana na ukosefu wa fedha.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo ili wananchi wa maeneo hayo wapate huduma za afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa jengo la Kituo cha Afya Mima ulianza mwaka 2008/2009 ambapo mpaka sasa umegharimu kiasi cha shilingi milioni 60. Jengo la wagonjwa wa nje (OPD) liko katika hatua ya umalizaji. Kazi ambazo hazijakamilika ni uwekaji wa dari, samani pamoja na vifaa tiba. Ili kumaliza kazi hiyo zimetengwa shilingi milioni 15 katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Aidha, imejengwa nyumba ya watumishi ambayo imekamilika kwa gharama ya shilingi milioni 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa jengo la Kituo cha Afya Mbori ulianza katika mwaka wa fedha 2011/2012 ambapo mpaka sasa umegharimu kiasi cha shilingi milioni 82. Kazi zilizofanyika ni upauaji, upakaji rangi nje na ndani, uwekaji wa madirisha ya vioo pamoja na kupiga dari. Kazi zilizobaki ni pamoja na ufungaji wa umeme, ufungaji wa milango ya ndani 16, ufungaji wa taa na uwekaji wa mfumo wa maji safi na taka. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, kituo hiki kilitengewa shilingi milioni 15 ili kumaliza kazi zilizobaki na shilingi milioni 35 zimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 ili kujenga nyumba ya watumishi (two in one).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, pamoja na kutenga shilingi milioni 15 kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Mima na shilingi milioni 35 kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya cha Mbori, je, Mheshimiwa Waziri haoni fedha hizi zilizotengwa ni kidogo kiasi kwamba vituo hivi vitachukua zaidi ya miaka mitano kukamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna majengo ya zahanati ya Kijiji cha Igoji Kaskazini na Igoji Kusini Salaze yamekamiliika na kinachohitajika sasa ni huduma za dawa.

Je, yuko tayari sasa majengo haya yakaanza kutumika kwa ajili ya huduma za dawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, kama nilivyosema wiki iliyopita kwamba yeye ni greda za zamani lakini makali yale yale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Mima kimetengewa shilingi milioni 15 na Mbori shilingi milioni 35, Mbunge anasema fedha hizi hazitoshi. Hata hivyo, katika mchakato wa bajeti tulikuwa tunapokea mapendekezo mbalimbali ambapo wahandisi wetu walifanya *analysis* ya kila jengo linahitaji kiasi gani ili liweze kukamilika. Kama fedha hizi hazitoshi basi tutaangalia nini cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika jibu langu la swali la msingi la wiki iliyopita nilisema, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Afya na Kamati ya Bunge tulifanya zoezi moja ambalo tunaendelea kulifanya mpaka hivi sasa na tumeshapeleka maelekezo mbalimbali kwa Wakurugenzi wetu wa Halmashauri, wabainishe miradi yote ambayo haijakamilika halafu tuifanyie *analysis* tuone ni jinsi gani tutafanya ili mradi miradi hiyo yote iweze kukamilika. Kwa sababu ukiachia kwa Mheshimiwa Lubeleje sambamba na hilo kuna maeneo mbalimbali miradi mingi sana iliyojengwa miaka ya nyuma bado haijakamilika. Kwa hiyo, ndiyo maana Ofisi yetu ikaamua ni vyema tubainishe miradi yote na tuifanyie tathmini ya kina ili tujue tunahitaji pesa kiasi gani ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuahidi Mheshimiwa Lubeleje kwamba lengo letu ni kukamilisha maeneo haya nikijua wazi kwamba

Halmashauri ya Mpwapwa na Jimbo lake la Mpwapwa na Kibakwe ambapo kijiografia ni eneo kubwa sana, wananchi wake lazima wapatiwe huduma. Kwa hiyo, tuna kila sababu kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikisha huduma za wananchi hasa huduma za afya zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwamba vituo vya afya vimekamilika lakini kuna tatizo kubwa la ukosefu wa dawa na vifaa tiba, naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyofanya siku chache zilizopita kutembelea Jimbo lake na kubaini huduma na changamoto mbalimbali, tutajitahidi kadiri iwezekanavyo vituo hivi viweze kufanya kazi ili wananchi wapate huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Karema ni kituo ambacho kimekamilishwa ujenzi na Serikali lakini tatizo kituo hicho hakina umeme ili kiweze kufanya kazi. Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kukamilisha kituo hicho ili kiweze kuwahudumia wananchi wa Tarafa ya Karema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali limeulizwa kuhusu umeme, sijui kama Naibu Waziri wa Nishati na Madini amelisikia angekusaidia hili.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Jimbo la Mpanda hadi sasa linapata umeme kwa kutumia mafuta kitu ambacho ni gharama kubwa sana. Hata hivyo, tumeshakaa na Mheshimiwa Kakoso, tumeainisha vijiji vyote vya Mpanda na Katavi, vijiji vyote vya eneo lake pamoja na hospitali na maeneo mengine yatapata umeme kuanzia Julai, 2016. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa hospitali inayotegemewa na wananchi wa Loliondo, Mkoani Arusha ni Hospitali ya Misheni ya Waso ingawa hospitali hii ina changamoto nyingi sana; na kwa kuwa hatuna Hospitali ya Wilaya ya Ngorongoro, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kujenga Hospitali ya Wilaya ili wakazi wa maeneo yale wapate huduma ya matibabu ipasavyo maana wakazi wengi wa maeneo yale ni wafugaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue ombi hili kutoka kwa Mheshimiwa Catherine Magige kwamba Ngorongoro ijengwe Hospitali ya Wilaya na nikitambua kwamba katika maeneo haya kuna changamoto kubwa sana. Juzi juzi nilikuwa na Mbunge wa eneo hilo akishirikiana na wananchi wake na Madiwani ambapo walikuja ofisini kwangu kuelezea changamoto zinazowakabili wananchi wa maeneo hayo.

Kwa hiyo, jambo kubwa kama nilivyosema katika miradi kama hii, naomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu yeye ni wa mkoa mzima ashirikiane na Mbunge wa Jimbo na najua ni mpambanaji mkubwa sana katika sekta ya afya, wafanye mchakato mpana wa kuliibua vizuri jambo hili ili badala ya kutumia Hospitali ya DDH ambayo ni ya Misheni tuhakikishe wananchi tunawapatia Hospitali yao ya Wilaya ili mradi na wao waweze kunufaika na huduma ya afya katika nchi yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ina majimbo matatu na Hospitali ya Wilaya ni moja. Je, ni lini sasa Serikali itapanua hospitali ile hasa wodi ya akinamama wajawazito?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba si chini ya wiki tatu au nne Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Shangazi walikuja ofisini kwangu. Lengo la kuja ofisini kwangu ilikuwa ni ajenda ya barabara halikadhalika huduma ya afya katika maeneo yao. Licha ya ajenda ya kuhakikisha tunapanua hospitali ile lakini miongoni mwa ajenda walizokujanazo ni kuimarisha vile vituo vyao vya afya viweze kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, kama nilivyomuahidi Mheshimiwa Shekilindi alivyokuja ofisini, jukumu letu kubwa ni kubainisha na aliniambia nipite route tofauti nione jiografia ya eneo lake, nikija naomba anipitishe niione vizuri lakini tupange mikakati ya pamoja kuwasaidia wananchi wetu. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, napenda kuongeza majibu kwenye swali la Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto kwamba katika sera ya afya sasa hivi tunataka kuondoka kwenye Hospitali ya Wilaya twende kwenye Hospitali za Halmashauri.

Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote ambao Wilaya zao zina Halmashauri zaidi ya mbili, tatu, sasa hivi kiseru tunapendekeza kila Halmashauri iwe na hospitali yake badala ya kuwa na Hospitali ya Wilaya. Kwa kufanya hivi tunaamini tutaweza kutatua mlundikano wa wagonjwa katika hospitali mbalimbali za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutatoa maelekezo rasmi ya kiseru katika Halmashauri mbalimbali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Na. 337

### **Utekelezaji wa TASAF III – Zanzibar**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. HALIMA ALI MOHAMMED)**  
aliuliza:-

Serikali imejipanga kupiga vita suala la ajira kwa watoto na imekuwa ikiunga mkono matamko ya Umoja wa Mataifa kuhusiana na ajira za watoto.

Je, kupitia Mradi wa TASAF III Serikali ina mikakati gani ya makusudi kuwasaidia watoto na tatizo la ajira za utotoni kwa upande wa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Ali Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini au TASAF III ulianza utekelezaji wake mwezi Agosti mwaka 2012. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, mpango umeandikisha jumla ya kaya milioni 1.1 Tanzania Bara na

Zanzibar. Kati ya hizo, kaya 33,532 zimeandikishwa na zinapata ruzuku ya malipo kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji, mpango unatilia mkazo uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini zilizoandikishwa. Uhawilishaji wa fedha umeziwezesha kaya hizi maskini kuwa na uhakika wa chakula, kupata huduma za afya na kuwawezesha watoto walio na umri wa kwenda shule kuanza shule na kwa walio katika shule za msingi na sekondari kupata mahitaji muhimu ya shule. Aidha, kaya hizi zinapata kipato cha ziada kupitia ajira za muda kwa wanakaya wenye uwezo wa kufanya kazi kwa kufanya kazi kwenye miradi midogo-midogo inayotekelezwa na TASAF.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini umewezesha watoto waliokuwa katika ajira za utotoni katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuongeza kipato cha kaya kutoka katika ajira hizo na kuweza kuhudhuria shule kwa kiwango cha 80% au zaidi. Kwa wale ambao hawajafikia umri wa kwenda shule waliweza kupata huduma za afya kwa kufuata taratibu za sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliowekwa unashirikisha viongozi wa maeneo ya utekelezaji katika ngazi zote kufuatilia mahudhuria ya watoto shuleni ili waweze kufikia viwango vilivyowekwa. Kwa kaya ambazo watoto wao hawafikishi idadi ya siku zilizopangwa za kwenda shule hupunguziwa ruzuku kama njia ya kuwahimiza kutimiza masharti ya kuhakikisha kwamba watoto wao wanahudhuria shuleni ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo ya Serikali kwamba Waheshimiwa Wabunge watashirikiana na viongozi wa Serikali katika ngazi zote ili kufanikisha mpango huu kwa kuhakikisha kwamba watoto walio na umri wa kwenda shule wanaotoka katika kaya maskini wanaandikishwa na kutimiza masharti ya Mpango kwa kuhudhuria shule kama inavyotakiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne, swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwa kuwa ongezeko la ajira kwa watoto wadogo ni kubwa sana hapa nchini; na kwa kuwa tatizo hilo kuchangiwa na kuvunjika kwa ndoa kwa kutokuwa na msingi na kuachiwa akina mama kulea hao watoto. Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi na wa haraka kuleta mabadiliko ya sheria ya mwaka 1971 ili wanawake na watoto hawa waweze kupata haki? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa TASAF III imeonesha mpango mzuri sana na mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwenye mashamba makubwa watoto hao wapo wengi na wanaonekana kama vile kwenye mashamba ya tumbaku, kahawa, chai, pamba na kadhalika, je, Waziri yuko tayari kuwakusanya hawa watoto na kuwapa elimu ya kutosha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa swali lake la kwanza kuhusiana na kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, bahati nzuri suala hili limekuwa likizungumzwa katika nyakati mbalimbali na hata katika Bunge hili na Mkutano huu wa Tatu, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria amelisemea sana, lakini vilevile Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto pia ameweza kulizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurudia kwa mara nyingine tena, ni kweli sheria hii ilionekana kuna upungufu. Ukiangalia viko baadhi ya vifungu vinavyoruhusu masuala mazima ya ndoa za utotoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kutambua kwamba katika masuala haya ya ndoa kuna mkanganyiko wa masuala ya kimila na kidini, ikaonekana kwamba ni vema suala hili likapatiwa suluhu kwa kupata maoni ya wananchi wengi zaidi kupitia mchakato wa *White Paper*. Mwanzo wakati zoezi hili Wizara ya Katiba na Sheria ilipotaka kulianza, taratibu zote karibia zilikuwa zimeshakamilika, lakini ikawa imeingiliana na mchakato wa Mabadiliko ya Katiba. Ikaonekana itakuwa si wakati mzuri kuwachanganya wananchi, huku wanatakiwa watoe maoni kuhusiana na Katiba Mpya lakini wakati huo huo unawapelekea zoezi lingine kuhusiana na marekebisho ya Sheria ya Ndoa. Vilevile ilionekana kwamba huenda wakati ule kwenye kukusanya maoni ya Mabadiliko ya Katiba wananchi wangeweza kulisemea jambo hili lakini kwa kiasi kikubwa halikusemewa sana. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa upande wa Wizara ya Katiba na Sheria bado wanasubiria wakati mzuri zaidi wa kuweza kulipeleka lakini ni lazima liende kupitia Waraka wa Maoni kupitia *White Paper*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili kwamba je, Serikali iko tayari kutoa elimu kwa watoto ambao wamekuwa wakifanya ajira mbalimbali za utotoni, niseme tu kwamba kupitia Wizara ya Kazi kwa Mheshimiwa Jenista, wamekuwa wakifanya kazi hii na wanaendelea kufanya kazi hii kuhakikisha kwamba watoto hawa ambao wako katika ajira za utotoni wanaelimishwa, lakini zaidi kuhakikisha kwamba wazazi wao wanapewa elimu hii. Ndiyo maana kupitia TASAF kama nilivyoeleza, nichukulie tu kwa upande wa Zanzibar, zaidi ya watoto laki moja na mbili wamekuwa wakinufaika na ruzuku hii ili kuwawezesha kwenda shule.



Kwa hiyo, ni imani yangu bado kupitia Serikali kwa ujumla wake na mipango mbalimbali na TASAF ikiwemo tutahakikisha tunatoa elimu hii, lakini vilevile kuona ni kwa namna gani watoto wengi zaidi wanaweza kunufaika nayo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa TASAF III imekuwa ikihamasisha sana hizi kaya maskini kujiunga na Mfuko wa Bima za Jamii (CHF). Je, mpaka sasa ni kaya ngapi zimeweza kujiunga na huu Mfuko huu? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tu niombe uniruhusu niweze kutoa maelezo ya utangulizi kidogo kabla sijajibu hoja yake. Kumekuwa na hoja na watu wengi wamekuwa wakitoa ushauri kwamba katika hizi kaya ambazo zinanufaika na ruzuku hii ya uhawilishaji, walazimishwe kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii.

Kwanza kabisa niseme duniani kote katika taratibu za uendeshaji wa mipango ya uhawilishaji wa fedha katika jamii huwa ni hiari. Kwa hiyo, tunachokifanya sisi kama TASAF ni kuhakikisha kwamba katika kila siku wanapoenda kupokea malipo tunawaelimisha kuhusiana na umuhimu wa kuweza kujiunga na Mfuko huu wa Bima ya Afya. Hadi sasa kaya 54,924 kutoka katika Halmashauri 28 zimeweza kujiunga na Mfuko huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu pongezi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chato ambayo zaidi ya 90% ya walengwa wake wameshajiunga na Mfuko wa Bima ya Afya. Nitoe pia pongezi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ambapo 60% ya walengwa wake tayari wameshajiunga na Mfuko wa Bima ya Afya.

Vilevile nitoe pongezi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Halmashauri au Manispaa ya Mtwara pamoja na Kibaha lakini na nyingine nyingi. Niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge na ninyi pia mtusaidie kuendelea na uhamasishaji ili kuhakikisha kwamba walengwa hawa wanaweza kujiunga ili waweze kupata huduma ya matibabu ya afya pale wanapohitaji. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.



**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wandereko wote na Warufiji, naomba swali langu lipatiwe majibu.

Na. 338

### **Vyama vya Msingi kuwaibia Wakulima**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** aliuliza:-

Wakulima wa zao la korosho Jimbo la Rufiji wameibiwa zaidi ya shilingi 900,000,000 kwa mwaka 2011 kutoka kwa Vyama vya Msingi vya Kimani, Mwasani, Kibiti na Ikwiriri.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua kali dhidi ya vyama hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa kuna Wandengereko tunakaa maeneo mengine. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Mifugo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012 Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini alifanya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika wa Korosho katika Mkoa wa Pwani na kubaini upotevu wa fedha wa shilingi 2,655,182,760.46 uliosababishwa na viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika. Aidha, uhakiki uliofanywa na Ofisi ya Mrajisi huyo unaonesha kuwa wakulima wa korosho wa Mkoa wa Pwani wanavidai vyama vya msingi jumla ya shilingi 3,195,135,103, deni ambalo linatokana na sababu mbalimbali za kibiashara kama vile anguko la bei ya korosho katika soko la dunia. Mchanganuo wa deni hilo kwa kila Wilaya ni kama ifuatavyo; Mkuranga ni shilingi 1,931,224,587, Rufiji shilingi 1,215,018,100, Kibaha Mjini shilingi 758,880, Bagamoyo ni shilingi 10,275,960 na Mafia shilingi 7,857,576.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukaguzi huo ilibainika kwamba Mkoa wa Pwani ulikuwa na viongozi 822 wa Vyama vya Ushirika waliodaiwa kuhusika na upotevu wa fedha za wakulima wa korosho. Kwa Wilaya ya Rufiji viongozi 41 wa vyama walibainika kufanya ubadhirifu huo na hivyo kwa kutumia kifungu cha 95 cha Sheria ya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, Mrajisi aliwaandikia hati ya madai na kuwataka kulipa fedha zilizopotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa Vyama vya Mwaseni 11, Kilima Ngorongo tisa, Ikwiriri 11 na Kibiti 10 walihusika. Kiasi wanachodaiwa viongozi hao ni shilingi 68,878,188 katika mchanganuo ufuatao:- Mwaseni shilingi 5,152,906, Kilima Ngorongo shilingi 22,104,384, Ikwiriri shilingi 20,549,494 na Kibiti shilingi 21,071,398. Viongozi wa vyama hivi vyote kutoka Wilaya ya Rufiji bado hawajalipa fedha wanazodaiwa na taratibu zinakamilishwa za kuwapeleka mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 5 Novemba, 2015 ni viongozi 79 tu kati ya 822 wa Mkoa wote wa Pwani waliokuwa wamerejesha jumla ya shilingi 24,260,163.19. Kwa viongozi ambao hawajarejesha, taratibu zimeandaliwa za kuwafikisha katika vyombo vya sheria ili hatua ziweze kuchukuliwa ambapo hadi tarehe 8/06/2016 tayari majalada 11 yalikuwa yamefunguliwa polisi na kufikishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mkoa wa Pwani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza, lakini nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yamenipa faraja kuliko majibu ya juzi yaliyotolewa na Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza la nyongeza, katika kuwasaidia wakulima hao hao, bajeti ya Wizara hii ya Kilimo na Mifugo kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 imetenga maeneo ya kipaumbele na katika maeneo hayo ya kipaumbele Rufiji si maeneo ya kipaumbele kwa mujibu wa bajeti hii ya mwaka 2016/2017. Kama Wizara hii ingeweza kutoa kipaumbele kwa Rufiji inamaanisha kwamba tatizo la sukari hapa nchini lingeweza kwisha kabisa kwa Serikali kuwekeza na kutengeneza viwanda vikubwa vya sukari. Nataka nifahamu hawa wataalam waliomsaidia Mheshimiwa Waziri kuandaa bajeti hii wana elimu gani, darasa la saba au ni *form four*? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Serikali kupitia Wizara hii ya Kilimo ilituletea sera ya kutuletea RUBADA. RUBADA hii wamekuwa wabadhirifu wakubwa wa fedha za umma ambao pia ni madalali wa viwanja na mashamba, wamesababisha anguko kubwa la uchumi Rufiji kwa kushindwa kusaidia kuleta wawekezaji katika kilimo lakini pia kushindwa kusimamia Bonde la Mto Rufiji? Nataka nisikie kauli ya Mheshimiwa Waziri hapa ni lini ataifuta hii RUBADA na kutuletea mradi mkubwa wa kilimo kwa ajili ya Wanarufiji? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, swali la kwanza nadhani ni fupi sana, ni kutaja tu elimu yao halafu ujibu hilo la pili.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya watendaji walionisaidia kutayarisha majibu haya, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kama zilivyo Wizara nyingi za Serikali zina wataalam waliobobea katika fani mbalimbali. Kwa hiyo, kuhusu uwezo wao hatujawahi kuutilia maanani. Kuna changamoto ndiyo katika utekelezaji tunadiriki kusema hivyo lakini haitokani na uwezo wa wataalam wetu. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unamaanisha hamjawahi kuutilia mashaka na siyo maanani? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nijibu swali lake kuhusu RUBADA. Ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mchengerwa kwamba kumekuwepo na changamoto nyingi kuhusiana na RUBADA lakini Serikali imeifanyia marekebisho makubwa RUBADA. Mnafahamu kwamba tayari tumeshabadilisha uongozi na tunaendelea kufanyia marekebisho na bado tunaamini kwamba RUBADA itaendelea kuwa ni chombo muhimu katika lengo la Serikali la kutumia Rufiji kama sehemu muhimu sana kwa ajili ya kilimo.

Vilevile nimfahamishe Mheshimiwa Mchengerwa kwamba hatujaitenga Rufiji katika vipaumbele vyetu na ndiyo maana katika nchi nzima sehemu ya pekee ambayo imepata fedha katika bajeti yetu kwa ajili ya kilimo kwa ajili ya vijana ni Rufiji. Kwa hiyo, nimfahamishe tu kwamba Rufiji ni sehemu muhimu sana, ni bonde ambalo ni muhimu sana kwa kilimo katika nchi yetu na tutaendelea kulitumia kwa ajili ya kilimo cha mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na namna ya kutatua changamoto tulionayo ya sukari, tunafahamu ni bonde muhimu sana. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hatujaisahau Rufiji, hatujaisahau RUBADA tutaendelea kufanyia kazi changamoto zilizopo ili tuweze kutumia eneo hilo vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aweso.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ...

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aweso naomba ukae, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na majibu sahihi. Nilitaka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mara kwa mara amekuwa akija hata ofisini kufuatilia jambo hili pamoja na mambo mengine ya wapiga kura na mimi niwapongeze wapiga kura wake kwa kumpigia kura na kwa kweli anastahili kuwa mwakilishi wao. Nimhakikishie kwamba mimi binafsi baada ya Bunge la Bajeti nitapanga ziara na nitaongozana naye kwenda kupita haya maeneo yote ambayo amekuwa akiyalalamikia na ambayo amekuwa akiyaleta ili Serikali iweze kuchukua uamuzi tukiwa kwenye eneo la tukio.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aweso swali fupi.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa matatizo ya Jimbo la Rufiji yanafanana kabisa na Jimbo langu la Pangani katika sekta ya kilimo na uvuvi. Nataka nijue ni lini Serikali itakuwa tayari kuwakumbuka wavuvi pamoja na wakulima wa zao la korosho katika Jimbo langu la Pangani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Mifugo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa changamoto za Pangani zimefanana kwa kiasi kikubwa na Rufiji na nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama alivyosikia kwenye wasilisho la Wizara ya Fedha kuhusu bajeti ya Serikali, korosho ni moja kati ya mazao ambayo tayari tuna mkakati mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata ahueni. Mmesikia tunaondoa tozo tano ambazo zimekuwa za usumbufu mkubwa kwa wananchi wetu. Tunategemea kwamba bei ya korosho itaendelea kuimarika na kuwa nzuri kwa sababu tayari tozo ambazo zilikuwa ni kero ziko mbioni kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimhakikishie kwamba hata kuhusu uvuvi, nina hakika alifuatilia tulipowasilisha bajeti yetu, tumeweka mikakati mizuri sana ya kuhakikisha wavuvi wetu wananufaika na mipango mbalimbali ya Serikali ukiwepo mpango wa kutoa mikopo kwa ajili ya vikundi vya wavuvi, kutoa elimu kuhusu uvuvi mzuri lakini kuwasaidia wavuvi wetu kuweza kupata nyenzo za uvuvi. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba wananchi wa Pangani katika uvuvi lakini vilevile katika kilimo hawajasahauliwa na Serikali. Hata hivyo, kwa sababu ni Mbunge makini na mara nyingi sana tumeongea naye, nimhakikishie tu kwamba kwa yale ambayo anafikiri tunahitaji kuelekeza nguvu zetu zaidi, naomba tukutane naye na ikibidi niko tayari kuandamana naye kwenda Pangani tukaangalie changamoto zilizopo.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

Na. 339

**Ahadi ya Serikali kwa Wakulima wa Korosho  
kuhusu Malipo kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Serikali iliwaahidi wakulima wa korosho kupata malipo halali ya mauzo ya korosho kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

(a) Je, ni lini Serikali itawahakikishia wakulima wa korosho wa Wilaya ya Masasi wanalipwa malipo yao ya mwisho wanayostahili?

(b) Je, Serikali imekuchukua hatua gani kwa Vyama vya Ushirika ambavyo haviwapi wakulima wa korosho fedha zao kama korosho zilivyouzwa kwenye mnada?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Mifugo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya wakulima wa korosho katika baadhi ya vyama vya msingi ambao hawakulipwa *bonus* baada ya kuuza korosho zao kama ilivyostahili. Hii ilisababishwa na baadhi ya vyama hivyo kukiuka taratibu za makato ya korosho kama ilivyokubaliwa katika Mkutano Mkuu wa wadau uliofanyika mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha suala la *bonus*, wakulima wote walilipwa malipo ya awali ya korosho kwa bei elekezi ya shilingi 1,200 na waliongezewa malipo ya pili kutegemeana na bei iliyopatikana sokoni. Nyongeza ya malipo ya pili yalianzia shilingi 800 kwa kilo na kufanya malipo ya chini aliyopata mkulima kuwa shilingi 2,000 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la *bonus* Serikali inafuatilia kuona kama kuna ubadhirifu uliofanyika katika Vyama vya Ushirika kwa kufanya ukaguzi na iwapo itadhihirika, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa waliohusika ikiwa ni pamoja na kuamuru wahusika kurudisha fedha hizo na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa mapunjo ya malipo ya ziada hayatokei tena, Serikali kupitia Bodi ya Korosho imejipanga kuendelea kuvihamasisha na kuvielimisha vyama vya msingi umuhimu wa kukusanya korosho kutoka kwa wanachama wake na kuziua badala ya kuchukua mikopo yenye riba kubwa kutoka kwenye mabengi na kununua korosho hali inayosababisha malipo ya awamu yasiyokuwa na tija kwa mkulima. Vilevile wakulima wote wa korosho wanashauriwa kufungua akaunti benki kwa lengo la kukabiliana na ubadhirifu wa fedha unaochangiwa na zoezi la usafirishaji wa fedha kutoka benki kwenda kwa wakulima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bwanausi swali la nyongeza.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru majibu ya Naibu Waziri. Swali langu la kwanza, kwa kuwa malipo ya *bonus* ni haki ya wakulima kwa maana ni malipo ya tatu ya korosho na wananchi wale tangu mwezi Disemba wanazungushwa kupata fedha yao. Je, Serikali haioni kuna haja ya kutoa kauli sana kwamba wananchi wale waweze kulipwa fedha zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa mchanganuo wa fedha zinazopaswa kulipwa kwa wakulima ulishatolewa Bodi ya Korosho tangu Aprili na Serikali imepata kigugumizi hadi sasa kutotoa kauli ya wananchi wale kulipwa na Waziri naye aliahidi kuja pale. Je, leo Waziri anaweza kutoa kauli ya Serikali kuhusu ujio wake katika eneo hilo? Pia ni kwa nini asitoe tamko kuwaambia vyama kuanzia sasa wawalipe wakulima? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu *bonus* ni kweli kabisa kwamba wananchi wamepunjwa *bonus* mpaka Sh.200 katika kilo. Kama nilivyosema awali, Serikali inaendelea na uchunguzi kuhusu ubadhirifu ambao umefanywa na Vyama vya Ushirika ili wale wote ambao wamehusika na mapunjo hayo waweze kuchukuliwa hatua za kisheria. Nitumie fursa hii kuvitaka Vyama vya Msingi kuhakikisha kwamba wakulima wanapata salio la *bonus* yao ambayo hawajalipwa mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la sisi kwenda, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara baada ya Bunge la Bajeti tutafanya utaratibu kwenda kuongea na wananchi na kufuatilia kwa ukaribu zaidi ili waweze kulipwa bonasi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwaeleza na kuwashauri Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wa maeneo yanayolimwa korosho kwamba kinacholeta changamoto kubwa katika malipo stahili kwa ajili ya korosho ni kwa sababu Vyama vya Msingi pamoja na wakulima wanachukua madeni kutoka kwenye mabenki ili kuwalipa wakulima kabla korosho ile haijapata mteja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuwashauri kwamba wawe na subira, wasiwe na haraka ya kwenda kuchukua mikopo, badala yake wakusanye korosho kwa utaratibu wetu ule wa stakabadhi ghalani ili korosho ile iweze kununuliwa na hivyo kuondokana na utaratibu ambao inabidi ulipe *interest* za benki. Mara nyingine viongozi ambao siyo waadilifu wa Vyama vya Ushirika pamoja na Maafisa Ushirika wanatumia mtindo huo kama ni mwanya wa kuwaibia na kufanya makato ambayo yanawafanya wakulima wasiweze kupata fedha wanayostahili. Wawe na subira, waweke korosho yao, wauze kwa pamoja, waache kuchukua kwanza mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 340

### **Kutatua Tatizo la Maji Wilaya ya Simanjiro**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. JAMES K. MILLYA)** aliuliza:-

Tangu kuanzishwa kwake Wilaya ya Simanjiro haijawahi kupata maji ya uhakika licha ya ahadi mbalimbali ikiwemo ile ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kuwa Simanjiro itatengewa shilingi bilioni 30 ili kuleta maji kutoka Mto Ruvu hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Orkesumet.

Je, Serikali itatekeleza lini ahadi hiyo ili kuwakomboa wananchi wa Simanjiro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, huyo ni Mbunge wa Simanjiro siyo Mbunge wa Viti Maalum. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, naomba nirudie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Simanjiro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (BADEA) na Mfuko wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (OFID) inatekeleza mradi wa maji safi utakaohudumia Mji wa Orkesumet ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro. Mradi huu utagharimu dola za Marekani milioni 18.4 ambapo BADEA watatoa dola za Marekani milioni nane, OFID watatoa dola za Marekani milioni nane na mchango wa Serikali kwa mradi huo ni dola za Marekani milioni 2.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu umepangwa kutekelezwa katika vipande viwili, yaani *lots* mbili. Kipande cha kwanza kitahusu ujenzi wa chanzo cha maji kutoka Mto Pangani eneo la Ruvu, mtambo wa kusafisha maji pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka. Makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha kwanza yamewasilishwa BADEA kwa ajili ya kupata kibali yaani *no objection* cha kutangaza zabuni. Kipande cha pili kinahusu ujenzi wa bomba kuu, matanki ya kuhifadhi maji na mabomba ya usambazaji maji. Kibali cha kutangaza zabuni kimepatikana na taratibu za kutafuta mkandarasi zimekamilika na Wizara inasubiri kibali kwa ajili ya kuanza ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo. Mradi huo utakapokamilika, utahudumia wakazi wapatao 52,000.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro, naomba niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kusikia kilio chetu, lakini sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linahusu ahadi za viongozi; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alipopita kwenye maeneo mbalimbali alitoa ahadi kuhusu maji ikiwepo Wilaya ya Kilolo maeneo ya Ilula na aliahidi kwamba suala la maji litakuwa ni historia kwa Wilaya ile. Je, Serikali inasemaje na mwaka huu imetenga fedha kwa ajili ya wananchi wa Ilula?



Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tatizo la maji linatatuliwa kwa ujenzi wa mabwawa na kwa kuwa kuna mabwawa yaliyojengwa sehemu za Nyanzwa, Ilindi, Ruaha Mbuyuni na Mahenge na wakati yanajengwa wananchi walikuwa wachache, sasa wameongezeka kwa hiyo maji yale hayatoshi. Serikali itakuwa tayari kuongeza fedha ili wananchi wale waweze kupata maji ya uhakika? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza suala la ahadi, ahadi zote zimeishaainishwa. Wizara ya Maji tuna ahadi zaidi ya 60 ambazo Mheshimiwa Rais wetu Magufuli wakati anapiga kampeni aliwaahidi wananchi. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba tunatekeleza ahadi za viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ilula nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari mazungumzo yanaendelea na Serikali ya Australia na mradi huu wa Ilula utagharimu dola milioni tisa, kwa hiyo, tunaufanyia kazi. Pia katika mwaka huu wa fedha kwenye bajeti tumemtenga shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mabwawa, hii ni ahadi yetu, kama tumejenga mabwawa, sasa hivi wananchi wameongezeka, tutakachofanya moja ama ni kulipanua bwawa lile kama lina uwezekano wa kupanuliwa lakini pili ni kuongeza bwawa jipya. Kwa sasa tumeshaagiza Wakurugenzi wote wajaribu kufanya utafiti, waainishe maeneo yote ya kujenga mabwawa na walete ili tuweze kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa eneo hili la Simanjiro na hasa eneo la Orkesumet ambako ametoa majibu Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala la maji katika eneo la Orkesumet limekuwa likiimbwa kuanzia mwaka 2005. Orkesumet ni eneo dogo tu tofauti na maeneo mengine ambayo yana shida kubwa ya maji. Lile ni eneo la wafugaji ambako akina mama wanatoka kwa saa zisizopungua nane kwenda kutafuta maji. Naomba kauli ya Serikali ni lini haidhuru wananchi wa Simanjiro katika Kata za Narakauo, Kimotorko, Emishie, Naberera, Kitwai, Lobosoiret watapata maji? Pia ni lini hasa mradi huo utaanza rasmi?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza huwa ni moja tu, kwa hiyo chagua moja kati ya hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari awamu ya kwanza ya kusaini mkataba mazungumzo yamekamiliwa. Kwa hiyo, wakati wowote ule pengine kwenye mwezi wa saba, tutakuwa tumesaini mkataba wa awamu ya kwanza na kuanza hiyo kazi. Pia vijiji alivyovitaja, vyote vitapewa maji ikiwa ni pamoja na maji ya mifugo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na Jimbo la Mbeya Vijijini kuwa na vyanzo vya uhakika wa maji kutoka Mlima Mbeya, lakini maji yamekuwa yakipelekwa Jijini Mbeya badala ya kupelekwa kwenye sehemu zenye uhaba mkubwa wa maji kwenye vijiji vya kata ya Mjele na Utengule Usongwe. Je, ni lini Wizara itapeleka maji safi kwenye vijiji vya kata za Mjele na Utengule Usongwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru ameuliza swali zuri sana, ni swali la kisera. Nimhakikishie kwamba tayari tumeshatoa maelekezo eneo lolote ambalo chanzo cha maji kinaanzia pale, vijiji vilivyo karibu na chanzo ndiyo viwe vya kwanza kupata maji.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tunalielekeza kwa Wakurugenzi wa mamlaka ambao wanahusika na huo mradi, wahakikishie katika eneo hilo kwanza wanawapa maji wananchi waliopo pale baadaye sasa ndiyo wanapeleka maeneo mengine ya mjini. Kwa hili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitalifuatilia mimi mwenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 341

### **Miradi ya Maji katika Kijiji cha Mwankoko na Kisaki-Irao**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Miradi ya kuboresha huduma ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Kiarabu (BADEA), Shirika la Mafuta Ulimwenguni (OFID) na Serikali ya Tanzania katika Kijiji cha Mwankoko na Kisaki katika eneo la Irao inaleta changamoto kubwa.

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kulipa fidia kwa wananchi waliopisha miradi hiyo ambapo tayari uthamini ulishafanyika kwa mara ya pili ambapo Mwankoko wanadai shilingi 1,510,427,634 na uthamini ulifanyika tarehe 13 Machi, 2014 na mradi wa Irao shilingi 2,932,001,058/=?

(b) Mradi wa maji wa Irao katika visima vyake vyote viwili vinapoteza uwezo wa kutoa maji kutoka Q250-170 kwa saa na kisima cha pili ni Q150-70 kwa saa. Je, Serikali ina mpango gani juu ya kukabiliana na tatizo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha uhakiki wa fidia kwa eneo la Mwankoko na imetuma kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kulipa fidia ya eneo hilo. Kwa upande wa Irao inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 2.9 zitahitajika kulipia fidia katika eneo hilo. Serikali inaendelea na tathmini ya uhakiki wa gharama za fidia hiyo na uhakiki huo ukikamilika fidia hizo zitalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa mradi wa maji safi Mjini Singida, kumejitokeza tatizo la kushuka kwa viwango vya uzalishaji maji katika visima viwili vya Irao. Kutokana na tatizo hilo, Serikali imechukua hatua za haraka ikiwemo kusafisha visima hivyo, kushusha pampu za visima vyote ili kuongeza kina cha kuchota maji. Baada ya jitihada hizo, imeonekana uwezo wa visima kutoa maji uliongezeka kwa kiasi. Aidha, Serikali imepanga kubadilisha pampu hizo ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuboresha huduma ya maji, Serikali imepanga kufunga pampu kwenye visima vitatu vya akiba vilivyochimbwa awali wakati wa utekelezaji wa mradi mkubwa katika Manispaa ya Singida. Kazi hii itatekelezwa pamoja na shughuli ya ulazaji wa mabomba kutoka kwenye visima hivyo vitatu hadi kwenye tanki dogo la kukusanya maji yanayovutwa na kusukumwa kwenda kwenye matenki makubwa katika eneo la karakana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba sasa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali tayari imekiri kusambaza mabomba na kupeleka pampu, napenda kujua ni lini sasa utekelezaji wake unaanza kufanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la maji ni kubwa katika Jimbo la Singida Mjini hususani kata za pembeni, Serikali inawaambia nini wananchi wa Jimbo la Singida Mjini kwa ajili ya kuhakikisha tatizo hili linaisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni lini mradi wa kusambaza maji katika Mji wa Singida utafanyika, tunahitaji shilingi milioni 730 na tayari tuna vyanzo viwili vya kupata hiyo fedha. Kwanza tumeshaomba fedha kutoka BADEA, lakini pili tumetoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Mamlaka wa Singida kuna fedha kidogo ambazo zipo, kwa hiyo wakati wowote mradi huu utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni lini tutakuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba Mji wa Singida unakuwa na maji ya kudumu. Kama nilivyojibu wakati wa bajeti kwamba tunaanza kujipanga ili tuweze kufanya usanifu wa kutoa maji Igunga kuyaleta Mji wa Singida ili kuhakikisha kwamba sasa tatizo la maji katika Mji wa Singida tunalimaliza. Tutamuagiza Mhandisi Mshauri, aanze kufanya kazi hiyo ili kuona ile *pressure* iliyoko Igunga inaweza ikafika Singida? Kama itakuwa inapungua basi wataalam watatushauri tufanyeje lakini Mji wa Singida ni mkame tutahakikisha kwamba tunawapa chanzo cha maji chenye uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa kuleta maji katika Mji wa Singida. Mahali ambapo mitambo, mashine na matanki yale yalipo katika Kata ya Mwankoko ambako ndiko maji yanatoka kwenda kwenye Mji wa Singida wao wenyewe hawana maji. Je, Serikali sasa iko tayari kutumia yale maji kuwasambazia wananchi wa Kata ya Mwankoko ili na wenyewe waweze kufaidi maji ambayo yako kwenye chanzo cha eneo lao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nijibu kwamba Serikali iko tayari na ndiyo malengo yetu kuhakikisha kwamba sehemu ya chanzo cha maji wananchi waliopo pale lazima

tuwaheshimu kwa sababu kwanza wamelinda kile chanzo hawajakiaribu, kwa hiyo lazima wafaidi juhudi waliyoifanya na pili wataendelea kulinda miundombinu yetu. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo na swali linalofuata.

Na. 342

### **Uhaba wa Maji Safi na Salama Mlimba**

**MHE. MARTIN M. MSUHA (K.n.y. MHE. SUSAN L. KIWANGA)** aliuliza:-

Pamoja na Jimbo la Mlimba kuwa na vyanzo vingi vya maji ikiwemo mito mikubwa, wananchi bado wanakumbwa na uhaba mkubwa na maji safi na salama.

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha mpango wa usambazaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Mlimba?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha skimu za umwagiliaji ili kuvipa tija vyanzo vya maji vilivyopo katika Jimbo la Mlimba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Halmashauri zote nchini. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero inatekeleza miradi 14, kati ya miradi hiyo miradi nane ipo katika Jimbo la Mlimba. Ujenzi wa miradi mitano katika vijiji vya Mlimba A, Mlimba B, Viwanja Sitini, Kamwene na Masagati umekamilika na inatoa huduma ya maji kwa wananchi wapatao 24,632. Miradi mitatu ya Idete, Namwawala na Matema ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Lengo la Serikali ni kukamilisha ujenzi wa miradi hiyo ili wananchi waweze kupata huduma ya maji kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza Skimu ya Umwagiliaji ya Njage yenye eneo la hekta 325 kupitia Mfuko wa Wilaya wa Kuendeleza Umwagiliaji (DIDF) na hivi sasa skimu hii imeingizwa katika mradi wa *Expanded Rice Production Project* ili kukamilisha ujenzi wa skimu hiyo.

Aidha, Serikali kupitia Gereza la Idete, inajenga skimu ya umwagiliaji yenye jumla ya eneo la hekta 1,000. Vilevile shamba la *Kilombero Plantation Limited (KPL)* lenye eneo la hekta 4,000 litaendelea kuzalisha mazao na liko katika hatua ya uendelezwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani, kupitia Mfuko wa *Feed the Future* inafanya upembuzi yakinifu katika maeneo yaliyoainishwa katika mpango kabambe wa umwagiliaji wa mwaka 2002 ya Kisegese, Udagaji na Mpanga – Ngalmila. Maeneo yatakayofaa yataingizwa kwenye hatua ya usanifu wa kina.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msuha swali la nyongeza.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kuuliza maswali mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mazingira ya Jimbo la Mlimba yanafanana kabisa na mazingira ya Jimbo Mbinga Vijijini, je, Serikali itapeleka maji lini katika Miji ya Maguu, Matiri na wa Rwanda ambao una taasisi nyingi sana zikiwemo sekondari za *form five* na *six*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Jimbo la Mbinga kuna miradi miwili ya maji iliyokuwa ikiendelea katika Kata ya Mkako lakini pia mradi mwingine katika Kata ya Ukata kupitia Kijiji cha Litoho. Ni lini Serikali itakamilisha miradi hii ya Mkako pamoja na Ukata ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji salama na safi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itahakikisha inapeleka maji katika maeneo ya Mbinga Vijijini, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba tayari tumeanza Programu ya Pili ya Utekelezaji wa Maendeleo ya Sekta ya Maji Nchini. Kama nilivyokwisha toa majibu kwamba wafadhili wametuhidi dola za Kimarekani bilioni 3.3 ambazo zitatumika kutekeleza miradi ya maji hapa nchini, hii ikiwa ni pamoja na miradi ya Mbinga Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha Mbinga Vijijini tumewatengea fedha. Niagize na naomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane tutengeneze mpango mzuri wa matumizi ya fedha hizi tulizozitoa katika hii bajeti ya mwaka wa fedha unaoanza mwezi Julai ili kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo ya Mbinga Vijijini wote wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili umesema kwamba kuna miradi miwili ambayo bado haijakamilika. Tumeshaelekeza kwamba miradi ile ambayo haikukamilika katika Programu ya Kwanza ya Utekelezaji wa Sekta ya Maji ndiyo tunaanza kuikamilisha kabla hatujaanza miradi mipya. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane na Halmashauri yake kuhakikisha kwamba kwanza tunakamilisha miradi hii kabla hatujaanza kuingia kwenye miradi mipya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Jimbo la Mlimba inafanana kabisa na hali ya Mkoani Pwani kuwa na vyanzo vingi na vikubwa vya maji ikiwemo Mto Ruvu na Mto Rufiji lakini bado wananchi wake wa Wilaya za Kibiti, Rufiji, Mkuranga na Kisarawe wanakabiliwa na adha kubwa ya maji safi na salama.

Je, ni lini sasa Serikali itaanzisha mradi wa kuyavuta maji ya Mto Rufiji ili kuwanufaisha wanawake wa Mkoa wa Pwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze, Mheshimiwa huyu mara nyingi sana amekuwa ananifuata na kuniuliza maswali mengi kuhusu miradi ya maji na ameniuliza pia hata kuhusu DAWASCO au DAWASA wanapelekaje maji Pwani, lakini nikuhakikishie kuhusu swali lako moja hili tayari tumeanza mazungumzo ya kufanya utafiti wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji kuyaleta Dar es Salaam ikipitia na maeneo uliyoyataja ya Ikwiriri, kuja Kibiti, kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tufahamu kwamba tunataka pia kufanya mradi mkubwa wa kujenga bwawa la Kidunda wa kuleta maji. Sasa kama tutakamilisha huu mradi wa Kidunda basi tutaangalia uwezekano kwamba tufanyaje je, tupeleke maji kutoka Kidunda kupeleka huko kwako au tufanye mradi wa Rufiji kwa sababu wakati mwingine unaweza ukafanya miradi miwili mikubwa yale yakawa mengi sana mpaka watu wakashindwa kuyatumia au taasisi za Serikali zikashindwa kuyatumia. Lakini ni kwamba swali lako la msingi ni kwamba ni kweli Serikali sasa hivi inaanza kujiweka tayari kufanya utaratibu wa kufanya utafiti wa kutoa mto Rufiji na kuyaleta Mikoa ya Pwani pamoja na Dar es Salaam.



**NAIBU SPIKA:** Tuendeleo Waheshimiwa Wazara ya Nishati Mheshimiwa Kanyasu Constatine John Mbunge wa Geita Mjini swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Vicky Kamata Likwelile.

Na. 343

### **Maeneo Waliyonyang'anywa Wananchi wa Geita**

**MHE. VICKY P. KAMATA (K.n.y MHE. CONSTATINE J. KANYASU)** aliuliza:-

Mgodi wa GGM - Geita umepewa eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 192 kwa ajili ya kuchimba dhahabu wakati wananchi wamenyang'anywa maeneo yao.

Je, ni lini maeneo waliyonyang'anywa wananchi yatarudishwa kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constatine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Vicky Kamata Likwelile, Mbunge wa Geita Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Geita Gold Mine Limited* yaani GGM inamiliki leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini kupitia leseni namba SML45/99 yenye ukubwa wa kilometa za mraba 196.27 iliyopewa kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo ambayo mgodi GGM waliyahitaji ndani ya leseni yao kwa ajili ya uchimbaji walifanya mazungumzo na wamiliki wa maeneo hayo na kulipa fidia kwa mujibu wa Sheria Namba Nne ya Madini ya 2010 pamoja na Sheria Namba Tano ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaomiliki ardhi ndani ya leseni ya GGM kwa ajili ya makazi na shughuli mbalimbali ambazo siyo shughuli za uchimbaji wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo baadhi ya wamiliki wa leseni za uchimbaji mdogo ambao hawakufikia makubaliano na mgodi wa GGM bado wanamiliki leseni zao za uchimbaji mdogo. Baadhi ya wananchi hao ni pamoja na Bwana Jumanne Mtafuni mwenye leseni ya uchimbaji mdogo PML0001044 pamoja na Bwana Leonard John Chipaka mwenye leseni namba PML0001331



wachimbaji wadogo hawa wanaendelea na shughuli za uchimbaji katika maeneo yao kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na maelezo haya sasa wananchi ambao wamepisha maeneo baadhi yao walilipwa fidia kwa mujibu wa taratibu za nchi hii.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Nyamalembo, Nyamasagata, Semina na sehemu zote ambazo hawa wawekezaji wa GGM wamechukua maeneo yao ningependa kufahamu ni nini manufaa ya moja kwa moja wanayoyapata wananchi hao ambao waliruhusu maeneo yao yanatumiwa na GGM?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imekuwa ikiahidi mara kwa mara kuwapatia maeneo ya uhakika na ya kudumu wachimbaji wadogo na kwa kuwa mpaka sasa bado haijawapatia wachimbaji hawa. Je, Serikali inapanga nini kutatua tatizo hilo, ukizingatia hivi karibuni mwezi wa saba ile PML ya STAMICO ina expire ni kwa nini Serikali isitoe tamko hili sasa hivi hapa kwamba mara baada ya hii PML ku-expire basi lile eneo litapewa wachimbaji wadogo wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya wananchi wa Geita kulingana na mgodi huu ni kweli kabisa Watanzania wengi na wananchi wa Geita hasa wa maeneo yanayozunguka mgodi huu wamekuwa wakitarajia manufaa makubwa sana. Lakini hata hivyo mambo ambayo wananchi wa maeneo hayo wamenufaika ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mgodi ulipoanza mwaka 1999 wananchi wanaozunguka mgodi huo walifanyiwa fidia. Wananchi ambao waliofanyiwa fidia ni pamoja na maeneo ya Nyamalembo, wananchi wa Nyamalembo wapatao 346 walilipwa fidia jumla ya shilingi bilioni sita nukta nane, lakini wananchi wa Katoma ambao wanafikia karibu 732 walilipwa shilingi bilioni 2.7 kama fidia na wananchi wengine wa Nyakabale, Nyamatagata ambao wanafikia 700 walilipwa shilingi bilioni 732 hayo ni manufaa ambayo wananchi hao waliyapata.

Lakini hata hivyo, pamoja na manufaa hayo mgodi wa GGM umeendelea kutoa ushuru kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo ambayo ni service levy. Hadi sasa mgodi huo umeshatoa takribani shilingi bilioni 4.7 kama service levy lakini manufaa mengine wanayoyapata wananchi hawa ni pamoja na ajira. Mgodi wa GGM hivi sasa unaajiri Watanzania wanaofikia 1568 kama nilivyozungumza kwenye jibu langu la msingi wakati wa bajeti yetu. Lakini kadhalika bado mgodi GGM wananchi wanaozunguka maeneo ya

Geita, Nyamatagata, Katoma, Nyakabale, pia wamezungumzia kujengewa hospitali, vituo vya afya pamoja na shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, kuhusu kuwapatia maeneo hasa ya Mgodini wa Bacliff ambao sasa hivi unamilikiwa na STAMICO pamoja na wabia wenzake. Niseme tu nitumie nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge Kamata ameendelea kupambana sana kwa wananchi wa Geita na mimi nimuombe aendeleo kupambana. Lakini nimhakikishie tu sasa hivi Serikali inakamilisha mazungumzo kupitia STAMICO pamoja na wabia wake ili kuona sasa ni eneo gani kampuni yetu ya STAMICO pamoja na wabia wake kwenye Mgodini wa Bacliff maeneo yapi wanaachi kwa ajili ya wananchi wa Geita. Hata hivyo Serikali inaendelea kuwategea maeneo mengine mbadala karibu na mgodi huo. Maeneo ambayo Serikali itayatenga kama ambavyo tunasema kila siku pamoja na maeneo ya Mgusu pamoja na maeneo mengine machache sana ya kule Nyakabale pamoja na Nyamalembu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumeshatenga maeneo mengine kule Kasubuya, Mheshimiwa Mbunge Kamata unajua ulikwishakuja tukazungumza sana tumewatengea hekta 432; kule Kasubuya. Lakini kule Matabe tumewatengea hekta 568; kule Chato kule kwangu kule tumewatengea hekta 1258; lakini pia bado tunawatengea maeneo mengine hekta 232 maeneo ya Geita.

Kwa hiyo, nimuomba sana Mheshimiwa Vicky Kamata bado tuko na wewe naomba uje ukae tena tuendeleo kukaa tupange kama ambavyo huwa tunapanga siku zote kwa niaba ya wananchi wa Geita, ahsante.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kusikia pia kauli ya Serikali kuhusu pia wachimbaji wadogo wa Biharamulo wakiwemo wa Busiri, Kalukwete, Mavota, Kalenge na wale Nyanchimba Wilaya Chato kwa sababu nao wanapenda kusikia kauli ya kutengewa hekta kadhaa 500, 600 kama ilivyofanyika kwenye maeneo ya Geita.

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema na nitumie nafasi hii nikushukuru sana rafiki yangu Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo kwa sababu ni jirani yangu, maeneo ya Biharamulo mwaka jana tumetenga hekta 1332 kwa Mheshimiwa Oscar, lakini Mheshimiwa Oscar bado tunakutengea eneo pale kwenye Mgodini wa Tulawaka, pale Mavota tunafanya mazungumzo. Tumeshakaa na wewe na Mbunge wa Bukombe tumeainisha mahektari kama hekta 2100 tuzitenge kwa ajili ya wananchi wako, lakini bado nikushukuru sana kwa sababu umependa pia nizungumzie kwangu kule Chato. Kule Chato Kampuni ya Wakawaka

imeachia eneo takribani ya hekta mbili ambako wananchi wako wa Biharamulo na wangu tutawagawia kwa utaratibu huo huo.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Jimbo la Handeni Vijiji kwenye Kata ya Kang'ata eneo la Magambazi, kuna mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji lakini kwa sasa mgogoro huo unasubiri maamuzi kutoka kwenye Wizara ya Nishati na Madini. Lakini wakati huo huo mgogoro huo umeweza kusimamisha shughuli nyingi ambazo kwa namna moja ama nyingine zingeweza kunufaisha wananchi wa Kata ya Kang'ata na eneo la Magambazi. Je, ni lini Wizara itatoa maamuzi juu ya utatuzi wa mgogoro huu ili shughuli ziweze kuendelea? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maeneo ya Handeni pamoja na maeneo mengi ya Kilindi kuna migogoro mingi sana kati ya wachimbaji wadogo, wananchi pamoja na wawekezaji kutoka nje. Lakini kwa jitihada ambazo tumechukua hasa kwa maeneo ya Handeni wiki iliyopita tulimtuma mkaguzi wa migodi kwenda kukagua migogoro iliyopo kati ya wananchi wa Magambazi pamoja na wawekezaji wanaochimba pale. Hivi sasa kampuni ambayo ilikuwa inachimba pale Kampuni ya Scanda ambayo pia ilifanya utafiti haijakamilisha kazi zake. Lakini nimhakikishie tu timu yetu ipo pale sasa na tukitoka hapa Mheshimiwa wa Handeni tukae tukubaliane tufuatilie timu imefikia hatua gani lakini tumeipa muda wa wiki mbili na wiki ijayo wataleta taarifa na taarifa hiyo tunahakikisha kwamba itatoa suluhisho na mgogoro wa wananchi wa Handeni pamoja na wachimbaji hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Bashe, swali fupi.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naomba kumuuliza swali fupi Mheshimiwa Waziri pamoja na jitihada alizozifanya katika Mgodi wa Resolute, Nzega. Je, sasa Serikali iko tayari leseni iliyokuwa chini ya MRI iweze kugawia kwa wachimbaji wadogo wa Mwaishina ambayo maarufu kwa namba saba *original* katika mji wa Nzega?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lililokuwa likimilikiwa na kampuni maarufu sana ya uchimbaji iliyoanza hapa nchini Resolute lilimilikiwa sasa na Serikali kupitia Chuo chetu cha Madini (MRI). Ni kweli kabisa lengo kubwa la mgodi kumilikisha kwa Serikali ili ku-*plan* kutoa fursa kwa wanafunzi wa Tanzania ambao wanasoma masomo kwa nadharia waweze sasa kupata eneo kwa kufanya kwa vitendo ndiyo maana tunawagawia eneo lile. Lakini nikubaliane na hoja ya Mheshimiwa Bashe tumeshazungumza naye, tumeshaweka mikakati ili tuone ni eneo gani ambalo Serikali kupitia MRI hawalihitaji ili waweze kugawia wananchi wa Nzega lakini

hata hivyo tumechukua hatua mbadala zaidi ya hapo. Mheshimiwa Bashe nikuhakikishie Kampuni ya *Zari Exploration* imeachia kilometa nyingine kumi karibu na eneo hilo ambao wananchi wako wa Nzega tutawagawia kwa utaratibu wa Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, ninayo matangazo machache tutaanza na tangazo la wageni waliotufikia siku ya leo. Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge na wapo wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo.

Tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, ambao ni watu wenye ualbino kutoka Shirika la *Save Vulnerable Foundation*. Mheshimiwa Waziri siwaoni lakini wageni mkitajwa mnasimama ili tujue mpo humu ndani, wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama. (Makofi)

Wageni watano wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni viongozi wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka sehemu zote Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa *Union* ya Kaskazini mwa Tanzania yaani *NTUC* Mchungaji Godwin Lekundayo na wenyewe hawapo.

Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani Naibu Waziri wa Nishati na Madini wanaotokea Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Mwishitinywa Swai, karibuni sana. (Makofi)

Wageni 17 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao ni wachungaji wa madhehebu mbalimbali kutoka kijiji cha Pwaga, Jimbo la Kibwake wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mchungaji Madondora, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni 56 wa Mheshimiwa Joyce Mukya, ambao ni wanafunzi 49 na walimu saba wa shule ya *St. Thomas School* kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Ndugu Wilson Lazaro, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Maria Kangoye ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na wajasiriamali kutoka mjini Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Ester Mahawe ambao ni wanafamilia na wanafunzi *Intel Schools* iliyoko Mkoani Arusha wakiongozwa na Ndugu Alexander Samson ambae ni mume wake. Yupo pia Ndugu Lulu

Alexander ambaye ni mtoto wake na Ndugu Kababa Loi ambaye ni Meneja wa *Intel Schools*, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaye ni watoto wake Ndugu Seif Yahaya Mhata na Ndugu Nasra Yahya Mhata, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni kumi wa Mheshimiwa Rose Kamil ambao ni wafanyakazi wa *BQ Contractors* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Ladslaus Sule, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni tisa wa Wabunge Wanawake wakiongozwa na Ndugu Lilian Liundi, Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Kijinsia Tanzania, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo tunaanza na kundi la kwanza ni wanafunzi 58 na walimu 12 kutoka Shule Msingi *Holy Trinity* - Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Wapo pia wageni 72 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambao ni walimu wanafunzi wa darasa la saba, Shule ya Msingi Montessori kutoka Ilemela Mkoani Mwanza, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni 61 wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambao ni wanafunzi wa hitimu wa Chuo cha Mipango kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Venelanda Njau, karibuni sana hao ndiyo wageni waliotufikia asubuhi hii. (Makofi)

Lakini tunalo tangazo lingine hapa na hili linatoka Ofisi ya Bunge, Wabunge wote wanawake mnatangaziwa kuwa leo tarehe 10 Juni, kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote itakayofanyika katika ukumbi mkubwa wa Msekwa kuanzia saa saba mchana mnaombwa wote kuhudhuria semina hiyo. Tumemaliza matangazo tunaendelea Katibu.

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Miswada ya Sheria ya Serikali, Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuweka kutoza na kubadili baadhi ya kodi, tozo, ada na ushuru na kufanya mabadiliko ya sheria mbalimbali zinazohusu ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya umma yaani (*A bill for an Act to impose and alter certain taxes, duties, levy's and fees and to amend certain written laws, letting to the collection and management of public revenues*).

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Muswada umesomwa kwa mara ya kwanza sasa ninatangaza kuwa Muswada huo upelekwe kwenye Kamati husika ili uweze kufanyiwa kazi. Katibu.

### HOJA ZA SERIKALI

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Hoja ya Waziri wa Fedha na Mipango kwamba Bunge likubali kujadili hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kwamba Bunge sasa likubali kupitisha mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. (Makofi)

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni 105(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016; naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kufanya tathmini katika maeneo mbalimbali yanayohusu masuala ya sera ya fedha na kodi kwa madhumuni ya kutoa maoni na mapendekezo kuhusu sura halisi na mwelekeo wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017. Pamoja na Serikali kuendelea kutambua umuhimu wa Bunge katika mchakato wa Bajeti, bado Kamati imebaini kuwa Serikali haijaonesha utayari wa kupokea ushauri hususan eneo la ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo vipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kuwa hii ni changamoto kubwa inayosababisha kutokuwepo kwa mabadiliko katika eneo muhimu la upanuzi wa wigo wa vyanzo vya mapato. Hata hivyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Bajeti itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishatoa kwa kina maelezo juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka wa 2015. Taswira ya Hali ya Uchumi wa nchi inaonyesha kuwa ukuaji wa Uchumi Jumla kupitia Pato la Taifa umeongezeka kwa asilimia saba, sawa na kiwango cha ukuaji wa uchumi mwaka 2014. Mfumko wa bei umeendelea kubaki katika kiwango cha tarakimu moja hadi mwezi Aprili, 2016 umepungua hadi kufikia asilimia 5.1 ikilinganishwa



na asilimia 6.1 ya mwaka 2014; Thamani ya shilingi imeendelea kushuka dhidi ya dola za Kimarekani ambapo hadi kufikia Disemba, 2015 dola moja ya Kimarekani imebadilishwa kwa kiwango kati ya shilingi 2,150 na 2,180.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha, Deni la Taifa limeendelea kukua kutoka shilingi trilioni 42.3 mwezi Juni, 2015 hadi trilioni 45.6 mwezi Machi, 2016 hili ni ongezeko la asilimia 6.34. Hadi kufikia mwezi Februari 2016, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ilipungua kwa asilimia 39.8 na kufikia nakisi ya dola za Kimarekani milioni 2,809.9, kutoka nakisi ya dola za Kimarekani milioni 4,668.5 kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mwenendo huu mzuri wa ukuaji wa uchumi unaochangiwa na sekta ya mawasiliano kwa asilimia 15, utawala wa umma asilimia 12.6, ujenzi asilimia 10.5, sekta ya fedha asilimia 10.4 na uchukuzi asilimia 9.5, bado kuna changamoto kubwa inayojitokeza ya namna mafanikio haya ya uchumi jumla yanapunguzaje viwango vya umaskini kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba sekta hizi ambazo zimeonesha kukua kwa kiwango kikubwa zinagusa idadi ndogo ya watu katika Taifa ukilinganisha na sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji ambayo inachukua zaidi ya asilimia 75 ya wananchi ambazo zinaajiri pia wananchi wengi. Hali hii inaashiria kuwa bado Serikali ina changamoto kubwa ya kuendeleza sekta hizi kupitia hatua za makusudi za kuongeza rasilimali na vivutio ili kuendeleza maeneo haya na kupunguza umaskini wa watu hasa wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2015/2016 ulikuwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011-2012 hadi 2015-2016) uliokuwa umebeba dhana ya kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii. Aidha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016 uligawanyika katika maeneo ya Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa na Miradi ya Kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2015/2016 tulizielezea kwa ukamilifu wakati wa tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Kwanza wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa kipaumbele kwenye miradi iliyopo kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017 ambao umegawanyika katika makundi manne ambayo ni:-

(i) Kukuza uchumi kupitia uchumi wa viwanda;

- (ii) Kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu;
- (iii) Kuweka mazingira wezeshi ya uendeshaji biashara na uwekezaji; na
- (iv) Usimamizi na utekelezaji wa mpango husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote inayotaka kupiga hatua za haraka kiuchumi ni sharti iwekeze vya kutosha katika viwanda. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua hilo na kuja na mikakati thabiti itakayowezesha nchi yetu kufanya mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imepanga kutekeleza miradi ya Magadi Soda katika bonde la Engaruka, Chuma – Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma, kufufua kiwanda cha *General Tyre*, kuendeleza mradi wa kiwanda cha viwadudu pamoja na uendelezaji wa viwanda vidogo - *SIDO*. Kamati inaishauri Serikali ikamilishe miradi ya maendeleo yake inayohusu ujenzi wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo ambayo kwa muda mrefu imekuwa katika mikakati tu bila ya kutekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wajasiriamali nchini wana mitaji midogo, viwanda vidogo ndiyo suluhisho pekee la kuwafanya washiriki kikamilifu katika mageuzi ya viwanda. Viwanda vidogo vitakavyoanzishwa na wajasiriamali wetu siyo tu vitaliingizia Taifa mapato kupitia kodi na tozo mbalimbali bali vitaongeza ajira, vitatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini pamoja na kuwepo na uhakika wa upatiakanaji wa bidhaa na huduma hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) pamoja na Benki ya Rasilimali (*TID*) zianagalie uwezekano wa kufungua dirisha maalum kwa ajili ya kutoa mikopo ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba bila ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza mpango wa mapinduzi ya viwanda, nchi yetu itachukua muda mrefu kufikia malengo iliyojiwekea. Duniani kote sekta binafsi ndiyo msingi mkuu wa ujenzi wa uchumi imara wa nchi husika. Jukumu la msingi la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kufanya kazi yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikaja na mikakati madhubuti ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.



Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja Serikali imeainisha miradi saba ya kielelezo itakayohitaji mitaji mikubwa ya uwekezaji. Miradi hiyo ni ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, ununuzi na ukarabati wa meli kwenye maziwa makuu, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania, ujenzi wa barabara ya Kidahwe - Nyakanazi; Mtwara - Newala – Masasi - Mbinga-Mbamba Bay pamoja na pamoja na mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na Mradi wa Liganga.

Kamati inaamini kwamba miradi hii ikitekelezwa kikamilifu itakuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi na itakuwa chachu ya ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama vile usafirishaji, kilimo, nishati, viwanda na utalii. Kamati inaitaka Serikali katika bajeti ya kila mwaka kuainisha miradi itakayotekelezwa kwa mfumo wa PPP na gharama za mradi husika ili Bunge liweze kujua na kufuatilia utekelezaji wa miradi husika. Aidha, Serikali ihakikishe inatoa fedha za kutosha kwa miradi yote iliyopanga kutekeleza kwa kutumia fedha za ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo haukuwa wa kuridhisha. Kwani hadi kufikia Februari, 2016 ni kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kilichotolewa kwa mafungu mbalimbali kilikuwa ni asilimia sita tu. Kamati inaona kuwa umefika wakati muafaka Serikali kuhakikisha kwamba inahusisha sekta binafsi kugharamia miradi kwa njia ya shirikishi yaani PPP hasa miradi ile yenye mtizamo ya kibiashara na kutumia fedha zake za ndani ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipokea hoja kuu tano zenye maslahi ya Taifa kutoka kwako ili ikutane na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa hoja hizo. Kamati ilifanya mashauriano na kukubaliana na Serikali kuhusu hoja mbili ambazo ni Mfuko wa Hifadhi wa Mazingira na Mfumo wa Upelekaji wa Shilingi Milioni 50 katika kijiji kati ya hoja tano ilizozipokea. Matokeo ya mashauriano yaliyofikiwa mpaka sasa kati ya kamati na Wizara ya Fedha ni kama inavyoonekana katika jedwali katika bajeti yangu. Hoja tatu Serikali iliomba iendelee kuzifanyia kazi ili iweze kufikiwa muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hoja hizi tano, Wenyevitani wa Kamati wa Kisekta kwa nyakati tofauti waliwasilisha hoja mbalimbali ambazo kupitia Kamati zao waliona zina umuhimu kwa maslahi ya Taifa. Hata hivyo baadhi ya hoja hizo zilipatiwa ufumbuzi wakati wa majadiliano na nyingine wangependa Serikali izitambue na kuzichukua ili kuzifanyia kazi kwa kadri hali itakavyoruhusu. Kamati ya Bajeti ingependa Bunge lako tukufu izitambue hoja hizi na kuishauri Serikali namna itakavyohakikisha inazitatusa ili kuleta tija kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hizo ni pamoja na ufufuaji wa Kiwanda cha *General Tyre*, Kiwanda cha Kushona Sare na Upatikanaji wa Chakula cha Mahabusu na Wafungwa kutoka Magereza na JKT, kuongeza fedha kwa ajili ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kuongeza fedha za utafiti katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, upatikanaji wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uhamiaji na pia hoja ya kuziongezea fedha Taasisi ya Moyo ya JK na Saratani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hoja hizi chache, bado kuna hoja mbalimbali ziliwasilishwa ambazo zilizohusu upungufu wa fedha kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, malipo ya fidia kwa miradi ya EPZ na malimbikizo ya madeni ya watumishi, malimbikizo ya madeni ya MSD pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo ya balozi zetu. Kamati ya Bajeti inatambua changamoto iliyonayo Serikali katika utekelezaji wa malengo yake ya kibajeti, hata hivyo ni muhimu ikachukua hoja hizi na kuzipangia utaratibu wa utekelezaji wake na kulifahamisha Bunge hapo baadae.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti kwa nyakati tofauti pia ilishauriana na Serikali na kufanikiwa kuongeza fedha kwa baadhi ya mafungu ili kuwezesha kutekeleza bajeti ya mwaka 2015/2016 kama yalivyoidhinishiwa katika jedwali hapo chini. Wizara Fedha iliweza kuongeza katika mafungu mbalimbali ambayo yameoneshwa katika bajeti yetu; nisingesoma kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016 ni kama inavyoonekana katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kuona hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuongeza mapato ya kodi. Sura hii inatupa hali halisi ya utekelezaji wa sera ya kodi kwenye maeneo husika hasa yanayohusu mapato ya ndani, mapato ya Halmashauri, mikopo na misaada toka nje na mikopo ya ndani. Uchambuzi unaonyesha kuwa katika baadhi ya maeneo ya mapato na matumizi kumekuwepo ongezeko na katika baadhi ya maeneo kumekuwa na punguzo kwa asilimia kadhaa kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura ya Bajeti ya mwaka 2016/2017 inaonyesha kuwa kutakuwepo na ongezeko kiasi cha shilingi trilioni saba sawa na asilimia 31 ya jumla ya bajeti yote. Serikali kupitia hotuba yake ya bajeti imeainisha maeneo mbalimbali ambayo yatasaidia kupata ongezeko hili la fedha ili iweze kutekeleza malengo yake ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Changamoto iliyopo ni namna gani Serikali itahakikisha kuwa fedha hizi zinapatikana kwani uzoefu unaonyesha mpaka sasa mafungu mengi

hayajaweza kupata fedha yaliyoidhinishiwa na Bunge kwenye Bajeti ya mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeweza kuona tofauti kadhaa kati ya Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 na hii ya sasa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 29.5 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 31 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22.5 zilizotengwa mwaka 2015/2016. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 17.7 sawa na asilimia 60 ya Bajeti yote zitatumika katika matumizi ya kawaida. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia saba la matumizi ya kawaida ukilinganisha na bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/2016, inaonyesha kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali itaongeza mapato ya ndani kwa asilimia 32, mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa yataongezeka kwa asilimia 28, misaada na mikopo toka nje itaongezeka kwa asilimia 35, mikopo ya ndani itaongezeka kwa asilimia 33; matumizi ya kawaida kwa asilimia saba na matumizi ya maendeleo yataongezeka kwa asilimia 100 sawa na jedwali hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sura hii ya Bajeti, Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa kupunguza matumizi ya kawaida na kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa zaidi ya asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Bajeti imeainisha hatua mbalimbali zitakazochukukuliwa na Serikali katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yatakayofikiwa jumla ya shilingi trilioni 29.5 kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla ongezeko hili kubwa la mapato kutoka vyanzo vya ndani linategemea kupatikana kutokana na usimamizi thabiti wa Serikali kwa upande wa sheria na taratibu za ukusanyaji wa mapato pamoja na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vilivyopo na vile vipya ambavyo Serikali imevianisha katika hotuba yake. Hata hivyo, sura ya Bajeti bado haijaanza kuonesha kiasi cha fedha kitakachopata kutokana na Mfuko wa Mapato ya Gesi na Mafuta kutokana na ugunduzi wa kiwango kikubwa cha gesi ambacho kimepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri utaratibu huu uanze kutumika kwa siku zijazo ili kutoa picha halisi ya mapato ya gesi na iwe chachu ya kuleta maendeleo ya nchi kwa kusimamia matumizi bora ya mapato ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi trilioni 11.8 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi shilingi trilioni 8.7 ni fedha za ndani na shilingi

trilioni 3.11 ni fedha za nje ikilinganishwa na mwaka 2015/2016. Serikali imeamua kutenga asilimia 40 ya bajeti yote kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefuatilia ugawaji wa fedha za maendeleo kwa sekta mbalimbali na kuona kuwa sekta zilizopewa kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni uchukuzi shilingi trilioni 2.4, ujenzi shilingi trilioni 2.1, maji shilingi bilioni 917, elimu shilingi bilioni 897, afya shilingi bilioni 527 na viwanda shilingi bilioni 40. Aidha, bado sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na huduma hazipewi kipaumbele na zimetengewa fedha kidogo ukilinganisha na mahitaji husika kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti inapongeza hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato yatokanayo na ajira kutoka asilimia 11 hadi asilimia tisa. Pamoja na hatua hii ukifuatilia jedwali la viwango vya sasa ukurasa 60 na 61 viwango vinavyopendekezwa si rafiki kwa mtumishi wa umma na hatua ya kupunguza shilingi 3,000 kila ngazi na wakati asilimia ya makato inabaki palepale haina unafuu wowote kwa mtumishi umma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi Bunge limekuwa mstari wa mbele katika kujadili na kupendekeza watumishi wa umma kusamehewa kodi kwenye malipo ya viinua mgongo wanavyolipwa. Bunge limekuwa likishauri uzingatiaji kuwa mishahara ya watumishi wa umma na hata viongozi wa siasa imekuwa ikikatwa kodi, hatua hii inayopendekezwa na Serikali inakuwa ni *double taxation*. Ni muhimu Serikali ikafikiria suala hili upya kurekebisha kodi hii, kama ikishindikana basi ijumuishe viongozi wote wa kisiasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda ieleweke na wananchi kwamba Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote wa kisiasa wanalipa kodi kupitia mishahara yao kila mwezi. Hivyo kukata kodi katika kiinua mgongo ni kuwakata kodi mara mbili. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali suala hili iendelee kulifikiria zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya bajeti ya Serikali ukurasa wa 66 hadi ukurasa wa 80 umeainisha marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa forodha yaliyofanywa na nchi wanachama kwa makubaliano ya kuendeleza uchumi wa viwanda kwenye ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kamati ya Bajeti imefanya tathmini ya huduma na bidhaa zinazosamehewa kodi na kugundua kuwa hatua hiyo hainufaishi sana viwanda vilivyopo ndani ya nchi. Kwa nyakati tofauti, Kamati ya Bajeti ilimtaka Waziri wa Fedha na Mipango afike kwenye mashauriano kuhusu yale anayotegemea kuyawasilisha kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo Kamati iweze

kumshauri ipasavyo. Suala hili limekuwa gumu kufanyika, hivyo Kamati inashuri Serikali kuwa na sheria inayomtaka Waziri wa Fedha kushauriana na Kamati ya Bajeti kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya hatua za kodi zitakazojadiliwa na wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza tozo ya kuendeleza ufundi stadi yaani *Skills Development Levy* kutoka kiwango cha sasa cha asilimia tano hadi asilimia 4.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Bajeti katika mchakato mzima wa ushiriki wa Kamati ya Bajeti kuanzia uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, ufuatiliaji pamoja na tathmini. Kamati ya Bajeti kama mshauri mkuu katika masuala ya kibajeti kupitia sheria ya bajeti imepewa jukumu la kuhakikisha Serikali na taasisi zake zinafuata mfumo bora wa kiutendaji katika mchakato wa bajeti. Kuwepo na nidhamu ya bajeti, kuweka msingi wa kuzingatia mipango, mapato na matumizi na kuwepo na bajeti inayoaminika yenye kuzingatia utekelezaji kama ilivyoidhinishwa na Bunge pamoja na kuweka masharti ya uhamishaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016 haijatoa ufafanuzi wa kutosha kuhusu utaratibu wa kujadili hoja zitakazokuwa zimejitokeza Bungeni wakati wa mijadala ya Bajeti ya Wizara mbalimbali. Ni jukumu la kiti kuamua ni hoja zipi ziende kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya mashauriano au ni Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati za Kisekta kuangalia hoja gani zimezua mjadala wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti za Wizara husika.

Aidha, Kanuni bado ipo kimya kuhusu utaratibu wa kufuatwa ikiwa Kamati ya Bajeti na Serikali hazijafikia makubaliano baada ya mashauriano. Kamati inashauri mapungufu haya yafanyiwe kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kuwa shughuli za utafutaji wa gesi na mafuta bado zinaendelea nchini. Wananchi wana mategemeo makubwa kwamba mapato yatoakanayo na gesi yatakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi. Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi iliandaliwa mwana 2015 ili kutoa mwongozo wa kuanzisha mfumo maalum wa usimamizi wa mapato na matumizi hayo pamoja na kuainisha vyanzo vya mapato maalumu ya mafuta na gesi. Hata hivyo, tofauti na ilivyokuwa mwaka 2015/2016; katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017 haijaweza kuonyesha makadirio ya mapato yatakayoweza kupatikana kutoka na vyanzo mbalimbali vya mafuta na gesi kama ilivyocainishwa katika bajeti ukurasa wa 141 hadi ukurasa wa 142.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa wakati wa majumuisho ya hoja mbalimbali zenye maslahi ya Taifa zilizowasilishwa na Kamati za Kisekta, Kamati ya Bajeti na Serikali hazikuweza kufikia makubaliano ya kuongeza tozo kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli ili kupata kiasi cha shilingi Bilioni 250, ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 30 zingechukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya nchi nzima na kinachobaki kingepelekwa kwenye Mfuko wa Usambazaji Maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliomba suala hili iachiwa ilifanyie kazi, tunaiomba Serikali bado iendelee kulifanyia kazi kwa sababu viwango hivi wakati vinawekwa bei ya mafuta ilikuwa ni shilingi 2,100 na 2,400. Punguzo la mafuta kutoka shilingi 2,400 mpaka tulipo sasa halikuonekana katika manufaa ya wananchi. Hakuna nauli ya basi iliyopungua wala huduma yoyote inayohusiana na mafuta. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kutumia fursa zinazojitokeza za mabadiliko ya bei yanayotokea duniani katika kuendeleza Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuhakikisha kwamba Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinatumia vifaa na mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato. Ni dhahiri kuwa bado eneo la ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi ulikuwa haufanyi vizuri hasa katika maeneo ya ada, mrahaba na tozo zinazotozwa na Wizara, Idara na za Taasisi mbalimbali. Hatua hii itaongeza upatikanaji wa mapato ya ndani na hivyo kusaidia Serikali kuweza kugharamia bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 haikufafanua ipasavyo ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa njia ya ubia. Serikali imejitahidi kuainisha miradi michache itakayotekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na mwenendo huu hasa ikizangitwa kuwa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ingeweza kuchochea maendeleo ya nchi ikiwemo miradi ya reli, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika kutegemea fedha za Serikali peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kamati inaendelea kusesitiza kuwa Serikali ilete orodha ya miradi yote ambayo imefanywa upembuzi yakinifu na ile ambayo haijafanywa ambayo Serikali ina nia ya kuitekeleza kwa ubia na sekta binafsi. Kufanikiwa kwa utekelezaji wa miradi hiyo kutapunguza mzigo wa bajeti ya Serikali wa maendeleo na kodi kwa Watanzania na kukuza sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yote iingie kwenye *Hansard* kama ambavyo tumeiomba.



Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa nimalizie kwa kuomba Serikali kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi ili kukuza uwekezaji na Kamati inapendekeza kuwa Serikali ichukue hatua zifuatazo:-

Kwanza, kuunganisha vyombo vinavyofanya kazi zinazofanana, kwa mfano *TBS*, *TFDA*, *TAEC* na *WMA*. Pia kuunganisha vyombo vya udhibiti kwa pamoja ili kupunguza vyombo hivi kwenda kwa wawekezaji mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunapendekeza kuunganisha taasisi na mamlaka zote zinazohusiana na masuala ya uwekezaji kama vile *TIC*, *EPZA* na *BRELA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa hatua yake ya kutenga shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kuanzisha mahakama inayoshughulikia masuala ya rushwa na uhujumu uchumi pamoja na kutenga shilingi bilioni 72.3 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za *TAKUKURU*. Hatua hii itasaidia vyombo hivi kufanya kazi vizuri kulingana na majukumu ukizingatia kuwa vinategemeana katika majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili Kamati inaona kuwa utekelezaji wa majukumu ya vyombo hivi unategemea sana upatikanaji wa taarifa za Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ipo haja ya Serikali kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ili kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Mahakama ya Uhujumu Uchumi na *TAKUKURU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kutenga kiasi cha shilingi trilioni mbili nukta nne tisa kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu za abiria. Hata hivyo, utaratibu sasa hivi duniani kote hakuna mahali ambapo ndege zinakwenda kununuliwa kwa kulipa pesa zote taslimu. Utaratibu ulipo ni kwamba unalipa malipo ya awali halafu kinachobaki kinalipwa kidogo kidogo hata ndani ya zaidi ya miaka 15. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali, inaweza kutenga hata shilingi bilioni 200 ikalipa kwa ndege zote tatu na pesa nyingine zikapelekwa katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine ambayo tumeyasisitiza katika bajeti yetu ni suala zima la ugatuaji wa madaraka ili kuzifanya Serikali za Mitaa ziweze kufanya kazi zake kwa umakini. Kwa hiyo, katika kupunguza kodi na ushuru tuangalie pia kuziachia Mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kuweza kujiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kupiga marufuku utengenezaji, uingizwaji, uuzaji na ununuzi wa matumizi ya mifuko ya *plastic* yenye vipimo vya unene wa chini ya *microns* 50. Kamati



inaitaka Serikali kupiga marufuku uuzaji wa pombe inayowekwa kwenye mifuko ya *plastic*, maarufu kama viroba. Pombe hiyo inaweza kuendelea kuzalishwa kwa kuwekwa katika vifungashio vya chupa badala ya ilivyo kwenye viroba sasa hivi ambapo watoto hata wa darasa la kwanza wanaweza kuji-serve na hivyo kupunguza na hivyo kupunguza maadili yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ambao wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Nakupongeza wewe mwenyewe kwa umahili wako wa kuliongoza Bunge hili na ujasiri wako pamoja na figisufigisu zinazojitokeza; hizo ni changamoto tu naomba uendelee kukaza uzi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtwara Vijijini pamoja na wazazi wangu na familia yangu akiwemo mume wangu Bwana Yahya Ali Mhata pamoja na watoto wangu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu na Makatibu Wakuu, Makamishna wa Bajeti na wataalam wao wote kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni kutoka katika Kamati na bado tunawaomba waendeleo kushirikiana na Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2015 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2016/17, PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2015/16 NA MAPENDEKEZO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni 105 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/17 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kufanya tathmini katika maeneo mbalimbali yanayohusu masuala ya sera ya fedha na kodi kwa dhumuni la kutoa maoni na mapendekezo kuhusu sura halisi na mwelekeo wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/17.

Pamoja na Serikali kuendelea kutambua umuhimu wa Bunge katika mchakato wa Bajeti, bado Kamati imebaini kuwa Serikali haijaonesha utayari wa kupokea ushauri hususan eneo la ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo vipya. Kamati inaona kuwa hii ni changamoto kubwa inayosababisha kutokuwepo kwa mabadiliko katika eneo muhimu la upanuzi wa wigo wa vyanzo vya mapato. Hata hivyo napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ya bajeti itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 na Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya kamati imegawanyika katika Sehemu Kuu Tano. Sehemu ya kwanza inahusu hali ya uchumi; sehemu ya pili inahusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2015/16 na mapendekezo ya mpango huo kwa mwaka fedha 2016/17; sehemu ya tatu inahusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/16; sehemu ya nne ni Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17 na sehemu ya mwisho ni maoni na mapendekezo ya kamati ya bajeti

## 2.0. HALI YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekwishatoa kwa kina maelezo juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka wa 2015. Taswira ya Hali ya Uchumi wa nchi inaonyesha kuwa ukuaji wa Uchumi Jumla kupitia Pato la Taifa umeongezeka kwa asilimia 7.0, sawa na kiwango cha ukuaji cha Mwaka 2014, mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika kiwango cha tarakimu moja hadi Mwezi aprili 2016 umepungua hadi kufikia asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 6.1 kwa mwaka 2014; Thamani ya shilingi imeendelea kushuka dhidi ya Dola za Kimarekani ambapo hadi kufikia Desemba, 2015 Dola moja ya Kimarekani ilibadilishwa kwa kiwango kati ya shilingi 2,150 na 2,180. Aidha, Deni la Taifa limeendelea kukua kutoka shilingi trilioni 42.3 (Mwezi Juni 2015) hadi trilioni 45.6 (Mwezi Machi, 2016) hili ni ongezeko la asilimia 6.34. Hadi kufikia mwezi Februari 2016, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*) ilipungua kwa asilimia 39.8 na kufikia nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 2,809.9, kutoka nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 4,668.5 kwa mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mwenendo huu mzuri wa ukuaji wa uchumi unaochangiwa na sekta ya mawasiliano (asilimia 15), utawala wa umma (asilimia 12.6), ujenzi (asilimia 10.5), sekta ya fedha (asilimia 10.4), na sekta ya uchukuzi (asilimia 9.5), bado kuna changamoto kubwa inayojitokeza namna Mafanikio haya ya Uchumi Jumla yanapunguzaje viwango vya umaskini kwa wananchi waliowengi. Ukweli ni kwamba Sekta hizi hugusa idadi ndogo ya watu katika Taifa, ukilinganisha na sekta ya Kilimo, Uvuvi, Ufugaji (asilimia 75) ambazo zinaajiri wananchi wengi. Hali hii inaashiria kuwa bado Serikali ina changamoto kubwa ya kuendeleza sekta hizi kupitia hatua za makusudi za kuongeza rasilimali

na vivutio ili kuendeleza maeneo haya na kupunguza umaskini wa watu hasa wa kipato

### **3.0. MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA**

#### **3.1. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2015/16**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2015/16 ulikuwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mpango wa maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) uliokuwa umebeba *Dhana ya kufungua fursa fishe za ukuaji Uchumi Tanzania*. Aidha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/16 uligawanyika katika maeneo ya Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN) na Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati.

##### **3.1.1 Miradi ya Matokeo Makubwa sasa (BRN)**

**Mheshimiwa Spika**, mfumo wa matokeo makubwa sasa ulianza kutumika mwaka 2013/14 kwa lengo la kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16).

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwepo kwa mfumo huu, Kamati inaona bado kuna changamoto kubwa katika upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi; upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kipaumbele pamoja na udhaifu wa mfumo ya ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi na matokeo yake. Aidha baadhi ya miradi iliyopata fedha, utekelezaji wake hauendani na thamani ya fedha zilizotolewa (Value for Money)

##### **3.1.2 Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Maendeleo.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati iliyopo katika sekta ya Miundombinu (Reli, Bandari na barabara), Nishati, Viwanda, Maji na Kilimo. Takwimu zinaonyesha kuwa Serikali imeweza kutekeleza vizuri miradi ya maendeleo kwa upande wa miradi ya barabara ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2016, Serikali imeweza kukamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami km 542.6 kati ya km 560.3 sawa na asilimia 96.84 ya lengo. Kwa upande wa sekta ya reli, Serikali imeboresha njia ya Reli ya TAZARA, imekarabati mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo – Mbeya. Hata hivyo, haikuweza kufanya vizuri katika kukarabati njia ya reli ya kati iliyokusudiwa kubadili ratili 80 kwa yadi kwa lengo la kubadilisha Km 2,707 za reli; Hadi sasa imekamilisha kubadili Km 197 tu. Aidha, Serikali iliahidi kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya za Mbegani (Bagamoyo) na Mwambani (Tanga). Vile vile, kuzipa kipaumbele bandari za Mwanza, Kigoma, Kasanga (Rukwa) na

Itungi (Mbeya). Changamoto kubwa imebaki kwa upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam na kuboresha gati namba 1 -7 na ujenzi wa gati namba 13 na 14,

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya Nishati imefanya vizuri hasa katika usambazaji wa umeme vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (Rural Energy Electrification - REA). Hii imewezekana kutokana na Bunge lako tukufu kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa fedha kupitia tozo ya mafuta ya dizeli na petrol (*ring-fenced*) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es salaam (Kinyerezi) na kukamilika kwa usimikaji wa mitambo minne (4) ya kufua umeme yenye uwezo wa kuzalisha MW 150 kumeongeza umeme zaidi kwenye gridi ya Taifa hivyo kuwezesha upatikanaji wa uhakika wa umeme kwa viwanda na wananchi wengi zaidi.. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa miradi ya Nishati kwa vyanzo vya makaa ya mawe (Kiwira, Mchuchuma na Ngaka), umeme kwa njia ya upepo (Singida na Makambako) ili kuwa na umeme wa uhakika utakaoweza kusaidia kujenga uchumi wa viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa maji mijini na vijijini bado haujawa wa kuridhisha. Serikali ilianzisha Mfuko wa Maji kwa lengo la kusambaza maji vijijini hata hivyo bado fedha hizo hazitoshi na hata zinazokusanywa hazipelekwi zote kwenye Mfuko kwa wakati kama ilivyokusudiwa. Aidha, bado kuna changamoto ya kuvuna na kuhifadhi maji yatokanayo na mvua pamoja na uchimbaji wa visima virefu kama Mpango unavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali bado haijaweza kusimamia na kutekeleza vizuri miradi ya kilimo cha miwa, mahindi na Mpunga pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya maji (umwagiliaji) na malisho; uimarisha mashamba ya uzalishaji mitamba pamoja na uimarishaji vituo vya uhamilishaji. Aidha bado kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa maeneo ya kilimo pamoja na utaratibu wa ugawaji wa ruzuku za pembejeo kwa wakulima.

### **3.1.3. Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2015/16**

**Mheshimiwa Spika**, inatarajiwa ifikapo Juni 30, 2016 utekelezaji wa mpango huu unakadiriwa utafikia asilimia 60 tu. Sababu zilizopelekea kutofikiwa kwa lengo la utekelezaji wa mpango huu ni pamoja na ufynywa wa rasilimali fedha kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo; uwezo mdogo katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Taratibu ndefu na gharama kubwa za ununuzi wa umma na ushiriki mdogo wa sekta binafsi kutokana na mazingira yasiyo wezeshi ya kufanya biashara nchini

## **3.2 MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17**

### **3.2.1 Malengo ya Mpango na Miradi ya Kipaumbele 2016 2017**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetoa kipaumbele kwenye miradi iliyopo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 ambao umegawanyika katika makundi manne ambayo ni: Kukuza Uchumi kupitia ujenzi wa uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu; kuweka Mazingira wezeshi kwa Uendeshaji biashara na uwekezaji; pamoja na Usimamizi na utekelezaji wa Mpango husika.

**Mheshimiwa Spika**, Nchi yoyote inayotaka kupiga hatua za haraka kiuchumi ni sharti iwekeze vya kutosha katika viwanda. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua hilo na kuja na mikakati thabiti itakayoweza nchi yetu kufanya mapinduzi ya viwanda.

### **3.2.2 Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda**

**Mheshimiwa Spika** katika Mwaka wa fedha 2016/17 Serikali imepanga kutekeleza miradi ya Magadi Soda katika bonde la Engaruka, Chuma –Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma, kufufua kiwanda cha General tyre, kuendeleza mradi wa kiwanda cha viudadu pamoja na uendelezaji wa viwanda vidogo - SIDO. Kamati inaishauri Serikali ikamilishe miradi ya maendeleo yake inayohusu ujenzi wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo ambayo kwa muda mrefu imekuwa katika mikakati tu bila ya kutekeleza kwa vitendo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa wajasiriamali nchini wana mitaji midogo, viwanda vidogo vidogo ndiyo suluhisho pekee la kuwafanya washiriki kikamilifu katika mageuzi ya viwanda. Viwanda vidogo vitakavyoanzishwa na wajasiriamali wetu siyo tu vitaliingizia taifa mapato kupitia kodi na tozo mbalimbali bali vitaongeza ajira, vitatumia malighafi zinazozalishwa hapa hapa nchini pamoja na kuwepo kwa uhakika wa upatikanaji wa bidhaa na huduma hapa nchini. Jambo la msingi ni kuunganisha mnyororo mzima wa thamani kutoka kwa mzalishaji, mchakataji na mwisho mtumiaji. Hii itawezekana endapo Serikali itaanzisha au kuboresha maeneo ya viwanda vidogo katika kila Wilaya. Aidha, Benki ya maendeleo ya kilimo (TADB) pamoja na benki ya rasilimali nchini (TIB) ziangalie uwezekano wa kufungua dirisha maalum kwa ajili ya kutoa mikopo ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo.

### **3.2.3 Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuboresha elimu na Mafunzo ya ufundi kwa kuimarisha mifumo, majengo na miundombinu mingine katika shule za awali, msingi na sekondari, pia kukarabati, kupanua na kujenga vyuo vikuu, kuboresha Hospitali za rufaa na kuboresha upatikanaji wa maji safi na kuondosha maji taka. Ni dhahiri watu wenye elimu bora na wenye afya nzuri watakuwa na uwezo wa kuzalisha vizuri na kukuza uchumi wa nchi yao. Pamoja na jitihada za Serikali kutoa elimu bure kwa Shule za msingi na

Sekondari bado changamoto kubwa iliyopo ni uwepo wa miundombinu bora ya elimu na waalimu wenye ujuzi wa kutosha ili waweze kutoa elimu bora. Vinginevyo udahili wa wanafunzi utaongezeka kutokana na elimu hiyo kutolewa bure lakini ubora wa elimu utashuka.

### **3.2.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji na ushiriki wa Sekta Binafsi**

**Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli usiopingika kwamba bila ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza mpango wa mapinduzi ya viwanda, nchi yetu itachukua muda mrefu kufikia malengo iliyojiwekea. Duniani kote sekta binafsi ndiyo msingi mkuu wa ujenzi wa uchumi imara wa nchi husika. Jukumu la msingi la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kufanya kazi yake vizuri. Lazima tukubali kwamba nchi yetu haijafanya vizuri sana katika kuweka mazingira bora kwa sekta binafsi kushiriki katika kuinua uchumi. Kulingana na Ripoti ya UNCTAD inayohusu mazingira ya Kufanya Biashara ya mwaka 2015 (*Doing Business Report 2015-UNCTAD*) inaonyesha Tanzania tunashika nafasi ya 139 kati ya nchi 189 duniani na inashika nafasi ya 15 kati ya nchi 47 za kusini mwa Jangwa la Sahara. Ni vema Serikali ikaja na mkakati madhubuti wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

### **3.2.5 Miradi Mikubwa ya Kielelezo (Flagship projects)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja Serikali imeainisha miradi Saba (7) ya kielelezo itakayohitaji mtaji mkubwa wa uwekezaji. Miradi hiyo ni **ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge, ununuzi na ukarabati wa meli kwenye maziwa makuu, kuboresha shirika la ndege Tanzania, ujenzi wa barabara ya Kidahwe-Kanyani; Kasulu-Kibondo – Nyakanazi na barabara ya Masasi –Songea-Mbambabay, pamoja na mradi wa makaa ya mawe wa mchuchuma na mradi wa chuma Liganga**. Kamati inaamini endapo miradi hii itatekelezwa kikamilifu itakuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi na itakuwa chachu ya ukuaji wa sekta nyingine za uchumi kama vile usafirishaji, kilimo, nishati, viwanda na utalii. Kamati inaitaka Serikali kuainisha miradi itakayotekelezwa kwa mfumo wa PPP na muda wa kukamilika kwake pamoja na gharama za mradi husika ili Bunge liweze kujua na kufuatilia utekelezaji wa miradi husika. Aidha, Serikali ihakikishe inatoa fedha za kutosha (100%) kwa miradi yote iliyopanga kutekeleza kwa kutumia fedha za ndani.

### **3.3 Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2015/16 mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo haujawa wa kuridhisha. Mfano mzuri tunauona kuwa hadi kufikia mwezi februari 2016 kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kilichotolewa kwa mafungu mbalimbali kilikuwa chini ya asilimia 60. Aidha, hakuna hata mradi mmoja mkubwa ambao Serikali inaweza kujivunia na kusema umegharamiwa kwa mfumo wa ubia na sekta binafsi (PPP).



**Kamati inaona kuwa imefika wakati Serikali kuhakikisha inahusisha Sekta Binafsi kughramia miradi kwa njia ya shirikishi (PPP) pamoja na kutumia fedha zake za ndani ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi hiyo.**

#### **4.0. MAJUMUISHO YA HOJA ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA MAJADILIANO BUNGENI KUHUSU BAJETI ZA WIZARA MBALIMBALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17**

##### **4.1. Hoja zenye maslahi ya Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipokea Hoja Kuu Tano (5) zenye Maslahi ya Taifa kutoka kwako; Ili ikutane na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa hoja hizo. Kamati ilifanya mashauriano na kukubaliana na Serikali kuhusu hoja mbili (Mfuko wa Hifadhi ya Mazingira na Mradi wa *Village Empowerment*) kati ya Tano ilizozipokea. Matokeo ya mashauriano yaliyofikiwa mpaka sasa kati ya kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha na Mipango yapo kwenye jedwali lifuatalo: -

<b>Na.</b>	<b>FUNGU</b>	<b>HOJA</b>	<b>MATOKEO YA MASHAURIANO</b>
1	<b>FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA</b>	Kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Hifadhi ya Mazingira	<b>Kamati ya Bajeti imeshauriana na kukubaliana na Maelezo ya Serikali kuhusu kutenga kiasi cha shilingi Bilioni 2 kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira. Kamati imepitia Randama Na Kitabu cha Maendeleo kwa Fungu 21; Ofisi ya Rais-Mazingira na kujiridhisha kuwa Kiasi cha shilingi Bilioni 2.1 kimetengwa kwa ajili ya upandaji wa miti.</b>
2	<b>FUNGU 49 – WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI</b>	Kuongeza tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta petrol/diesel na kufika shilingi 100 ili fedha itakayopatikana ipelekwe kwenye Mfuko wa Taifa wa Maji kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji vijijini	<b>Kamati ya Bajeti na Serikali hawajafikia makubaliano.</b>
3	<b>FUNGU 56 ; OFISI YA RAIS - TAMISEMI</b>	Ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya ndani ya miaka 5 (2016 – 2020).	<b>Kamati ilipendekeza kuwa kiasi cha shilingi Bilioni 30 zitolewe kwa ajili ya</b>



			<b>utekelezaji wa Ujenzi wa Zahanati na vituo vya Afya nchi</b>
4	<b>FUNGU 96 ; WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO</b>	Serikali itoe kwa Shirika la Taifa la Utangazaji (TBC) Kiasi cha shilingi bilioni 18 katika Mwaka huu wa Fedha ili uboreshaji wa Mradi wa Upanuzi wa Usikivu uanze mara moja na kuweza kusikia wilaya 81 zilizibakia	<b>Kamati ya Bajeti na Serikali hawajafikia makubaliano.</b>
5	<b>FUNGU 22 - HAZINA</b>	Mradi wa Village Empowerment maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. Mradi huu unalenga "Kutenga Kiasi cha Milioni 50 kila Kijiji kwa ajili ya Kukopesha Vikundi vya Wajasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji husika".	<b>Kamati imeshauriana na kukubaliana na majibu ya Serikali kuhusiana na hoja hii. Kamati inaridhia kiwango cha shilingi bilioni 59.5 (asilimia 47 ya mahitaji kwa mwaka wa Fedha 2016/17) kilichotengwa kwa ajili ya kutumika kama Mpango wa Majaribio (Pilot Program) kwa Wilaya zote ambazo zitakuwa na vikundi na SACCOS. Kamati inasisitiza takwimu za idadi za vijiji na mitaa ziangaliwe vizuri ili kiasi kitakachotolewa kwa kila mwaka iwe 20% ya mahitaji halisi kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango huu.</b>

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hoja hizi Tano, kwa nyakati tofauti Wenyevidi wa kamati za kisekta waliwasilisha hoja mbalimbali ambazo kupitia Kamati zao waliona zina umuhimu kwa Maslahi ya Taifa. Hata hivyo baadhi ya hoja zilipatiwa ufumbuzi wakati wa majadiliano na nyingine wangependa Serikali izitambue na kuzichukua kufanyia kazi kwa kadiri hali itakavyoruhusu. Kamati ya Bajeti ingependa Bunge lako tukufu izitambue hoja hizi na kuishauri Serikali namna itakavyohakikisha kuzitatua ili kuleta tija kwenye maendeleo ya Taifa letu:

- i. *Kiwanda cha General Tyre; fedha zilizotengwa kwa ajili ya kufufua kiwanda hiki hazitoshi (imetengewa Milioni 500 kwa mwaka wa fedha*

2016/17), Serikali ifanye jitihada ya kufufua kiwanda hiki kwa kutumia mifuko ya hifadhi ya jamii;

- ii. Kiwanda cha kushona sare na upatikanaji wa chakula cha mahabusu na wafungwa (magereza na JKT); kila mwaka Serikali imekuwa ikipokea maombi makubwa ya kibajeti kuhusu upatikanaji wa sare kwa majeshi yake pamoja na upatikanaji wa chakula kwa mahabusu na wafungwa. Kamati inashauri Serikali ianze mchakato wa kuvifufua viwanda vya kushona sare vya magereza na JKT ili kupunguza gharama ya kibajeti. Aidha, Serikali isimamie ufufuaji wa mashamba makubwa ya magereza pamoja na kukopesha matrekta na kutenga fedha za kutosha ili magereza waweze kujiendesha kupitia kilimo na hivyo kupata chakula cha ziada kwa ajili ya mahabusu, wafungwa na Ghala la Taifa la Chakula. Serikali ipime maeneo ya Magereza ili iweze kukopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo;
- iii. Kuongeza fedha kwa ajili ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo; suala hili ni muhimu; hata hivyo, Kamati ilikubaliana na Serikali kuanza kufanya tathmini ya utekelezaji wa ruzuku inayotolewa pamoja na marekebisho makubwa ya mfumo mzima wa utoaji wa pembejeo nchini ili kuhakikisha zinawafikia walengwa;
- iv. Kuongeza utafiti katika sekta ya kilimo, mifugo na Uvuvi; Serikali itafute namna ya kuongeza fedha za utafiti kupitia COSTECH ili sekta hizi zifanye utafiti wa kutosha kwa ajili ya maendeleo;
- v. Upatikanaji wa vitendea kazi kwa jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uhamiaji; Serikali ilikwisha pokea mahitaji mbalimbali yaliyowasilishwa yanayohusu majeshi haya ikiwa ni pamoja na yale yanayohusu upatikanaji wa mafuta, vilainishi, dawa na vifaa vya kuzimia moto, oparesheni maalumu na mashine za Viza. Kamati ya Bajeti inaona ni busara Serikali ikayafanyia kazi maombi haya;
- vi. Taasisi ya Moyo (JKCI) na Saratani (Ocean Road Institute); Serikali inatambua hoja za msingi zilizowasilishwa na Kamati za kisekta husika kuhusu mahitaji ya taasisi hizi, Ni vema maombi hayo yakafanyiwa kazi;

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hoja hizi chache, bado kuna hoja mbalimbali ziliwasilishwa ambazo zilizohusu upungufu wa fedha kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, malipo ya fidia kwa miradi ya EPZ, malimbikizo ya madeni ya waalimu, malimbikizo ya madeni ya MSD pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo ya balozi. Kamati ya Bajeti inatambua changamoto iliyonayo Serikali katika utekelezaji wa malengo yake ya kibajeti, hata hivyo ni

muhimu ikachukua hoja hizi na kuzipangia utaratibu (Mkakati) wa utekelezaji wake na kulifahamisha Bunge.

#### 4.2. Mafanikio ya kamati ya Bajeti katika mafungu mbalimbali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti kwa nyakati tofauti ilishauriana na Serikali na kufanikiwa kuongeza fedha kwa baadhi ya mafungu ili yaweze kutekeleza bajeti ya Mwaka 2015/16 kama yalivyoidhinishiwa na Bunge:-

Na	Miradi	Fedha zilizotolewa/ Ahadi ya Serikali
1.	Fedha za Maendeleo Shirika la Utangazaji TBC	Serikali ilitoa fedha za maendeleo za TBC Milioni 800 kati ya Shilingi 1 bilioni zilizoidhinishwa mwaka 2015/16.
2.	Fidia ya Mradi wa Kurasini	Serikali ilitoa Bilioni 3.2 za kulipa fidia kwa ajili ya Mradi wa <i>Kurasini Logistic Hub</i>
3.	Mradi wa Umeme Vijijini (REA)	Serikali ilitoa Shilingi bilioni 80 kati ya shilingi bilioni 161 zilizosalia kupelekwa mradi wa REA
4.	Mfuko wa Maji	Serikali iliahidi kutoa fedha zilizobaki za mfuko wa maji Shilingi bilioni 86. 811
5.	Railway Development Levy (1.5)	Serikali iliahidi kupeleka fedha zilizokusanywa kati ya Desemba mpaka Machi 2016, kwenye mfuko Reli
6.	Fedha za Mfuko wa Mahakama	Serikali imetoa shilingi Bilioni 2.5 kwa ajili ya uanzishwaji wa Mahakama ya Rushwa na Makosa ya Uhujumu uchumi

#### 5.0. MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2015/16

##### 5.1. Mwenendo wa Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Katika Bajeti ya Mwaka 2016/17 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 22.49 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Aprili Serikali ilikuwa imekusanya kutoka vyanzo mbalimbali jumla ya Shilingi trilioni 16.57 sawa na asilimia 73.67 ya mapato yote yaliyokusanywa. Kati ya Fedha hizo Mapato ya ndani ya Kodi, yasio ya Kodi na ya Halmashauri yalikuwa shilingi trilioni 11.48, Misaada na Mikopo ya nje yenye masharti nafuu Shilingi trilioni 1.15 na Mikopo ya ndani yenye masharti ya Kibiashara ilikuwa Shilingi trilioni 3.94.

##### 5.2. Mwenendo wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, Hadi mwezi Aprili, 2016, Serikali ilitoa mgao wa Jumla ya Shilingi 16.86. Kati ya fedha hizo Shilingi trilioni 13.65 ni kwa ajili ya matumizi ya

kawaida na Shilingi trilion 3.21 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kwa ujumla utekelezaji wa Bajeti nzima ya Serikali ni asilimia 74.96 hadi Aprili 2016.

#### 6.0. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17

**Mheshimiwa Spika**, kamati imepitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kuona hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuongeza mapato ya kodi. Hatua hizo ni kuanzisha tozo na kodi mbalimbali, kuongeza au kupunguza viwango vya kodi kwenye maeneo mbalimbali pamoja na kupunguza misamaha ya kodi kwenye baadhi ya maeneo. Hatua hizi za kupata mapato ni za kisheria na hivyo Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi huu ili kupata hali halisi ya mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na kuona kwamba tunatekelezaje malengo ya bajeti tuliojiwekea kwa mwaka huu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Sura hii inatupa hali halisi ya utekelezaji wa sera za kodi kwenye maeneo husika hasa yanayohusu Mapato ya Ndani (Mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi), Mapato ya Halmashauri, Mikopo na Misaada toka nje na Mikopo ya Ndani. Uchambuzi unaonyesha kuwa katika baadhi ya maeneo ya mapato na matumizi kumekuwepo ongezeko na katika baadhi ya maeneo kumekuwepo punguzo kwa asilimia kadhaa inavyoonyeshwa katika jedwali namba 1 hapa chini.

#### Jedwali Namba 1. Ulinganisho wa Sura Ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2015/16 na 2016/17 (Bilioni)

N a		2015/16	2016/17	TOFAUTI	UHALISIA	ASILIMIA
	<b>MAPATO</b>					
1	<b>Mapato ya Ndani</b>	<b>13,475,644</b>	<b>17,798,118</b>	<b>4,322,474</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>32%</b>
	• Mapato ya Kodi	12,362,959	15,105,100	2,742,141	Ongezeko	22%
	• Mapato Yasiyo ya Kodi	1,112,685	2,693,018	1,580,333	Ongezeko	142%
2	<b>Mapato ya Halmashauri</b>	<b>521,879</b>	<b>665,415</b>	<b>143,536</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>28%</b>
3	<b>Mikopo/Misaada kutoka Nje</b>	<b>2, 322, 518</b>	<b>3,600,807</b>	<b>1,278,289</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>55%</b>
	• Mikopo ya Masharti Nafuu	660,337	483,002	177,335	Punguzo	27%
	• Misaada na Mikopo ya	1,463,155	2,745,659	1,282,504	Ongezeko	88%

	Miradi				o	
	• Misaada na Mikopo ya Kisekta	199,026	372,147	173,121	Ongezeko	87%
<b>4</b>	<b>Mikopo ya Ndani</b>	<b>6,175,452</b>	<b>7,475,264</b>	<b>1,299,812</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>33%</b>
	• Mikopo ya masharti ya Kibiashara	2,142,469	2,100,995	41,474	Punguzo	2%
	• Mikopo ya asilimia 1.5 ya GDP	1,432,983	1,597,157	164,174	Ongezeko	11%
	• Mikopo – Rollover	2,600,000	3,777,112	1,177,112	Ongezeko	45%
	<b>MATUMIZI</b>					
<b>5</b>	<b>Matumizi ya Kawaida</b>	<b>16,576,439</b>	<b>17,719,100</b>	<b>1,142,661</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>7%</b>
	<b>o/w ( i) Deni la Taifa</b>	<b>6,396,602</b>	<b>8,000,000</b>	<b>1,603,398</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>25%</b>
	• Malipo ya Riba Ndani	964,893	1,092,162	<b>127,269</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>13%</b>
	• Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover)	2,600,000	3,777,112	<b>1,177,112</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>45%</b>
	• Malipo ya Riba na Mtaji Nje	1,061,361	1,586,640	<b>525,279</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>50%</b>
	• Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	1,085,615	1,141,144	<b>55,529</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>5%</b>
	• Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu	684,733	402,942	<b>281,791</b>	<b>Punguzo</b>	<b>41%</b>
	<b>(ii) Mishahara</b>	<b>6,466,481</b>	<b>6,600,000</b>	<b>133,519</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>2%</b>
	<b>(iii) Matumizi Mengineyo (OC)</b>	<b>3,713,356</b>	<b>3,119,100</b>	<b>- 594,256</b>	<b>Punguzo</b>	<b>16</b>
	• Matumizi yanayolindwa (protected expenditure)	2,775,046	2,492,934	- 282,112	Punguzo	10%
	• Matumizi ya Halmshauri	208,751	266,166	-57,415	Ongezeko	28%

	• Matumizi Mengine ya kuendesha ofisi	729,559	360,000	-369,559	Punguzo	51%
<b>6</b>	<b>Matumizi ya Maendeleo</b>	<b>5,919,053</b>	<b>11,820,503</b>	<b>5,901,450</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>100%</b>
	• Fedha za Ndani	4,256,873	8,702,697	<b>4,445,824</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>104%</b>
	• o /w Matumizi ya Halmashauri	313,128	399,249	<b>86,121</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>28%</b>
	• Fedha za Nje	1,662,181	3,117,805	<b>1,455,624</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>88%</b>
	<b>JUMLA YOTE</b>	<b>22,495,492</b>	<b>29,539,603</b>	<b>7,044,111</b>	<b>Ongezeko</b>	<b>31%</b>

**Mheshimiwa Spika**, Sura ya Bajeti 2016/17 inaonyesha kuwa kutakuwepo na ongezeko la kiasi cha **Shilingi trilioni 7 (sawa na asilimia 31)** ya jumla ya bajeti yote. Serikali kupitia hotuba yake ya bajeti imeainisha maeneo mbalimbali ambayo yatasaidia kupata ongezeko hili la fedha ili iweze kutekeleza malengo yake ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17. Changamoto iliyopo ni namna gani Serikali itahakikisha kuwa fedha hizi zinapatikana kwani uzoefu unaonyesha mpaka sasa mafungu mengi hayajaweza kupata fedha yaliyoidhinishiwa na Bunge kwenye Bajeti ya Mwaka 2015/16. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali umeendelea kuwa chini ya kiwango cha asilimia 85 ya bajeti yote.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeweza kuona tofauti kadhaa kati ya Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16 na hii ya sasa ya mwaka wa fedha 2016/17. Serikali imepanga kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 29.5** kwa mwaka wa fedha 2016/17; kiasi hiki ni sawa na **ongezeko la asilimia 31** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 22.5** zilizotengwa mwaka 2015/16. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 17.7**; sawa na **asilimia 60 ya Bajeti yote** zitatumika katika **Matumizi ya Kawaida**. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 7 la Matumizi ya Kawaida ukilinganisha na shilingi **trilioni 16.7** zilizotengwa mwaka wa fedha 2015/16. Kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, Serikali imepanga kutumia **Shilingi trilioni 11.8**; sawa na asilimia 40 ya Bajeti yote; kiasi hiki ni sawa na **ongezeko la asilimia 100** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 5.9** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya mwaka 2016/17 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/16, inaonesha kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali itaongeza **mapato ya ndani kwa asilimia 32**; mapato ya mamlaka za **Serikali za Mitaa**

yataongezeka kwa asilimia 28; Misaada na mikopo toka nje itaongezeka kwa asilimia 55; mikopo ya ndani itaongezeka kwa asilimia 33; matumizi ya kawaida yataongezeka kwa asilimia 7 na matumizi ya maendeleo yataongezeka kwa asilimia 100. (Angalia jedwali Na.1 na kielelezo Na. 2).

**Mheshimiwa Spika**, kwa Sura hii ya Bajeti, Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa kupunguza matumizi ya kawaida na kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa asilimia 100.

**Kielelezo Na. 2: Ulinganisho wa Mapato ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 na 2016/17.**



**Chanzo:** Wizara ya Fedha

#### 6.1. Sera ya Mapato (kodi, yasiyo ya kodi, halmashauri na mikopo)

**Mheshimiwa Spika**, Hotuba ya Bajeti imeainisha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali katika kuboresha ukusanyaji wa Mapato yatakayofikiwa jumla ya kiasi cha Shilingi trilioni 29.5 (**sawa na ongezeko la asilimia 31 ukilinganisha na ongezeko la asilimia 13.3 kwa mwaka wa fedha 2015/16**). Kwa upande wa mapato ya ndani, Serikali inalenga kukusanya jumla ya kiasi cha **Shilingi trilioni 17.7 (sawa na ongezeko la asilimia 32)**; kati ya hizo Mapato ya kodi (TRA) ni **shilingi trilioni 15.1 (sawa na ongezeko la asilimia 22)**; Mapato yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 2.7 (sawa na ongezeko la asilimia 142)** na Mapato ya Halmashauri **shilingi bilioni 665 (sawa na ongezeko la asilimia 28)**. Aidha, kwa upande wa mikopo ya ndani Serikali inategemea kupata kiasi cha **shilingi trilioni** kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali vya mikopo, hata hivyo



kwa upande wa mikopo yenye masharti ya kibiashara imepungua kwa **asilimia 2** ukilinganisha na kiwango ilichokopa kwa mwaka 2015/16.


**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla ongezeko hili kubwa la mapato kutoka vyanzo vya ndani linategemea kupatikana kutokana na usimamizi dhabiti wa Serikali kwa upande wa sheria na taratibu za ukusanyaji mapato pamoja na kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vilivyopo na vile vipya ambavyo Serikali imevianisha katika hotuba yake. Hata hivyo Sura ya Bajeti bado haijaanza kuonyesha kiasi cha fedha kitakachopata kutokana na Mfuko wa Mapato ya Gesi na Mafuta (Oil and Gas Fund) kutokana na ugunduzi wa kiwango kikubwa cha gesi (futi za ujazo trilioni 55.08). Kamati inashauri utaratibu huu uanze kutumika kwa siku zijazo ili kutoa picha halisi ya mapato ya gesi na iwe chachu ya kuleta maendeleo ya nchi kwa kusimamia matumizi bora ya mapato ya gesi.

**Mheshimiwa Spika**, Sura ya Bajeti inaonyesha kuwa Serikali inategemea kupata misaada na mikopo ya miradi kiasi cha **shilingi trilioni 2.7**; hii ikiwa ni ongezeko la **asilimia 88** ukilinganisha na Bajeti ya mwaka 2015/16. Hata hivyo, mwelekeo unaonyesha Serikali itaendelea kukopa kutoka vyanzo vya ndani kiasi cha **shilingi trilioni 7.4**.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 25.30 ya Bajeti yote ya Serikali**, pia ni ongezeko la **asilimia 33** ikilinganishwa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16. Kamati ya Bajeti inatambua kuwa nia ya Serikali ni kukopa na kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo, hata hivyo ni muhimu kuzingatia athari za mikopo hii katika kukua kwa Deni la Taifa pamoja na kuathiri uwezo wa mabanki kukopesha sekta binafsi na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi kupitia sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya maeneo ambayo Kamati ya Bajeti inatoa angalizo ni kuhusu upatikanaji wa uhakika wa fedha za washirika wa maendeleo (wahisani) ambao kwa siku za hivi karibuni wamekuwa wakipitisha fedha kwa kiasi kikubwa kwa utaratibu wa miradi ya maendeleo (Direct Project Fund) badala ya Misaada ya Kibajeti (General Budget Support). Mfano mzuri tunauona kwa kipindi cha mwaka 2014/15 na 2015/16; Serikali imekuwa ikihangaika kupata fedha toka kwa wahisani kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti yake, je kwa mwaka 2016/17 Serikali imejizatiti vipi katika kuhakikisha wahisani wanatoa fedha walizoahidi; na Je? Serikali imefanya nini kuondoa vikwazo vilivyofanya tusikopesheke mwaka 2014/15 na 2015/16 ili tuweze kukopesheka mwaka 2016/17. Kielelezo namba 3; kinaonyesha picha halisi ya mapato ya Serikali kwa Mwaka 2016/17.

**Kielelezo Namba. 3: ULINGANISHO WA MAPATO YA SERIKALI KWA MWAKA 2015/16 NA 2016/17**  
(Tsh. Milioni)




**Chanzo:** Wizara ya Fedha

## 6.2. Sera ya Matumizi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi trilioni 29.53** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizi kiasi cha **shilingi trilioni 17.72** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (**sawa na asilimia 60 ya bajeti yote**) na **shilingi trilioni 11.82** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (**sawa na asilimia 40 ya bajeti yote**). Kupungua kwa Matumizi ya Kawaida kwa mwaka fedha 2016/17 kunatokana na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuelekeza asilimia 40 ya Bajeti yote kwenye Miradi ya Maendeleo. Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi trilioni 8.70** za makusanyo ya fedha za ndani kwenye Miradi ya Maendeleo; kiasi hiki ni sawa na **ongezeko la asilimia 104** ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2015/16. Aidha kwa upande wa Fedha za Nje, Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi trilioni 3.11** tu kwenye Miradi ya Maendeleo. Hatua hii inaonyesha, kama Serikali itakusanya mapato yake na kusimamia matumizi yake vizuri, basi itakuwa na uhakika wa kukamilisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kutumia fedha za ndani badala ya kutegemea fedha za wahisani/ washirika wa kimaendeleo na hivyo kupunguza utegemezi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonyesha kuwa mapato ya ndani yamezidi matumizi ya kawaida kwa kiasi cha **shilingi bilioni 79.018** (sawa na asilimia 0.267) ya bajeti yote. Hii ina maana kwamba kwa **MARA YA KWANZA** tunategemea kwamba fedha zote tunazokusanya ndani ya nchi zitatoshwa kugharamia matumizi ya kawaida, Hata hivyo, pamoja na hatua hii nzuri ya Serikali ya kugharamia matumizi ya kawaida, bado Deni la Taifa linachukua kiasi kikubwa **cha asilimia 45 (sawa na shilingi trilioni 8)** ya matumizi ya kawaida; mishahara inachukua **asilimia 37.28 (sawa na shilingi trilioni 6.6)** ya matumizi ya kawaida na Matumizi Mengineyo (OC) yanachukua **asilimia 17.56 (sawa na shilingi trilioni 3.11)**. Kwa ujumla **Deni la Taifa na Mishahara** imechukua takribani kiasi cha **shilingi trilioni 14.6** ya bajeti yote ya Matumizi ya Kawaida (**trilioni 17.7**) na kiasi kinachobaki cha **shilingi trilioni 3.1** kinagawanywa kwa kuendeshea Ofisi za Wizara, Halmashauri na matumizi mengine yanayolindwa (*protected expenditure*). Kamati inaona kuwa, Serikali umejielekeza zaidi kulipia Deni la Taifa na mishahara, badala ya kujikita kugharamia Matumizi Mengineyo. Jitihada zaidi zinahitajika kuona namna Serikali itakavyoweza kupata mapato ya kugharamia mafungu mbalimbali kwa matumizi mengineyo (OC) (ambayo yamepunguziwa fedha kwa kiasi cha asilimia 60) ili yaweze kusimamia utekelezaji wa fedha zilizotengwa kwenye Miradi ya Maendeleo ipasavyo.

**Kielelezo Na. 4: ULINGANISHO WA BAJETI ZA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 2015/16 NA 2016/17 (TSh.Milioni)**



**Chanzo:** Wizara ya Fedha

### 6.3. Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17; Serikali imetenga kiasi cha **shilingi trilioni 11.82** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi kiasi cha **shilingi trilioni 8.7** ni fedha za ndani na **shilingi trilioni 3.11** ni fedha za nje. Ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2015/16, fedha za maendeleo zimeongezeka kwa kiasi cha takribani **shilingi trilioni 5.9 (sawa na asilimia 100)**. Serikali imeamua kuelekeza asilimia 40 ya Bajeti yote kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo; ambapo kiasi cha **shilingi trilioni 8.7 (sawa na ongezeko la asilimia 104)** zinategemewa kupatikana kutoka kwenye vyanzo vya ndani na **shilingi trilioni 3.1 (sawa na ongezeko la asilimia 88)** kutoka vyanzo vya nje; ili kugharamia utekelezaji wa miradi husika. Hiki ni kiashiria kwamba Serikali imeamua kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani ili kupunguza utegemezi wa fedha za wahisani/ washirika wa kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya bajeti imefuatilia ugawaji wa fedha za maendeleo kwa sekta mbalimbali na kuona kuwa, sekta zilizopewa kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni Uchukuzi (trilioni 2.4), Ujenzi (trilioni 2.1), Maji (bilioni 915), Elimu (bilioni 897), Afya (bilioni 527) na Viwanda (bilioni 40). Aidha, bado sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na huduma hazipewi kipaumbele na zimetengewa fedha kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya sekta husika kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya bajeti inaona bado kuna changamoto kubwa mbili ambazo Serikali inabidi izitatue ili kuhakikisha inatekeleza vizuri bajeti yake ya miradi ya maendeleo kwa mwaka huu wa fedha:-

**Moja**; Ni kwa namna gani Serikali itaweza kupata fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ukizingatia kuwa mahitaji ya ulipaji wa Deni la Taifa (trilioni 8) na mishahara (trilioni 6.6) yanachukua **takribani ya asilimia 49.5 ya Bajeti yote ya Serikali**;

**Mbili**; ukifuatilia utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa miaka iliyopita utaona kuwa bado kuna upungufu wa utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Serikali Kuu na za Mitaa. Mfano mzuri tunaona katika ripoti ya CAG iliyowasilishwa Bungeni mwezi Aprili, 2016; inaonyesha katika mwaka wa fedha 2014/15 fedha za maendeleo ambazo hazikutolewa kwa ajili ya Serikali Kuu zilifikia kiasi cha **shilingi trilioni 1.4** (sawa na asilimia 32.69) na kwa Serikali za Mitaa zlikuwa kiasi cha **shilingi bilioni 197.2** (sawa na asilimia 26). Hata hivyo, Kati ya fedha zilizotolewa kwa Serikali Kuu, **asilimia 1.29** (sawa na billioni 38.02) hazikutumika na kwa Serikali za Mitaa kiasi cha shilingi **billioni 101.3** hazikutumika (sawa na asilimia 18). Kamati inaona kwamba mwenendo huu wa utoaji pungufu wa miradi ya maendeleo umekuwa ukijirudiarudia kwenye Bajeti ya Serikali kwa mwaka hadi mwaka.

## **7.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17.**

### **7.1. Utekelezaji wa hatua za kodi, ada, tozo na hatua nyingine**

#### **7.1.1. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya bajeti inapongeza hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato yatoyotokana na ajira kutoka asilimia 11 hadi asilimia 9. Pamoja na hatua hii ukifuatilia jedwali la viwango vya sasa ukurasa 60-61 viwango vinavyopendekezwa si rafiki kwa mtumishi wa umma (disincentive) na hatua ya kupunguza shilingi 3000 kila ngazi na wakati asilimia ya makato inabaki palepale haina unafuu wowote kwa mtumishi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi bunge limekuwa mstari wa mbele katika kujadili na kupendekeza watumishi wa umma kusamehewa kodi kwenye malipo ya viinua mgongo wanavyolipwa. Bunge limekuwa likishauri hivi ukizingatia kuwa mishahara ya watumishi wa umma na hata viongozi wa siasa imekuwa ikikatwa kodi, hivyo hatua hii inayopendekezwa na Serikali inakuwa *double taxation*. Ni muhimu Serikali ikafikiria suala hili upya kurekebisha kodi hii, kama ikishindikana basi ijumuishe viongozi wote wa kisiasa sio wabunge peke yao.

### **7.1.2. Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya Mwaka 2004**

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya bajeti ya Serikali ukurasa wa 66-80 umeainisha marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa forodha (EAC *Common External Tariff* 'CET') yaliyofanywa na nchi wanachama kwa makubaliano ya kuendeleza uchumi wa viwanda kwenye ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati ya bajeti imefanya tathmini ya huduma na bidhaa zinazosahewa kodi na kugundua kuwa hatua hiyo hainufaishi sana viwanda vilivyopo ndani ya nchi. Kwa nyakati tofauti, Kamati ya bajeti ilimtaka Waziri wa Fedha na Mipango afike kwa mashauriano kuhusu yale anayotegemea kuyawasilisha kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ili na hivyo Kamati iweze kumshauri ipasavyo. Suala hili limekuwa gumu kufanyika, hivyo Kamati inashuri Serikali kuweka utaratibu wa Waziri mwenye dhamana kushauriana na Kamati ya Bajeti kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya hatua za kodi zitakazojadiliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### **7.1.3. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza Tozo ya kuendeleza ufundi stadi (Skills Development Levy) kutoka kiwango cha asilimia 5 hadi asilimia 4.5. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa pamoja na punguzo hili bado waajiri wanamzigo wa tozo ya mchango wa mwajiri wa asilimia 0.5 ya mishahara kwenye Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi. Hivyo hatua iliyochukuliwa kwenye Tozo ya SDL haijaweza kumpa nafuu mwajiri.

## **7.2. Uzingatiaji wa Majukumu ya Kamati ya Bajeti na Sheria ya Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, mantiki wa uanzishwaji wa Kamati ya Bajeti na Sheria ya Bajeti ilikuwa ni kuwa na chombo cha kisheria na mfumo wa kisheria utakaosaidia kusimamia mchakato wa Bajeti ya Serikali kuanzia uandaji, uidhinishaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa. kamati ya Bajeti kama mshauri Mkuu wa Bunge katika masuala ya kibajeti kupitia sheria ya bajeti imepewa jukumu la kuhakikisha Serikali na Taasisi zake zinafuata mfumo bora wa kiutendaji katika mchakato wa bajeti, kuwepo kwa nidhamu ya bajeti kwa kuweka misingi ya kuzingatia mipango, mapato na matumizi; kuwepo kwa

bajeti inayoaminika yenye kuzingatia utekelezaji kama ilivyo dhinishwa na Bunge pamoja na kuweka masharti ya uhamisho wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, ni masikitiko ya Kamati ya Bajeti kuwa katika utekelezaji wa Bajeti hii ya Mwaka 2016/17; kwa kiasi kikubwa Serikali imeshindwa kutambua majukumu ya Kamati ya Bajeti kama mshauri Mkuu wa Bunge kwa masuala ya kibajeti pamoja na kwa kiasi kikubwa kushindwa kuzingatia Sheria ya Bajeti kama ilivyo elekeza. Kamati inaona kuwa serikali inataka turudi tulipotoka **‘Bunge kuwa rubber stamp katika uidhinishaji wa Bajeti ya Serikali’**. Kimsingi suala hili sio sahihi, Wabunge kama wawakilishi wa wananchi wanahitaji kujua namna Serikali itakavyotekeleza mahitaji ya wananchi ikiwa ni pamoja na kutatua kero za wananchi zinazowasilishwa na wabunge kupitia Kamati zao za Kisekta.

**Mheshimiwa Spika**, uanzishwaji wa Kamati ya Bajeti na Sheria ya Bajeti umetoa fursa kwa Serikali kuwa na **‘Bajeti Shirikishi’** na Bunge kupitia mawazo ya Wabunge na wananchi wanaowawakilisha. Lakini Kamati inachelea kusema kuwa katika mwaka wa **KWANZA WA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA BAJETI** hili halipo. Je? Kama Bunge, Wabunge na Kamati ya Bajeti tunapata fursa gani ya kuweza kuelewa na kuishauri Serikali kuhusu makadirio ya Bajeti iliyoyawasilisha? Kamati ya Bajeti imekuwa tayari siku zote kutekeleza majukumu ya kamati kwa kuzingatia Sheria na kanuni zilizopo, hata hivyo Serikali imekuwa ikisita mara kwa mara kukubaliana na Kamati hasa katika kupatikana kwa baadhi ya taarifa (kutoiamini Kamati), mapendekezo ya vyanzo vipya vya mapato au kutotoa taarifa kuhusiana na hatua mbalimbali za kifedha na kodi inayotegemea kuchukua kadiri Sheria inavyotaka. Kamati inaitaka Serikali itambue majukumu ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kama chombo cha ushauri wa masuala ya kibajeti kwa Bunge pamoja na uwepo wa Sheria ya Bajeti ili kuhakikisha Bajeti ya Serikali inakuwa **‘shirikishi’**.

### 7.3. Utaratibu wa Kikanuni wa Kupokea hoja za kamati za Kisekta

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la 2016 haijatoa ufafanuzi wa kutosha kuhusu utaratibu wa kujadili hoja zitakazokuwa zimejitokeza Bungeni wakati wa mijadala ya Bajeti ya Wizara mbalimbali. Je ni jukumu la kiti kuamua ni hoja zipi ziende kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya mashauriano au ni kamati ya Bajeti pamoja na Kamati za Kisekta kuangalia hoja gani zimezua mijadala wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti za Wizara husika. Aidha, Kanuni bado ipo kimya kuhusu utaratibu wa kufuatwa ikiwa Kamati ya Bajeti na Serikali hazijafikia makubaliano baada ya mashauriano. Kamati inashauri mapungufu haya yafanyiwe kazi.



#### 7.4. Mapato ya Sekta ya Mafuta na Gesi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa shughuli za utafutaji wa gesi na mafuta bado zinaendelea nchini. Wananchi wana mategemeo makubwa kwamba mapato yatokanayo na gesi yatakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yao. Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi (2015) iliandaliwa ili kutoa mwongozo wa kuanzisha mfumo maalumu (mfuko) wa usimamizi wa mapato na matumizi hayo pamoja na kuainisha vyanzo vya mapato maalumu ya mafuta na gesi. Hata hivyo, tofauti na ilivyokuwa mwaka 2015/16; katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17, Serikali haijaweza kuonyesha makadirio ya mapato itakayoweza kupata kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mafuta na gesi vilivyodainishwa ukurasa wa 141-142 wa kitabu cha Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2015. Aidha, Serikali haijaweza kueleza kwa kina namna itakavyolisaidia Shirika la Maendeleo la Mafuta na Gesi (TPDC) kuweza kujiendesha lenyewe kama kampuni ikiwa ni pamoja kuliaachia fedha za 'Retention' ili liweze kufanya utafiti na usimamizi madhubuti wa sekta hii. Kamati ya Bajeti inaona kuwa bado Serikali inajukumu la kuufahamisha umma faida tutakayoipata sasa baada ya ujenzi wa Bomba la gesi kukamilika kutokana na kiasi kikubwa tulichokopa (Shilingi trilioni 2.695) kwa ajili ya ujenzi wa Bomba hilo. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa madeni wanayodai TPDC kutoka kwa Songas (**Shilingi bilioni 80**) na Pan African (**Shilingi bilioni 64**) pamoja na wengine yanalipwa haraka iwezekanavyo ili kutunisha Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi.

#### 7.5. Kuongeza fedha Kwa ajili ya Mfuko wa Maji

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa wakati wa majumuisho wa hoja mbalimbali zenye maslahi ya Taifa zilizowasilishwa na Kamati za Kisekta, Kamati ya Bajeti na Serikali hazikuweza kufikia makubaliano ya kuongeza kiasi cha tozo kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petrol na diesel ili kupata kiasi cha shilingi Bilioni 250, ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 30 zingechukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya nchi nzima na kinachobaki (bilioni 220) kingepelekwa kwenye mfuko wa maji kwa ajili ya usambazaji wa maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kuwasilisha mapendekezo haya tena ili Bunge lako tukufu liamue ukizingatia kuwa hoja iliyokuja nayo Serikali kuhusu athari za ongezeko hili litaongeza mfumuko wa bei na kuathiri shughuli zingine za kiuchumi sio sahihi kwani; Wakati tunafikia makubaliano ya kuweka tozo hii ya Shilingi 50 mwaka 2015/16, bei ya petrol na dizeli ilikuwa ikiuzwa kati ya shilingi 2100 na 2400, na kwa sasa bei ya petrol na dizeli inauzwa kati ya shilingi 1700 na 1900 na bei za vitu na nauli zimeendelea kubaki palepale bila kushushwana wafanyabiashara. Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa hizi za mabadiliko ya bei kwa ajili ya maendeleo ya wananchi hasa kwa ajili ya maeneo nyeti kama maji na ujenzi wa zahanati na vituo vya afya

## 7.6. Baadhi ya Mafungu kupewa zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2015/16 baadhi ya mafungu yamepewa fedha zaidi ya zile zilizoidhinishwa na Bunge. Mfano **Fungu 28**-Wizara ya Mambo ya ndani ilipewa **asilimia 143** ya Bajeti, **Fungu 20** Ofisi ya Rais ilipewa **asilimia 102** ya Bajeti, Fungu 61 Tume ya Uchaguzi ilipokea **asilimia 145** ya bajeti na Mkoa wa Dar es salaam ulipewa **asilimia 124** ya Bajeti. Vilevile kwenye miradi ya maendeleo kuna baadhi ya mafungu yamepokea fedha za ndani za maendeleo zaidi ya kilichoidhinishwa na Bunge. Mfano; **Fungu 98** - Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilipewa **asilimia 117** ya bajeti, **Fungu 59** Wizara ya Nishati na Madini ilipewa **asilimia 131** ya bajeti, **Fungu 38** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujanga Taifa ilipewa **asilimia 127**. Kamati ya Bajeti inajuliza ni kwa utaratibu upi Serikali imejipa mamlaka ya kutoa fedha zaidi ya ile iliyoidhinishwa na Bunge? na hivyo kuathiri utekelezaji wa mafungu mengine. Kamati inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi kuhusu suala hili ukizingatia kuwa imekiuka utaratibu kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti kifungu cha 42 Kifungu kidogo cha Tano (5) (a); ambacho kinamkataza Waziri wa Fedha na Mipango kuhamisha fedha kutoka fungu moja kwenda fungu jingine bila kupitisha Bungeni.

## 7.7. Ukusanyaji wa Maduhuli kwa vifaa na mfumo wa kieletroniki

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuhakikisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinatumia vifaa na mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato, Ni dhahiri kuwa bado eneo la ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi (*maduhuli*) ulikuwa haufanyi vizuri hasa katika maeneo ada, mrabaha na tozo zinazotowwa na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Hatua hii itaongeza upatikanaji wa mapato ya ndani na hivyo kusaidia Serikali kuweza kugharamia bajeti yake.

## 7.8. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa njia ya Ubia (PPP)

**Mheshimiwa Spika**, Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa fedha 2016/17 haikufafanua ipasavyo ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa njia ya ubia. Serikali imejitahidi kuainisha miradi michache itakayotekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi, hata hivyo Kamati haijaridhishwa na mwenendo huu, hasa ikizingatiwa kuwa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ingeweza kuchochea maendeleo ya nchi ikiwemo miradi ya reli, bandari, viwanja vya ndege n.k kutegemea fedha za Serikali peke yake. Hivyo Kamati inaendelea kusistiza kuwa Serikali ilete orodha ya miradi yote ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu na ile ambayo haijafanyiwa ambayo Serikali ina nia ya kuitekeleza kwa ubia na sekta binafsi. Kufanikiwa kwa utekelezaji miradi ya ubia kutapunguza mzigo wa bajeti ya maendeleo na kodi kwa wataanzania na kukuza sekta binafsi.

#### **7.9. Mazingira ya Uwekezaji na Ufanyaji Biashara Nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Urahisi wa Kufanya Biashara ya Benki ya Dunia ya mwaka 2015, Tanzania ni nchi 139 kati ya nchi 189. Kamati imefanya tathmini na kuangalia vigezo vinavyotumika katika upangaji ambavyo ni upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, vibali vya ujenzi, upatikanaji wa nishati, uanzishwaji wa biashara, ulipaji wa kodi, usimamizi wa mikataba na upatikanaji wa mikopo na kubaini kwamba Tanzania haifanyi vizuri kutokana na masuala yafuatayo; wingi wa Mamlaka za Usimamizi, urasimu katika utoaji wa maamuzi, tatizo la kutopatikana umeme wa uhakika na uwepo wa lundo la Taasisi zinazojihusisha na Masuala ya uwekezaji na ufanyaji Biashara. Mfano, Nchi ya Rwanda ni nchi ya 62 kwasababu ya uwepo wa *Rwanda Development Board* inayosimamia shughuli zote za uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuchukua hatuz zifuatazo:-

**Kwanza** ni kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa vyombo vya Udhibiti Tanzania (*Tanzania Regulatory Authority*) kwa lengo la kusimamia Mamlaka zote za Usimamizi na Udhibiti kama TBS, TFDA, TAEC, WMA, na OSHA ambazo zitakuwa Idara katika mamlaka hiyo;

**Pili**; kuunganisha Taasisi na Mamlaka zote zinazohusiana na masuala ya uwekezaji kama Vile TIC, EPZA na BRELLA ili kuwa na usimamizi bora na kupunguza urasimu.

#### **7.10. Marekebisho ya Sheria ya Manunuzi ya Umma (*Public Procurement Act 2011*).**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza matumizi makubwa hasa katika maeneo ya malipo ya huduma (Hati za ununuzi –LPO's), kupunguza gharama kubwa za ujenzi, kutumia mfumo wa nakala laini (soft copy), ununuzi wa samani, ununuzi na uendeshaji wa magari, safari nje ya nchi n.k. Pamoja na hatua hizi, haya yote yatawezekana kutekelezwa vizuri pale Bunge litakavyofanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011. Kwa kuwa Serikali inakusudia kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Manunuzi kwa njia ya hati ya dharura, ni vema Wabunge wakapata nakala ya muswada huo mapema ili wapate fursa ya kusoma na kuelewa vipengele vinavyokusudiwa kurekebishwa na hivyo kuwa na nafasi nzuri ya kuishauri Serikali.

### **7.11. Uanzishwaji wa Mahakama inayoshughulikia makosa ya rushwa na hujumu uchumi.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya bajeti inapenda kuipongeza Serikali kwa hatuayake kutenga Shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kuanzisha Mahakama inayoshughulikia masuala ya rushwa na hujumu uchumi pamoja na kutenga shilingi bilioni 72.3 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za TAKUKURU. Hatua hii itasaidia vyombo hivi kufanya kazi nzuri kulingana na majukumu ukingatia kuwa vinategemeana katika majukumu yao. Sambamba na hili, Kamati ya Bajeti inaona kuwa utekelezaji wa majukumu ya vyombo hivi unategemea sana upatikanaji wa taarifa za Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG). Ipo haja ya Serikali kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) ili kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Mahakama ya uhujumu uchumi na TAKUKURU.

### **7.12. Utaratibu wa kubakiza sehemu ya makusanyo (*Retention*)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia hotuba ya bajeti imeeleza uamuzi wa kufuta mfumo wa kubakiza maduhuli-*retention* kwa Idara na taasisi zake ili kuongeza mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Pamoja na hatua hii nzuri, kamati ya Bajeti inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Mwongozo au utaratibu utakaotumika kufuta mfumo huu, kwa kuwa kuna baadhi ya Idara na taasisi za Serikali kisheria zinatakiwa kubaki na kiasi cha fedha ili ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mfano mzuri ni TANAPA, Ofisi za Ubalozi, Serikali za Mitaa n.k. Hata hivyo kamati inaishauri Serikali pamoja na utaratibu huu mzuri, mgawanyo wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali uzingatie majukumu na bajeti ya Idara au Taasisi husika pamoja na muda wa uwasilishwaji wa mgao huo.

### **7.13. Usimamizi na Uendeshaji wa Mashirika ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Makampuni na Mashirika ya Umma kujiendesha Kibiashara ni jambo la muhimu ili kuongeza ukusanyaji wa mapato. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuanza kutumia huduma zinazotolewa na Mashirika yake ya Umma pamoja na hatua ya kulipa moja kwa moja wizara ya Fedha na Mipango (centrally) madeni yatokanayo na huduma za maji, umeme kwa kutumia bajeti za mafungu husika. Hatua hii itasaidia Maafisa masuuli kubana matumizi ya Ofisi zao kutegemeana na mahitaji ya msingi. Aidha, kamati inashauri Serikali kufanya uwekezaji wa kutosha katika mashirika yake kama TTCL, TANESCO, ATC, UDA, Shirika la Posta na TBC ili kutoa huduma bora zenye ushindani.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, kamati inaipongeza serikali kwa hatua ya kutenga kiasi cha shilingi trilioni 2.49 kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu za abiria, ujenzi wa reli ya kati (standard gauge) ununuzi na ukarabati wa meli ziwa victoria na tanganyika pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya bandari na viwanja vya ndege. Kamati inaishauri Serikali kufanyia maboresho menejimenti ya ATCL iweze kusimamia shirika hili vizuri pamoja na kuhamasisha usafiri wa ndani wa anga kwa kutumia ndege za Serikali zenye gharama nafuu. Pia Serikali iweke bei ya ukomo kwa nauli za tiketi ya ndege kulingana na uasilia.

#### **7.14. Mapato ya Serikali za Mitaa.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa unasimamiwa na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (*Local Government Finance Act*). Aidha, ukusanyaji wa Mapato katika Halmashauri ni utekelezaji wa Sera ya ugatuaji wa madaraka (*Decentralization by Devolution*). Hata hivyo kumekuwepo na mwingiliano wa vyanzo vya mapato vinavyopaswa kukusanya na halmashauri kuchukuliwa na Serikali Kuu. Mfano tunauona katika kodi ya matangazo (mabango), majengo, na maduka ya jumla. Kamati inaona sasa dhana ya utekelezaji wa Sera ya ugatuaji wa madaraka mikoani imeanza kukiukwa kwa kuwa halmashauri zinaachiwa kukusanya vyanzo visivyo na uhakika au vyenye mapato kidogo ya fedha na hivyo kupelekea kushindwa kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi.

#### **7.15. Sekta ya Viwanda.**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa awamu ya pili (2016/17-2020/21) umejielekeza katika kuimarisha uchumi wa viwanda itakayofungamanisha maendeleo ya viwanda na watu. Kamati inatambua umuhimu wa viwanda katika kuleta maendeleo ya nchi kupitia ajira, ukusanyaji wa kodi mbalimbali na mauzo ya bidhaa mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuiweka sekta ya viwanda kama moja ya vipaumbele vyake katika bajeti. Hata hivyo, uamuzi huu usiishie kwenye vitabu, ni lazima utekelezwe kwa vitendo kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa (2016/2017- 2020/2021). Taarifa ya Kamati ya Maadumu ya Spika iliyohusu upatikanaji wa Mapato na Matumizi ya Serikali (maarufu kama Taarifa ya Chenge I) imetoa mapendekezo mbalimbali hasa katika kuanzisha, kusimamia na kuboresha viwanda mama pamoja na vingine vinavyohusu usindikaji wa mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi (*agroprocessing*). Kamati inaitaka Serikali kufanyia kazi mapendekezo hayo ili kuweza kupata mapato tarajiwa kupitia sekta ya viwanda pamoja na kuweka mkakati wa makusudi katika kuvikuza, kviendeleza na kuvilinda viwanda vya ndani.

### 7.16. Deni la Taifa,

**Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa limeendelea kukua kila mwaka kuanzia mwaka 2007/8 hadi 2014/15 kutokana na kuwepo kwa nakisi kwenye bajeti ya Serikali inayolazimu Serikali kukopa ndani na nje ya nchi ili kuziba pengo hili na kugharamia miradi ya maendeleo. Kabla ya kipindi hicho deni la Taifa lilikuwa limepunguwa kutokana na msamaha wa madeni uliotolewa na nchi wahisani chini ya utaratibu wa HIPC na MDRI kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2006.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Februari, 2016, Deni la Taifa lilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 36,390.28 ikiwa ni ongezeko la asilimia 26.3 ukilinganisha na shilingi bilioni 28,808.72 ya mwezi Juni, 2015. Kati ya hizo, deni la nje ni shilingi bilioni 26,926.42 na shilingi bilioni 9,463.86 ni deni la ndani. Ongezeko hilo limechangiwa na kukopa ndani na nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na malimbikizo ya riba kwa mikopo ya nje. Hivyo, ni vyema mikopo ikalipwa kwa wakati ili kuepuka kulimbikiza riba na kuhakikisha mikopo yote inayokopwa ni kwa ajili ya maendeleo tu.

### 7.17. Misamaha ya kodi kwenye bidhaa za watumishi wa vyombo vya Ulinzi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuondoa misamaha ya kodi iliyokuwa inatolewa kupitia kwenye migahawa na maduka maalum ambayo yanauza bidhaa mbalimbali kwa mahitaji ya askari na badala yake kuwapatia askari wetu posho maalum ili kuwawezesha kununua mahitaji yao wenyewe. Ni ukweli usiopingika kwamba utaratibu unaotumika sasa wa kutoa misamaha ya kodi hauwanufaishi walengwa na badala yake unawanufaisha wajanja wachache. Pamoja na kuunga mkono utaratibu mpya ambao Serikali inakusudia kuutumia, Kamati ingependa kujua endapo fedha za posho hizo zimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 na zimetengwa katika fungu na kifungu gani?

### 7.18. Kupiga Marufuku uuzwaji wa pombe kwenye vifungashio vya Viroba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kupiga marufuku utengenazi, uingizwaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya plastiki yenye kipimo cha unene chini ya microns 50. Kamati inaitaka Serikali kupiga marufu uuzaji wa pombe inayowekwa kwenye mifuko ya plastiki maarufu kama Viroba. Pombe hiyo inaweza kuendelea kuzalishwa na kuwekwa kwenye vifungashio vingine kama chupa.



## 8.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, ambao wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
9. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb
16. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb
17. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
18. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
19. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
20. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
21. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
22. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
25. Mhe. Dalaly Peter Kafumu, Mb
26. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga, Mb
27. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
28. Mhe. Mussa A. Zungu, Mb

Aidha, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt Philip Mpango Mb, Naibu Waziri Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji Mb, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa Bajeti pamoja na wataalamu wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na



Mipango kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kasililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Lina Kitosi, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Mathew Kileo na Ndg. Michael Kadebe pamoja na Sekretarieti ya Kamati Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Ruva Tunze, Ndg. Maombi Kakozi, Ndg. Lilian Masabala, na Ndg. Wilson E Machaine kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Hawa A. Ghasia (Mb)  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**  
10 Juni, 2016.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango.

**MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU WAZIRI KIVULI NA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YAUPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Kiti cha Spika, ambacho sasa hivi tunawasilisha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani yenye page 80, sasa kwa sababu ya ukubwa wa hotuba itaingia yote kama ilivyo...

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde naomba ukae, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA BUNGE KAZI AJIRA VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, kwa mujibu wa taratibu za Bunge na Kanuni zetu za Bunge kiti cha Spika kitakuwa *addressed* kwa jina la Spika, Naibu Spika ama Mwenyekiti kwa kuzingatia ni *Presiding Officer* gani ambaye anaongoza kiti. Kwa hiyo, nilikuwa naomba anayewasilisha hoja sasa hivi aki-address kiti kwa kuzingatia kanuni ambazo tunazo ndani ya Bunge. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, nadhani hilo lilishawahi kusemwa hata hapo mwanzo, tafadhali fuata Kanuni zinavyosema.

**MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YAUPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Halina shida. Kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Serikali...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, kama mimi ninavyokuita wewe Mheshimiwa ni kwa sababu wewe ni Mbunge, kwa hiyo, wewe hata kama humpendi Tulia yeye ni Naibu Spika kwa sasa, kwa hiyo, wewe address kiti inavyopaswa. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YAUPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Sio lazima Mheshimiwa, hata ndugu ni kawaida.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Kanuni za Bunge unazijua...

**MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YAUPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Huwezi kung'ang'ania kuitwa ndugu.

**NAIBU SPIKA:** Wewe huitwi ndugu, unaitwa Mheshimiwa kwa sababu ya heshima yako waliyokuheshimu watu kukuleta humu ndani, naomba uendelee.

**MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YAUPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Kwa kuwa unataka uheshimiwa, sawa, haina shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, *issue* si uheshimiwa. Kabla sijatoa Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017 napenda kuweka *records* sawa kuhusu upotoshaji unaofanywa na kiti chako kwamba Wabunge wa Upinzani wanasaini mahudhurio Bungeni na kuchukua posho bila kufanya kazi. *(Vigelele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda mkumbuke kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikisisitiza kufutwa kwa posho za vikao, kwa maana ya *sitting allowance*, lakini Serikali imekuwa ikipata kigugumizi, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema kwamba Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kama inania thabiti ya kubana matumizi ya Serikali ionyeshe uthabiti

huo kwa kuifuta posho ya vikao na fedha hizo zipelekwe kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo hususan kuwapatia Watanzania maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imekuwa ikisisitiza kufutwa kwa posho za vikao kwa maana ya *sitting allowance*, lakini Serikali imekuwa ikipata kigugumizi. Hivyo basi, Kambi Rasmi inasema kwamba, kama Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli inania thabiti ya kubana matumizi ya Serikali yake, basi ioneshe uthabiti huo kwa kufuta posho ya vikao kwa sababu fedha za mishahara zinatoshwa na fedha hizo zipelekwe kwenye miradi ya maendeleo hususan kuwapatia Watanzania maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tunataka Bunge lako liweze kuwaeleza Watanzania zile pesa tulizoziacha wakati wa Bunge la Katiba ambapo kila Mjumbe wa UKAWA aliacha shilingi milioni 30 na zenyewe zipelekwe kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunashauri, wale wanaokaa Bungeni bila kuchangia...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilize hotuba.

**MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** ...hata kwa maandishi na kuchukua posho, wafuatiliwe na wakatwe mishahara ama posho zao kwa kuwa hawajafanya kazi na *Hansard* zitumike katika kuwabaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama katika jitihada za kuongeza mapato yake, Serikali katika bajeti hii imekusudia kukata kodi ya asilimia tano kwenye kiinua mgongo cha Wabunge. Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na pendekezo hilo kabisa na inaitaka Serikali kwenda mbali zaidi kwa kufanya marekebisho Sheria hiyo ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa, ambayo kwa sasa imewapa misamaha ya kodi ya viinua mgongo viongozi wakuu wa kisiasa kama Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Spika, Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, hivyo basi, nao wanatakiwa wakatwe kodi hiyo, tuwasaidie, tuweke usawa kwa Watanzania.

Hata hivyo, Kambi Rasmi inalikumbusha Bunge lako na Serikali yake kwamba kiinua mgongo cha Wabunge hutolewa mwisho wa uhai wa Bunge, hivyo haioni mantiki ya kutoa pendekezo hili kwa wakati huu kwani haina *impact* katika Bajeti ya sasa ya mwaka 2016/2017 bali itakuwa na *impact* mwaka 2020/2021, ambao tunataka iingie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Serikali ya Hapa Kazi, imeleta Bajeti Hewa Bungeni. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ni wajibu wa Bunge kupanga na kuidhinisha mapato na matumizi ya serikali kila mwaka wa fedha. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 137(1), Rais atatoa maagizo kwa watu wanaohusika kwamba watengeneze na kuwasilisha kwenye Bunge katika kila mwaka wa fedha wa Serikali, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa ajili ya kipindi cha mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema kuwa, Serikali hii imeleta bajeti hewa hapa Bungeni na nitathibitisha maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kitabu cha Mapato ya serikali katika mwaka huu wa fedha *Volume I Financial Statements and Revenue estimates for the year 1<sup>st</sup> July, 2016 to 30<sup>th</sup> June, 2017*, kilicholetwa hapa Bungeni kinaonyesha kuwa mapato ya Serikali, yaani mapato ya kodi, yasiyo ya kodi, mikopo, misaada ya kibajeti itakuwa jumla ya shilingi trilioni 22.06.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mapato yatokanayo na kodi na tozo mbalimbali, yaani shilingi trilioni 17.7;
- (ii) Mapato yasiyokuwa ya kodi ni shilingi bilioni 665.6;
- (iii) Mikopo na misaada ya kibajeti ni shilingi trilioni 3.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Waheshimiwa Wabunge wakatambua kwamba Serikali hii haijaonyesha chanzo kingine kipya cha mapato ambacho hakijathibitishwa na au hakikupitishwa na Bunge. Hii kwa mujibu wa Katiba na ijulikane pia Bunge halipitishi kitabu na hotuba ya Waziri bali hupitisha mafungu yaliyopo kwenye vitabu vya bajeti ya Serikali yaani *Volume I, II, III na IV*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kitabu cha Matumizi ya Kawaida - *Volume II, Estimates of Public Expenditure Consolidated Fund Services for the year 1<sup>st</sup> July, 2016 to 30<sup>th</sup> June, 2017* na kitabu cha Maendeleo yaani *Volume IV - Public Expenditure Estimates Development Votes part A* kama vilivyowasilishwa Bungeni, tayari bunge limeshaidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi trilioni 23.847.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo huo wa fedha ni kama ifuatavyo:-

- (i) Fedha za Matumizi ya Kawaida yaani *Volume II* ni Trilioni 13.3.
- (ii) Fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo - *Volume IV* ni shilingi trilioni 10.511.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua kitabu cha Mapato ya Serikali (*Revenue Book Volume I*) utaona kuwa jumla ya mapato yote ya Serikali ni shilingi trilioni 22.063, ila Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi trilioni 23.847 ambacho ni kiasi tofauti na mapato ambayo Serikali imepanga kukusanya na tofauti yake ni kuwa kuna nakisi ya shilingi trilioni 1.783 jambo ambalo linafanya bajeti hii kukosa uhalali kwani nakisi hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Fedha, mapendekezo ya kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 kwenye mkutano wa Wabunge wote katika ukumbi wa JNICC mnamo tarehe 6 Aprili, 2016 pamoja na maelezo ya hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni ukurasa wa 91, ameeleza Bunge na dunia kuwa, katika mwaka huu wa fedha, Serikali ina bajeti ya kiasi cha shilingi trilioni 29.539.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri wa Fedha katika ukurasa wa 92; Mfumo wa Bajeti wa Mwaka 2016/2017 inaonyesha kuwa kiasi cha shilingi trilioni 7.475 ni mikopo ya ndani yenye masharti ya kibiashara. Fedha hizi kwenye kitabu cha mapato hazipo na pia hazionekani zitakopwa kutoka benki gani kama ambavyo mikopo ya nje yote imeonyeshwa kwenye kitabu cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri wa Fedha ukurasa wa 58 anasema kuwa moja ya chanzo chake cha mapato ni pamoja na kurekebisha Sheria ya Mapato Sura 332 ya kuondoa msamaha wa kodi ya mapato kwenye malipo ya kiinua mgongo kinacholipwa kwa Wabunge kila mwisho wa muhula wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kupata majibu ya kina kuhusu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge linapitisha takwimu zipi hasa? Ni kitabu cha hotuba ya Waziri au ni vitabu vya Mapato na Matumizi na pamoja na kile cha Miradi ya Maendeleo?

Fedha ambazo Waziri wa Fedha kwenye hotuba yake amesema ni mikopo ya ndani ya masharti ya kibiashara, zinakopwa ili kugharimia miradi ipi? Au ni miradi hewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha anaposema kuwa fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi trilioni 17.7, ambayo ni kinyume cha uhalisia wa kitabu cha Matumizi ya Kawaida, ambacho kinataja shilingi trilioni 13.336 na zilipitishwa na Bunge kifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa CAG anakagua kasma zilizopo kwenye vitabu yaani *Volume I, II, III na IV* katika bajeti hii atakagua kasma ipi?

Maana fedha za kulipia deni la Taifa hazipo kwenye kitabu cha *Volume II* na hata mikopo yenye masharti ya kibiashara inayosemwa itakopwa haipo kwenye *Revenue Book* yaani *Volume I*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuingizia malipo ya kiinua mgongo cha wabunge ambacho kulipwa mwaka 2020 kwa mujibu wa Sheria na kuwa chanzo cha mapato katika Mwaka huu wa Fedha hiki si chanzo hewa? Maana Wabunge watalipwa kiinua mgongo mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Kambi ya Upinzani Bungeni, tunaitaka Serikali iwasilishe vitabu vyenye kumbukumbu na takwimu sahihi (*addendum*) kabla ya kulitaka Bunge hili kujadili bajeti hii na kuamua kuipitisha au kuikataa, la sivyo Bunge litakuwa halitimizi wajibu wake kikamilifu kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa ndege za ATCL kuna harufu ya ufisadi. Kwa mujibu wa kitabu cha fedha za maendeleo *Volume IV, Part A*, Fungu 66 Kasma 4294 zimetengwa jumla ya Bilioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya kununua ndege za abiria kwa ajili ya Shirika la Ndege la ATCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, alipokuwa anawasilisha Mpango wa Maendeleo hapa Bungeni, alisema kuwa, Serikali imeamua kununua ndege Mbili aina ya Q 400 mbili na CS 300 Moja. Kutokana na uamuzi huo ni kuwa ndege aina ya Q 400 mwaka jana ilikuwa dola milioni 31.3 na ndege aina ya CS 300 ilikuwa dola milioni 82.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kimahesabu ni kuwa ndege Mbili aina ya Q 400 na ndege Moja aina ya CS 300 jumla yake itakuwa shilingi Bilioni 318.120 kwa *exchange rate* ya dola moja sawa na shilingi 2,200, na hivyo kufanya kiasi cha shilingi bilioni 181.8 kikisalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua ni kwanini tulitenga kiwango hicho cha fedha bilioni 500 wakati bei halisi za ndege zinajulikana? Hizo fedha zinazosalia baada ya manunuzi ya ndege zitatumika kufanya shughuli gani? Je kuna Wakala katika ununuzi wa ndege hizo ambaye atapata Kamisheni, na kama yupo ni nani na atalipwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna fedha za kuendesha ATCL. Pamoja na Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kununua ndege tatu. Jambo la kushangaza ni kuwa hakuna fedha za uendesaji ambazo zimetengwa na Serikali kwa ajili ya Shirika letu la ndege ATCL. Hata kwenye Mashirika ya Serikali ambapo yatakata ruzuku kwa mujibu wa kitabu cha *Volume II - Public Expenditure* kifungu cha 62, kama ya 2006 kifungu cha 270846 ATCL, zimetengwa shilingi bilioni 3.221 kwa ajili ya mishahara. Fedha kwa ajili ya uendesaji kwa maana *other charges* hakuna hata senti moja iliyotengwa kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua baada ya serikali kununua ndege hizo shirika litapata wapi fedha kwa ajili ya uendesaji na hasa ikizingatiwa kuwa Shirika mpaka sasa ni mufilisi? Serikali haikuona umuhimu wa kulipatia Shirika hilo ruzuku kwa ajili ya uendesaji wa shirika hilo? Mtaji wa kuanzia utatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mwalimu Nyerere *Phase II*; ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere wa awamu ya pili uko katika hatihati ya kusimama kutokana na Serikali kutokutii makubaliano ya mkataba ambapo waliingia na Kampuni ya Ujenzi ya *BAM International* ya Uholanzi. Hii ni baada ya Wizara ya Fedha kuamua kukiuka masharti ya mkataba baina ya TAA na *BAM International* kuwa fedha za kutekelezea mradi zitatolewa na *HSBC* kwa awamu zote mbili yaani *phase I* na *II* na badala yake wizara ya fedha imeamua kwenda kutafuta Mkopo Mpya nje ya makubaliano ya mkataba baina ya *BAM* na TAA wa Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua ni sababu gani zimepelekea Wizara ya Fedha kutafuta mkopo mwingine kutoka Taasisi nyingine nje ya makubaliano ya awali ya mkopo? Na nani atanufaika na utaratibu huo wa kutafuta mkopo mpya badala ya kukamilisha taratibu zilizokuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanja cha ndege Chato; ukisoma Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika eneo la usafiri wa anga moja ya kipaumbele cha mpango ukurasa wa 76 sehemu ya 10 ni ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Chato. Mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuanza kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama paliwahi kufanyika kwa utafiti wa kina na majibu ya utafiti huo kuonyesha kuwa ujenzi wa kiwanja cha Chato ndio kipaumbele cha Taifa kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Presidential Delivery Bureau*; Serikali katika mwaka huu wa fedha wameamua kukaa kimya kuvunja kitengo hiki kwa kutotenga hata senti moja kwa ajili ya mishahara na marupurupu mengine kwa



ajili ya wafanyakazi wa kitengo hiki, yaani Vote 6 na badala yake zimetengwa kiasi cha shilingi milioni 397 kwa ajili ya kulipia kodi ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ukiangalia bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha 2015/2016 kifungu hiki kilitengewa kiasi cha shilingi milioni 602 kwa ajili ya kodi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata maelezo ya kina juu ya mambo yafuatayo; waliokuwa watumishi wa kitengo hiki wamehamishwa, wamefukuzwa au wamesimamishwa kazi? Mbona hakuna fedha wala marupurupu mengine kwa kitengo hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za mishahara, ni sababu zipi zimepelekea kitengo hiki kutokupatiwa fedha za uendeshaji? Ni nani ataenda kusimamia fedha za maendeleo takribani bilioni 27 ambazo zimetengwa katika kitengo hiki ambacho hakina wafanyakazi au ndio kusema *DFID* na *UNDP* itakuwa ikisimamia fedha zake moja kwa moja? Tangu kuanzishwa kwa kitengo hiki kimetumia kiasi gani cha fedha na ufanisi wake umekuwa ni kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Millenium Challenge Corporation (MCC)*; kwa mujibu wa randama ya Wizara ya Fedha na Mipango kifungu 1007 katika mwaka wa fedha 2016/2017 Idara wameomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 500 kama bajeti yake ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 60 ambayo kasma ya 210300 zinaombwa kwa ajili ya kuwalipa posho ya majukumu kwa watumishi 12 wa *MCA-T Compact II*, watakaofanya kazi ya uchambuzi wa miradi inayohitaji ufadhili wa MCC. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 280, kasma 220700 ni kwa ajili ya kulipia pango la ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya MCC mnamo tarehe 28 Machi, 2016 ilisimamisha kutoa fedha kwa Tanzania katika mradi wa *MCA-T Compact II* zaidi ya shilingi trilioni moja kwa maana ya dola za Kimarekani milioni 472.8 ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Wakurugenzi ya MCC ilimuandikia Rais barua wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 31 Machi, 2016 na kumjulisha rasmi juu ya uamuzi wake .Pamoja na Rais kujulishwa kwa barua Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina taarifa kuwa hadi mwezi Mei, barua hiyo ya Bodi ya MCC ilikuwa haijapatiwa majibu na Ikulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupatiwa majibu ya kina juu ya mambo yafuatayo:-

i. Ni kwa nini serikali inaomba fedha kwa ajili ya kulipa watumishi ambao watachambua miradi ya MCC ambayo haipo?

ii. Ni lini serikali itaijibu barua ya Bodi ya MCC hasa ikizingatiwa kuwa katikati ya mwezi huu, Bodi ya MCC itakaa na itatoa uamuzi wa mwisho juu ya jambo hili?

iii. Hivi kulipia kiasi cha shilingi milioni 280 cha kodi ya ofisi kwa mwaka ambayo ina watumishi 12 kinaendana na dhana ya kubana matumizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha, *Stanbic Bank* na Sakata la Mkopo wa dola milioni 600 - utakatishaji wa fedha haramu; mwaka 2012/2013 Serikali ya Tanzania iliomba mkopo wa dola milioni 600 kwa malengo ya kugharamia mpango wa Taifa wa miaka mitano. Mkopo huu ulizihusisha benki zenye mahusiano ya kibiashara *Stanbic* (Tanzania) na *Standard Bank PLC* kwa sasa inafahamika kama *ICBC Standard Bank PLC*, *Standard Bank* ya Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana kwamba mchakato huo ulihusisha udanganyifu wa ada ya mkopo, taarifa zinaonyesha kwamba ada halali iliyotakiwa kulipwa ni asilimia 1.4 ya mkopo wote. Hata hivyo, ada hiyo iliyokuja kulipwa ni asilimia 2.4 ya mkopo wote. Kutokana na udanganyifu huo, kuna kesi inayoendelea mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio dhamira ya Kambi Rasmi ya Upinzani kujadili wahusika kwa kuwa tunatambua, Kanuni zetu za Bunge zinatuzuia kujadili suala ambalo liko mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo nyaraka mbalimbali, mojawapo ikiwa ni barua toka TAKUKURU (Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa) kwenda kwa Mwanasheria Mkuu Mheshimiwa George Masaju yenye kumbukumbu namba CACE255/362/01/104 ya tarehe 20/01/2016. Barua husika inaainishwa mambo mbalimbali ikiwemo na kutaja majina ya watu wanaochunguzwa kwa kukiukwa vifungu mbalimbali vya Sheria ya Makosa ya Adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watuhumiwa wakiwa ni *Stanbic Bank*, Harry Kitilya (Aliyekuwa Kamishna Mkuu TRA), Peter Anandi Nyabuti, Bashir Awale, Shose Sinare, Sioi Sumari, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Alfred Paul Misana, Bedason Shalanda, Ramadhan Kijjah na Ngosha Said Magonya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iliambie Bunge hili Tukufu; ni vigezo gani vilivyotumika kuwachuja watuhumiwa kutoka 11 mpaka 3? Ni kwa vigezo gani Wizara ya Fedha iliruhusu fedha za umma kuingia katika akaunti binafsi? Ni kwa kiwango gani Wizara ya Fedha inadhani ilitekeleza wajibu wake ipasavyo katika mchakato mzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini mpaka sasa Katibu Mkuu na Kamishna wa Wizara ya Fedha hawajafunguliwa mashtaka na wanaendelea kuitumikia Serikali inayojinasibu kutumbua majipu wakati sheria ni msumeno na inakata pande zote mbili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba mibovu ya Sekta ya Madini na Nishati inayolikosesha Taifa mapato. Kwa mujibu wa kitabu cha mapato - *Volume I* kinaonesha kuwa gesi italiingizia Taifa katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 115.127. Aidha, sekta ya madini inategemewa kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 180.3 kwa mrahaba wa madini na kiasi cha shilingi bilioni 29.494 ni kodi mbalimbali kutoka sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mara zote imekuwa ikijitapa hapa Bungeni na huko nje kwa wananchi kuwa kwa sasa uchumi wa gesi unakwenda kutuondolea umasikini, kumbe ni hadaa. Hali hii ya kuendesha Serikali kila mwaka kwa fedha za pombe na sigara ambazo ni nyingi kuliko fedha za Sekta ya Nishati na Madini haikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mapato ya VAT kutokana na sigara na bia kwa mwaka uliopita ni shilingi bilioni 263.940. Mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye bia, sigara na vinywaji vikali ni kiasi cha shilingi bilioni 544.112 (kwa mujibu wa Kitabu cha Mapato ya sasa - *Volume I*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tunaitaka Serikali kuiwasilisha mikataba yote ya sekta ya nishati na madini hapa Bungeni ili Bunge liweze kupitia na kuchukua hatua za kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba. Aidha, tunamtaka Waziri aeleze, huu uchumi wa gesi ambao unasemwa kila mara uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya majengo; kwa miaka mingi kodi ya majengo ilikuwa ikikusanywa na Halmashauri, lakini kwa sasa Serikali imeamua kodi hiyo ikusanywe na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupelekwa Hazina. Agizo hilo litaathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri zetu nchini kwa kuwa kodi hiyo ya majengo ilikuwa chanzo kikuu cha mapato ya Halmashauri, hasa za Miji, Manispaa na Majiji. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunalishauri Bunge kutafakari kwa kina ushauri huu wa Serikali na kutazama madhara yake kwa kina na kwa uchumi wa uendeshaji wa halmashauri zetu kabla ya kuupitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufutwa kwa misamaha ya kodi kwa majeshi yetu. Wakati Waziri wa Fedha akiwasilisha hotuba ya Bajeti alisema kuwa moja ya hatua ambazo Serikali inachukua ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali ni pamoja na kufutwa kwa misamaha ya kodi kwa majeshi ya ulinzi na usalama

na badala yake alipendekeza kuwepo kwa posho maalum kwa ajili ya kuwawezesha wanajeshi wetu kununua mahitaji yao muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha katika hotuba yake ukurasa wa 88, alisema kuwa tarehe ya kuanza kutumika kwa utaratibu huu ni kuanzia tarehe 1 Julai, 2016. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kupatiwa majibu juu ya masuala yafuatayo:-

Fedha za kulipa majeshi yetu (posho maalum) zipo katika fungu lipi la fedha za bajeti na hasa ukizingatia kuwa mafungu yote katika Wizara husika yaliyopitishwa na Bunge hili na hiyo posho hayakuwepo?

Je, zile bidhaa na vifaa vilivyopo kwenye Bohari za Majeshi yetu zitapelekwa wapi na zipo kiasi gani, kwani utekelezaji wa jambo hili umekuwa wa ghafla sana yaani chini ya wiki tatu kabla ya utekelezaji wake kuanza. Kwa nini Serikali isingewachukulia hatua wajanja wachache waliokuwa wanajinufaisha na msamaha huo na badala yake imeamua kuyaadhibu majeshi yetu yote?

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahitaji majibu juu ya hoja zote, zikwemo, tuna hoja nyingi kwenye kurasa 80 za Hotuba Rasmi ya Kambi ambayo tunataka yote iingie katika *Hansard* kwa faida ya Taifa letu, na tumeainisha mpaka vyanzo vya mapato, tumeainisha Bajeti mbadala ambayo Serikali inaweza ku-copy na ku-paste na kuifuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE  
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHU  
HALI YA UCHUMI WA TAIFA, MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA NA MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 – KAMA  
ILIVYOWEKWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo  
la Januari, 2016*

## **1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Mwanafalsafa **Baron Montesquieu** aliwahi kuandika ifuatavyo kuhusu mgawanyo wa madaraka "*Pale ambapo madaraka ya Bunge na ya Serikali kuu yanakuwa yamehodhiwa na mtu mmoja, au katika*

chombo hicho hicho cha hukumu, hakutakuwa na uhuru, kwa sababu hofu itazuka, utawala huo huo au bunge litatunga sheria kandamizi na kuzitekeleza kwa mfumo kandamizi. Pia hakutakuwa na uhuru endapo madaraka ya Mahakama, Bunge na Serikali hayatatenganishwa. **Pale ambapo madaraka ya Serikali kuu yanapokuwa yamefungamanishwa na Bunge, uhai wa Bunge na Uhuru wake unakuwa katika hatari kubwa ya kudhibitiwa kiholela:** kwa kuwa Jaji hawezi kuwa mtunga sheria. Pale ambapo Serikali kuu imefungamanishwa na mahakama, basi Jaji anaweza kuwa na tabia ya mabavu na ukandamizaji. Inakuwa mbaya zaidi, pale ambapo mtu huyo huyo au chombo hicho hicho, iwe ni wateule wa Serikali au watu wengine wanapotumia hayo madaraka ya kutunga sheria, kutekeleza maazimio ya umma na kutoa hukumu za jinai au tofauti za watu"

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mada iliyowasilishwa na Profesa P.J. Kabudi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam juu ya **"Mafundisho ya Mgawanyo wa Madaraka na jinsi yanavyotumiwa Tanzania" (Doctrine of Separation of Powers and its Application in Tanzania: Success, Challenges and Prospects)** ni kwamba; hakuna mgawanyo dhahiri wa madaraka baina ya mihilimili mikuu ya dola na kwamba bado Tanzania ina 'hang-over' ya ulevi wa siasa za chama kimoja . Sehemu ya Mada hiyo inasomeka hivi: nanukuu; "Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 bado inatumika mpaka leo pamoja na kuwa marekebisho yalikuwa mfano wa Ustawishaji wa mfumo wa chama kimoja nchini Tanzania. Katiba pia iliendelea kustawisha dhana ya Ukuu wa Chama kushika hatamu.

Ibara ya 3 na 10 zilibainisha kuwa CCM ndio chama pekee cha Siasa Tanzania na kuwa shughuli zote za Serikali ilibidi zifuata sera na miongozo ya chama. Hii ilimaanisha kuwa Bunge na Mahakama vilitakiwa kufuata maelekezo ya chama katika kutenda majukumu yao. Zaidi ya yote, kama ilivyokuwa kwa Katiba ya Mpito, ibara ya 63(4) ya Katiba ililifanya Bunge kuwa kamati maalumu ya Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa. Ilikuwa ni jambo la kawaida pale ambapo bajeti ya wizara imekwama basi wabunge waliahirisha mkutano na Bunge lilikaa kama kamati ya Chama ili kujadili hilo suala. Mara tu uamuzi unapofikiwa basi Bunge linarejea na bajeti inapitishwa bila kuwa na upinzani mkubwa"

Katiba ya mwaka 1977 imerekebishwa mara kadhaa. Marekebisho makubwa zaidi yalikuwa ni yale ya tano, ambayo yaliingiza Haki za Binadamu katika Katiba, na marekebisho ya nane yaliyofanyika mwaka 1992 yaliyorejesha tena Mfumo wa Vyama Vingi Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maudhui ya nukuu ya mwanafasafa wa kale wa Sayansi ya Siasa Montesquieu, mada ya Profesa Paramagamba John Kabudi, na tabia isiyokubalika ya Serikali kuendelea kushawishi Mahakama na kulidhibiti Bunge kwa hila mbalimbali ni kwamba, Tanzania sasa iko katika hatari

kubwa ya kuingia katika mfumo wa Dola la Kidikteta na tayari dalili zote za utawala wa namna hiyo zimeanza kuonekana.

**Mheshimiwa Spika**, vitendo vya hivi karibuni vya Serikali hii kukanyaga uhuru wa vyombo vya habari kwa kufuta kabisa usajili wa baadhi ya vyombo vya habari, kupiga marufuku urushwaji wa matangazo ya moja kwa moja ya mijadala ya Bunge kupitia televisheni ya Taifa, kuingiza polisi ndani ya ukumbi wa Bunge na kuwapiga na kuwadhalilishwa wabunge; kuzuia mikutano ya vyama vya siasa ni sehemu tu ya tabia za utawala wa kidikteta.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakemea kwa nguvu zote ukandamizaji wa demokrasia na ukiukaji wa haki za binadamu unaofanywa na Serikali ya Tanzania dhidi ya watu wake. Aidha, tunataka Jumuiya ya Kimataifa ijue na dunia ijue kwamba sasa Tanzania hakuna utawala wa kidemokrasia tena – kinachofanyika ni utekelezaji wa amri za Rais – yaani *Presidential decrees*.

**Mheshimiwa Spika**, kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Serikali ya 2016/17, napenda kuweka rekodi sawa kuhusu upotoshaji unaofanywa na Wabunge wa CCM kwamba Wabunge wa Upinzani wanaisaini mahudhurio bungeni na kuchukua posho bila kufanya kazi. Napenda mkumbuke kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikisisitiza kufutwa kwa posho za vikao kwa maana ya "Sitting allowance", lakini serikali imekuwa ikipata kigugumizi, hivyo basi Kambi Rasmi inasema kama kweli Serikali ya Rais John Pombe Magufuli inania thabiti ya kubana matumizi ya Serikali basi inoneshe uthabiti huo kwa kuifuta posho ya vikao na fedha hizo zipelekwe kwenye miradi ya maendeleo hususani kuwapatia Watanzania maji safi na salama. Hata hivyo, tunashauri, wale wanaokaa bungeni bila kuchangia hata kwa maandishi na kuchukua posho, wafuatiliwe na wakatwe mishahara yao, kwa kuwa hawajafanya kazi na hansard itumike kuwabaini.

**Mheshimiwa Spika**, katika jitihada kuongeza mapato, Serikali katika bajeti hii imekusudia kukata kodi ya asilimia 5 kwenye kiinua mgongo cha wabunge. Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na pendekezo hilo, ila inaitaka Serikali kwenda mbali zaidi kwa kuifanyia marekebisho sheria ya mafao ya viongozi wa kisiasa ambayo kwa sasa imewapa misamaha ya kodi ya kiinua mgongo viongozi wakuu wa kisiasa kama Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Spika, Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili sasa na wao walipe kodi hiyo. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kwamba kiinua mgongo cha wabunge hutolewa mwisho wa uhai wa bunge husika, hivyo haioni mantiki ya kutoa pendekezo hili sasa kwa kuwa halina impact kwa bajeti ya 2016/17.



## 2. HALI YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika**, tunaposema hali ya uchumi tunaangalia uchumi kwa ukubwa wake (Macro economy) katika nchi, mataifa yanayotuzunguka na kwa dunia nzima, na ni kwa vipi sera zetu za uchumi zinavyoathirika na uchumi wa dunia, na ni kwa jinsi gani watunga sera wanatakiwa kuwa na mikakati itakayoweza kukabiliana na sera za wale tunaotengamana nao kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, Na katika hili ni lazima tuangalie ni jinsi gani uchumi mdogo (micro-economy) ambao ndio nguzo kuu ya nchi kwa maana unaowafanya wananchi waweze kuishi, au sera za uchumi zinazoendesha biashara ndogo ndogo kati ya kampuni na kampuni, na zinaangalia jinsi biashara zinavyoweza kufanikiwa kwa kiwango cha juu na aidha, namna gani maamuzi ya biashara yanatakiwa kufanywa ili biashara ziweze kufanikiwa, kwa maana nyingine ni kushughulika na “**supply and demand**”, jinsi ya kufikisha uchumi kwenye mifuko ya watu mmoja mmoja.

**Mheshimiwa Spika**, kukua au kutokukua kwa uchumi kutaonekana na jinsi pato la taifa litakavyokua ambalo ni matokeo ya shughuli za uzalishaji na utoaji wa huduma katika mzunguko mzima wa uchumi. Katika makadirio yaliyokuwa yametolewa na serikali katika mpango wa maendeleo awamu ya kwanza kwenye ukuaji wa uchumi ilitarajiwa kuwa ukuaji wa pato la taifa lifikie asilimia 8. Hii iliwekwa kutokana na ukweli kuwa kwa mwaka 2011 GDP ilikuwa 7.9%, 2013 GDP ikawa 7.3% na miaka miwili mfululizo GDP ikawa 7.0% na matarajio kwa mwaka 2016 ni 7.2%.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho ukuaji wa baadhi ya sekta za uzalishaji pamoja na shughuli za utoaji wa huduma ulikuwa kama ifuatavyo; Mawasiliano (14.9%), Huduma za fedha na Bima (10.4%), Ujenzi (10.3%), Kilimo - kwa maana ya mazao, ufugaji, misitu na uvuvi (3.1%) kwa kulinganisha na 3.4% mwaka 2014. Sekta hii licha ukuaji wake kuwa mdogo kwa kulinganisha na mwaka wa nyuma lakini mchango wake katika Pato la Taifa uliongezeka na kuwa 31.4% kulinganisha na 28.9% kwa mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za Serikali, inaonesha kuwa kiwango cha riba za amana za muda maalum kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 9.02 Januari, 2015 hadi asilimia 9.08 Januari, 2016, kiwango cha riba za amana kwa mwaka kiliongezeka hadi 11.01% kutoka 10.66% 2015. Riba za mikopo kiliongezeka kutoka 15.75% Jan. 2015 hadi asilimia 16.28 Jan.2016, wastani wa riba za amana za mwaka na riba za mikopo za mwaka iliongezeka kutoka wastani wa 3.14% Jan.2015 na kufikia 3.33% Jan.2016 Kambi Rasmi ya Upinzani inasema riba hizi zingeweza kuongezeka kama Serikali isingekuwa inafanya biashara kubwa na mabenki na hivyo kupelekea mabenki kushindwa kuhamasisha wananchi kufanyabiashara nayo.



## 2.1 USIMAMIZI WA TAASISI NDOGO-NDOGO ZA FEDHA

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani inapenda kusesitiza tena kwa Serikali kuleta muswada wa sheria ambao utaanzisha mamlaka ambayo itatoa kisheria muundo wa kudhibiti na kusimamia taasisi ndogondogo za fedha nchini ambazo kwa sasa zimekuwa zikisimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania pamoja na taasisi nyingine za kifedha kama mabenki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona haja ya kuwa na mamlaka huru iliyo chini ya Benki Kuu ya Tanzania ya kusimamia taasisi ndogondogo kama ambavyo Benki Kuu ya Tanzania imeruhusu uanzishwaji wa mamlaka za kusimamia mifuko ya hifadhi za jamii, bima na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** kuundwa kwa chombo chenye mamlaka ya kusimamia taasisi ndogondogo za fedha ni lazima kwa kuwa kwa sasa hakuna mrandamo wa viashiria kwa mabenki na taasisi ndogondogo za fedha. Kutokana na utofauti wa muundo wa mabenki na taasisi ndogondogo za fedha, inakua ni vigumu kudhibiti riba na utoaji wa vigezo vya kifedha katika kuhudumia wananchi na kutoa mikopo yenye unafuu.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni kuwepo na chombo chenye mamlaka tofauti na Benki kuu ya Tanzania itakayosimamia na kuratibu taasisi ndogo ndogo za fedha na kuziwezesha katika kutoa mikopo kwa wananchi hasa walio katika sekta isiyo rasmi. Hivi sasa kumekuwapo na taasisi ndogondogo za kifedha ambazo zinawapa fursa wananchi kujiunga katika vikundi vidogo vidogo na kuwapa elimu ya ujasiriamali kisha kuwasaidia katika suala la mikopo ambayo utakaoweza kuwapa fursa wataanzania waliopo katika sekta isiyo rasmi kama wamachinga, mama lishe, mafundi uashi na wajenzi, mafundi magari na seremala ambao chombo hicho kingeweza kusimamia ukusanyaji wa fedha kutoka katika makundi haya na kuweza kuwekeza kwa ajili ya kusaidia kutoa mitaji pale inapohitajika.

**Mheshimiwa Spika,** hili ni suala zuri ambalo linalenga kuboresha maisha ya wananchi wa vijijini na maeneo mbalimbali ya mijini. Pia, zipo Saccoss (vyama vya kuweka na kukopa) na benki jamii (vicoba) ambazo zimekuwa na wanachama wengi wanaoendelea kujiunga ili kujikwamua kiuchumi. Lakini kumekuwana mapungufu kwa kuwa taasisi ndogondogo za fedha zimeendelea kutumia masharti sawa na zile za mabenki ambazo zimekuwa ni mzigo kwa mlengwa ambaye ndiye analipa riba kubwa kutokana na masharti mazito yenye kulingana na vigezo vya kutoa mikopo kwa mabenki chini ya Benki kuu ya Tanzania. Kwa mfano, taasisi za fedha chini ya Benki Kuu bado zimeendelea kumtaka mtu awe na dhamana ya mali isiyohamishika na zile wanazojidhamini kwa vikundi. Je, itawezekanaje kwa Mwananchi mwenye hali duni kuwa na dhamana ya mali isiyohamishika?

**Mheshimiwa Spika**, kuwepo kwa chombo chenye mamlaka pia itasaidia kuwa na **Credit Reference Bureau** itakayokuwa na taarifa za wakopaji kutoka taasisi ndogondogo za fedha tofauti na itakayosimamia wadaiwa wa mabengi na taarifa hizi zitasaidia udhibiti wa wateja wa taasisi hizi kuchukua zaidi ya mkopo mmoja kwenye taasisi tofauti tofauti ambapo hali hii husababishwa na uchelewashaji wa mikopo unaotolewa na taasisi hizi pamoja na uhafifu wa mikopo katika kumsaidia mlengwa.

### **3. MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO 2016/17**

#### **3.1 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya sifa kubwa ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliomaliza muda wake (2011/12 – 2015/16) ni kuweka msingi wa kibajeti ulioitaka Serikali kutenga asilimia 35 ya Mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mpango ulisema hivi: nanukuu, ***“kwa kuelewa kuwa wakati wote kutakuwa na miradi ya uwekezaji nje ya mpango, serikali, kuanzia sasa, itakuwa inatenga asilimia 35 ya makadirio ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo kila mwaka” mwisho wa kunukuu.***

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uhalisia kwamba Mpango huo haukutungiwa sheria ya utekelezaji; Serikali ilijificha katika kichaka cha udhaifu huo; na matokeo yake kwa miaka yote mitano ya utekelezaji wa Mpango huo, Serikali haikuwahi hata mara moja kutenga asilimia 35 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuna wakati mwingine haikutenga hata senti moja. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2012/13 Serikali haikutenga fedha yoyote kutoka katika mapato yake ya ndani kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Serikali kugoma kutoa asilimia 35 ya mapato yake ya ndani kutekeleza miradi ya maendeleo, miradi mingi ya maendeleo haikukamilika hadi mwisho wa muda wa utekelezaji wa Mpango.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na aibu ambayo Serikali iliipata kwa miaka yote mitano ya utekelezaji wa Mpango huo kwa kushindwa kutekeleza utaratibu iliyojiwekea yenyewe wa kutenga asilimia 35 ya Mapato yake ya ndani kugharamia mpango wa Maendeleo; safari hii Serikali imefuta utaratibu huo katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri rahisi ya uamuzi wa Serikali hii ya CCM inayojinasibu kwa kauli ya *“hapa kazi tu”* kufuta msingi wa kibajeti wa kugharamia mpango wa maendeleo kwa kutenga asilimia 35 ya mapato yake ya ndani ni hofu ya kushindwa kutekeleza commitment hiyo kama ambavyo ilishindwa kufanya

hivyo katika Mpango uliomaliza muda wake lakini pia ni kukwepa kuwajibika au kuwajibishwa na Bunge kwa hofu hiyo hiyo ya kushindwa kutekeleza. Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inadhani ni bora Serikali hii ikakubali uhalisia kwamba imetawaliwa na *hofu tu* na sio *kazi tu* kwa kuwa inakimbia kivuli chake yenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza kwamba: **“Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake, Bunge laweza; kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo;** hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta Muswada wa Sheria ya Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo unaopendekezwa kabla ya kupitishwa na Bunge. Aidha; Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Muswada huo uitake Serikali kutenga asilimia 40 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, suala la kutuga sheria ya kutekeleza Mpango huu sio ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni – ni takwa la kikatiba. Ikiwa Serikali hii itapuuzia jambo hili basi ijulikane na iingie kwenye rekodi kwamba Serikali imevunja Katiba ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika** imebidi sasa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ichukue jukumu la kusimamia misingi ya Katiba ili Serikali hii isiendelee na tabia yake ya kuwa na ndimi mbili katika jambo moja. Nasema hivi kwa sababu; Serikali hii imekuwa na historia ya kulidanganya bunge, na kwa kuwa wanajivunia wingi wa wabunge CCM basi mambo yamekuwa yakipitishwa kiholela bila kuzingatia matakwa ya Katiba, Sheria za Nchi na hata Kanuni za Bunge.

Kwa mfano; Serikali imesema katika Mpango wake wa Maendeleo wa 2016/17 kwamba imetenga **shilingi trilioni 11.82** sawa na asilimia 40 ya bajeti yote kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo; lakini ukisoma kitabu cha Matumizi ya Fedha za Maendeleo (Public Expenditure Estimates Development Votes) VOLUME IV, fedha zilizotengwa ni **shilingi trilioni 10.511**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapokuwa na tarakimu tofauti katika suala nyeti kama hili la Bajeti ya Serikali, tunapata mashaka makubwa sana na weledi wa watendaji wa Serikali akiwemo kiongozi wao mkuu. Katika hali kama hiyo, ni lazima kuwa na sheria itakayotoa mwongozo kwa Serikali juu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ambao unatumia fedha za umma.

### **3.2. Mpango wa Taifa wa Maendeleo na Agenda 2030 ya Dunia ya Maendeleo Endelevu**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 25 Septemba, 2015 Dunia iliingia mkataba wa kutekeleza malengo 17 ya agenda 2030 ya kuibadilisha Dunia na kuwa mahali salama zaidi pa kuishi kwa kuweka malengo ya kuwa na maendeleo endelevu. Malengo hayo ni kama ifutavyo:-

Lengo Na. 1. Kuondoa umasikini wa aina zote

Lengo Na. 2. Kuwa na kilimo endelevu, Kuondoa njaa na kuwana uhakika wa chakula na lishe bora kwa watanzania wote.

Lengo Na. 3. Kuhakikisha kuwa jamii ya rika zote inakuwa na afya bora.

Lengo Na. 4. Kuhakikisha fursa ya elimu bora na iliyo shirikishi kwa watanzania wote.

Lengo Na. 5. Kutoa usawa kwa jinsia zote na kuwawezesha akina mama na wasichana wote.

Lengo Na. 6. Kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama kwa watanzania wote.

Lengo Na. 7. Kuwa na uhakika wa upatikanaji wa nishati endelevu na ya kisasa kwa wote.

Lengo Na. 8. Kukuza ajira endelevu na zenye staha na ukuaji wa uchumi shirikishi.

Lengo Na. 9. Kujenga miundombinu bora na shirikishi ili viwanda viwe endelevu kwa kupokea mabadiliko yoyote.

Lengo Na. 10. Kupunguza tofauti za ndani na baina ya mataifa kwa walionacho na wasio nacho.

Lengo Na. 11. Kufanya miji yetu na makazi shirikishi, endelevu na salama.

Lengo Na. 12. Kuhakikisha uzalishaji endelevu utakaoendana na matumizi.

Lengo Na. 13. Kuchukua hatua za haraka kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Lengo Na.14. Kutunza na matumizi endelevu kwa maendeleo ya rasilimali za baharini.

Lengo Na.15. Kulinda na kuwa na matumizi endelevu ya **'terrestrial ecosystem'**, kutunza misitu na kupambana na ukame na kurudisha uhalisia wa ardhi.

Lengo Na.16. **Kuwa na taasisi imara ili kuwa na haki na amani.**

Lengo Na.17. Kuimarisha ushiriki wa pamoja katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Tanzania ni sehemu ya dunia, na kwa kuwa Tanzania haiwezi kusimama peke yake na kufanikiwa katika kufikia malengo yake ya maendeleo kama haishirikiani na mataifa mengine, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetekeleza kwa kiwango gani agenda ya Dunia ya 2030 kuhusu malengo ya maendeleo endelevu?

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa malengo yote 17 ya maendeleo endelevu ya dunia ni muhimu kwa nchi yetu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mchanganuo wa kina wa jinsi kila lengo lilivyotekelezwa na kiwango cha utekelezaji (asilimia) kwa kila lengo. Aidha, tunaitaka Serikali kutoa majibu ya ziada na ya kipekee ya namna ilivyotekeleza lengo la 16 la **Kuwa na Taasisi imara ili kuwa na Haki na Amani.**

**Mheshimiwa Spika**, Tumeweka msisitizo katika lengo hili kwa kuwa haki inaleta amani na amani ni tunda la Maendeleo. Kwa hali ilivyo sasa hapa nchini, kuna dalili zote kwamba taasisi zetu haziko imara jambo ambalo linafifisha jitihda za kuwa na haki na amani katika nchi yetu. Kama taasisi zetu hasa za kutoa haki zingekuwa imara ni dhahiri Zanzibar kusingekuwa na hitajio la uchaguzi wa marudio. Jambo hilo linatia mashaka kama Tanzania tutaweza kukidhi malengo endelevu ya maendeleo kama Agenda 2030 ya Dunia inavyohitaji.

#### 4. UCHUMI WA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika**, kwa nchi yoyote Duniani ambayo uchumi wake unaendelea kukua ni dhahiri kuwa sekta ya viwanda inakua kwa kasi inayoridhisha na sekta hiyo ina uhusiano wa moja kwa moja na sekta zinazotoa malighafi kwa sekta ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kuwa na uchumi wa kipato cha kati kupitia ujenzi wa uchumi wa viwanda ni lazima kama nchi iwe na malengo ambayo yako wazi kuhusu aina ya sekta zitakazowekezwa ili iwe chachu ya kututoa hapa tulipokwama kwa kipindi chote. Ili malengo yawe wazi ni lazima kuangalia mazingira yetu ya ndani na mazingira ya nje ambayo kwa njia moja au nyingine yana uhusiano wa moja kwa moja na uzalishaji wa viwandani.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaposema malengo yaende sambamba na mkakati mzuri wa utekelezaji, ni kwamba utakapo chagua viwanda viwe katika sekta kama: bidhaa za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, kemikali, misitu na/au huduma; nk. Ni lazima ujenzi wa viwanda kufuatana na sekta tajwa hapo juu uhitaji upembuzi yakinifu wa hali ya juu hadi kufikia maamuzi ya wapi viwanda hivyo vijengwe kwa kulingana na kiwango cha rasilimali zilizopo na kiwanda kitakachojengwa ni kwa muda gani kitaweza kurudisha mtaji na ajira kiasi gani zitazalishwa. Na pia kuangalia nchi za jirani zina kiwanda kama hicho na uwezo wake wa kuzalisha bidhaa na ubora wa bidhaa zake ukoje (uhimili wa ushindani wa bidhaa). Je, aina ya teknolojia itakayotumika kuzalisha bidhaa itaweza kutumiwa na wananchi wetu (rasilimali watu ya hapa hapa ndani ya nchi) au kitakuwa tegemezi kwa wataalamu wa nje?

**Mheshimiwa Spika,** Mojawapo ya malengo ni kuhakikisha yanakidhi mahitaji ya ndani kwa bidhaa zinazozalishwa, kuwa soko la malighafi ya bidhaa za kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini kwa kuwa nguzo kuu ya mnyororo wa thamani, kwa kuubadili mfumo wa uchumi ambao ulikuwa tegemezi kwa sekta za kilimo, madini na huduma na kuwa uchumi tegemezi kwa sekta ya viwanda. Pia kuwezesha bidhaa zinazozalishwa kuwa shindani katika soko la Afrika ya Mashariki na soko la nchi za Kusini mwa Afrika<sup>1</sup>.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema ili kuwa kweli nchi yenye uchumi wa viwanda na hivyo kupelekea kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati, tuna hitaji mkakati mzuri na utekelezaji wake wa kutufikisha huko na sio matamania na mahubiri tu, kama yanavyotolewa na viongozi wetu. Viwanda siyo tu vinakuza uchumi kwa kuongezea bidhaa thamani bali pia vinatengeneza ajira nyingi kwa haraka na kwa sekta nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa mwaka huu wa bajeti 2016/17 ni mwaka wa kwanza kwa awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa 2025, japokuwa ni mwendelezo wa awamu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo, hivyo basi ni muhimu kuangalia uwekezaji ambao tayari umefanyika katika sekta nzima ya uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya China wameanzisha kituo cha Biashara kwa ajili ya bidhaa toka China (Kurasini Logistic Center) ambapo hadi sasa Tanzania imekwishatoa **shilingi 65,279,464,100/-** ambazo ni

---

<sup>1</sup> Col. (Rtd) J. L. Simbakalia, R. Eng. (T)- Progress in industrial development – targets and goals, achievements, challenges and the way forward

sawa na Asilimia 72% ya fedha zilizotakiwa kutolewa na Serikali kwa ajili ya fidia kwa wakazi wa kurasini.

**Mheshimiwa Spika**, dhana nzima ya uwekezaji wa pamoja katika kuanzisha Kituo hiki, kwamba bidhaa mbalimbali toka China zitakuwa zinaletwa hapo na wafanyabiashara wa nchi za Afrika ya mashariki na zile za Kusini mwa Afrika badala ya kwenda China kufuata bidhaa, basi watakuwa wanapata bidhaa zote Dar es Salaam. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba uwekezaji uliokwishafanywa na unaoendelea kufanywa katika kuanzisha kituo hicho ni dhahiri kwamba unapingana na dhana nzima ya awamu ya pili ya Mpango wa maendeleo wa 2025 kuwa ni kuifanya nchi kuwa na uchumi wa viwanda.

#### 4.1. SEKTA YA NYUMBA NA UKUAJI WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa mwaka 2011, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mhe. Freeman Mbowe (Mb) akiwasilisha Bungeni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, alipendekeza kuwa pamoja na mambo mengine kuna ulazima kama taifa kuwa na mamlaka udhibiti wa sekta ya nyumba (Real Estate Regulatory Authority) itakayokuwa na jukumu la kusimamia sekta ya nyumba nchini hasa majengo makubwa ili kuwa chanzo cha mapato ya serikali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pendekezo hilo kutolewa wakati huo serikali wakati wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imependekeza mwaka ujao wa fedha 2016/2017 imeahidi kuleta Bungeni muswada wa sheria ambayo itasimamia sekta ya nyumba nchini. Ni msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa pendekezo hili limechelewa sana. Kama serikali ingelitekeleza jambo hili mapema, serikali ingelipata chanzo cha mapato.

**Mheshimiwa Spika**, majirani zetu wa Kenya ndani ya jumuiya ya Afrika ya Mashariki, sekta ya nyumba imechangia pato la taifa kwa 10.6% sekta hiyo ikiwa ya nne katika kuchangia katika uchumi wa nchi hiyo. Aidha athari za kuanguka kwa bei ya mafuta duniani haijaathiri uchumi wa Dubai kwa sababu ya kuwa na mafanikio makubwa katika sekta ya nyumba.

**Mheshimiwa Spika**, tamwimu zinaonesha kuwa Tanzania kuna uhitaji wa nyumba 200,000 kila mwaka na uhaba wa nyumba milioni 3. Hii ni kutokana na ongezeko la kasi la idadi ya watu nchini pamoja na uhitaji wa nyumba zenye hadhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa serikali haijawa na mkakati madhubuti wa kuhakikisha tunatumia fursa ya sekta ya makazi kukuza uchumi wa nchi yetu kama ambavyo mataifa mengine yamepiga hatua kubwa kwa kutumia fursa hiyo.



## 4.2 KODI YA MAJENGO (PROPERTY TAX)

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi kodi ya majengo ilikuwa ikikusanywa na halmashauri, lakini kwa sasa serikali imeamua kodi hiyo ikusanywe na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupelekwa Hazina. Agizo hili litaathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri zetu nchini kwa kuwa kodi ya majengo ilikuwa chanzo kikuu cha mapato ya Halmashauri hasa za Miji, Manispaa na Majiji.

**Mheshimiwa Spika**, ieleweke kuwa kama fedha zitakusanywa na Hazina na kama utaratibu wa kutoa fedha hizo kwenda Halmashauri utaendelea kama ilivyo sasa ambapo fedha za maendeleo kutoka Serikali Kuu zinachelewa kupelekwa kwenye Halmashauri basi tusitegemee kuwa fedha za kodi ya majengo zitanuifaisha tena Halmashauri zetu.

Dhana hii ni kutokana na ukweli halisi ambao upo kwenye kodi ya ardhi ambayo ilikuwa inakusanywa na Halmashauri na kuwasilishwa Wizara ya Ardhi ilionyesha wazi kuwa ikishafika wizarani ilikuwa vigumu sana kurejeshwa kwenye Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, Hii ni kutokana na sababu kuwa serikali mara nyingi imekuwa ikipeleka fedha Halmashauri katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa serikali itafikiria upya uamuzi huu ambao utapunguza sana mapato ya Halmashauri zetu na kuzifanya kushindwa kutoa huduma kwa wananchi wake.

## 4.3 SEKTA YA UTALII

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya utalii ni sekta ambayo inachangia fedha za kigeni katika sekta nzima ya uchumi (**foreign exchange earner**), kwa kuwa na watalii milioni moja wanaoachangia asilimia 17.7 ya pato la Taifa (GDP). Kwa mujibu wa takwimu za nchi nzuri duniani<sup>2</sup> ni kwamba; Tanzania ni namba 8 kati ya mataifa 20 yenye vivutio vizuri na vingi Duniani kwa ajili ya watalii. Lakini kuwa na vivutio vingi sio sababu ya kuwa na watalii wengi, ila sababu kubwa ni jinsi gani unajitangaza na unawavutia vipi watalii? Takwimu zinaonesha kuwa Ufaransa ndiyo nchi inayoongoza kuwa na watalii milioni 83.77 kwa mwaka wakati katika zile nchi 20 haimo. Afrika ya Kusini inapokea watalii 9,616,964<sup>3</sup> kwa mwaka,

<sup>2</sup> <https://www.buzzfeed.com/travelguru/the-20-most-beautiful-countries-in-the-world>

<sup>3</sup> Department of Tourism-Republic of South Africa.

lakini katika orodha inachukua namba 1, Kenya ambayo ilikuwa imefikisha watalii milioni 1.7 kabla ya tishio la ugaidi, sasa inatarajia watalii milioni 1.6, Uganda inapokea watalii 1,266,000 kwa mwaka, Zimbabwe inapokea watalii 1,905,000 na Msumbiji 1,661,000<sup>4</sup>

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kama tutaweza kuongeza idadi ya watalii hata kufikia milioni 5 kwa mwaka ni dhahiri uchumi wa Tanzania unaweza kuendeshwa na sekta ya utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Ili Tanzania iweze kupata watalii milioni 5 kwa mwaka, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba Serikali iimarisha kwanza usafiri wa anga. Hali ilivyo sasa, watalii wanapata tabu sana kufika Tanzania kutokana na gharama kubwa inayosababishwa na kutokuwepo usafiri wa uhakika wa ndege.

Tunashauri kwamba Serikali iweke mkakati mahususi wa kuwashawishi marafiki zetu wa China ili shirika lao la ndege lianzishe safari za kuja Tanzania, na vile vile mashirika ya ndege toka Marekani kuwa na safari za Tanzania kila wiki. Pili, tozo katika viwanja vyetu vya ndege zipunguzwe ili kuvutia watalii. Tatu huduma zinazotolewa kwa watalii huko mbugani ziboreshwe na kuwa na kiwango cha kimataifa ili kuwavutia watalii zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na misimamo ya Serikali isiyokuwa ya kibiashara ni kwamba utalii kuwa na faida sana inategemea na idadi ya watalii wanaoingia, hivyo kama Serikali itakubali kuwa kipindi kisichokuwa cha msimu wa utalii ni vyema bei zikashuka ili idadi ya watalii na siku za kukaa nchini iongezeke. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuja kwa watalii kuna wanufaisha watu wengi sana mbali ya Serikali kupata mgawo wake, ni muda mwafaka sasa Serikali kuwa-**“flexible”** ili kuwa kibiashara zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaitaka Serikali kutumia mfano wa jirani zetu Kenya, ambapo Rais Uhuru Kenyatta amefuta tozo za kutua kwa ndege zote za kukodi zitakazokuwa zinaleta watalii nchini Kenya<sup>5</sup>.

## 5. VITUO VYA KUUZA UTALII WA TANZANIA NJE

**Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Utalii imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa muda mfupi wakati wa maonyesho mbalimbali ya utalii yanayofanyika nje ya nchi. Ili kuwe na ujio endelevu wa watalii nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Serikali iweke vituo vya utangazaji wa utalii wetu katika balozi zetu katika nchi za Marekani, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Italia,

<sup>4</sup> <http://www.data.worldbank.org/indicators/ST.INT.AR.V>

<sup>5</sup> Taarifa hii ni kwa mujibu wa Kaimu Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Utalii ya Kenya.

Uchina, Japani, Canada na nchi za Scandinavia na kuwe na watumishi maalumu watakaoajiriwa katika vituo hivyo kwa kazi maalum ya kuhakikisha kuwa wanatangaza vivutio vyetu na kuongeza idadi ya watalii wanaokuja hapa nchini. Mkakati huo ukifanikiwa ni dhahiri kwa mwaka mmoja tunaweza kupokea watalii zaidi ya milioni tano.

**Mheshimiwa Spika**, fursa hii si kila mtu anaweza kuiona, hivyo ni muda muafaka kuwashawishi wachina wawekeze katika hoteli za kitalii, badala ya wawekezaji hao kushindana na wataanzania katika maduka ya vifaa vya ujenzi pekee. Kwa njia hii tutaweza kuvuta soko la watalii wengi toka China.

## 6.0 SERIKALI YA HAPA KAZI TU, IMELETA BAJETI HEWA BUNGENI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ni wajibu wa Bunge kupanga na kuidhinisha mapato na matumizi ya serikali kila mwaka wa fedha .Hii ni kwa mujibu wa ibara ya 137(1)'Rais atatoa maagizo kwa watu wanaohusika kwamba watengeneze na kuwasilisha kwenye Bunge katika kila mwaka wa fedha wa Serikali, makadirio ya **'Mapato na Matumizi'** ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kipindi cha mwaka wa fedha unaofuata'

**Mheshimiwa Spika**, nasikitika kusema kuwa katika mwaka huu wa fedha 2016/17 serikali imewasilisha bajeti hewa hapa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, ninasema kuwa serikali hii imeleta bajeti hewa hapa Bungeni na nitathibitisha maoni yangu haya kama ifuatavyo;

1. Kwa mujibu wa Kitabu cha Mapato ya serikali katika mwaka huu wa fedha **volume 1 'Financial Statements and Revenue estimates'** for the year 1st July ,2016 to 30th June 2017 kilicholetwa hapa Bungeni kinaonyesha kuwa mapato yote ya serikali yaani mapato ya kodi, yasiyokuwa ya kodi ,mikopo na misaada ya kibajeti itakuwa jumla ya shilingi **Trilioni 22.063**.

i. **Mheshimiwa Spika**, upatikananji wa mapato hayo ni kama ifuatavyo Mapato yatokanayo na kodi na tozo mbalimbali ni shilingi **Trilioni 17.797**

ii. Mapato yasiyokuwa ya kodi ni shilingi **Bilioni 665.664**

iii. Mikopo na misaada ya kibajeti ni shilingi **Trilioni 3.600**

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu Waheshimiwa Wabunge wakatambua kwamba Serikali hii haijaonyesha chanzo kingine kipya cha mapato ambacho hakijathibitishwa na au kupitishwa na Bunge hili kwa mujibu wa katiba na

ijulikane pia kuwa Bunge halipitishi kitabu cha hotuba ya waziri bali hupitisha mafungu yaliyopo kwenye vitabu vya bajeti ya serikali.

2. Kwa mujibu wa kitabu cha matumizi ya waida ,volume II Estimates of Public Expenditure Consolidated Fund Services for the year 1<sup>st</sup> July ,2016 to 30<sup>th</sup> June, 2017 na kitabu cha Maendeleo, Volume IV Public Expenditure Estimates Development Votes (part A) kama vilivyowasilishwa Bungeni , tayari bunge limeshaidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi **Trilioni 23.847**

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

i. Fedha za Matumizi ya Kawaida (Volume II) **shilingi 13,336,042,030,510**

ii. Fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (Volume IV) **shilingi 10,511,945,288,575**

3. Ukichukua kitabu cha Mapato ya Serikali (*Revenue Book Volume I*) utaona kuwa jumla ya mapato yote ya serikali ni shilingi **Trilioni 22.063** , ila serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi **Trilioni 23.847** ambacho ni kiasi tofauti na Mapato ambayo serikali imepanga kukusanya na tofauti yake ni kuwa kuna nakisi ya shilingi **Trilioni 1.783** jambo ambalo linaifanya bajeti hii kukosa uhalali kwani nakisi hii ni kubwa sana.

4. Kwa mujibu wa maelezo ya waziri wa fedha 'Mapendekezo ya kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 kwenye mkutano wa wabunge wote katika ukumbi wa JNICC' mnamo tarehe 06 Aprili, 2016 pamoja na maelezo ya hotuba yake aliyoyatoa hapa Bungeni uk. 91 ameendelea kulidanganya Bunge na Dunia kuwa katika mwaka huu wa fedha serikali ina bajeti ya kiasi cha shilingi **Trilioni 29.539**

5. Hotuba ya waziri wa fedha katika ukurasa wa 92 'Mfumo wa Bajeti wa Mwaka 2016/17' inaonyesha kuwa kiasi cha shilingi trilioni 7.475 ni mikopo ya ndani yenye masharti ya kibiashara. Fedha hizi kwenye kitabu cha mapato hazipo na pia hazionekani zitakopwa kutoka Benki gani kama ambavyo mikopo ya nje yote imeonyeshwa kwenye kitabu cha mapato na hata kwenye kitabu cha miradi ya maendeleo hazionekani kwenye kutekeleza mradi wowote ule na hivyo ni sahihi kusema kuwa ni fedha hewa , maana hazina hata kasma yake na Bunge hili tunapitisha kasma .

6. Hotuba ya waziri wa fedha uk.58 anasema kuwa moja ya chanzo chake cha mapato ni pamoja na kurekebisha sheria ya Kodi ya Mapato SURA 332 (i)'kuondoa msamaha wa kodi ya mapato kwenye malipo ya kiinua mgongo kinacholipwa kwa wabunge kila mwisho wa muhula wa miaka mitano.'

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni**, inataka kupata majibu ya kina kuhusu mambo yafuatayo;

i. Bunge linapitisha takwimu zipi hasa? Ni kitabu cha hotuba ya waziri au ni vitabu vya mapato na matumizi pamoja na kile cha Miradi ya maendeleo?

ii. Fedha ambazo waziri kwenye hotuba yake anasema kuwa ni mikopo ya ndani ya masharti ya kibiashara, zinakopwa ili kugharimia miradi ipi? Kwani tayari kitabu cha miradi ya maendeleo VOLUME IV kimeshataja miradi yote na kiasi cha fedha ambazo kila mradi utatumia. Hii miradi inayosemwa kuwa fedha itakopwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni miradi ipi hiyo? Mbona haijapitishwa na bunge au ni miradi hewa?

iii. Waziri wa fedha anaposema kuwa fedha za matumizi ya kawaida ni shilingi **Trilioni 17.719** na hapo hapo anasema kuwa tunakwenda kulipa deni la taifa kiasi cha shilingi **trillion 8**, mbona hizi fedha hazipo kwenye kitabu ambacho kinapitishwa na Bunge? Kitabu cha matumizi ya kawaida VOLUME IV?

iv. Kwa kuwa CAG anakagua kasma zilizopo kwenye vitabu yaani VOLUME IV na VOLUME II, katika bajeti hii atakagua kasma ipi? maana fedha za kulipia deni la taifa hazipo kwenye kitabu cha VOLUME II na hata mikopo yenye masharti ya kibiashara inayosemwa itakopwa haipo kwenye **Revenue Book**

v. Huu mkanganyiko wa vitabu vya serikali moja imesababishwa na nini au kuna mikopo na miradi hewa? Ni kwanini kitabu cha mapato (revenue book) kinaonyesha mapato madogo kuliko kiwango cha matumizi?

vi. Kuingiza malipo ya kiinua mgongo cha wabunge ambacho kinatakiwa kulipwa mwaka 2020 kwa mujibu wa sheria na kuwa chanzo cha mapato katika mwaka huu wa fedha 2016/17 hiki si chanzo hewa? Nasema hivi kwa kuwa, kila mwaka tutakuwa tukipitisha bajeti na hiki kilipaswa kuwa chanzo ifikapo mwaka 2020 ambapo ndio kiinua mgongo hiki kinalipwa na ndio kingekuwa chanzo cha mapato au serikali imepanga kulipa kiinua mgongo hicho kila mwaka wa fedha?

Mwisho **Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, tunaitaka serikali iwasilishe Vitabu vyenye kumbukumbu na takwimu sahihi kabla ya kulitaka Bunge hili kujadili bajeti hii na kuamua kuipitisha au kuikataa, la sivyo Bunge litakuwa halitimizi wajibu wake kikamilifu kwa mujibu wa katiba ya Nchi yetu.

## 7. WIZARA YA FEDHA NA JUKUMU LA UTEKELEZAJI MPANGO WA KWANZA WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2011/12-2015/16

**Mheshimiwa Spika**, Mpango huu ni wa kwanza kati ya mipango mitatu ya miaka mitano mitano inayotumika kama chombo katika dhamira ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa maendeleo wa miaka ishirini na mitano (Tanzania Development vision(TDV)-2025). Malengo yakiwa ni Tanzania iwe ya kipato cha kati ifikapo 2025 ambayo pamoja na mambo mengine litakuwa taifa lenye:

- i) Kiwango cha juu cha mapinduzi ya viwanda
- ii) Ushindani na hali nzuri/bora ya maisha kwa wananchi wake
- iii) Utawala wa sheria
- iv) Jamii ya wasomi waliobobea

Vipaumbele vya msingi (Core Priorities) katika mpango huo ni:

- i) Miundombinu / Infrastructure
- ii) Viwanda / industry
- iii) Maendeleo ya rasilimali watu /human capital development
- iv) Nishati

**Mheshimiwa Spika**, tuangalie mafanikio ya wizara ya fedha katika utekelezaji wa jukumu lake la kusimamia utekelezaji wa mpango wa miaka mitano 2011/12-2015/16.

1) **Reli**- mpango ulipanga kukarabati **KM 2,707** ya reli ya kati, imefanikiwa kukarabati **km 150** tu za Reli

2) **Barabara** – Kujenga na kukarabati **km 5,204** za barabara. Zimejengwa **km 2,775**

3) **Nishati**- Ongeza uzalishaji wa umeme kufikia 2,780 **MW**. Sasa hivi tunazalisha **MW 1,461**

4) **Kilimo** - Ukuaji wa mwaka **kwa 6%**, ukuaji kwa sasa 3.2% (ukuaji huu ni wa kipindi chote toka tupate uhuru...).Kiwango cha umwagiliaji toka **345,690 – 1,000,000**. Matarajio yalikuwa ni kuongeza eneo jipya la umwagiliaji lenye ukubwa wa **hekari 645,690**. Mafanikio ni nyongeza ya hekari **115,656** tu!

5) Maendeleo ya viwanda na uzalishaji – **kukua kwa 11%**. Mafanikio ni **ukuaji wa 6.6%**

6) **Elimu** - Nyongeza kada ya wasomi wa kiwango cha juu toka 2.7% mpaka 4.3% ifikapo 2015. **Idadi imepungua mpaka 2.5%**. Halikadhalika kuongeza kada ya wasomi wa kiwango cha kati toka 13.6% mpaka 17.8% ifikapo 2015. Imeongezeka kwa 1% tu kufikia 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Hakuna ubishi kwamba tukiwa tunaelekea katika mpango wa pili wa miaka mitano, wizara ya fedha imeshindwa kutekeleza wajibu huu kikamilifu, hali hii inatia mashaka ufanisi wa utekelezaji wa mpango wa pili, wakati mpango wa kwanza umeisha kwa kusuasua!

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali ilieleze Bunge hili tukufu, Ni kwa namna gani serikali imejipanga kuweza kufidia ombwe hili! Ili miaka tisa ijayo Tanzania liwe Taifa lenye mapinduzi ya viwanda ya hali ya juu, hali bora ya maisha kwa wananchi wake, utawala bora na Taifa **lenye wasomi waliobobea (Rejea taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya jamii)** ambayo ilitamka bayana kwamba hali ya elimu nchini ni hatari kwa usalama wa Taifa. Ninukuu maneno ya kamati 'Taifa letu limejenga mfumo wa elimu ambayo haikidhi DIRA na Mahitaji ya Nchi'<sup>6</sup>.

## 7.1 UPATIKANAJI FEDHA KUTOKA HAZINA

**a) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi:** Hadi kufikia Machi 2016, wizara ilikuwa imepokea shilingi 660,333,375,957/- kati ya shilingi 816,080,198,000 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya Wizara, mishahara ilikuwa 52%, matumizi mengineyo ilikuwa 47% na kwa upande wa bajeti ya maendeleo ni 1% tu.<sup>7</sup>

**b) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:** kwa miradi ya maendeleo iliidhinishwa shilingi bilioni 232.1. Mpaka Februari, 2016 Wizara ilipokea shilingi bilioni 40 tu, sawa na asilimia 17.2 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

**c) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:** Bajeti ya maendeleo iliyotengwa 2015/16 ni bilioni 440.6, mpaka mwezi machi ikiwa ni robo ya tatu ya mwaka hakuna fungu hata moja ambalo wizara hiyo ilikuwa imepata zilizoidhinishwa na Bunge kwa angalau 50%.

<sup>6</sup> Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 uk.17

<sup>7</sup> Taafira ya Kamati ya Bunge ya mambo ya nje, ulinzi n usalama, 2016/17, pg. 8



Halikadhalika Fungu 52 – Idara kuu Afya hadi kufikia tarehe 31 March 2016 kiasi cha fedha kilichopokelewa ni 31% tu ya Bajeti , halikadhalika fungu 53 kwa Idara Kuu ya Maendeleo ya jamii jinsia na watoto.

**d) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi:** Katika kipindi cha mwaka 2015/16 wizara ilitengewa jumla ya shilingi 213,079,803,000/- kati ya fedha hizo 32,713,073,000 ilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2016, fedha za maendeleo zilizokuwa zimepatikana ni bilioni 5.1 ambazo ni sawa na 15.9% tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, ikubukwe kwamba; Mpango wa kwanza wa miaka mitano (FYDP 1) uliweka malengo ya kibajeti katika sekta ya kilimo (miaka mitatu ya mwanzo) ya shilingi za kitanzania Bilioni 2,710.65 (Trillion 2.7). (Ambayo ingewezesha kilimo kukua toka 3.2% ya sasa mpaka 6%). **Fedha iliyokuja kutolewa kwa kipindi chote hicho ni shilingi 250.12 billioni sawa na 9.23% ya mahitaji.**

**e) Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:** Wizara iliidhinishwa shilingi 511,525,227,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka, yaani Machi 2016 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 316,402,868,828.00 sawa na 68%. Kuhusu bajeti ya maendeleo, wizara imepokea jumla ya shilingi 360,922,754,359.61 sawa na 61.9% ya fedha iliyoidhinishwa 582,670,597,884.49.

Bodi ya mkopo ambayo ni sehemu muhimu sana ya wizara hii kupitia fungu 46 iliidhinishwa shilingi 418,300,000,000 kwa ajili ya Mradi Namba PT 4340 uliojulikana kama Higher Education Students Loans ambao ni mradi wa kutoa Mikopo. Hadi kufikia tarehe 15 Machi ,2016 Bodi ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 245 sawa na asilimia 55.9% tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge . Fedha hizo zingetolewa zote kwa 100% wanafunzi wengi zaidi wangepata mikopo.

**f) Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:** Wizara hii ni miongoni mwa wizara (chache sana) zilizopata fedha zilizopangwa katika bajeti na zaidi, hususan katika sekta ya ujenzi (barabara). Katika mwaka wa fedha 2015/16. Sekta hii ilitengewa **shilingi 883,832,338,500/-** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, fedha za ndani kutoka mfuko mkuu wa hazina wa serikali ni **shilingi 191,619,568,500** na **shilingi 85,572,770,000** zilikuwa fedha za nje. Kwa upande wa fedha za mfuko wa barabara zilitengwa shilingi 606,640,000,000.

Hadi Aprili, 2016 fedha zilizotolewa ni shilingi 1.080,804,942,594. Kati ya fedha hizo **shilingi 607,350,007,730** ni fedha za ndani kutoka mfuko mkuu wa hazina/serikali (Ongezeko la **shilingi 415,730,439,230**) ,shilingi 149,502,934,864 ni fedha za nje na

shilingi 323,952,000,000 ni fedha za mfuko wa barabara. Sehemu kubwa ya fedha za ndani zilizotolewa imetumika kulipa madeni ya Makandarasi na wahandisi washauri wa miradi ya barabara.<sup>8</sup>

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya mabilioni yanayotumika kujenga barabara na kulipa madeni yenye riba kubwa sana kutokana na serikali kuchelewa kulipa madeni ya barabara, wakati kamati ikikagua miradi mbali mbali ya barabara nchini imebaini kuwepo kwa changamoto ya kuharibika kwa barabara mapema mara baada ya barabara kujengwa!<sup>9</sup> Licha ya visingizio vilivyotolewa vya uharibifu huo, sababu hizo hazina mashiko /msingi wa kuhalalisha upotevu huo wa mabilioni ya fedha. Barabara zote hizi lazima zifanyiwe ukaguzi wa kitaalam ili kujiridhisha na thamani ya fedha na kazi iliyofanywa. Hii inatokana na ukweli kwamba kwa muda mrefu sana (tokea kipindi ambacho Rais alikuwa waziri wa miundombinu) Wizara hii imekuwa ikihusishwa na uchakachujaji katika ujenzi wa barabara.

**g) Wizara ya Nishati na Madini:** Wizara hii nayo ilipata fedha kuliko kiasi kilichotengwa kwenye bajeti. Katika mwaka wa fedha 2015/16. Wizara iliidhinishiwa na Bunge Jumla ya Shilingi bilioni 642.12. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 502.30 sawa na 78% ya bajeti yote ilikuwa kwa miradi ya maendeleo na shilingi 139.82 sawa na 22% zikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hata hivyo bajeti iliongezeka kutoka **bilioni 642.12 mpaka bilioni 762.12 (Nyongeza ya bilioni 120.12)**

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya nyongeza hiyo, miradi ya REA inayogharimiwa na fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini ambao vyanzo vyake vya mapato ni pamoja na tozo ya shilingi 100 katika kila lita ya mafuta ya petrol na Dizeli; na shilingi 150 katika kila lita ya mafuta ya taa bado inasua sua. Hii inatokana na fedha ambazo wananchi wanatozwa katika mafuta tajwa hapo juu kwa makusudi ya kupeleka huduma ya UMEME vijijini kutumika kwa matumizi mengine yasiyokusudiwa! Licha ya fedha hizo kuwa zimewekewa wigo kisheria (Ring Fenced). Takwimu zinaonyesha kwamba tangu tozo hizi zilipoanza kukusanywa Julai 2013 mpaka Machi 2016, fedha zilizopatikana toka kwenye tozo ya petrol na Dizeli ni **shilingi bilioni 493.8**, Mafuta ya taa **shilingi bilioni 448.5** na **shilingi bilioni 45.4** kutoka kwenye 'Custom Processing Fee'. Licha ya makusanyo ya

<sup>8</sup> Hotuba wa waziri wa Ujenzi, uchukuzi na mawasiliano, Prof. Makame Mabarawa (MB) akiwasilisha Bungeni Mpango na Makadirio ya mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2016/17, uk. 8

<sup>9</sup> Taarifa ya kamati ya kudumu ya Bunge ya miundombinu, Taafifa kuhusu utekelezaji wa Bajetui ya wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa mwaka wa fedha wa 2015/16: Pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/17, uk 15

**shilingi bilioni 987.7** (tozo ya petrol na dizeli) kiasi kilichopelekwa kwenye umeme vijijini mpaka mwezi April 2016 ni **shilingi bilioni 366.95 tu** sawa na **37.15%** ya makusanyo yote. Katika mazingira kama haya, kamwe serikali ya CCM haiwezikujitapa imetekeleza wajibu wake kikamilifu. Kwa lugha nyepesi imewaibia mamilioni ya wananchi wanaoishi vijijini ambao mfuko huu uliundwa mahususi kwa ajili ya kusogeza huduma za umeme kwao. Ikumbukwe hii fedha sio ya hisani bali ni fedha ya nyongeza iliyoongezwa kwa kila lita inayonunuliwa na wananchi kwenye mafuta ya taa, petrol au dizeli.

**h) Wizara ya Maliasili na Utalii:** Katika mwaka wa fedha 2015/16 wizara ya maliasili na utalii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 66,313,757,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida . Kati ya fedha hizo shilingi 45,235,955,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mishahara na shilingi 21,077,802,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Mpaka Machi 2016, wizara ilipokea 43,487,894,012.34 sawa na 65.5% ya bajeti iliyoidhinishwa ambapo 32,714,043,166.18 ikiwa ni mishahara na 10,773,850,856 ni kwa matumizi mengineyo. Fedha iliyoidhinishwa kwa miradi ya maendeleo ni 7,709,150,000/= . Fedha zilizotolewa ni bilioni 1 na yenyewe ni fedha ya NJE sawa na asilimia 12.9 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kutokana na hali hiyo katika miradi 10 ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa hakuna hata mradi mmoja uliotekelwa kwa ufanisi.<sup>10</sup>

**i) Wizara ya Viwanda na Biashara:** Katika mwaka 2015/16 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 87,470,349,000 ambapo 52,082,968,000 zilikuwa ni matumizi ya kawaida (mishahara na matumizi mengineyo) na shilingi 35,387,381,000/- za matumizi ya maendeleo (shilingi 26,588,200,000 ni fedha za ndani na shilingi 8,799,181,000 ni fedha za nje). Mpaka mwezi Machi 2016 Wizara ilipokea 29,752,487,320/- sawa na 34% ya fedha iliyotengwa. Kati ya fedha hiyo fedha za maendeleo zilizotolewa ni 1,602,111,662 tu ambayo ni fedha za nje! Kwa lugha nyingine fedha za ndani za maendeleo zilizotoka ni 0%, na fedha ya nje iliyotoka ni 18% tu!<sup>11</sup>

## **j) Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii, licha umuhimu wake mkubwa katika uchumi wa Tanzania katika mwaka wa fedha 2015/16, pamoja na mafungu yake nane (8) iliidhinishwa kutumia jumla ya shilingi 7,326,769,737,771. Kati ya fedha hizo shilingi

<sup>10</sup> Taarifa ya kamati ya kudumu ya Bunge yaa Maliasili na Utalii, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2015/16 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017, u.3 na 4.

<sup>11</sup> Kiambatanisho cha taarifa ya utoaji fedha za matumizi ya maendeleo kwa kipindi cha mwezi Julai 2015 hadi Machi 2016.

72,659,909,000 kwa ajili ya Mishahara (PE) Shilingi 7,218,508,850,128 kwa ajili ya Matumizi mengineyo (kati ya hizo shilingi 6,381,430,000,000 ni kwa ajili ya deni la Taifa).

Kwa upande wa fedha za maendeleo fedha zilizoidhinishwa ni shilingi 1,022,924,905,000 ambapo fedha za ndani zilikuwa shilingi 651,541,992,000/- na fedha za nje 371,382,913,000. Mpaka mwezi machi 2016 wizara ilipokea fedha za maendeleo **shilingi 25,908,256,142**, sawa na **3% tu** ya fedha zote zilizoidhinishwa!

## **8. MWENENDO WA MAPATO YA NDANI NA MKANGANYIKO WA TAARIFA ZA SERIKALI YA HAPA KAZI TU**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka huu wa fedha, na hususan miezi ya karibuni mwenendo wa mapato umekuwa sio wa kuridhisha sana! Kodi ya ushuru wa forodha haikufikia lengo na kwa kadiri siku zinavyozidi kwenda hali inazidi kuwa mbaya! Idadi ya meli zilizohudumiwa **Januari - Aprili 2015** (TPA- Kontena) **zilikuwa 41** ukilinganisha na **meli 16 tu** zilizohudumiwa **Januari- Aprili 2016**. Pungufu ya meli 25, **badiliko la - 61%**. Halikadhalika kwa Meli ya Mzigo Mchanganyiko **'General Cargo' meli zilizohudumiwa Jan- April 2015 zilikuwa 53 ukilinganisha na meli zilizohudumiwa Jan – April 2016 ambazo ni 33 tu. Pungufu ya meli 20 sawa na badiliko la -37%**

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo ya waziri wa fedha na Mipango kwenye kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2015/16 kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 na mwelekeo hadi juni 2016<sup>12</sup> anaeleza sababu za upungufu kuwa ni ;

- i) kupungua kwa uingizaji wa mizigo kutoka nje kutokana na hofu ya wafanya biashara katika kipindi cha uchaguzi
- ii) Udanganyifu uliokuwa unafanywa na wafanyabiashara kwa kukwepa kodi ya ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazopitia bandarini
- iii) kushuka kwa bei ya bidhaa katika soko la dunia
- iv) Na kwa upande wa kodi ya ongezeko la thamani upungufu umetokana na marejesho ya VAT (VAT inputs) kuwa kubwa kutokana na uwekezaji katika viwanda vya sementi pamoja na kupungua kwa mahitaji.
- v) Halikadhalika tatizo la kutoa/kuomba risiti za kielekroniki katika huduma mbalimbali.

---

<sup>12</sup>Mei 2016, uk 6

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wizara ya fedha ikitoa visingizio tajwa hapo juu, Mamlaka ya usimamizi wa Bandari Tanzania katika maelezo yake ya Takwimu za uingizaji mizigo katika Bandari ya Dar es salaam kwa kipindi cha 2013-2015 na kipindi cha Jan - April 2016 inaeleza sababu zilizopelekea kupungua kwa shehena ya mizigo kuwa ni:

i) Kudorora kwa uchumi wa china (Hii imeleta madhara katika bandari nyingi duniani)

ii) Hofu ya wateja kutokana na kuanzishwa kwa sheria ya VAT katika huduma zinazotolewa na mawakala kwenye mizigo ya nchi jirani (VAT on Transit GOODS) ambayo ni kinyume na sheria za kimataifa

iii) Tatizo la Single customs Territory. Mizigo inayopatikana kwa mfumo wa single customs territory unatozwa kodi kwa asilimia 100%, baadhi ya wafanyabiashara wanaona kupitisha mizigo Tanzania ni gharama kubwa.

iv) Kushuka kwa bei ya shaba duniani kumesababisha migodi mingi nchini Zambia na DRC kufungwa na hata ile inayofanya kazi uzalishaji umepungua.

v) Tozo la barabara (Road tolls) USD 16 kwa KM 100 hapa Tanzania ulikilinganisha na USD 8 kwa kila KM 100 zinazotozwa kwa nchi nyingine kwa magari yenye ekseli zaidi ya mbili.

vi) Muda mfupi (Short grace period) kwa mzigo wa mafuta wa nchi jirani. Tanzania ni siku 30 mzigo unatakiwa uwe umesafirishwa kabla ya kuwa localised tofauti na nchi nyingine ambazo zinawapa siku 60 hadi 70.

vii) Kuongezeka kwa Tozo kutokana na "Government Chemical Agencies" kutoa USD 1.00 kwa Tani badala ya USD 100 kwa " Bill of Lading" kwa bidhaa ambazo wanazikagua kama vile mbolea hivyo kuongezeka kutoka wastani wa USD 500 hadi USD 20,000 au Zaidi kutokana na ukubwa wa mzigo.

viii) Mfumo wa TANCIS wa TRA kutoruhusu kugawanywa kwa "Bill of Landing" ili kuruhusu kutoa mizigo ambayo haina tatizo panapokuwa na tatizo la mzigo mmoja badala ya mzigo wote kuzuiwa na kusababisha gharama za tozo za hifadhi kwa mteja ambazo sio lazima.

**Mheshimiwa spika,** Ni aibu kubwa, kwa vyombo viwili vya serikali kuzungumza lugha tofauti katika suala moja! Hiki ni kiashiria kwamba ama serikali hii haifanyi kazi kama timu...ama waziri wa fedha amedhamiria kulipotosha Bunge kwa kutoa sababu nyepesi huku zile za msingi akiziweka kibindoni (sijui kwa manufaa ya nani).

Kambi rasmi ya upinzani inaitaka Serikali ya CCM na Magufuli kutambua kwamba Tanzania sio kisiwa na kwamba Bandari ya Dar es salaam inakabiliwa na ushindani kutoka kwenye bandari za Mombasa (Kenya), Beira, Nacala na Maputo (Msumbiji) , Durban (Afrika ya Kusini ), Walvis Bay (Namibia) na Lobito (Angola) kama kuna vikwazo vyoyote vinavyoikwamisha bandari yetu na nchi kushindana katika soko la ushindani vikwazo husika lazima vishughulikiwe mara moja. Na wizara ya fedha iliyopewa jukumu kubwa la kusimamia uchumi wa Tanzania haiwezi kukwepa jukumu hili.

## 9. UNUNUZI WA NDEGE ZA ATCL KUNA HARUFU YA UFISADI!

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa kitabu cha fedha za Maendeleo Volume IV Part A fungu 62 kasma **4294** zimetengwa jumla ya shilingi **Bilioni 500** fedha za ndani kwa ajili ya kununua ndege za abiria kwa ajili ya shirika la Ndege la ATCL.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa hotuba ya waziri wa ujenzi ,uchukuzi na mawasiliano kifungu cha 185 alisema kuwa, nanukuu:-

*Kazi inayoendelea ni kukamilisha taratibu za ununuzi wa ndege mbili mwaka 2016. Wizara kwa kushirikiana na ATCL na wadau wengine imekwishaainisha ndege zinazofaa kununuliwa baada ya kukutana na wawakilishi wa viwanda vya ndege vya Boeing ya Marekani, Airbus ya Ufaransa, Embraer ya Brazil na Bombardier ya Canada. Ndege mbili za awali zinazotarajiwa kununuliwa zitakuwa na uwezo wa kubeba abiria 78 kila moja. Ndege ya tatu na ya nne zitakazonunuliwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 zitakuwa na uwezo wa kubeba abiria 155.*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Fedha na Mipango ni kwamba; serikali imeamua kununua ndege kutoka kiwanda cha Bombardier ya Canada na hii ni kutokana na ushauri ambao wizara ilipokea kutoka kwa wataalam wake .Aidha tuna taarifa kuwa ndege mbili za mwanzo ambazo zitanunuliwa sio mpya bali ni ndege ambazo tayari zilishatumika (kuukuu) **kama taarifa hizi ni za kweli , Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa kwa Bunge hili sababu za kina zilizopelekea serikali kwenda kununua ndege chakavu kinyume cha sheria ya manunuzi ya mwaka 2011.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa utafiti wetu kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tuliamua kutafuta taarifa za kina na za uhakika juu ya Bei za ndege mpya kwenye Viwanda ambavyo serikali ilisema kuwa iliwasiliana nao na kufanya nao mazungumzo yaani Viwanda vya ndege vya **Boeing** ya Marekani, **Airbus** ya Ufaransa, **Embraer** ya Brazil na **Bombardier** ya Canada na na kukuta bei za ndege mpya kuwa kama ifuatavyo;

**Kiwanda cha Bombardier.**

<b>Aina ya Ndege</b>	<b>Idadi ya Viti</b>	<b>Bei (Januari 2015) Mil USD</b>
Q 400	90	31.3
CRJ 700	70	41.0
CRJ 900	76-90	46.0
CRJ 1000	100	49.0
CS 100	100-133	71.8
CS 300	160	82.0

**Kiwanda cha Air Bus**

<b>Aina ya Ndege</b>	<b>Idadi ya Viti</b>	<b>Bei (January 2015) Milion USD</b>
A 320	100-240	97.0
A 318		74.3
A 340	260-400	284.6
A 350	270-350	351.9

**Kiwanda Cha Boeing**

<b>Aina ya Ndege</b>	<b>Idadi ya Viti</b>	<b>Bei (January 2015) Milion USD</b>
737-700	85-215	80.6
747-8	467	379.1
767-300 ER	181-375	197.1
787-8	250-290	224.6



**Mheshimiwa Spika**, kwa bei hizo hapo juu Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni tunataka kujua ni kwanini Serikali imeamua kununua ndege zenye uwezo wa kubeba abiria 78 wakati fedha zilizopitishwa na Bunge hili ni Bilioni 500 ambazo zingetosha kununua ndege mpya kubwa na za kubeba abiria wengi zaidi na hivyo kuwa na ufanisi na hata uwezo mkubwa wa kwenda safari za mbali. Au ndio yaleyale ya kutumia Mawakala ambao wanajiwekea asilimia kama ilivyokuwa huko nyuma katika ununuzi wa ndege ya Rais ?

Aidha kwa mujibu wa waziri wa Fedha alipokuwa anawasilisha mpango wa maendeleo hapa Bungeni alisema kuwa serikali imeamua kununua ndege mbili aina ya Q 400 mbili na CS 300 Moja.

Kutokana na uamuzi huo ni kuwa ndege aina ya Q400 mwaka jana ilikuwa dola milioni 31.3 na ndege aina ya CS 300 ilikuwa dola milioni 82.0. Hivyo basi kimahesabu ni kuwa ndege 2 aina ya Q400 na ndege 1 aina ya CS 300 ni jumla yake itakuwa shilingi **Bilioni 318.120** (usd1= 2,200) na hivyo kufanya kiasi cha shilingi **Bilioni 181.880** kikisalia .

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua ni kwanini tulitenga kiwango hicho cha fedha (500bilioni) wakati bei halisi za ndege zinajulikana? Hizi fedha zinazosalia baada ya manunuzi ya ndege hizo zitatumika kufanya shughuli gani ? Je kuna Wakala katika ununuzi huu wa ndege ambaye atapata Kamisheni, na kama yupo ni kiasi gani ?**

#### **9.1 Hakuna fedha za kuendesha ATCL**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na serikali kutenga fedha kwa ajili ya kununua ndege mbili, jambo la kushangaza ni kuwa hakuna fedha za uendeshaji ambazo zimetengwa na serikali kwa ajili ya shirika letu la ndege ATCL .Hata kwenye mashirika ya serikali ambayo yatapata ruzuku kwa mujibu wa kitabu cha Volume II 'Public Expenditure' kifungu 62 kasma 2006 kifungu 270846 ATCL zimetengwa shilingi **bilioni 3.221** kwa ajili ya mishahara. Fedha kwa ajili ya uendeshaji 'other charges' hakuna hata senti moja iliyotengwa kwa mwaka huu wa fedha.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, inataka kujua baada ya serikali kununua ndege hizo mbili shirika litapata wapi fedha kwa ajili ya uendeshaji na hasa ikizingatiwa kuwa shirika mpaka sasa ni mufilisi? Serikali haikuona umuhimu wa kulipatia shirika hili ruzuku kwa ajili ya uendeshaji wa shirika, mtaji wa kuanzia utatoka wapi?

## 9.2 UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA MWL.JK NYERERE PHASE II

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwl.Julius Nyerere awamu ya pili uko katika hatihati ya kusimama kutokana na Serikali kutokutii makubaliano ya mikataba ambayo waliingia na Kampuni ya Ujenzi ya BAM International ya Uholanzi. Hii ni baada ya wizara ya fedha kuamua kukiuka masharti ya mkataba baina ya TAA na BAM International kuwa fedha za kutekeleza mradi zitatolewa na HSBC kwa awamu zote mbili yaani phase 1&2 na badala yake wizara ya fedha imeamua kwenda kutafuta Mkopo Mpya nje ya makubaliano ya mkataba baina ya BAM na TAA wa Octoba 2015.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili la wizara ya fedha kuingilia na kuanza kutafuta mkopo sehemu nyingine nje ya makubaliano ya awali linahatarisha ukamilikaji wa ujenzi wa uwanja huu na hata mkandarasi ametishia kusimamisha ujenzi kama fedha za ziada hazitaongezwa kwa ajili ya mradi huu. **Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, inataka kujua ni sababu gani zimeipelekea wizara ya fedha kwenda kutafuta mkopo mwingine kutoka taasisi nyingine nje ya makubaliano ya awali ya kimkataba? Nani ananufaika na utaratibu huu wa kutafuta mkopo mpya badala ya kukamilisha taratibu zilizokuwepo? Je, Kitendo cha kuanza kutafuta mkopo upya kitachelewesha ukamilikaji wa mradi huu kwa kiwango gani? Nani atalipia hasara itokanayo na kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huu?

## 9.3 UJENZI WA KIWANJA CHA NDEGE CHATO

**Mheshimiwa Spika**, ukisoma Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika eneo la usafiri wa Anga moja ya kipaumbele cha mpango katika uk.76 sehemu (x) ni ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Chato. Mradi huu unahusisha ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege Chato kwa ajili ya huduma za usafiri wa anga kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 mpango wa maendeleo umetenga kiasi cha shilingi **bilioni 2** kwa ajili ya kuanza kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua kama paliwahi kufanyika kwa utafiti wa kina na majibu ya utafiti huo kuonyesha kuwa ujenzi wa kiwanja cha ndege Chato ndio kipaumbele cha taifa kwa sasa na kuwa mradi huu umelenga malengo mapana ya taifa ya kukuza uchumi wa taifa letu. Kwanini fedha hizi zisingeongezwa kwenye kuimarisha viwanja vilivyopo kwa sasa na hasa ikitiliwa maanani kuwa serikali ndio kwanza inawaza kununua ndege tatu kwa shirika letu la Ndege.

## 10 .PRESIDENTIAL DELIVERY BUREAU-BRN

**Mheshimiwa Spika**, kitengo hiki ambacho kilianzishwa kwa mbwembwe nyingi na serikali ya awamu ya nne na hata Bunge hili kushawishiwa kuwa ndio njia pekee ya kuongeza ufanisi serikalini chini ya kauli mbiu ya Matokeo Makubwa Sasa! Kimeshindwa kabisa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Itakumbukwa kuwa wakati kitengo hiki kinaanzishwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tulipinga uanzishwaji wa kitengo hiki kwani kilikuwa ni kwa ajili ya ulaji tu.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali katika mwaka huu wa fedha wameamua kimya kimya kukivunja kitengo hiki kwa kutotenga hata senti moja kwa ajili ya mishahara na marupurupu mengine kwa ajili ya wafanyakazi wa Kitengo hiki (VOTE 6) na badala yake zimetengwa kiasi cha shilingi **397,278,000** kwa ajili ya kulipia kodi ya pango , **(kasma 220700-rental expenses )**.

Aidha, ukiangalia bajeti ya mwaka wa fedha ulioisha 2015/2016 kifungu hiki kilitengewa kiasi cha shilingi **602,800,000** kwa ajili ya kodi hiyo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, ukisoma katika kitabu cha Maendeleo - Volume IV utaona kuwa fungu 06 President's Delivery Bureau zimetengwa kiasi cha shilingi bilioni **27,218,829,000** ambazo zote ni fedha kutoka nje (DFID & UNDP) na maelezo yake ni kuwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya matokeo makubwa sasa ambayo kimsingi haijaainishwa kwa ufasaha kwenye randama na vitabu vya bajeti.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** inataka kupata maelezo ya kina juu ya mambo yafuatayo;

- i. Waliokuwa watumishi wa kitengo hiki wamehamishwa, wamefukuzwa au wamesimamishwa kazi? Mbona hakuna fedha za mishahara na marupurupu mengine kwa kitengo hiki?
- ii. Ni sababu zipi zimepelekea kitengo hiki kutokupatiwa fedha za uendeshaji mwaka huu wa fedha?
- iii. Ni nani ataenda kusimamia fedha za Maendeleo takribani bilioni 27 ambazo zimetengwa kama kitengo hakina wafanyakazi? Au ndio kusema kwamba DFID & UNDP itakuwa ikisimamia fedha zake moja kwa moja?
- iv. Tangu kuanzishwa kwa kitengo hiki kimetumia kiasi gani cha fedha na ufanisi wake umekuwa upi?

v. Fedha za malipo ya pango/kodi ni kwanini mwaka huu imepungua kwa zaidi ya aslimia 48 kulinganisha na ya mwaka jana? Nani watakaa kwenye jengo hilo wakati hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya mishahara yao?

## 11. MILLENIUM CHALLENGE CORPORATION (MCC)

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa randama ya Wizara ya Fedha na Mipango kifungu 1007 katika mwaka wa fedha 2016/17 idara wameomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **milioni 500** kama bajeti yake ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **milioni 60** (kasma 210300) zinaombwa kwa ajili ya kuwalipa posho ya majukumu kwa watumishi 12 wa MCA-T Compact II watakaofanya kazi ya uchambuzi wa miradi inayohitaji ufadhili wa MCC. Aidha kiasi cha shilingi **milioni 280** (kasma 220700) ni kwa ajili ya kulipia pango la ofisi.

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa Bodi ya wakurugenzi ya MCC mnamo tarehe 28, Machi 2016 ilisimamisha kutoa fedha kwa Tanzania katika mradi wa MCA-T Compact II zaidi ya **shilingi triloni moja (USD. 472,824,825)** ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya umeme nchini kutokana na serikali hii ya CCM kupitisha sheria mbaya na kandamizi ya Makosa ya Mtandao (Cyber Crime Act), Sheria ya Taifa ya Takwimu na kuminywa kwa Demokrasia Nchini hasa kufutwa kwa matokeo halali ya Uchaguzi wa Zanzibar ya Octoba 25, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Marekani kusimamisha utoaji wa fedha kwa ajili ya mradi huu, bodi ya wakurugenzi ya MCC ilimuandikia rasmi barua Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Mhe. John Magufuli tarehe 31 Machi, 2016 na kumjulisha rasmi juu ya uamuzi wake. Pamoja na Rais kujulishwa kwa barua Kambi rasmi ya Upinzani ina taarifa kuwa mpaka tarehe 11/05/2016 barua hiyo ya Bodi ya MCC ilikuwa haijapatiwa majibu na Ikulu.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** inataka kupatiwa majibu ya kina juu ya mambo yafuatayo:-

i. Ni kwanini serikali inaomba fedha kwa ajili ya kulipa watumishi ambao watachambua miradi ya MCC ambayo haipo?

ii. Ni lini serikali itaijibu barua ya bodi ya MCC? Kwanini imechukua muda mrefu kiasi hicho kutoa majibu kwa barua yao? Hasa ikizingatiwa kuwa katikati ya mwezi Juni Bodi ya MCC itakaa pamoja na mambo mengine itatoa uamuzi wa mwisho juu ya jambo hili.

iii. Hivi kulipia kiasi cha shilingi **milioni 280** cha kodi ya ofisi kwa mwaka ambayo ina watumishi 12 ni kiwango sahihi? Kinaendana na dhana ya kubana matumizi?

## 12. WATUMISHI HEWA SERIKALINI

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 01 Mei, 2016 wakati wa sherehe za maadhimisho ya Mei mosi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. John Magufuli alilitangazia taifa kuwa jumla ya watumishi hewa walikuwa wamefikia 10,295 na alisema kuwa kati ya watumishi hao hewa 8,373 wanatoka TAMISEMI na watumishi 1,922 wanatoka Serikali Kuu. Aidha, aliendelea kusema kuwa watumishi hao hewa walikuwa wakiligharimu taifa shilingi **Bilioni 11.6** kwa mwezi sawa na shilingi **Bilioni 139** kwa mwaka na kwa miaka 5 ni shilingi **Bilioni 695**.

**Mheshimiwa Spika**, fedha hizi ni nyingi sana kwa nchi maskini kama hii ya kwetu kupotea kwa sababu tu ya uzembe na kukosekana kwa usimamizi ulio makini na dhabiti katika kusimamia rasilimali za taifa letu. Jambo hili halikubaliki hata kidogo katika ulimwengu wa sasa na teknolojia ilikofikia ya watumishi kupokea mishahara kupitia Benki.

**Kambi rasmi ya upinzani Bungeni**, kupitia hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa umma; ilitoa suluhisho la kuweza kushughulikia ufisadi huu wa watumishi hewa ambao unalelewa na mfumo.

Aidha, leo tunataka kujua hatua ambazo zimechukuliwa dhidi ya Maafisa maduhuli, wakuu wa idara na vitengo pamoja na wahasibu ambao ndio wanaondaa na kupitisha orodha ya watumishi ambao wanastahili kulipwa kila mwezi 'pay roll'. Hawa ndio wanaoondaa orodha, mbona mpaka leo bado wapo kazini?

## 13. WIZARA YA FEDHA, BENKI YA STANBIC NA SAKATA LA MKOPO WA DOLA MILIONI 600-UTAKATISHAJI FEDHA HARAMU

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2012/13 serikali ya Tanzania iliomba mkopo wa dola milioni 600 kwa malengo ya kugharamia mpango wa Taifa wa miaka mitano. Mkopo huu uluzihusisha benki zenye mahusiano ya kibiashara stanbic (Tanzania) na Standard Bank PLC (kwa sasa inafahamika kama ICBC Standard Bank PLC) (Standard Bank) ya Uingereza. Standard Bank ilihusishwa kutokana na ukweli kwamba aina ya mkopo ambao serikali ilikuwa inautaka Benki ya Stanbic Tanzania ilikuwa haitoi hiyo huduma ya aina hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Inasemekana kwamba mchakato huo ulihusisha udanganyifu wa ada ya mkopo, taarifa zinaonyesha kwamba ada halali iliyotakiwa kulipwa ni 1.4 % ya mkopo wote, hata hivyo ada iliyokuja kulipwa ni 2.4% ya mkopo wote. Kutokana na udanganyifu huo, kuna kesi inayoendelea mahakamani ikiwahusisha aliyekuwa kamishna Mkuu wa Mamlaka ya mapato Tanzania, ndugu Harry Kitilya (na mwenyekiti wa bodi ya EGMA, inayohusishwa

katika sakata hili), aliyekuwa Mkuu wa idara ya ushirikiano na uwekezaji wa Benki ya Stanbic Tanzania, Shose Sinare pamoja na aliyekuwa mwanasheria Benki ya Stanbic Tanzania, Bwana Sioi Solomon SUMARI.

**Mheshimiwa Spika**, Sio dhamira ya Kambi Rasmi ya Upinzani kujadili wahusika tajwa hapo juu kwa kuwa tunatambua, kanuni zetu za Bunge zinatuzuia kujadili suala ambalo liko Mahakamani, lakini kwa kuwa leo ni siku ya kujadili Bajeti ya Serikali ni wajibu wetu kama kambi kuhoji nini kilichopelekea udanganyifu huo na kwa kiwango gani Serikali hii ilitekeleza wajibu wake kikamilifu ili kuepusha makosa kama hayo kujirudia hasa ukizingatia kwamba katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2016/17, **serikali inatarajia kukopa mikopo ya kibiashara ya aina hii ili kufidia ombwe la bajeti yenye thamani** ya shilingi trillion 7.4. Na wahusika wakuu katika mchakato mzima ndio hao wahusika!

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo nyaraka mbali mbali, moja wapo ikiwa ni barua toka TAKUKURU (TAASISI YA KUPAMBANA NA KUZUIA RUSHWA) kwenda kwa mwanasheria mkuu wa serikali, Mhe. George M. Masaju yenye kumbukumbu namba CACE255/362/01/104 ya tarehe 20/01/2016. Barua husika imeambatanishwa na barua kwenda kwa Kitengo cha kimataifa cha makosa ya jinai (International Criminal Unit) kikiomba msaada wa uchunguzi wa wahusika katika sakata husika, huku ikirejea vifungu vya sheria vilivyovunjwa!

**Mheshimiwa Spika**, Barua husika ina ainisha mambo yafuatayo:

1. Imewataja majina ya watu wanaochunguzwa kwa kukiuka:

a) vifungu 22,23,31,32 na 34(1) sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa (The Prevention and Combating of Corruption Act 2007.

b) Vifungu 333, 335 na 337 vya sheria ya kanuni za adhabu (The Penal Code (Cap 16 R.E 2002).

c) Vifungu 12,13 vya sheria ya kuzuia utakatishani wa fedha haramu ( Anti-Money Laundering 2006 (R.E 2012). Watuhumiwa wakiwa Stanbic Bank, Harry Msamire Kitilya (Aliyekuwa Kamishna Mkuu TRA), Peter Anandi Nyabuti, Bashir Awale, Shose Sinare, Sioi Solomon Sumari, Dr Servacius Likwelile (Katibu Mkuu Wizara ya Fedha), Alfred Paul Misana, Bedason Shalanda, Ramadhan Kijjah na Ngosha Said Magonya

2. Mpaka mwezi Februari 2012 makubaliano ya ada ya mkopo kwa benki zote mbili ( Standard na Stanbic ) ilikuwa 1.4% ya Mkopo wote

3. Mchakato ulisuasua sana /ulikwama mpaka mwezi septemba 2012 pale ambapo Stanbic 'iliongeza' ada mpaka 2.4% .

4. Nyongeza hiyo ya 1% angelipwa 'local partner' na kwamba mgao huo ulikuwa na malengo ya **kumshawishi ndugu Harry Kitilya** na pengine '**maafisa wengine wa serikali ya Tanzania**' ili wawape upendeleo wa kuchukua mkopo toka benki tajwa hapo juu.

5. Mara tu baada ya nyongeza ya 1%, mchakato ulikwenda kwa kasi ya ajabu. Mwezi Novemba 2012 barua ya 'mandate and fee' ilisainiwa kati ya standard bank, Stanbic Bank na **Wizara ya fedha**.

6. Makubaliano husika hayakuelezea chochote kuhusiana na '**local partner**' au '**mtu wa tatu**' zaidi ya kuainisha ada ya ujumla ya 2.4% iliyoogezwa kiaina toka 1.4%

7. Pamoja na yote, utaratibu uliopangwa na pande **zote tatu** (Stanbic/Standard na wizara ya fedha) **uliruhusu fedha ya UMMA** (MKOPO wa kibiashara) kuingizwa kwenye akaunti **binafsi** ya 'local partner' **badala ya fedha husika kuingizwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Serikali ya Tanzania**.

8. Pamoja na kwamba kulikuwa na **viashiria vyote vya hatari ya rushwa na udanganyifu, hakuna afisa yeyote ya serikali (wizara ya fedha) ,wala timu ya benki ya standard bank aliyeonekana kujali, wala kuhoji chochote na wala hawakutaka kuchunguza au kuhoji uhalali wa huyo 'third party' au 'local partner' ambaye sio sehemu ya mkataba /makubaliano kuingiziwa 1% ya fedha ya Mkopo**

9. Baada ya fedha husika kuingizwa kwenye akaunti ya 'Local Partner' mwezi Machi 2013. Kiasi kikubwa cha fedha kilianza kuondolewa haraka haraka na ndugu Fratern Mboya. Ikumbukwe akaunti hii ilifunguliwa mahsusi mwezi mmoja kabla (February 2013)

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali iliambie Bunge hili tukufu;

i) Ni vigezo gani vilivyotumika kuwachuja watuhumiwa kutoka 11 mpaka 3?

ii) Ni kwa vigezo gani wizara ya fedha iliruhusu fedha za Umma kuingia katika akaunti binafsi huku ikifahamu (kama ilivyoainishwa kwenye barua) anayeingiziwa fedha hajatajwa/hayuko kwenye mkataba baina ya serikali na benki tajwa hapo juu?

iii) Ni kwa kiwango gani wizara ya fedha inadhani, ilitekeleza wajibu wake ipasavyo katika mchakato mzima? Kama ndio kwa nini? Kama sio ni hatua gani



zilizochukuliwa dhidi ya maafisa wa serikali (Wizara ya Fedha) waliopewa dhamana kusimamia mchakato mzima?

iv) Barua ya TAKUKURU inamtaja bwana Franten Mboya kuhusika na utoaji wa mabulungutu ya fedha kwa kipindi cha siku 10 mfululizo, na kiasi kilichobaki kuhamishiwa kwenye akaunti nyingine ya 'local partner'. Japokuwa Kambi Rasmi haijui hayo 'mabulungutu' yalienda kwa nani?. Kwa nini ndugu huyu sio miongoni mwa washtakiwa? Kwa nini wameshtakiwa watatu tu?

v) Ni kwa nini mpaka sasa Dr. Servacus Likwelile , Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na ndugu Paul Misana kamishna wa wizara ya fedha hawajafunguliwa mashtaka na wanaendelea kuitumikia serikali hii inayojinasibu kwa kutumbua majipu? Mbona hii sheria sio msumeno tena? Inang'ata upande mmoja tu?

### **13.2 Uwezo Mdogo wa Benki Kuu Kufanya Ujasusi wa Miamala ya Fedha na Kuchukua Hatua Stahiki**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatilia mashaka uwezo na dhamira ya kitengo cha Financial Intelligence Unit (FIU) cha Benki Kuu kufanya ujasusi wa Miamala ya fedha katika kuzuia utakatishaji wa fedha haramu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kitengo cha Financial Intelligence Unit (FIU) kina mamlaka ya kiutawala pekee na huishia kufanya uchambuzi wa taarifa za miamala ya fedha na kuziwasilisha ama Jeshi la Polisi au PCCB, wakati huo huo PCCB inalazimika kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) ili atoe ruhusa ya kufungua mashitaka.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo yake ni kuwa FIU haina uwezo wa kufanya uchunguzi, wala kuendesha mashitaka dhidi ya utakatishaji wa fedha haramu jambo ambalo ni mwanya unaotumiwa na watu waovu na mafisadi kama ilivyokuwa katika wizi wa Mabilioni ya Rada, wizi wa fedha kwenye akaunti ya Tegeta Escrow na wizi wa fedha katika Mkopo wa Serikali dola milioni 600 kutoka Stanbic Bank.

**Mheshimiwa Spika**, mahakama ya mafisadi inayokusudiwa kuanzishwa na Serikali haitaweza kufanya kazi kwa ufanisi kama mifumo iliyopo yenye mianya ya kifisadi haitazibwa. Mfumo wa FIU ya Tanzania ni "administrative model" wakati mfumo imara zaidi ni ule wa "Judicial Model" ambao unakiongezea nguvu kitengo hicho cha kuzuia miamala ya biashara haramu za kutakatisha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa “Egmont<sup>13</sup> Group of Financial Intelligence Units” Judicial Model of FIU inamaanisha kuwa:-

*The Judicial Model is established within the judicial branch of government wherein “disclosures” of suspicious financial activity are received by the investigative agencies of a country from its financial sector such that the judiciary powers can be brought into play e.g. seizing funds, freezing accounts, conducting interrogations, detaining people, conducting searches, etc.*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuimarisha kitengo cha FIU kwa kukiundia Mfumo wa Judicial Model ili kuepuka aibu ambayo Taifa letu limekuwa likiipata kutokana na **Serious Fraud Office** ya Uingereza kuwana na uwezo wa kurudisha fedha za zilizoibiwa kwa njia ya kifisadi wakati kazi kama hiyo ingeweza kufanywa na vyombo vya hapa nchini endapo vingemarishwa kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inavyoshauri.

#### **14 MADENI AMBAYO SERIKALI INADAIWA NA MIFUKO YA HIFADHI ZA JAMII**

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina mifuko sita ya hifadhi ya jamii ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa taifa lakini pia maendeleo ya kiuchumi ya wanachama wake. Mifuko hii ni Parastatals Pensions Fund (PPF), Public Service Pension Fund (PSPF), Local Authorities Pension Fund (LAPF) National Social Security Pension Fund (NSSF), National Health Insurance Fund (NHIF) na Government Employees Pension Fund (GEPF).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mchango mkubwa wa mifuko hii ya jamii katika uchumi wa taifa na maendeleo ya kiuchumi ya wanachama wake; mifuko hii imeathiriwa vibaya na mikopo isiyo na tija (non- performing loans) inayotoa kwa Serikali na taasisi zake. Mifuko hii iko katika hatari ya kufilisika kutokana na mikopo hiyo kukosa dhamana (guarantee) au mikataba rasmi na Serikali jambo linalopelekea uwezekano wafedha hizo zilizokopeshwa kwa Serikali na taasisi zake kupotea au kurejeshwa kwa kasi ndogo sana na hivyo kukosa tija.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 madeni ya Serikali kutoka katika hifadhi za jamii yamekuwa yakiongezeka huku kukiwa na kasi ndogo sana ya urejeshaji wa mikopo hiyo na wakati mwingine hakuna kabisa urejeshaji unaofanyika.

---

<sup>13</sup><http://www.egmontgroup.org/about/financial-intelligence-units-fius> retrieved at Egmont Group on 28.05.2016, Financial Intelligence Units

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa ripoti hiyo ya CAG, mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2014, deni la Serikali kwa mifuko ya hifadhi ya jamii lilikuwa limefikia takriban shilingi **trilioni 1. 69** ambapo kati ya fedha hizo, kiasi cha takriban shilingi **bilioni 975** kilikuwa kimeiva tayari kulipwa katika mifuko hiyo ya hifadhi lakini Serikali haikulipa.

**Jedwali Na.1. Mchanganuo wa madeni ya Serikali katika kila mfuko wa hifadhi ya jamii, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2014**

<b>MFUKO WA HIFADHI YA JAMII</b>	<b>JUMLA YA DENI (Tshs)</b>	<b>KIASI KILICHOIVA TAYARI KULIPWA (Tshs)</b>
LAPF	173,231,417,845.00	94,655,371,891.00
PSPF	460,995,168,878.82	251,942,767,372.27
PPF	221,070,451,951.77	27,252,909,658.32
NHIF	105,792,983,055.76	26,325,247,799.96
NSSF	722,460,946,894.36	575,048,756,582.94
GEPF	14,333,964,512.22	0
<b>JUMLA</b>	<b>1,697,884,933,137.93</b>	<b>975,048,756,582.94</b>

**CHANZO: Ripoti ya CAG ya 2013/14**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia malimbikizo ya madeni ya Serikali katika mifuko ya hifadhi za jamii, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliitisha kikao cha baina ya Serikali na mifuko ya hifadhi za jamii tarehe 24 Oktoba, 2014 ili kupata maelezo ya Serikali kuhusu ulipaji wa madeni hayo. Katika kikao hicho, ilibainika kwamba kulikuwa na tofauti ya kiwango cha deni la mkopo katika taarifa ya Serikali na ile ya mifuko ya hifadhi za jamii. Kutokana na hali hiyo, kiliundwa kikosi kazi cha kilichojumuisha wadau kutoka Serikalini, taasisi za Serikali na mifuko ya hifadhi za jamii ili kufanya uchunguzi kujua kiwango halisi cha deni ambalo Serikali inadaiwa na mifuko ya hifadhi za jamii.

**Mheshimiwa Spika**, CAG anaeleza kwamba ripoti ya kikosi kazi hicho kilichoundwa ili kubaini deni halisi Serikali inayodaiwa na mifuko ya jamii ilionyesha kwamba hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2014 jumla ya deni halisi ambalo Serikali ilikuwa inadaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii ni takriban **shilingi**

**trilioni 1.875**, ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 937.865** kilikuwa kimeiva tayari kulipwa lakini Serikali ilikuwa haijalipa fedha hizo kwa mifuko ya hifadhi ya jamii. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 7 Machi, 2015 Serikali ilikuwa haijalipa kiasi hicho kilichoiva kwa mifuko ya hifadhi za jamii.

**Jedwali Na. 2 Mchanganuo wa madeni ya Serikali katika kila mfuko wa hifadhi ya jamii yaliyofanyiwa uhakiki na kikosi kazi hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2014.**

<b>MFUKO WA HIFADHI YA JAMII</b>	<b>JUMLA YA DENI HALISI</b>	<b>KIASI KILICHOIVA TAYARI KULIPWA</b>
LAPF	173,231,417,845.00	94,655,371,891.00
PSPF	478,564,986,495.99	273,422,154,530.03
PPF	275,682,357,071.87	53,269,846,358.40
NHIF	106,576,578,959.00	27,651,457,652.66
NSSF	827,506,941,339.53	488,866,404,953.71
GEPF	14,333,964,512.22	0
<b>JUMLA</b>	<b>1,875,896,246,224.49</b>	<b>937,865,235,385.80</b>

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa ripoti ya CAG, deni hili la trilioni 1.875 ambalo Serikali inadaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii, halijumuishi deni la shilingi trilioni 7.066 ambalo PSPF inadai Serikali kutokana na kuwahamishia wananchama waliokuwa chini ya mifuko ya pensheni kwenda PSPF ambao makato yao hayakuwa kwenye mfuko wa PSPF lakini Serikali ikaamuru walipwe penshini jambo ambalo ni kinyume na sheria ya mifuko ya hifadhi za jamii.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa deni hili la shilingi trilioni 7 litajumlishwa na lile la awali, Serikali sasa itakuwa inadaiwa na mifuko ya jamii Jumla ya shilingi **8,942,426,246,224.49 (trilioni 8.942)**, na hii ni mbali na madeni mengine ambayo Serikali inadaiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Seirkali kutoa maelezo mbele ya bunge hili, ni kwa nini hailipi madeni (tena yaliyoiva tayari kulipwa) kwa mifuko ya hifadhi ya jamii.

## **15 KODI KATIKA MISHAHARA YA WAFANYAKAZI- PAYE**

**Mheshimiwa Spika**, wakati Rais Magufuli akilihutubia Taifa wakati wa sherehe za siku ya Wafanyakazi Duniani alizungumzia suala la makato ya mishahara ya wafanyakazi (PAYE). Na kwa mamlaka aliyonayo kama Mkuu wa Nchi aliasema kuwa amepunguza makato hayo ya PAYE kutoka asilimia 11 hadi asilimia 9, na kuagiza kuwa suala hilo lianze kufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, kodi hii ya mshahara imekuwa ni kilio kikuu kwa wafanyakazi na ni ukweli ulio wazi kuwa kundi hili la wafanyakazi ndilo linalolipa kodi kubwa kuliko makundi mengine katika jamii yetu. Busara iliyotumiwa na Mhe. Rais Magufuli kupunguza Kodi hii ya PAYE kwa ngazi ya chini iliyokuwa inalipa asilimia 11 na kuwa asilimia 9 kwa wale wote ambao wanapokea mshahara wa kati ya shilingi 170,000 na 360,000/-, na kiwango kitakachokatwa hiyo asilimia 9 ni shilingi 190,000/- ambayo ni tofauti kati ya (360,000-170,000).

Kwa wale ambao mshahara wao ni shilingi 540,000/-, PAYE itakuwa 17,100 + **20%** ya tofauti kati ya shilingi 540,000- na 360,000/- ambayo ni shilingi 36,000/-, hii inafanya mshahara huo kukatwa **shilingi 53,100/-**. Na kwa wale wanaopokea Mshahara wa shilingi 720,000/- kwa mwezi kodi ya PAYE ni shilingi 53,100 + **25%** ya tofauti kati ya shilingi 540,000/- na 720,000/- ambayo ni shilingi 45,000/-, hivyo kufanya PAYE kwa mshahara wa shilingi 720,000/ kuwa **shilingi 98,100/-**.

**Mheshimiwa Spika**, na kwa wale wote wanaopokea zaidi ya shilingi 720,000/- kwa mwezi kodi ya Mshahara ni sawa na Tsh 98,100 + **30%** ya tofauti ya shilingi 720,000/- na kiwango cha juu cha mshahara. Mathalani kwa mtu anayepokea mshahara wa **shilingi 2,500,000/-** kwa mwezi, PAYE ni sawa na Tshs 98,100+ 30% ya 1,780,000/- (534,000) na hivyo makato ya PAYE kuwa **shilingi 632,100/-**

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri lengo la Mheshimiwa Rais lilikuwa zuri la kuwapunguzia mzigo wa kodi watumishi wa umma, lakini inawezekana kabisa Mheshimiwa Rais bado hajaelewa utaratibu mzima wa makato, kwani ingekuwa ni bora kama punguzo la asilimia 2 lingekwenda sambamba kwa kila ngazi ya mshahara (**yaani punguzo la 2% kwa 20%, 25% na 30%**) kwa kulingana na utaratibu wa makato kama ulivyowekwa na TRA.

**Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, kwamba Serikali itoe punguzo la 2% kwa ngazi zote za mshahara kama ambavyo Rais Magufuli alivyokuwa amedhamiria, kinyume na hapo punguzo hilo la PAYE kutoka asilimia 11 hadi 9 itakuwa ni kiini macho kwa wafanyakazi.

Na hii ni kutokana na ukweli kuwa wafanyakazi hawa bado wana mzigo mkubwa sana wa kodi katika kupata huduma mbalimbali ambazo ni mahitaji muhimu katika maisha yao ya kila siku kama vile VAT, na kodi nyinginezo, hivyo kuwapunguzia makato ya kodi katika mishahara yao itawawezesha kuwa na kipato cha kuwawezesha kuendesha maisha yao ya kila siku.

## **16 UPOTEVU MKUBWA WA MAPATO ITOKANAYO NA MISAMAHA YA KODI**

**Mheshimiwa Spika**, misamaha ya kodi imekuwa ikilikosesha taifa fedha nyingi. Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikishauri kila mara katika mapendekezo ya hotuba ya bajeti kuwa misamaha ya kodi angalau isizidi asilimia 1 ya Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia (Opening the gate 2012) Tanzania ilikuwa ikipoteza takribani trilionini 2.9 kwa upotevu holela wa kodi bandarini peke yake. Mwaka 2013/2014 misamaha ya kodi iliongezeka kutoka 1.4 trilionini mpaka 1.8 trilionini. Mwaka 2014/2015 serikali ilitoa misamaha ya takribani shilingi bilioni 1,627 sawa na 2% ya GDP.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takribani miaka mitano sasa serikali haijaweza kufikia lengo la kupunguza kudhibiti misamaha ya kodi angalau isiyozidi 1% ya GDP. Hii ni kutokana na uzembe mkubwa wa serikali katika kukusanya kodi, sera mbovu za ukusanyaji wa mapato, udhaifu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kukusanya kodi, vitendo vya rushwa kubwa na zile ndogo ndogo zinazotokana na uswahiba wa karibu na baadhi ya viongozi wasio waaminifu.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na misamaha ya kodi baadhi ya makampuni ya madini yenye mikataba maalumu yameruhusiwa kuwekeza nje mauzo yake yote kinyume na utaratibu wa kampuni nyingine ambazo hutakiwa kurejesha nchini mauzo yao. Kwa mujibu wa gazeti la Mwananchi la April 29, 2016, makampuni hayo yenye mikataba maalum yameruhusiwa kuwekeza mauzo yake nje ya nchi (illicit financial flows) ambapo jambo hilo limerasimishwa katika sheria ya madini ya mwaka 2010.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo hili linaisababisha hasara kubwa serikali, ikiwa ni pamoja na mapato yatokanayo na kodi zinazopotea tu kiholela. Ni wazi sasa serikali iko katika wakati mgumu kifedha na maisha ya wananchi yanazidi kuwa magumu kutokana na kupanda kwa gharama za bidhaa mbalimbali ikiwemo sukari, mafuta ya magari, vyakula n.k Hivyo ni aibu kwa serikali kuendelea

kulegeza, au kutojali kabisa hasara kubwa inayotokana na misamaha ya kodi, mianya ya udhibiti wa makusanyo ya kodi, mikataba na sera mbovu ambazo hazinufaishi taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa maelezo juu ya maswali yafuatayo:

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa maelezo juu ya maswali yafuatayo:

i. Je, ni kampuni zipi na ngapi zenye ruhusa ya kuwekeza mapato yake yote nje ya nchi?

ii. Je, serikali imefanya tathimini kuwa tunapoteza kiasi gani cha fedha za kigeni yaani (foreign reserves) kutokana na mikataba ya namna hii?

## 17. MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA-UKUSANYAJI KODI

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuijengea uwezo TRA kutokana na uwezo mdogo wa kukusanya mapato kulingana na vyanzo vilivyopo na uwepo wa mianya mingi ya ukwepaji kodi na kushindwa kusimamia sera za misamaha ya kodi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Serikali iridhie mpango wa kufanya mapitio makubwa ya Mfumo Mzima wa Ukusanyaji wa kodi nchini (Robust and Comprehensive Tax Regime Review) ili kuusuka upya kwa kuondoa na kuziba kabisa mianya yote ya upotevu mkubwa wa mapato uliosababishwa na uzembe wa Serikali kuisimamia TRA katika ukusanyaji wa Mapato.

## 18. KIZUNGUMKUTI CHA MABILIONI YA JK

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa toka serikali ya awamu ya nne iwepo madarakani uliimbwa wimbo maarufu wa mabilioni ya Kikwete au JK ambayo yalitolewa na serikali wakati huo ikiongozwa na Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete. Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia hoja mbalimbali za wabunge na maswali yao hapa Bungeni walizungumzia na kuhoji utaratibu wa mgawanyo wa mabilioni hayo na serikali haikuwahi kuweka wazi utaratibu mgawanyo huo zaidi ya kutoa majibu ya kisiasa kuliko uhalisia wa jambo husika.

**Mheshimiwa Spika**, wakati akijibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka (Viti Maalum) katika Mkutano huu wa Bajeti Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu Mheshimiwa Abdalah Possi alieleza Bunge hili kuwa kiasi cha shilingi bilioni 50.6 kilitolewa kama mikopo kwa ajili ya mabilioni ya Kikwete lakini ni kiasi cha bilioni 41.53 ndicho kilichorudishwa na wakopaji. Hii inamaanisha kuwa takribani bilioni 9 hazikuweza kurudishwa na walionufaika na mabilioni hayo.



**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoja masuala yafuatayo; mosi, ni kwa nini fedha hazikurudishwa zote? Kwa sasa fedha hizo zilizorudishwa zipo wapi na zinafanya kazi gani? Je serikali imechukua hatua gani kwa fedha ambazo hazijarudishwa? Na je ni utaratibu gani uliotumika kugawanywa fedha hizo na kwa vigezo gani?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka serikali kuwa pamoja na majibu ya maswali yaliyolizwa kuhusu mabilioni haya imwagize Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za serikali kufanya uchunguzi maalum juu ya fedha hizi na kuwasilisha taarifa yake kwa Kamati ya Bunge ya Fedha za Serikali (PAC) na taarifa ya Kamati kujadiliwa katika Bunge hili.

## **19 MIKATABA MIBOVU SEKTA YA MADINI NA NISHATI INALIKOSESHA TAIFA MAPATO**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na serikali kuendelea kuingia mikataba mibovu na ambayo haina maslahi kwa taifa na kuifanya mikataba kuwa ni siri hata kwa Bunge letu tumeendelea kupata hasara kama taifa kutokana na ukweli kuwa mikataba imekuwa mibovu na ambayo inawanufaisha zaidi wawekezaji kuliko taifa .

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kitabu cha mapato **volume I** kinaonyesha kuwa Gesi italiingizia taifa katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi **Bilioni 115.127** (kwa mujibu wa kifungu 140274 - sale of Gas). Aidha sekta ya Madini inategemewa kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi **Bilioni 180.803** ambazo ni fedha zitakazotokana na mrabaha wa madini (kifungu cha 140353 —Mineral Royalties) na kiasi cha shilingi **Bilioni 29.494** ni kodi mbalimbali kutoka sekta ya Madini (kifungu 140101 –mineral Rent)

**Mheshimiwa Spika**, serikali mara zote imekuwa ikijitapa hapa Bungeni na huko nje kwa wananchi kuwa sasa uchumi wa gesi unaenda kutuondoa katika umasikini kumbe ni hadaa na hali hii haikubaliki kila mwaka kuendesha serikali kwa fedha za pombe na sigara ambazo ni nyingi kuliko fedha za sekta ya nishati na madini –kwa mfano mapato ya VAT kutokana na sigara na bia ni shilingi **bilioni 263.940** mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye bia, sigara na vinywaji vikali ni kiasi cha shilingi **Bilioni 544.112** (kwa mujibu wa Kitabu cha Mapato volume 1)

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** , tunaitaka serikali kuiwasilisha mikataba yote ya sekta ya Nishati na Madini hapa Bungeni ili Bunge liweze kuipitia na kuchukua hatua za kuisimamia serikali kwa mujibu wa katiba, na hii ndio itakuwa njia sahihi ya kuliokoa taifa na upotevu huu wa mapato.Aidha tunamtaka waziri aeleeze huu uchumi wa gesi ambao unasemwa kila mara uko wapi ?

## 20. UUZWAJI WA HISA ZA TBL

**Mheshimiwa Spika**, Msajili mkuu hazina Lawrance Mafulu alinukuliwa wakati serikali ikipitisha bajeti ya mwaka 2015-2016 kuwa moja ya vyanzo vya mapato ni kodi na mapato yasiyo ya kodi ambayo yanapatikana na shughuli za kibiashara ambazo hufanywa na mashirika ya umma ambayo huleta faida katika mfuko wa serikali kwa njia ya gawio.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikuwa inamiliki hisa **milioni 11.7** katika Kampuni ya bia ya Tanzania, lakini kwa utaratibu ambao haukueleweka Serikali mwishoni mwa mwaka jana iliuzia hisa hizo kwa thamani ya **shilingi 15,200/-** kwa kila hisa na hivyo kufanya jumla ya mauzo kuwa **shilingi bilioni 177.84**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inalazimika kukubali na kutaka maelezo ya mauzo hayo, kutokana na ukweli kuwa katika bajeti ya mwaka 2015/16 Serikali kutokana na hisa hizo ilipata gawio la jumla ya **shilingi 5,700,000,000/-** na kwa mwaka huu wa bajeti 2016/17 kitabu cha mapato VOLUME I Kampuni ya Bia inatoa gawio la **shilingi 1,000/-** tu. Hoja ni kuwa inawezekanaje gawio liporomoke kutoka shilingi **Bilioni 5.7** mwaka jana hadi shilingi 1,000 mwaka huu?

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya wizara ya Fedha na Mipango uk.21 inaonesha kuwa mauzo ya hisa asilimia 4 za Kampuni ya Bia na asilimia 2.5 za Kampuni ya sigara zingeuzwa kwa shilingi bilioni 200. Aidha, taarifa hiyo inasema kuwa makusanyo hadi februari, 2016 zilikuwa ni shilingi 344,470,000,000/- Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata maelezo ni kwa nini fedha hizi hazikuwa zimeoneshwa kwenye makisio ya makusanyo kwenye kitabu cha JUZUU ya I uk. 10 hadi 13?

## 21. KUFUTWA KWA MISAMAHA YA KODI KWA MAJESHI YETU

**Mheshimiwa Spika**, wakati waziri wa Fedha akiwasilisha hotuba ya Bajeti alisema kuwa moja ya hatua ambazo serikali inachukua ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali ni pamoja na kufutwa kwa misamaha ya kodi kwa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na badala yake alipendekeza kuwepo kwa Posho maalum kwa ajili ya kuwawezesha wanajeshi wetu kununua mahitaji yao muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, Waziri wa Fedha katika hotuba yake uk. 88 alisema kuwa tarehe ya kuanza kutumika kwa utaratibu huu ni kuanzia Julai 1, 2016. **Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, inataka kupatiwa majibu juu ya masuala yafuatayo:-

i. Fedha za kulipa Majeshi yetu ‘posho maalum’ zipo katika fungu lipi la fedha za bajeti na hasa ikizingatiwa kuwa mafungu yote katika wizara husika yalishapitishwa na Bunge hili na posho hiyo haikuwepo?

ii. Je zile bidhaa na vifaa vilivyopo kwenye bohari za majeshi yetu zitapelekwa wapi na zipo kiasi gani kwani utekelezaji wa jambo hili umekuwa wa ghafla sana? yaani chini ya wiki tatu kabla ya utekelezaji wake kuanza

iii. Kwanini serikali isingewachukulia hatua wajanja wachache waliokuwa wanajinufaisha na msamaha huo na badala yake imeamua kuyaadhibu majeshi yetu yote?

## 22. BAJETI MBADALA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA MWAKA WA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, bajeti mbadala ya KRUB, ni tulivu na yenye kuleta matumaini yenye heri kwa Watanzania. Katika kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2015, cha mwezi Juni 2016 kilichotolewa na wizara ya fedha Sura ya I ukurasa wa 1 aya ya 2 kinaonesha takwimu za awali za Pato la Taifa kwa mwaka husika ni shilingi 90,863,681,000,000.

### Jedwali I

Maelezo	Shilingi	Asilimia
Mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya Pato la Taifa	18,172,736,200,000	20
Pato la Taifa	90,863,681,000,000	100

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli ulio wazi kwamba; tukiweka mazingira mazuri na rafiki kwa mlipa kodi, tukipanua wigo wa kodi, tukiwa na sera na viwango vya kodi vinavyotabirika na endelevu, ufanisi ukiongezeka TRA kwa asilimia 50, kudhibiti ukwepaji wa kodi, kupunguza misamaha isiyokuwa na tija hadi kufikia asilimia 1 ya Pato la Taifa, kuongeza ufanisi bandari ya Dar-es Salaam, kuweka mazingira mazuri na endelevu sekta ya Utali, kukusanya kwa ufanisi mapato kwenye sekta za madini, uvuvi, maliasili, nyumba, ardhi n.k. Tutaweza kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi hadi kufikia asilimia 20.

**Mheshimwa Spika**, inawezekana kutekeleza kwa mambo hayo hapo juu. Hivyo, KRUB inapendekeza kukusanya **shilingi 18,990,509,329,000/-** ambapo mapato ya kodi na yasiyo ya kodi **shilingi 18,172,736,200,000/-** sawa na **asilimia 20** ya Pato la Taifa. Aidha, mapato ya Halmashauri ni **asilimia 0.9** ya pato la Taifa sawa na **shilingi 817,773,129,000/-**

### SURA YA MBADALA YA BAJETI 2016/17

	MAELEZO	MAPATO KATIKA SHILINGI (TZ)		
<b>A</b>	Mapato ya ndani ya Kodi na yasiyo ya kodi	18,172,736,200,000/-		
<b>B</b>	Mapato ya Halmashauri	817,773,129,000/-		
	<b>JUMLA MAPATO YA NDANI</b>		<b>18,990,509,329,000/-</b>	
<b>C</b>	Mikopo na misaada ya mashart nafuu	383,002,000,000		
<b>D</b>	Misaada na Mikopo ya miradi	2,745,659,000,000		
<b>E</b>	Misaada na mikopo ya Kisekta	372,147,000,000		
	<b>JUMLA YA MIKOPO NA MISAADA YA NJE</b>		<b>3,500,808,000,000/-</b>	
<b>JUMLA YA MAPATO YOTE</b>			<b>22,491,317,329,000/-</b>	
	<b>MATUMIZI</b>			
<b>E</b>	<b>Matumizi ya Kawaida</b>		<b>15,410,000,000,000/-</b>	
	(i).Deni miradi ya maendeleo	8,000,000,000,000/-		
	(ii).Mishahara	6,600,000,000,000/-		
	(iii) Matumizi mengineyo			
	a. Wizara	360,000,000,000/-		
	b. Halmashauri	450,000,000,000/-		

H	Matumizi ya Maendeleo		7,081,317,329,000/-	
	1. Kukuza Uchumi Vijijini (35%)	2,478,461,065,150/-		
	2. Huduma za Jamii (28%)	1,982,768,852,120/-		
	3. Miundombinu (17%)	1,203,823,945,930/-		
	4. Usimamizi wa Ardhi (12%)	849,758,079,480/-		
	5. Utalii (8%)	566,505,386,320/-		
	<b>JUMLA YA MATUMIZI YOTE</b>			<b>22,491,317,329,000/-</b>

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti Mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani inategemea misaada toka kwa nchi wa hisani na kwa mashirika ya kimataifa (utegemezi) kwa 16% tu na tunaamini kwa mazingira mazuri yakiendelea kuwekwa bila ya kuwa kero kwa wadau wa sekta mbalimbali, na pia kuondoa mchwa wanaokula fedha za miradi katika halmashauri, ni dhahiri kwa miaka miwili ijayo tungeweza kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa inatilia mkazo juu ya ukuzaji uchumi vijijini (Rural Growth) na hivyo kuwa ni kipaumbele cha kwanza katika Bajeti zake Mbadala. Vivyo hivyo kwa mwaka huu imetenga 35%. Tunaamini kabisa kuwa ili Tanzania tuwe na uchumi wa viwanda ni lazima miundombinu ya barabara kutoka pembezoni mwa wilaya zetu, maji na nishati viwe ni vya uhakika, kwa njia hiyo hata uhamiaji wa vijana kutoka vijijini kuja mijini utapungua kabisa kwani wawekezaji watafungua viwanda vya uzalishaji na hata kilimo cha uhakika kitafanyika kwani masoko yatakuwa na uhakika vile vile.

**Mheshimiwa Spika,** Kipaumbele cha pili ni kwenye huduma za jamii ambazo kwa muktadha wetu ni elimu, afya na maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, ambapo Bajeti Mbadala imetenga 28% ya fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kipaumbele cha tatu ni Miundombinu kwa maana ya Barabara za kuunganisha wilaya na wilaya, usafiri wa reli, usafiri wa ziwani n.k na imetengewa 17% ya fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kipaumbele cha nne ni kwenye usimamizi wa ardhi, kwani tumeshindwa kutumia fursa ya ardhi yetu kukuza uchumi, na kwa kuwa tulipendekeza uwepo wa chombo cha kusimamia na kuratibu sekta nzima ya

majengo (**Real estate regulatory authority-Rera**) na pia kuhakikisha kuwa kodi za ardhi zinalipwa kwa utaratibu unaoeleweka, hivyo basi, imetengwa **12%** ya fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kipaumbele cha tano na cha mwisho ni kuwekeza katika sekta ya utalii, kwani sekta hii ndiyo itakayoleta fedha za kigeni na kwa muda mfupi kama tutapunguza vikwazo vinavyopunguza idadi ya watalii wanaoingia na kukaa nchini kwa muda mfupi. Hivyo basi,bajeti mbadala imetenga **8%** ya fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani haikopi mikopo ya kibiashara kwani mikopo ya kibiashara hasa kwa mabenki ya ndani ndio chanzo kikuu cha kuua sekta binafsi hapa nchini. Hivyo basi kwa kuliona hilo bajeti mbadala ni bajeti ya kuweka mazingira wezeshi kwa wajasiliamali wa ndani na nje kuwekeza maeneo ya vijijini kwa sekta zote za uchumi.

## 24. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kusema kwamba, Serikali hii ya awamu ya tano imeanza vibaya muhula wake wa uongozi kwa kulidanganya bunge kwa kuleta bajeti yenye takwimu zinazokinzana. Serikali imeeleza katika bajeti yake kwamba inakusudia kukusanya na kutumia **shilingi trilioni 29.539** lakini cha ajabu ni kwamba vitabu vya mapato vinaonyesha kwamba Serikali itakusanya **shilingi trilioni 22.063** na cha ajabu zaidi vitabu vya matumizi vinaonyesha kwamba Serikali itatumia **shilingi trilioni 23.847** ikiwa ni ongezeko la matumizi ya shilingi **trilioni 1.784** nje ya makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, Ukichukua jumla ya bajeti yote iliyotajwa na Serikali ya **shilingi trilioni 29.539** ukatoa jumla ya makusanyo halisi ya **shilingi trilioni 22.063** utapata tofauti ya **shilingi trilioni 5.476** ambazo haziko kwenye makusanyo wala haziko kwenye matumizi. Ukichukua tofauti hiyo ya **shilingi trilioni 5.476** ukajumlisha na **shilingi trilioi 1.784** ambazo ziliingizwa kwenye matumizi nje ya makusanyo utapata jumla ya **shilingi trilioni 7.26** ambazo hazimo katika makusanyo halisi ya Mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imetafakari kina jambo hili na kufikia uamuzi kwamba; Serikali imelihadaa bunge na wananchi kwa kuliaminisha Bunge na wananchi kwamba ina bajeti ya **shilingi trilioni 29.539** wakati ki-uhalisia Serikali hii ya awamu ya tano ina bajeti ya shilingi trilioni 22.063 tu ikiwa ni pungufu ya **shilingi bilioni 432** ukilinganisha na **shilingi trillioni 22.495** za bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

David Ernest Silinde (Mb)  
**NAIBU WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA  
KAMBI RASMI YAUPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA  
YA FEDHA NA MIPANGO**

10 Juni, 2016

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tumeshasikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri siku ya tarehe 08 Juni, tumesikia pia hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na sasa tumesikia hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango.

Sasa tutaanza majadiliano, nitawataja wachangiaji tutakaoanza nao asubuhi hii. Tutaanza na Mheshimiwa Andrew Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Joseph Kakunda wajiandae.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia kidogo tu katika hoja hizi mbili zilizo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa taarifa zake nzuri alizoziwasilisha siku ya Jumatano, tarehe 8 Juni humu Bungeni, kwa maana ya kwamba ile taarifa ya uchumi (*the state of the economy*) pamoja na taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Aliziwasilisha kwa ufasaha, na nimshukuru sana na timu yake, sio kazi rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hii ni bajeti ya kwanza kwa uongozi wa awamu ya tano ya nchi yetu. Lakini kama ilivyo bajeti yoyote, lazima uangalie kwa mwaka uliopita, kwa maana hiyo ni mwendelezo wa hayo mazuri ambayo yamefanyika huko nyuma, na tunaendelea kuyaboresha zaidi. Na unaiona sura ya bajeti hii, imebeba mambo mengi mazuri, ukianza kwenye mpango, na bahati nzuri mwaka huu tunaanza kutekeleza mpango huu wa pili wa maendeleo, na mwaka wa kwanza katika Mpango huo wa Pili wa Maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 30, ameeleza maeneo ya vipaumbele katika mwaka ujao wa



fedha; yapo katika makundi manne, kwa sababu ya muda sitaweza kuyasema, lakini ndiyo naona mwelekeo mzuri wa kule ambako Serikali inataka kuipeleka nchi yetu, lakini hasa katika kukuza uchumi na hivyo kuleta ustawi mzuri wa wananchi wetu, mimi naipongeza sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, niwapongeze sana, unafahamu ukiangalia mapato, ongezeko la makusanyo ya mapato, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuipongeze Serikali, tuipongeze TRA na wote hao walioifanikisha kwa sababu kwa mara ya kwanza tumeweza kwenda zaidi ya shilingi trilioni moja kwa mwezi, sio kitu kidogo, ukilinganisha na mwaka jana ambapo tuliweza kwenda mpaka shilingi bilioni 900 na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna changamoto kubwa ambayo Waziri wa Fedha ameielezea kwenye hotuba hii, kwamba tukiweza kuyasimamia maeneo ambayo tunajua ni oevu kwa mapato ya Serikali, tutaweza kufanya vizuri zaidi. Ameelezea matumizi ya mfumo wa zile mashine elektroniki. Tupende tusipende Waheshimiwa, najua bado utamaduni wetu wa kutodai risiti na kutotaka kufanya nini, bado, lakini huu ni mwanzo mzuri. Tukiweza kuyasimamia hayo sasa hii dhana nzima mimi naiona ya kuingiza mapato yasiyo ya kodi kwamba TRA iyakusanye, mimi naamini tutafanya vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la misitu na mazao yanayotokana na misitu, mimi naelewa *there is a lot to be collected* na ninarudia msembo wa Kiingereza; *taxes are never paid, taxes are collected*. Na tukiangalia maeneo ambayo tunajua yapo mapato halali ya Serikali tutayakusanya, na hilo nimpongeze sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuanza na kasi hiyo ya kuziba mianya ambayo ilikuwa inapoteza mapato ya Serikali. Kwa hiyo natoa pongezi hizo kwa nia njema kabisa na kuwataka wote tukaze buti, twende mbele kwa faida ya Taifa hili. (Makofi)

Kwa Watanzania, na sisi kama viongozi, mimi nasema kama tunataka Tanzania uchumi ukue, lazima tukubali wote sasa leo tutoe jasho kidogo kwa faida ya kesho. Unaumia leo, lakini unajua unajenga msingi imara wa uchumi wa nchi yako kwa faida ya watoto wako, kwa faida ya wajukuu zako, kwa faida ya Tanzania hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo moja, wataalam wa uchumi watasema, lakini mimi niliyefundishwa, unaiona kabisa bajeti ya Serikali, nia ni nzuri kabisa lakini nakisi ya bajeti tuliyonayo ni shilingi trilioni 7.48. Sasa imepanda kidogo ukilinganisha na huu mwaka tunaomaliza na ukiipima dhidi ya Pato la Taifa unaona imepanda kutoka asilimia 4.2 kwenda asilimia 4.5, sasa hii ina *implications* nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema wataalam wetu waliangalie hili, kwa sababu *standard norm* ni asilimia tatu, sasa tukiruhusu iende kwa *speed* hiyo, hii nakisi ya bajeti itatusumbua. Ukiangalia kwa sasa Waziri anapendekeza shilingi trilioni 5.37 zipatikane kutoka ndani, maana yake ni nini kwa benki zetu? Kwa benki zetu hizi, shilingi trilioni 5.37 ni pesa nyingi, na maana yake uwezo wa sekta binafsi kwenda kufika tena kwenye benki hizi tunaanza kuiminywa; tulione hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nasema lazima tukope na nilisema juzi, tunakopa pesa hizi kwa masharti yapi na tunazielekeza wapi? Naona haziendi kwenye matumizi ya kawaida, hongereni sana Serikali kwa hilo, zinakwenda kwenye maendeleo, zinakwenda kulipa hati fungani na dhamana za Serikali ambazo zimeiva, huo ni utaratibu wa kawaida. Lakini sehemu kubwa inakwenda kwenye maendeleo na ndiko tunakotaka tuone. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema juzi wakati tunajadili Fungu 50 (Vote 50), basi Serikali itueleze zoezi la nchi yetu kupata *sovereign rating* limeishia wapi? Kwa sababu tukiweza kupata *sovereign rating* na inakuwa inahuishwa kila wakati tutaweza ku-access mikopo hii kwa gharama nafuu lakini pia na *Private Sector* itaweza na yenyewe hivyo hivyo ikapata access kwenye masoko ya Kimataifa kupata fedha ambazo tunazihitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niunganishe hapo hapo miradi ya maendeleo kwa upande wa PPP. Kweli twende mbali zaidi, maana sasa hivi kila siku unaambiwa ni mradi wa Dar es Salaam, mabasi ya kasi yale; sawa ni PPP ile au kutengeneza dawa inasemwa inakuja, sawa, barabara ya Chalinze - Dar es Salaam, sawa, Kinyerezi umeme sawa. Lakini yapo maeneo mengi, kwa nini Serikali inakuwa nzito sana katika eneo hilo la ubia kati ya sekta binafsi? Kwa sababu hiyo ndiyo itaiwezesha Serikali kuachana, maeneo fulani yaende kwa sekta binafsi kwa ubia na Serikali, tufanye hivyo kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho, unaona ukurasa wa sita wa taarifa ya uchumi, kilimo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Ohoooo! Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, naunga mkono hoja hizi mbili. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Chenge. Mheshimiwa Mashimba Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi pia niweze kuchangia Hali ya Uchumi na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake pamoja na wasaidizi ambao amefanya nao kazi bega kwa bega na hatimaye kutuletea kitu kamili na kilichoiva vizuri cha namna hii kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa nia yake ya dhati kutaka kutuelekeza kwenye kujitegemea kama Taifa, kwa sababu ukiangalia bajeti ilivyotengenezwa, na hata maelezo yake ambayo yamesomwa na Mheshimiwa Waziri kwa kweli yanaonesha dhamira ya Serikali kujitegemea na yanaonyesha ya kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kabisa kupeleka maendeleo kwa wananchi baada ya kutenga asilimia 40 ya bajeti yake kwenye fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutoa mchango wangu kwa kuangalia mambo mawili tu kwenye hali ya uchumi. Jambo la kwanza ni lile la kujitegemea kwa kuimarisha viwanda kwa ajili ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wa suala hili unategemea uwekeshaji na tunapozungumza juu ya uwekezaji huu maana yake tunamzungumza mtu mwenye mtaji wa hapa ndani na mwenye mtaji wa nje ya nchi yetu. Lakini nadhani ni jambo moja tu ambalo limewekewa nguvu sana katika kuhakikisha kwamba tunapokuwa na uchumi wa viwanda tunatengeneza ajira na hatimaye tuweze kukusanya kodi, huo ni upande mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upande wa pili ambao naona kama tunausahau kidogo; kuwawezesha hawa Watanzania, hasa wakulima wetu wadogo wadogo ili na wenyewe wajumuishwe kwenye harakati hizi za kuinua uchumi wetu wa viwanda kwa wao pia kushiriki, si tu kuzalisha malighafi, sio kuwa vibarua au kulipwa mishahara au kuajiriwa kwenye viwanda au kwa wawekezaji; lakini wao pia kushiriki kama wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuangalia ninaona kuna pengo kubwa sana. Wazalishaji wetu wadogowadogo, hasa wakulima wanaunda nguvukazi ya asilimia 65 na kutokana na taarifa mbalimbali, wanatuzalishia malighafi za viwandani, wanatuzalishia chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye harakati zetu hizi za kujenga uchumi wa viwanda tunawaangalia kama waajiriwa peke yake,

hatujawaangalia kama watu ambao wanaweza wakaja pamoja na wao pia wakashiriki kama wawekezaji, wakaendelea kuzalisha kama ambavyo wameendelea kuzalisha toka uhuru wa nchi hii. Wamezalisha wametupa chakula, wamezalisha wametupa malighafi za viwandani, wamezalisha wametupa mazao ambayo tukiua nje tunapata fedha za kigeni. Sasa nilikuwa najaribu kuangalia Serikali imeweka mkakati gani jumuishi ili na wao waweze kushiriki kwenye uwekezaji huu ambao tunataka nchi yetu tuwekeze halafu hatimaye tuwe nchi ya kipato cha kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika wa wakulima hawa wadogo wote tunafahamu umekuwa hauna nguvu sana ni dhaifu sana. Mimi nilikuwa nafikiri kama ungetiliwa nguvu ungekuwa una nguvu za kutosha kuweza kutumika kuwafanya hawa wazalishaji wadogo wadogo ili wao wawe wawekezaji kwenye maeneo yao. Wamekuwa wawekezaji kwa muda mrefu sasa Serikali inatengeneza mazingira na kuweka mkakati gani ili kuwafanya hawa watu badala ya kutoa tu nguvu zao, badala ya kufanywa kama wafanyakazi na wenyewe wawe wawekezaji kwa namna ambavyo wamekuwa wawekezaji toka mwanzo?

Kwa hiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atakapojumuisha ajaribu kutufafanulia, kwamba hawa wakulima wadogo wadogo hasa wakulima wadogo wadogo wa wa vijijini wana wekewa mazingira ya namna gani ili na wenyewe waendele kuwa wawekezaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la thamani ya shilingi yetu, zimetajwa sababu zinazofanya shilingi yetu iendelee kuporomoka. Moja ni kuimarika kwa dola ya Kimarekani, lakini lingine ni kuchelewa kupatikana kwa fedha za kigeni hasa kwenye bajeti yetu, pia mapato kidogo ya fedha za kigeni. Lakini kuna moja ambalo tunaona na wachangiaji wengine wamekuwa wakilitaja hapa, la hawa watoa huduma pamoja na bidhaa kutaka kupata malipo kwa njia ya dola, halijatajwa hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili pia limekuwa kero kwa wananchi hasa wa kawaida na wananchi wengine kwamba ukitaka kununua bidhaa au ukitaka kununua huduma ulipe kwa dola. Suala hili nalo linasababisha thamani ya shilingi yetu kushuka. Kwa hiyo na lenyewe Mheshimiwa Waziri angetusaidia ni kwa namna gani Serikali inakuja na uamuzi uliothabiti na ulio wazi, kwa sababu sheria ipo inayozuia jambo hili lakini bado linaendelea.

Mheshimiwa naibu Spika, suala lingine la tatu ni hili linalohusiana na shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Naipongeza Serikali kwa sababu imeanza kwa kutenga shilingi bilioni 59 ili kwamba ziende kwenye vijiji zaidi ya 1000 kwenye nchi yetu yote. Hapa bado kuna kizungumkuti kwa sababu Serikali inasema itapeleka

pesa hizi kwenye SACCOS, sasa najaribu kujiuliza hizi SACCOS ambazo zitapelekwa hizi pesa Serikali inazifahamu na kama inazifahamu hizi SACCOS ziko kila kijiji? Maana vijiji vingine havina SACCOS, hii hela itapelekwa kwa nani? Kwa taasisi ipi ili iweze kuzitoa hizi pesa kama mikopo kwa watu wetu? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na mapendekezo kwenye jambo hili. Mimi nilikuwa nafikiri badala ya kutegemea SACCOS ambazo hatujazitathmini na hatujui kama ziko kila kijiji, kwamba badala ya kufanya hivyo tungeunda Bodi za Mikopo za Vijiji vile ambavyo vitapelekwa hizi pesa. Bodi hii ya mkopo iwe ndiyo inasimamia hizi pesa kujaribu kuzigawa au kuzitawanya kwenye vikundi au kwa watu ambao wako kwenye vikundi ili kupata hii mikopo lakini kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza kwamba hizi fedha ziwe ni *revolving* au ziwe za mzunguko; kwa sababu mpaka sasa hivi hatujaelewa kwamba zitakuwa ni za namna gani, maana zikienda kwenye SACCOS hauziiti tena za mzunguko.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ziwe za mzunguko, na hizi pesa zibaki kwenye kijiji husika zisiende kwenye vijiji mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilikuwa napendekeza kwamba usimamizi wa hizi bodi ufanywe na Maafisa Maendeleo wa Kata na Maafisa Maendeleo wa Wilaya zetu na hizi shilingi bilioni 59 wakati wakuzigawa hii mara ya kwanza vijiji vitakavyopewa viwe *pilot*, lakini kila Jimbo lazima liwe na kijiji au kimoja au viwili ili tujue kila Jimbo *performance* ya mpango huu unafananaje, vinginevyo ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba muda wako umekwisha, hiyo ilikuwa ni kengele ya pili

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Bajeti iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali yote kwa jinsi ambavyo imeleta mpango na bajeti ya kuthubutu, tusiogope kuthubutu, changamoto zitakazojitokeza huko mbele ya safari tutazitatua, lakini naipongeza sana Serikali pamoja na Waziri kwa uwasilisho mzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru sana Serikali kwa kuamua kujenga reli kwa *standard gauge*, kwetu sisi tunaotoka Tabora, Kigoma na Mwanza ni ukombozi mkubwa. Natunaomba mpango uanze mara moja mwaka huu wa fedha ili tusaidie kupunguza bei kutokana na usafiri wa reli utakaopunguza bei ya bidhaa zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeza Serikali kwa kuja na mpango wa maji, ombi langu mimi ni kwamba ili akina mama watokane na ubebaji wa maji kwenye vichwa, badala ya shilingi 50 kama walivyopendekeza Kamati ya Bajeti tuongeze zifike shilingi 100 ili akina mama vijijini wapate maji wajikomboe na wafanye kazi zingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika mimi nginganza na upandewa mtu ni afya. Bila afya hakuna chochote kinachowezekana. Ngingejikita zaidi kwa upande wa mama na mtoto. Ndugu zangu tuwapongeze wakinamama na nafasi ingeniruhusu ningewaomba akina mama na akina baba wote tusimame tuwape heshima akina mama wanaofariki kwa njia ya uzazi, wanafanya kazi kubwa na wanafariki katika kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona zimetengwa asilimia tisa ya bajeti nzima kwa ajili ya afya. Naiomba Serikali ifikishe asilimia 15 kama walivyokubaliana katika Azimio la Abuja. Lakini pia mimi ningependa katika kujumuisha tupate majibu mpango wa MMAM uliishia wapi? Kwa sababu mpango wa MMAM ulikuwa na lengo la kuongeza zahanati ili wakinamama wafike haraka kwenye zahanati ili wasipoteze maisha yao. Tunataka tathmini ya mpango wa MMAM. Zahanati nyingi hazijajengwa, lakini pia zina upungufu mkubwa wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapeni mfano wa Urambo tuna zahanati 20 ni zahanati tano tu zenye Maafisa Tatibu. Ni haki mama mjamzito mwenye *complication* kweli akapewe *prescription* ya dawa na muuguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali katika mwaka huu wa fedha iangalie; na ndiyo maana nasema iongezewe bajeti ili kuwe na wafanyakazi wengi wa kutosha wa hospitali na zahanati. Urambo ina uhaba wa wafanyakazi 150, na nimeshatoa mfano kwamba zahanati tano tu ndizo zina Maafisa Tabibu ambao siyo haki hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kulikuwa na mradi huu wa ADB. Mimi naiomba Serikali iangalie jinsi gani ya kukamilisha zile *theaters* zilizokuwepo, najua hii bajeti katikati huko italeta tu mabadiliko ya kuomba nyongeza ya fedha, kwa sababu Serikali hii inathubutu. Tuna *theater* Urambo na sisi tulikuwa tunafikiri kwamba njia mojawapo ya kupunguza vifo vya kina mama na watoto ni kuwa na *theater* katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha ajabu ni kwamba Urambo nzima yenye kata 18 tuna kituo cha afya kimoja tu halafu hakina *theater* ni haki hii? Halafu *theater* iliyokuwa inajengwa imeishia kwenye *linter* kwa mpango wa ADB.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Urambo jamani tunahudumia mpaka Uvinza na ile miji ya karibu ya Mkoa wa Kigoma kutokana na umbali, lakini cha ajabu *theater* iliyokuwa inajengwa Urambo imeishia kwenye *linter*. Ndugu zangu nipeni pole mimi Mbunge wa huko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa kuthamini afya ya mama na mtoto mpango wa ADB ulikuwa unajenga *clinic* ya mama na mtoto, jamani imeachwa imechimbwa msingi mpaka leo. Lakini pia kulikuwa na kliniki ya mama na mtoto katika sehemu ya Isongwa imeachwa katika hatua ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninasikitika, nina barua hapa kutoka Wizarani inayotutaka sisi wenyewe tumalize, Halmashauri inaweza kupata shilingi milioni 500 za kumaliza *theatres*? Na hayo ni majengo tu hayahusiani na vifaa. Nina barua hapa ya kusikitisha sana ya kutuambia sisi kama Halmashauri tumalize miradi ya ADB, kwa nini walileta mradi ya ADB kama walikuwa wanajua sisi tuna uwezo? Mimi ningeomba suala hili la *theatres* zilizoachwa bila kumalizwa zote pamoja na majengo ya kliniki yamaliziwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia sisi Kanda ya Magharibi hatuna Hospitali ya Rufaa, je, Serikali inafikiriaje kuhusu Kanda ya Magharibi nayo kupata Hospitali ya Rufaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye kilimo. Mimi naipongeza hii Serikali kwa kushughulikia sana suala la viwanda ili kuinua hali ya wananchi. Tunaomba badala ya tumbaku kutoka Tabora kupelekwa Morogoro tuwe na kiwanda, na sisi tuna hitaji viwanda kwa sababu vitatupa pia ajira kwa watu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 45 nimesoma, Serikali imeandika hapa kwamba inafahamu vizuri sana changamoto za wakulima. Nimeona hapa nikafarijika nikasema ahaa kumbe Serikali inajua. Ukurasa wa 35 inasema kwamba hata hivyo bado sekta hii ya kilimo inakabiliwa na



changamoto kadhaa zikiwemo za kodi na tozo za mazao zisizo na tija. Tumbaku ina kodi zaidi ya 12, halafu wanasema tena uhaba wa pembejeo ambazo pia zina kodi nyingi, vifaa duni, masoko na uhaba wa Maafisa Ugani, kumbe Serikali inajua? Je, Serikali inachukua hatua gani katika kutimiza haya kutatua changamoto hizo? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la zao la tumbaku, tumbaku ni jani, mwezi wa pili tu jani linaiva, jani likishaiva masoko yanatakiwa yaanze mara moja mwezi wa tatu, lakini utaona cha ajabu masoko yanasuasua hadi leo hii. Bodi ya Tumbaku haina fedha nimeongea nao hawana fedha, wakulima watafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumbaku ndugu zangu inavyokaa inapoteza ubora na inapoteza uzito. Inapofika Morogoro imepoteza uzito, je, ni haki hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nawashukuru, Naibu Waziri wa Kilimo amesema na mimi naomba nirudie sijui kama itakuwa ni vibaya, kwamba anakuja Tabora, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu waone shida zinazowakabili wakulima wa tumbaku waongee nao, vyama vya msingi vinakufa watafanyaje? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, makato kwenye pembejeo ni mengi, makato kwenye zao lenyewe mengi, kuna uhaba wa wanunuzi. Naomba mtuambie; kwa kuwa mnatambua; kwenye ukurasa wa 35; Serikali inachukua hatua gani ya kupata masoko zaidi ili kuwe na ushindani wa masoko? Haya makampuni matatu hayatoshi, yana ukiritimba, tunataka masoko mengine kutoka nje, nchi za Japan pamoja na China, Serikali inasema nini kuhusu hili?

Lakini pia wenzetu, kwa mfano wa Uganda wajanja wale wame-market kahawa yao wameiua ndiyo maana unaona watu wa Kagera wanapeleka kahawa kuuzia Uganda. Kwa nini na sisi tusishirikishe Wizara ya Mambo ya Nje ili tumbaku yetu iuzwe? Kwa sababu ladha na harufu iliyo kwenye tumbaku tunayolima sisi watu wa Tabora ndiyo inayofunika duniani kote waulizeni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini na sisi tusiitangaze kwa kutumia pia Wizara ya Mambo ya Nje, Mabalizi, nchi majirani ili tumbaku yetu na sisi ivutie tupate wanunuzi wengi zaidi. Mimi ninachoshukuru ni kwamba Mheshimiwa atakuja ajionee mwenyewe. Lakini naomba sana Bodi ya Tumbaku iwezeshwe ili iweze kufanya kazi, na pia nimesema kiwanda cha tumbaku kijengwe Mjini Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa kwa kweli siyo haki kama nikimaliza bila kusemea mtoto wa kike. Nimeona mipango mingi ya Wizara ya Elimu, mimi

naomba kujua elimu bure inayotolewa itamsaidiaje mtoto wa kike hapa katikati pasiwe na tatizo lolote la kumfanya atoke nje ya darasa ili amalize kuanzia kidato cha kwanza hadi mwisho? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Wizara itakapokuja kumalizia ituambie kutokana na wingi wa taasisi za elimu zilizo nchini ni lini Mamlaka ya Ukaguzi itaundwa ili ukaguzi kweli ufanyike kikamilifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mengi ambayo ningeongea lakini bado nawakumbuka walimu wangu, tunaomba chombo kile kinachoundwa kwa ajili ya walimu kifanye kazi ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Kangi Lugola ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naomba niseme kwamba wapinzani wamewasilisha malalamiko ya mtu mmoja bila ya kuleta bajeti mbadala ya upinzani. Hawa ni sawa sawa tu na Mbunge mmoja amesimama pale amechangia, lakini kusema hiyo ni hotuba ya upinzani kama bajeti mbadala hiyo ni bajeti hewa. Niliamini kama kweli ingekuwa ni Serikali kivuli basi ingewasilisha bajeti mbadala, mfano kama ameona shilingi trilioni 29.5 ni nyingi sana wao wanapendekeza trilioni ngapi? Tungesikia kutoka kwao, naamini Watanzania wamewaelewa hawa ndugu nadhani tuwaache kama walivyo na hawapo hapa Bungeni kwa sababu wamedharau. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimkakati bajeti yetu ni nzuri sana, na vyanzo vya mapato vya bajeti hivi vinakusanyika vizuri. Kwa mfano kuondoa kodi ya majengo (*property tax*) kutoka kwenye Serikali za Mitaa ambazo kwa pamoja zilikuwa na uwezo wa kukusanya kati ya asilimia tano hadi 10 tu ya fedha ya kodi yote ambayo inaweza kukusanywa ni jambo la kupongeza sana. TRA kama watajitahidi, kama ninavyowafahamu mimi, wanao uwezo mkubwa wa kukusanya kati ya asilimia 50 hadi 70 ya *potential*. Ina maana wanaweza wakakusanya hadi trilioni 1.8 ambayo ukilinganisha na pato la zamani la shilingi bilioni 300 ina maana tutakuwa tumepiga maendeleo makubwa sana kwa hiyo naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili, makusanyo ambayo yalikuwa ya *retention* yalikuwa yanatumika vibaya sana kwa hiyo kwa sasa hivi itakuwa ni fursa ya mapato hayo kutumika vizuri.

Suala lingine zuri tumepunguza mikopo ya nje kwa trilioni 0.03 kulinganisha na mwaka jana kwa ajili ya kupunguza utegemezi, kwa hiyo, hilo ni jambo lingine la kupongeza sana Serikali. Angalizo pekee hapo ni kwamba tumeongeza mikopo ya ndani kwa trilioni 1.34 hatua hii ni nzuri, lakini Wizara ya Fedha itahitaji udhibiti na ufuatiliaji wa karibu sana, kwa sababu riba za mikopo ya ndani zipo juu sana Wizara ya Fedha na Benki Kuu wakizembea kidogo tu tutatumbukia kwenye mizozo isiyo na tija inayoweza kusababisha sintofahamu kupitia matokeo hasi kama mfumuko wa bei. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya upinzani dhidi ya bajeti ya Serikali yana ukakasi wa hasira ya kugomea Bunge bila sababu za msingi. Kwa nini tuandikie mate na wino upo? Wanazo Halmashauri kadhaa ambazo wanaziongoza hivi huko kwenye Halmashauri zao wamesamehe ushuru wote na tozo zote? Badala yake wameongeza ushuru na kodi kwa hiyo ina maana kwamba hapa wanakuja kufanya mchezo wa maigizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Watanzania waelewe kwamba sisi Wabunge wa CCM tuko hapa kuwawakilisha na tuko makini katika kazi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka vipaumbele vya kujenga uchumi wa viwanda kwenye bajeti hii mpya. Katika vipaumbele hivyo nashauri Serikali ikamilishe maandalizi muhimu yanayotakiwa kwenye sekta wezeshi ili kuhakikisha kwamba bajeti hiyo itatekelezeka vizuri sana. Kwa mfano kule kwetu kuna barabara ya kutoka Chunya hadi Itigi na barabara ya Ipole hadi Rungwa, barabara hizo mbili ni barabara muhimu sana kwa kwetu kwa uchumi wa viwanda, tunaomba sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Ziwa Victoria ni mradi mmoja wezeshi ambao ni muhimu sana. Miradi ya umeme vijijini, zahanati, vituo vya afya, shule ni miradi wezeshi ambayo tunaomba sana fedha ambazo zimepangwa kwa mwaka ujao ziweze kutolewa zote zitumike zote kwa ufanisi. Na vilevile pale ambapo kutakuwa na upungufu mwaka 2017/2018 tuisahaulike kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kusimamia utekelezaji wa mpango na bajeti napenda kujua ni shilingi ngapi zimewekwa kwa ajili ya *monitoring and evaluation*? Kwa sababu haiku wazi kwenye Bajeti hii. Bila *monitoring and evaluation* tutapata matatizo makubwa. Kwa mfano Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepangiwa shilingi bilioni 34, kwa mtazamo wangu fedha hizo ni ndogo sana. Tunamtarajia Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ofisi yake iimarishwe zaidi ili afanye kazi vizuri zaidi. Tunahitaji awe na uwezo mkubwa wa kufanya ukaguzi wa kitaalamu au *technical audit* ambapo haiitaji wahasibu na wakaguzi wa ndani peke yake. Inahitaji wahandisi, wakadiriaji wa majengo, wachumi na wataalamu wengine wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunahitaji ofisi hii iweze kuimarishwa kwa nguvu kazi na uwezo wa kufanya kazi. Sasa hii pesa iliyowekwa hapa ni ndogo sana, kwa hiyo tunaomba sana ifikiriwe mara mbili ili kusudi bajeti hiyo iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kusesitiza ni bajeti ya utafiti. Kwenye sekta karibu zote ni bajeti ndogo sana imepangwa. Utafiti duniani kote ni jukumu la Serikali, kwa hiyo inatakiwa bajeti ya utafiti hasa kwenye mazao ya biashara na chakula iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni kwamba, Serikali imekiri hapa kwamba kuna ugumu wa kukusanyaji wa mapato kwenye sekta isiyo rasmi. Sasa Serikali imejua tatizo inatakiwa ikamilishe sasa sehemu muhimu ya namna gani ya kutatua tatizo hili, kwa sababu tunahitaji kukusanya mapato kutoka kwenye sekta isiyo rasmi. Nashauri Serikali iweke kipaumbele cha kuisajili sekta yote isiyo rasmi ili kujua vizuri na kurahisisha Serikali kukusanya mapato yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nafurahi kusikia kuwa deni letu la Taifa bado ni himilivu, na ili kudhibiti deni letu Wizara ya Fedha inatakiwa kuwa macho sana na madalali wa mikopo ya miradi mikubwa ambao hujiita *transaction agents*, ambao hujifanya wanasaidia nchi kupata mikopo mikubwa kutoka kwenye Serikali rafiki za nchi nyingine. Kama watu hao wasipodhibitiwa hatimaye tutakuwa na mikopo yenye gharama kubwa sana maana nao huwa wanatoza tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yetu mikubwa kama ya reli, bwawa la Kidunda, bomba la mafuta, itaathirika kwa kuiingiza nchi kwenye gharama kubwa zaidi kama hatutawadhibiti hao *transaction agents*. Naomba sana Serikali iwe makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nina wasiwasi na bajeti ndogo sana kwenye sekta ya ardhi kukidhi kazi muhimu za kupima viwanja nchi nzima, lakini hasa hasa lile swala ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikubali hapa, kwamba inatakiwa iteuliwe Kamati ya Kitaifa ambayo itaunganisha Wizara zaidi ya nne kwa ajili ya kufanya kazi ya kubaini maeneo yote ambayo yanahitaji kuongezwa ili kusudi wakulima na wafugaji wapate maeneo mengi zaidi ya kufanya shughuli zao. Hii bajeti iliyoko kwenye sekta ya ardhi ambayo ndiyo ingegharamia kazi hiyo hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali ifikirie mara mbili, kazi hiyo ni ya muhimu sana kwa maendeleo ya taifa. Na kwa ajili ya kuliweka taifa letu katika amani na utulivu ni muhimu sana mapori ya akiba ambayo yamekosa

sifa mpaka sasa hivi yako mengi sana hapa nchini hii timu inatakiwa iende ikafanye ukaguzi na kuleta mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulitolea maoni yangu, ni kukata kodi *gratuity* ya Wabunge. Sidhani kama kulikuwa na ulazima wa kuleta suala hilo mwaka huu, lakini vilevile si dhani kama kuna ulazima wa kukata hiyo *gratuity*. Najua, inaletwa ili kusudi makato yaanze kufanyika kuanzia mwezi wa saba unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Ofisi ya Mbunge ni Taasisi inayojitegemea, na ina majukumu mengi sana kwenye jamii, na wananchi wanaitegemea, na fedha hizi nyingi huwa hazitumiwi na Mbunge binafsi, fedha nyingi huwa zinakwenda kwenye jamii, Mbunge huwa anachangia miradi mbalimbali. Kwa hiyo, mimi naomba sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwa mwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Waziri wa Fedha. Hotuba ambayo ni muhimu sana; na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuipongeza Wizara na Watendaji wote, na wote waliohusika kutuandalia kwanza Mpango ule wa Maendeleo kama tulivyousikia; lakini pia hotuba hii nzuri. Niipongeze kwa dhati kwa sababu ukiangalia bajeti hii utaona imezingatia mambo muhimu sana, imezingatia pia mwelekeo ambao tunautarajia. Ukiisoma bajeti hii utaona yako maeneo muhimu sana. Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, imezingatia maboresho ya mfumo wa kodi na tozo na mabadiliko makubwa sana na sura ya bajeti na mambo mengi ambayo tumeyaona. Kwa hiyo, nipongeze kwa dhati juu ya kuwa na bajeti nzuri namna hii, inatupa matumaini kwamba kweli tunaelekea kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba mwaka huu ni mwaka wa kizio (*it's base year*) kwa hiyo upo umuhimu wa kuangalia *data* na kumbukumbu zetu za mwaka huu kwa ajili ya kuweza kuzitumia siku za usoni; ili kuona mwelekeo wa ukuaji wa uchumi unavyokuwa kuanzia mwaka huu. Ni mwaka ambao tumekuwa na Rais mpya, mchapakazi na ambaye anadhamira ya dhati kutupeleka sehemu nzuri, lakini ni mwaka ambao pia tuna Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano mpya na yamkini pia tuna Waziri wa Fedha

ambaye kama anavyoonesha kwamba atatusaidia sana ili tuweze kuona hali ya uchumi inakwenda kule tunakostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na mimi nichangie tu upande huu wa *data* zetu nikizingatia kwamba Ofisi ya Takwimu inafanya kazi nzuri. Nilikuwa nafikiri ni muhimu niseme kidogo hapa, kwamba hii Idara inafanya vyema. Lakini nilikuwa nafikiria nishauri idara hii sasa iwezeshe kwa haraka ili tuweze kupata *data* ambazo zitatusaidia kufanya *analysis* zaidi tunapo kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu utaona kwenye kitabu hiki cha hali ya uchumi ile *price index* iliyotumika ni ya mwaka 2007, inaonesha pale nyuma ilikuwa ina shida kidogo ya uwezesaji, lakini nilikuwa nafikiria kwa sababu tumeanza mwaka na mambo mapya ni vizuri sasa; hao wenzetu wa takwimu wawezeshwe mwaka huu ili basi tupate *price index* mpya ambayo itatufanya tuweze ku-*determine* ukuaji wa uchumi unavyokwenda kwenye hii miaka kumi inayofuata na tuweze kuwa na *indicator* mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu katika hali ya kawaida, tutazungumza kwamba hali ya uchumi inakuwa lakini utaona bado tunaweza kuwa na maswali mengi ambayo tunaweza kujiuliza. Kwa sababu kutakuwa kuna *gap* kati ya *nominal income* na *real income* hasa kwenye maisha yale ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba wakati tukizungumza juu ya kukua kwa hali ya uchumi lakini ukienda kule chini utaona kabisa kwamba bado kuna hali isiyo nzuri. Kwa hiyo Idara hii ya Takwimu iwezeshe ili basi takwimu zinavyokuja hapa tuweze kuona zinaenda na hali halisi. Utaona kabisa kwamba kama ni mishahara itaonekana haitoshi kulingana na hali ya maisha, utaona kama ni bei ya mazao haitoshi kulingana na maisha. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba Idara ya Takwimu iwezeshe ili iweze kuleta uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuja kuona kwamba bado tuna *income gap* kwenye *society*, kwa hiyo, tuone hili *gap* likizibwa ili lisitupe nafasi ya kuburuza wale wanaoishi maisha ya hali ya uduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuangalia kwenye kitabu cha hali ya uchumi, kumbukumbu nyingi zinaonesha zimechukuliwa hasa katika maeneo ya mjini, na sehemu kubwa utaona majedwali yanaonesha hali hii imechukuliwa katika masoko ya Dar es Salaam na yameacha kuchukua maeneo ambayo pia yametajwa kwamba ni maeneo ambayo yana umasikikini mkubwa, wananchi wanaishi chini ya mstari ule wa umaskini. Kwa Mikoa kama Kigoma, Geita, Kagera, Singida, Mwanza utaona kwamba upo umuhimu sasa hizi *data* zichukuliwe kwenye maeneo haya zikichanganywa na maeneo mengine, ili tukipata wastani uwe wastani ambao utakuwa unagusa wananchi walio wengi.



Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumze juu ya hii dhana ya ukuaji wa uchumi kwa ujumla hii; kwamba tunataka twende kwenye uchumi wa viwanda, tuwe na uchumi wa kati. Sasa nilikuwa najaribu kujiuliza, kwa sababu kama Mheshimiwa Waziri wakati anamalizia kusoma hotuba yake alizungumza juu ya umuhimu wa wananchi wote kutakiwa kushiriki katika kuhakikisha kwamba uchumi unakua. Lakini walio wengi tunaweza tusielewe tunavyozungumza juu ya tunahitaji kwenda kwenye uchumi wa kati. Je, wastani wa pato kwa mtu unatakiwa uwe wapi, iwe ni dola 1,500 kwa mtu au 3,000 kwa mtu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yako mambo ambayo tunahitaji pia ili wananchi wetu kwa ujumla, ambao pia kila mmoja ana mchango wake katika ukuaji wa uchumi, aweze kuelewa kwamba tunataka twende kwenye uchumi unaotegemea viwanda na biashara. Tunahitaji pia wastani wetu wa kipato kupanda kwenda dola 3,000 kwa mtu kufika mwaka 2025; kila mwananchi aweze kushiriki katika ujenzi wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii pia itawezesha wananchi wetu wengi ambao bado hawajapata ajira, wapate ajira ili waweze kushiriki vizuri katika ujenzi wa uchumi. Lakini pia bidhaa zetu tutakazozizalisha katika viwanda ziwe na ubora kiasi cha kumudu ushindani katika masoko ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni muhimu sana jambo hili litafsiriwe vizuri, wakati mwingine Wizara ifanye utaratibu wa kutoa vipeperushi virahisi ili wananchi mpaka aliyeko huko chini aweze kujua kwamba kwa pamoja tunaelekea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda nishauri kwamba ni vyema tutafsiri vizuri ili wananchi waelewe, na hasa watumishi walioko kwenye Halmashauri na watumishi wengine, waweze kujua hii dhana nzima ya kwenda kwenye uchumi wa kati na wa viwanda, na hivyo tuweze kuielewa vyema na kushiriki ujenzi wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kwamba Serikali imechukua hatua nzuri kwa sababu hapo nyuma tulikuwa na matatizo makubwa ya kutokukusanya kodi kiasi cha kutosha. Sasa inaonesha kabisa kwamba Serikali inafanya juhudi kubwa ya kufanya makusanyo. Ukiingalia hii bajeti ambayo imekuja leo utaona kabisa kwamba ipo dhamira ya Serikali ya kufanya tutegemee mapato yetu ya ndani; hili ni jambo la kupongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kulikuwa na tatizo la kutokutolewa kwa mafungu, kwamba mtiririko wake haukuwa mzuri. Naamini kama juhudi za makusanyo zitaongoezeka kile ambacho tumekipitisha hapa kikiweza kufika na kwa wakati tutayaona maendeleo kwa haraka. Pia ninaona Serikali ina



dhamira ya dhati kwa kusimamia nidhamu ya makusanyo na matumizi. Mwanzo ilikuwa ni shida lakini kwa hali iliyoko sasa hivi inatutia matumaini kwamba tunakwenda kwenye mwelekeo mzuri. Kwa hiyo, nishauri tu, tuweke hamasa kubwa kwenye makusanyo ya mapato ya ndani ili tuweze kujitegemea, lakini pia tusimamie nidhamu katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumze kidogo juu ya sura ya bajeti. Kuna mambo ambayo nilikuwa nafikiri niweze kushauri. Kwanza napongeza ukuaji wa bajeti hii, kutoka trilioni 22 kwenda trilioni 29, si jambo dogo, ongezeko la zaidi ya asilimia 23, ni jambo la kuipongeza Serikali. Pia uwiano wa matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo umeongezeka. Nilikuwa nafikiri kwamba tuiangalie vizuri kwa baadhi ya maeneo, kwa mfano kwenye Halmashauri zetu au Serikali za Mitaa bajeti ya maendeleo iongezwe. Kwa sasa hivi tuna kama trilioni 1.3 ambayo tunaipeleka kwenye Serikali zetu za Mitaa. Hali itakapokuwa nzuri tusukume hizi pesa za maendeleo ziende zaidi kwenye Serikali zetu za Mitaa ili isaidie kuondoa baadhi ya matatizo yaliyo mengi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa pia na juhudi za Serikali kuangalia suala zima la usimamizi wa kodi. Kwa hiyo, ni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa Kwandikwa.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, na kabla sijafika mbali Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango naomba masuala mawili haya ambayo kwenye hotuba yako hujayazingatia nipate ufafanuzi; sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuna ushuru na tozo mbalimbali ambazo toka Bunge lililopita tunapiga kelele kwamba wakulima katika sekta hiyo hawatafika mbali kwa sababu ya ushuru na tozo ambazo hazina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwenye hotuba yako hapa umebaki tu kutaja kwamba kuna hizo changamoto, lakini hujatuletea hizo sheria mbalimbali kwa ajili ya kuzifuta ili wakulima waweze kuifanya Tanzania yetu kuwa nchi ya viwanda. Na wewe Mheshimiwa Mwijage hivyo viwanda unavyovihubiri havitakuwepo kama sekta hii ya kilimo tunafanya nayo mzaha wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la maji. Maji vijijini tulitenga Shilingi 50 kila lita ya mafuta ya *petrol* na *diesel* kuanzia Bunge lililopita kuwekwa kwenye mfuko wa maji, lakini zile fedha zikapelekwa maji mjini matokeo yake

mpaka leo vijijini bado kunashida ya maji. Wabunge hapa tulisema na tukashauri tuongeze kutoka shilingi 50 kwenda shilingi 100, lakini kwenye hotuba yako ya bajeti unasema itabaki hivyo hivyo shilingi 50. Tunaomba tuweke shilingi 50 kwenye mafuta ili tuweze kuwa na mfuko mzuri wa maji vijijini; na hakutakuwa na mfumuko wa bei. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, John Pombe Maghufuli, kwa juhudi zake anazozifanya za kutumbua majipu katika nchi yetu na nimshukuru kwamba analeta Mahakama ya Mafisadi na zile rushwa kubwa za manyangumi. Lakini juhudi hizi za Mheshimiwa Rais, hatazifikisha mwakani endapo atabaki peke yake mtumbua majibu wakati mtambua na mbaini majipu ambaye ni CAG ataendelea kuwa na fedha shilingi bilioni nne katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kupunguza bajeti ya CAG ambapo mwaka jana alikuwa na shilingi bilioni 74; wakati fedha za miradi ya maendeleo zilikuwa ni kidogo kuliko mwaka huu, tuna trilioni 11 halafu ndipo mnampa shilingi bilioni 44. Hii ni dalili kwamba bajeti hii inataka kukumbatia mafisadi kwa sababu CAG ndiye anayekagua miradi na mikataba ambayo ni ya kifisadi. Kitendo cha kuminya Ofisi ya CAG, nakuambia Mheshimiwa Waziri Mpango, utumbuaji wa majibu utaishia mwaka huu; Rais hatakuwa na majipu ya kutumbua tena kama bajeti ya CAG haitaongezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niseme bayana, hata hawa watumishi hewa ambao sasa wanatumbuliwa, juhudi kubwa zilifanywa na CAG Bunge lililopita akawa anabaini watumishi hewa, miradi hii ambayo mingine tunapigwa kwenye barabara na sasa tunapeleka asilimia 40 kwenye miradi ya maendeleo, kama CAG ofisi yake itaminywa haya majipu yakifisadi nani atayabaini na hizi fedha mnazosema mnawezesha TAKUKURU; TAKUKURU atawachunguza mafisadi gani ambao hawajabainiwa na CAG?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwangu mimi bila kumwongeza fedha CAG ambaye ndio jicho, ambaye ndiye ameikomboa nchi hii kwa kubaini mafisadi, nakuhakikishia Mheshimiwa Rais wetu, mwakani hatakuwa hata na kijipu chungu; hata kipele cha kuweze kutumbua, kwa sababu CAG atakuwa hajafanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hii hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mpango ya kuondoa msamaha kwenye mafao ya Wabunge. Mheshimiwa Mpango naomba nikuulize, hawa Wabunge ambao unaondoa msamaha kwenye mafao yao unajua kwamba hawana pensheni? Unajua kwamba Wabunge hawa sio pensionable? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge sisi hufanya kazi yetu miaka mitano tu hapa, hatuna *pension*, matokeo yake tunaambulia hicho kidogo; fedha nyingine ni nauli, mizigo, vifedha vingine ndio vile ambavyo tumevidunduliza kwenye mshahara tunawekewa kila mwezi. Sasa wewe unataka kuondoa msamaha. Nataka nikuhakikishie kuanzia utawala Mkapa, Wabunge walikuwa wanaomba hata watumishi wengine mafao yao yasije yakakatwa kodi kwa sababu wamefanya kazi miaka 30, 40 watumishi wanakatwa fedha, wanaenda wengine wanakufa kesho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tumefika pazuri baada ya kuondoa kundi la Wabunge. Tulitarajia katika Bajeti hii sasa unatuletea sheria ya kwenda hata kufuta hizo kodi za mafao ya watumishi wengine Serikalini, sasa matokeo yake unatuletea tena kufuta za Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi, akiwepo Mheshimiwa Makinda hapa alisema amechoka kusumbuliwa Wabunge ambao walishastaafu wamekuwa wakija ofisini wanamwomba hela, wamekuwa ombaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge leo maslahi yetu tumedunduliziwa na kila mwezi tunakatwa kodi ya mapato halafu tena mafao yetu ambayo yamelimbikizwa na yenyewe yakakatwe kodi mnataka turudi mtaani halafu muanze tena kutucheka. Lazima Wabunge tulinde maslahi yetu, Mheshimiwa Waziri usicheze na maslahi yetu, lazima tulinde maslahi yetu. Hatuwezi kukubali fedha ambazo sisi kila mwezi tunakatwa kodi *Pay as You Earn* na nyingine ile tunawekewa pale halafu baada ya kutoka hapa uanze tena kututoza kodi. Waheshimiwa Wabunge tusikubali sisi hatuna pensheni lazima kodi hii isiwekwe kwenye fedha za Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mpango, sisi Wabunge mshahara wetu ni mdogo sana kuliko wa kwako, wewe mshahara wako ni mkubwa. Sisi Wabunge kule mtaani ndio ATM hata sasa hivi humu kila simu ya Mbunge sijui kuna msiba wapi, kuna kisima kimeharibika, kuna darasa upepo umeezua, ndipo hapo hapo tunapotoa pesa. Halafu Mheshimiwa Mpango unataka kucheza na maslahi ya Mbunge na wewe hapo ulipo wewe Jimbo lako ni Mheshimiwa Rais, sisi Jimbo letu ni wananchi kule. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiomba fedha hata za kukarabati chuma kidogo tu kwenye pampu ya maji kutoka Halmashauri unaambiwa wewe Mbunge saidia. Tunaomba Halmashauri kuna kadaraja pale kamekatika kidogo pelekoni fedha wanasema kazi ya Mbunge, kazi ya mwenge. Halafu leo hata hicho kidogo na ndiyo maana unanikumbusha lile tangazo kwenye TV walikuwa wameweka kakuku pale linakuja lile kama fisadi mara ya kwanza

likakata robo tatu ya kuku haadam! Halafu kakabaki karobo likamalizia tena haamm! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mpango asitupeleke huko, fedha zetu ni kidogo sana matokeo yake unaanza kuzikwangua tena, je, tutakapofika mwakani utakuja tena na ajenda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu wa CHADEMA hapa alikuwa anawasilisha bajeti hapa nikaona mhh! Huyu ndiye Silinde kweli? Anashabikia kwamba eti na sisi tunaunga mkono hii kodi wakatwe.

Mheshimiwa Mpango wewe ni mchumi kuna kitu kinaitwa *free rider problem*, huyu pamoja na kuipiga panga kwamba haitaki wanajua sisi tukiitetea na wao pia watapata *free rider problem*. Asidanganye wananchi hapa UKAWA wata-enjoy *free rider problem* baada ya sisi kuitetea na wewe ni mchumi unajua maana ya *free rider problem*, hatutakubali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, anazungumzia masuala ya *sitting allowance*, leo, mimi nadhani alikuwa anachomekea tu kwa sababu wana ugomvi na mama yetu pale wanachomekea chomekea vitu na sisi hivi vitu vya kuchomekea hivi mama wala usiwe na wasi wasi wewe ndiye Naibu Spika na wao walikuchagua na sisi tumekuchagua hicho kiti utakikalia mpaka wewe mwenyewe utakaposema sasa basi. (Makofi)

Mheshimiwa Mpango utakapokuja kutoa majumuisho fedha hizi za CAG bila kupanda na bila kutoa kauli hapa kwamba hicho ulichojaribu cha kutu-beep juu ya maslahi yetu hatutaelewana. Na ninashukuru umetu-beep na sisi tumeamua kukupigia. Tunakwenda wapi? Na watumishi wengine wote wale tulishasema fedha zao zile msizikate kodi zile. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi muda wako umekwisha.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye mawasilisho ya bajeti iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwa kuipongeza sana Kamati ya Bajeti, imefanya kazi kubwa, na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu

tusome sana hotuba ya Kamati ya Bajeti, wamekuwa wazalendo kweli kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane nao kuzungumzia masikitiko yangu kwamba kama kweli Bunge hili linataka kutumika kama *rubber stamp* Wabunge tukatae kwa nguvu zetu zote. Tulifanya kazi kubwa ya kuja na *Budget Act*, tukasema ni sheria inayokuja kututoa kwenye kufanya mambo kama *business as usual*. Ninyi leo mnataka kuturudisha kule?

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati inalalamika kwamba haikuzingatia maoni ya Kamati, Wabunge tusikubali asilani. Serikali hii ni sikivu, sikieni haya yanayosemwa na Kamati ya Bajeti, sikieni haya yanayosemwa na Wabunge. Nchi hii yetu sote, tukifika mahali kikundi fulani kikajiona chenyewe kinajua zaidi ya Wabunge tuna tatizo kama nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma mpango, Ripoti ya Hali ya Uchumi inatuambia sekta ya ujenzi imeongoza kwa kuchangia kwa asilimia 16.8, sekta ya habari na mawasiliano asilimia 12, sekta ya fedha na bima asilimia 11, sekta ya madini asilimia 9.1; lakini sekta zote hizi zinashughulisha watu wachache. Sekta inayoajiri asilimia 70 ukuaji umeshuka. Sekta ya kilimo ukuaji umeshuka kutoka asilimia 3.4 sasa ni asilimia 2.3 *and yet we are happy*, hii haikubaliki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nataka nijielekeze kwenye eneo moja, sekta ya uvuvi hivi tunataka tuambiweje ili tuelewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti ya mwaka 2014 ya *state of the fisheries* ya Shirika la Chakula Duniani inasema kwamba uzalishaji wa samaki kupitia ufugaji (*aquaculture*) ulikuwa ni tani milioni 100 ulimwenguni; pasipo kuzungumzia uvuvi bali ufugaji wa samaki; zenye thamani ya bilioni 144.4. Hivi watanzania hatutaki kushiriki kwenye uchumi mkubwa kiasi hiki? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uzalishaji huo Asia imezalisha asilimia 88 ya hizi, Amerika asilimia 4.7, Europe asilimia 4.3, Afrika asilimia 2.2, kwa maana kwamba imezalisha tani milioni 1.4. Lakini angalia kichekesho chake katika tani milioni 1.4. Lakini angalia kichekesho chake, katika tani milioni 1.4 Misri peke yake imezalisha tani milioni 1, nchi nyingine za Afrika ndio tunanyanganyia 0.4. Lakini Misri hii ufugaji huu wa samaki inategemea maji kutoka Mto Nile, Tanzania ikiwa sehemu ya uchangiaji wa maji ya Mto Nile. Sisi tuna ziwa Victoria, Tanganyika, tuna bahari, tuna Ziwa Nyasa tumelala usingizi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi mkubwa kama China wanaona umuhimu wa kushiriki kwenye uchumi huu, wanazalisha nusu ya samaki wanaofugwa ulimwenguni. Sisi Watanzania tunaona sekta hii ya kipuuzi,

tubadilike. Ni kwa kupuuza vitu kama hivi ndiyo maana leo hii mchango wa sekta ya uvuvi umeshuka, na umekuwa ukishuka tangu mwaka 2007. Mchango wa sekta hii ilikuwa asilimia 1.7, tumeporomoka mpaka asilimia 1.2 mwaka jana, lazima tubadilike. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati kwa kuzungumzia suala la mfuko wa maji, safari hii msitufanyie kiini macho. Mwaka wa jana tulisema fedha zile ziende vijijini mkazipeleka mijini safari hii pelekeni fedha zile vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti imesema tuweke tozo kwenye mafuta mbona Wakenya wameweka bajeti yao ya juzi? Tuweke tozo kwenye mafuta, twende tukajenge zahanati. Hii ni aibu kwamba tangu mwaka 2000 tunaweka kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwamba tutapeleka zahanati kwenye kila kijiji tumekwenda kwa asilimia 20 tu. Tutenge bajeti twende tukajenge zahanati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuongeze fedha za maji, wananchi wetu wanataabika vijijini. Pale Mkinga kuna *one stop border post*, tumeambiwa kimekamilika; kituo kile hakina maji. Mheshimiwa Mpango watu wako watakuwa kwenye ofisi ile haina maji; yatakuwa yanachukuliwa kutoka Kenya. Tuna mradi wa bilioni sita tupeni fedha tukafanye mambo pale. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitandula muda wako umekwisha.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante. (Makofi)

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsate kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa siku hii ya leo. Lakini kubwa nimpongeze Waziri wa Fedha na timu zake zote kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa kweli hotuba nzuri na mwelekeo wa bajeti hii ni mzuri, angalau unaweza ukapunguza makali ya umaskini wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Waziri wa Fedha nimeona kuna asilimia tano ya mapato ya Halmashauri zetu nchini ambao huwa wanatenga asilimia 10 vijana asilimia tano na wanawake asilimia tano.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mimi nikuombe, chonde chonde asilimia hii tano ni ya miaka dahari na dahari iko pale pale tunaondoaje umaskini na



tunapunguzaje umaskini? Lakini kama tuna nia ya dhati ya kupunguza umaskini; katika hotuba yako umesema ongezeko la makusanyo ya mapato yetu limeongezeka kwa kutokana na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mianya ya rushwa imezuiliwa, wafanyakazi hewa mshahara wake upo umeingia kwenye mapato, wakwepaji kodi ambao walikuwa wanakwepa mpaka kuingiza makontena hela yake ipo, mapato ya gesi na cement viwanda vyake vipo. Mimi nikuombe Mheshimiwa kwa heshima na taadhima kubwa hebu muangalie sekta hii ya waakina mama na vijana ajira haipo, lakini tunapobana tu asilimia tano umekuwa wimbo wa Taifa na Halmashauri hizo asilimia kubwa hawakidhi viwango vya kupeleke hii asilimia 10. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri, yeye kwa huruma yake atusaidie kwa hilo ili angalau sasa aongeze kwa njia moja au nyingine anavyoona yeye inafaa kwa mapato haya mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie shilingi milioni 50. Kuna Mbunge mwenzangu hapa amezungumzia; kwa sababu tukiipeleka kwenye SACCOS moja kwa moja yatarudi yale ya Mfuko wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa sababu wajanja wote ndio wenye SACCOS, vijijini kule hawana SACCOS, sasa inakuwa ni masharti makubwa kiasi ambacho watanuafaika watu wachache. Mimi nadhani Serikali ina wataalamu wazuri wa maendeleo ifanye utaratibu isifanye haraka ya kusambaza hela kupitia SACCOS. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Wenyeviti wa Mitaa, tuna Makatibu tarafa Wakuu wa Wilaya ndio wanaohodhi eneo la kijiji chote. Mimi ningeomba kabla hamjafanya maamuzi ya kupeleka kwenye SACCOS mimi naomba pesa hizi ziende kwa utaratibu wa vijiji, pia kila Jimbo wapewe maana ndiyo tupo shuleni sasa, ya kwanza ilipita *free*, sasa hii maadamu tunaipigia sasa; na kwa kuwa Rais hakutoa ahadi mijini, amepita kwenye kampeni yake vijijini kote pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais; isiwe kwa kuwa wale wa mjini kwa sababu ndio wenye SACCOS nyingi wapate, vijijini ambapo hakuna wakose. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba hilo liangaliwe sana kwa sababu tuna mengi ya kuongea, lakini niombe hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine afya. Mheshimiwa Waziri wa Fedha mimi niombe katika fedha za mwaka huu Wizara ya Afya tuna miradi mingi ambayo haijakamilika, tuna zahanati nyingi zimejengwa na zina hospitali ambazo zimejengwa hazina *theatre*, kuna wafadhili wamekuja wameweka vifaa vyao hivi mnawaambiaje? kwa sababu kila mwaka watafuatilia pesa zao ziko pale lakini mnasema daktari wa usingizi hayupo.



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kama Zahanati ya Bukene Mawaziri wote wamepita pale wameiona waakina mama wanakufa, hivi unapunguzaje vifo wakati ipo tayari vifaa vya kisasa ambavyo hata Muhimbili hawana, Bungando hawana vipo pale kwa ajili ya kuokoa maisha ya mama na mtoto. Kwa hiyo, mimi niombe kipaumbele Wizara ya Afya iangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nimeangalia kitabu hiki katika kupunguza kodi, kuondoa misamaha bado hujatoa misamaha kwa nguo za akina mama, kwa lugha nyingine mataulo yao bado sijaiona. Kuna wanafunzi wanashindwa hata kununua pedi, leo hakuna uondoaji wa kodi. Mimi ningeomba Serikali hata hii inapata kigugumizi gani kutoa iondoe kodi ili angalau viweze kuingia kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumzia tozo nyingi za tumbaku. Hivi unaweka tozo nyingi za tumbaku halafu unasema unamsaidia mkulima? Mheshimiwa Waziri wa Kilimo liangalieni hili mnapokaa kwenye Baraza la Mawaziri, tozo ni nyingi hazifai, wakulima wanazidi kuwa maskini, kilimo chenyewe cha mkono lakini hawapati msaada wowote kutoka Serikalini. Mimi naomba Serikali iangalie sana suala zima la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia pamoja na hayo sekta hii imetengwa haisaidiwi na Serikali, hawa wanunuaji wa tumbaku wanajipangia wenyewe bei, wanaamua juu ya soko wanavyotaka wenyewe. Waziri wa Fedha utapataje ongezeko la pesa ikiwa wakulima wa tumbaku wananyanyaswa ambao asilimia 60 ya tumbaku wanayolima inasaidia mapato ya Serikali? Kwa hiyo, hilo nalo ningeomba Serikali muangalie tuna hali ngumu sana huku wakulima wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee habari ya maji. Ukigusa umegusa wanawake, akina baba wote humu mnafuliwa nguo na akina mama, mnapikiwa na akina mama, lakini wao ndiyo wanahangaika na maji. Leo hakuna bajeti inayoeleweka ikaambiwa kwamba hii ni bajeti ya maji. Mheshimiwa Waziri, mimi nimesikia sana hotuba zako, umesifia wanawake, umewaonea huruma wanawake, sasa huu Mfuko wa Maji Vijijini toka kwenye 50, weka kwenye 100 hili suala usisumbuke... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwamuda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mchemba, muda wako umekwisha.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangiaji mchana, nitayasoma kwenu majina ya wale ambao wataanza kuchangia mchana.

Tutaanza na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Selemeni Kakoso, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Stephen Ngonyani, hao ndiyo tutakao anza nao mchana.

Lakini kuna wageni niliwasitangaza asubuhi, hawakuwa wamepata nafasi ya kuingia. Tunao wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu ambao ni watu wenye ualbino kutoka Shirika la *Save Vulnerable Foundation*, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Angellah Kairuki lakini idadi niliyotajiwa hapa siwaoni kama wapo. Wageni wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, nadhani wameshatoka nje, haya karibuni sana. Hapa nimetajiwa idadi lakini nimeambiwa wanaongozwa na Mchungaji Godwin Lekundai, karibuni sana. (Makofi)

Tangazo lingine kuna Mheshimiwa amepoteza miwani yake, anaomba yeyote atakayeiona miwani ambayo iko karibu nae au si ya kwake atufikishie ofisini ili aweze kuja kuichukua.

Tangazo lingine linahusu michezo, kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri kutakuwa na mechi ya mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club* na ndugu zetu wenye ualbino na wote mnakaribishwa. Tangazo limetoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*. (Makofi)

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi juu ya Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi kuonesha kitendo chenye kuashiria matusi wakati akitoka ukumbini baada ya kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhidhi wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge pia kuna Mwongozo ambao ningependa kuusoma kwenu, na huu ni Mwongozo kuhusu suala lililolombewa mwongozo na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kuhusu suala la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kuonesha kitendo chenye kuashiria matusi wakati akitoka

ukumbini baada ya kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumatatu tarehe 6 Juni katika Kikao cha 37 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi alisimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu suala la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kulidhalilisha Bunge na kudharau mamlaka ya Spika kwa kuonesha dole, kitendo ambacho ni matusi.

Ilielezwa kuwa kitendo hicho kilifanyika wakati Mheshimiwa Mbilinyi alipokuwa anatoka ukumbini baada ya kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa na mbinu za Kuongeza Nguvu nichezoni.

Katika kujenga hoja juu ya mwongozo huo, alisema:-

"Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani wakati alipokuwa amekuja kuwasilisha hapa, alipokuwa anaondoka kama wenzangu Wabunge wengine nadhani watakuwa wameona na pia imeoneshwa hata kwenye camera ameonesha dole, na hii ni matusi makubwa sana. Kwanza amelidhalilisha Bunge, lakini pia amedhalilisha kiti chako."

Mheshimiwa Sixtus Mapunda alikuwa pia amesimama sambamba na Mheshimiwa Msongozi kuashiria kuomba Mwongozo. Alipopewa nafasi alieleza kuwa, Mwongozo aliotaka kuomba ulikuwa ni hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge aliyepewa nafasi kabla yake.

Baada ya kuomba Mwongozo Mheshimiwa Msongozi nilieleza Bunge kwamba binafsi sikumuona Mheshimiwa Mbilinyi iwapo alionesha alama iliyolalamikiwa kuwa ni alama mbaya ama ni matusi. Nilieleza kuwa nitalifuatilia jambo hilo na nitalitolea maelezo.

Jambo linaloombewa Mwongozo linahusu maadili ya Bunge. Mwongozo huo unatokana na kitendo cha Mheshimiwa Mbunge kuonesha kitendo ambacho kinatafsiri ya matusi. Endapo itathibitika kuwa kitendo hicho kimetendeka itakuwa ni kinyume na masharti ya Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, kifungu cha 4(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge pamoja na majukumu mengine, imepewa jukumu ya kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge. Nitanukuu kwa sehemu:-

“Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo; (b) kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika.”

Kutokana na maelezo ya hapo juu na masharti ya Kanuni nilizozitaja, naelekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ifanye uchunguzi kuhusu kitendo kinachodaiwa kufanywa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na kuchukua hatua stahiki. Huu ndiyo mwongozo wangu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10 jioni leo.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi sa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaanza na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Joseph Raymond.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni bajeti ya Serikali wala siyo ya Dkt. Mpango. Wapo watu wengine wanalaumu kama vile Dkt. Mpango hii bajeti ni ya kwake, hii ni bajeti ya Serikali inayosomwa na Waziri wa Fedha Dkt. Mpango. Kwa hiyo niwaombe sana tunapojadili tujadili bajeti, tusijadili mtu alivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri kwa Dkt. Mpango kwa sababu yeye ndiye Waziri wa Fedha, yapo mawazo mazuri sana ya Kamati, nashauri kwa mfano suala zima la maji ile tozo kutoka sh. 50/= kwenda sh. 100/= Wabunge wote, Watanzania wote, kama itaongezwa iwe sh. 100 kwa ajili ya maji, nina uhakika Watanzania watanufaika, naomba suala hili ulitazame kwa jicho jema. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, mtoto mdogo anategemea maji, akinamama kule wanategemea maji, maji yakiwa mengi vijijini kero kwa chama changu itapungua. Nakuomba sana juu ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, imependekezwa, Mheshimiwa Waziri najua yeye ni muungwana sana, chombo chetu kikuu, kisemeo cha Serikali ni TBC, TBC ndiyo mdomo wa Serikali, TBC ndicho chombo ambacho

kinaweza kusema kwamba hapa sasa Serikali ifanye hivi, namwomba hebu atumie busara na watalaam wake, hili nalo alione. Mheshimiwa Waziri tukifanya hivyo kwa kweli tutakuwa tumefanya jambo jema. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nimelifurahia sana na niipongeze sana Serikali, nimekuwa Mbunge wa siku nyingi kidogo humu ndani, Wabunge wote wa Vyama vyote tulitakiwa tuipongeze sana Serikali kwa kutenga asilimia 40 ya pesa ya bajeti kwenda kwenye maendeleo, haijawahi kutokea. Nilitegemea Wabunge wote watapongeza kwa sababu pesa hizi asilimia 40 ya bajeti ya trilioni 29 inakwenda kwenye shughuli za maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba, ingekuwa ni amri yangu kwa sababu kweli tumetoka kwenye asilimia 23 tumekwenda sasa kwenye asilimia 40 lazima tuipongeze sana Serikali. Mbali na hilo katika ukurasa wa 98 wa kitabu chako, ninakushauri ile aya ya 102 unapoanza kwanza mpaka namba kumi nishauri hii ndiyo iwe kama ndiyo amri kumi kwa sababu yako maagizo kumi, hii ndiyo iwe amri kumi, sitaki kusema kwa sababu ya muda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri maelezo aliyoyaeleza hapa kuanzia kipengele cha Kwanza, Pili, Tatu, Nne, Tano, Sita, Saba, Nane, Tisa na Kumi, iwe ndiyo mwongozo kwa Maafisa Masuuli wote Tanzania. Atakayekiuka haya wala tusimwonee aibu, kwa sababu ili pesa hizi ziende kufanya kazi yake vizuri, hii asilimia 40 ya bajeti yote kama hizi amri kumi alizoziorodhesha zikisimamiwa vizuri, nina uhakika tutasonga mbele, tukifanya hivyo na naomba nirudie kusema tena hapa, Maafisa Masuuli wote waandikiwe *secular* kuhusu hizi amri kumi wazitekeleze. Mimi naziita amri kumi kwa sababu kwa jinsi alivyozipanga na kama kila mtu akifuata moja baada ya nyingine, nina uhakika tutafika mbali sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naunga mkono, kwanza niipongeze sana TRA kwa kufanya kazi vizuri sana. Tunawaamini, mmepewa jukumu zito, lakini niwaombe hasa kwa upande wa kodi za majengo, tukisimamia vizuri kodi za majengo, Dar es Salaam tukafanya tathmini ya kutosha, Mwanza tukafanya tathmini ya kutosha, Arusha na maeneo mengine tukafanya tathmini ya kutosha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna pesa nyingi sana pale, tutaboresha miji yetu, tutaboresha miundombinu yetu, kwa sababu pesa zilizoko pale zilikuwa zinapotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine kwa Waziri wa Fedha na Wabunge wenzangu, naomba kuhusu misamaha ya kodi, sikubaliani nayo, lakini hebu mkae vizuri na Wataalam wako mwangalie hasa upande wa madhehebu ya dini, tusiwahukumu kiujumla tukae, tufanye tathmini ya kina,

najua mmeshafanya, kwa sababu madhehebu ya dini mengine yanatoa huduma upande wa hospitali, upande wa shule. Kwa hiyo, naomba sana kuhusu hili, mkae mfanye tathmini ya kutosha ili tusilete mgogoro na madhehebu ya dini. Najua Serikali yangu ni sikivu hili italifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine niipongeze Serikali na niweke tu msisitizo, nimesema leo kazi yangu ni kushauri bajeti ijayo ndiyo tutakwenda kwa *detail*. Kuhusu ujenzi wa reli naipongeza sana Serikali, ununuaji wa ndege hili wala msichelewe, msisikilize yale maneno ya kule, kwa sababu najua Serikali imekaa. Nawashangaa watu wengine tulikuwa tukisimama humu tunasema Tanzania hatuna ndege sasa Serikali imekuja na mpango mzuri wa kununua ndege tatu, watu wengine wanaanza kuhoji! Jamani hivi tunataka Serikali ifanye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nashauri asiwe na kigugumizi kununua hizi ndege tatu, atwange mzigo, alete ndege tatu hizo ili kusudi Watanzania watumie ndege zao, siyo ndege zile zingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni ununuzi wa meli, chonde chonde! Meli hizi kwa jinsi ambavyo mmejipanga kama Serikali zinunuliwe bila kusuasua, hivyo maeneo ambayo tumeshaahidi kuwa tutanunua meli au kukarabati tufanye bila kuchelewa. Ili tufanye hivyo niwaombe sana wenzetu wa TRA kwa sababu tunawategemea. TRA ni kama mshipa kwenye mwili wa binadamu, ukikatika mshipa mmoja au ukisimama mshipa mmoja, ina maana eneo moja lita-*paralise*, kwa hiyo ili tutekeleze haya ambayo Dkt. Mpango Waziri wa Fedha ameyaaisha humu ndani ni lazima makusanyo yakusanywe na yasimamiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukusanya matumizi yetu yawe na nidhamu, tukifanya hivyo tutakwenda vizuri. Kwa kweli naunga mkono sana bajeti hii kwa sababu ina mambo mengi sana mazuri na imegusa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo Waziri wa Kilimo ni muhimu kuliangalia, hebu tazama kwenye tozo za mazao, tumeyasema mwanzo tozo ni nyingi, ni kero, hebu ziondoeni kwa sababu zinawapa matatizo watu wetu, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Waziri wa Ardhi, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Maliasili wakae pamoja waangalie namna ya kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji, yale maeneo ambayo sasa hayana sifa tena ya kuwa mapori ya hifadhi, wakae na waangalie namna nzuri wayagawe ili watu wetu, wakulima na wafugaji waweze kuyatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kipekee kabisa namshukuru Mungu kwamba, ametuweka tena hapa kuzungumzia maendeleo ya nchi yetu, hii ni fursa ya pekee kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeze sana Waziri wetu wa Fedha na Mipango. Bajeti hii ni nzuri na imeweka mazingira ambayo yataweza kuwavutia wawekezaji wa nje na ndani, lakini kuna maeneo ambayo yanatakiwa tuyaangalie kwa undani zaidi, nitaongelea kwa hawa wawekezaji wetu wa ndani ambao ni wakulima, wavuvi, wafugaji na wachimbaji wadogo wadogo, kwa sababu hao ndiyo walio karibu zaidi na wale wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu lazima iweke mazingira rafiki kwa watu hawa kuweza kufanya shughuli zao, hawa wakifanya biashara zao vizuri au wakifanya mafanikio katika biashara zao watawezesha wale wananchi wa kawaida ambao wanatumia bidhaa zao wapate chochote ili waweze kukitumia na hivyo basi kwa kutumia vile ambavyo hawa wanazalisha kodi itapatikana na itachangia katika bajeti yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ina maeneo mawili, kuna ukusanyaji wa mapato na matumizi ya mapato. Ni muhimu kabisa wote tulio hapa na walio nje waone jinsi gani makusanyo yanafanyika na yanafanikiwa. Mara nyingi makusanyo yakishakuwa kidogo hata matumizi hayapatikani kabisa. Bajeti ya mwaka uliopita, mwaka 2015/2016 tuliona jinsi gani makusanyo yalisuasua na haya yalipelekea matumizi kutokufanyika kwa wakati. Suala hili la wakati ni suala ambalo linafanya mambo yote yanakuwa hayatekelezeki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kabisa ambavyo watu wamekuja kupewa hela miezi miwili kabla au wanapewa hela kipindi ambacho hawawezi kuzitumia tena. Hii inawapelekea wale watu kutumia vibaya kwa ubadhirifu au inaleta mambo mengine ambayo siyo mazuri. Naomba kuanzia sasa tusimamie makusanyo na hapa nipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano, tumeona makusanyo ambavyo ni mazuri, tunaambiwa kwa mwezi ni triloni moja na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuyasimamie makusanyo hayo na yaende sasa na jinsi bajeti ilivyopangiliwa, makusanyo yaende kama yalivyopangiliwa kwenye matumizi. Wale ambao wanapewa kutumia wasimamiwe, kwa sababu kama hujampa huna cha kumsimamia na wewe sasa huwezi kumuuliza chochote, unamuulizaje na hukumpatia? Naomba hilo liwe angalizo na wote tushirikiane kuona inaendaje. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia hapa ni kuhusu vijana na wanawake, nikisema vijana ile dhana kwamba kijana ni mtoto wa kiume tu hapana hata mabinti zetu ni vijana, vijana ni 'ke' na 'me' sasa inapokuja kwamba wanafanya shughuli zao mathalani wengi wa vijana wetu wanafanya mambo ya saluni za kike na kiume, lakini pia wana ujasiriamali wa lishe, kuna hawa ambao wanapika na kuna wengine ambao wanatengeneza vitu ambavyo vimekaushwa, kama ndizi za kukausha, popcorn na vitu vingine, yote hiyo ni vitu vya ujasiriamali mdogomdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanatakiwa wawezeshwe kwenye vifungashio ili wafanye vitu vyao kwa usafi. Nani atakayewawezesha? Ni Serikali iweke mazingira rafiki ya wale ambao wanawapatia vifungashio hivyo vipatikane kwa wingi na kwa urahisi. *SIDO* ndiyo mahali ambapo vifungashio hivyo vingetoka kwa urahisi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona maeneo ambayo *SIDO* imetamkwa kwamba itasaidika au itafunguliwa zaidi. Nimeona Mkoa wa Mbeya, nimeona Mkoa wa Pwani lakini sikusikia Kilimanjaro ikitajwa, naomba kwa vile ile *SIDO* ya Kilimanjaro iko vizuri na vitu hivi vinafanyika, Mheshimiwa Waziri wetu wa Viwanda na Biashara aweke jicho lake kule. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mengi ya kutaka tushirikiane lakini sasa muda siyo rafiki kwangu; naomba nirudi kwenye jambo moja ambalo naona nisipolisema leo nitaweza nikakosa usingizi, kuhusu Serikali kulipa madeni yake ya ndani. Tulizungumza hapa na wakatueleza ambavyo taasisi zake zinadaiwa na mojawapo ikiwa ni taasisi ya maji inayoitwa MUWSA kule katika Mkoa wa Kilimanjaro. Mamlaka ya maji ile imefinywa sana, wametoa maji katika Chuo cha Polisi (CCP) na maeneo mengine ya Serikali kama Magereza lakini maji yale hayalipiwi. Itamkwe wazi kama Serikali inaona taasisi hizo zitumie maji bure ijulikane!

Mheshimiwa Naibu Spika, napata uchungu, inabidi sasa maji yapandishwe bei na anayeumia kwenye maji zaidi ni mwanamke, mwanamke yule atasaidiwa! Inawezekanaje taasisi za Serikali zitumie maji bure na zile mamlaka zinajilipa mishahara zenyewe hazitegemei Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena naomba Serikali ilipe madeni yake mapema iwezekanavyo, taasisi zile zifufuke ziweze kununua vitendea kazi kama magari. Tumeambiwa kwamba, kuanzia sasa madeni ya taasisi yatalipwa *centrally*, naomba Hazina ilipe haya madeni mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu hizi milioni 50 za kila Kijiji. Nauliza, inapozungumziwa hapa kama ndiyo kwanza imeanza inakuwaje? Tulikuwa na hela za uwezeshaji kwa wanawake kuanzia enzi za Mwalimu

Nyerere, zikaja mabilioni ya Kikwete, lakini zikishatolewa hivyo hakuna ufatiliaji, nendeni kule kwenye zile benki, achene kuziachia benki zinaateseka na pesa ambazo zinawekwa kwenye *suspense*. Naomba Serikali ikadai kupitia Wizara ya Fedha, hatuanzi kwenye *clean plate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo najua kwamba zile zikipatikana na hizi milioni 50 zitakuwa zimekuwa nyingi tutakuwa tumefungua wigo wa kuwawezesha wanawake na vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru nisingependa kengele ya pili inigongee. Naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa muda na mimi nichangie. Kwanza na-*declare interest* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na nimefurahi sana kusoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, hotuba yake ni nzuri inajieleza vizuri sana kwa sababu imegusa maeneo muhimu yote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo limenifurahisha sana ni kwamba, hotuba ya Waziri imegusa sana malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, mambo ambayo tuliahidi, Mheshimiwa Rais aliahidi na Wabunge huwa tunasema kwenye Majimbo yetu, yote yameandikwa humu. Tunakuombea sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha haya tuliyoandika Mungu atusaidie tuweze kukusanya vizuri kodi ili tuweze kutekeleza. Jambo lolote ili lifanyike vizuri lazima kuwe kuna fedha, bila fedha hatuwezi kufanya kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimempenda sana Mheshimiwa Waziri ameweka mikakati jinsi ya kupata hizi trilioni 29. Kupata trilioni 29 ni nyingi sana ukilinganisha na mwaka 2015/2016 tulikuwa na bajeti ya trilioni 22 sasa hivi imeongezeka tuko trilioni 29, kukusanya mpaka tufike trilioni 29 ni muziki mkubwa. Ameeleza vizuri sana kwenye hotuba yake kwamba atapataje hizo trilioni 29, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumeeleza vizuri sana kwenye bajeti. Namwomba tu Waziri wakati anahitimisha hotuba yake hii aangalie na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti ni ya msingi na ukiyasoma vizuri pale utakuta kuna mambo mengine tunaenda sawa, kuna mambo mengine tumetoa ushauri. Jambo ambalo limenifurahisha, tumesema kwamba Tanzania itakuwa Tanzania ya viwanda na tumesema

lengo kubwa kuwa Tanzania ya viwanda ni kugusa watu wa kima cha chini. Hiyo ni kweli kabisa nami hiyo nimeipenda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya Viwanda ili ikamilike vizuri kuna mambo Mheshimiwa Waziri ameeleza, amesema kwamba, atahakikisha anajenga reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Tunajua ni mwaka huu wa fedha wa 2016/2017, lakini hatujui kwamba reli itakwisha kwa mwaka mmoja, tunaweza tukaanza mahali pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana katika uchukuzi, ukiangalia bajeti ya Uchukuzi na ukachukua bajeti ya Ujenzi tuki-*compare* pamoja inatenga trilioni nne. Hizi trilioni nne zikisimamiwa vizuri, tukaanza kujenga vizuri hiyo reli ya kati, itatusaidia sana na hii *concept* ya viwanda itakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kitu kimoja, reli hizi tunazo nyingi sana. Tuna reli ya Kati, tuna TAZARA, tuna reli nyingine hii inatoka Tanga inakuja Moshi mpaka Arusha. Tunapozungumza viwanda maana yake malighafi zote tutatumia reli kwa kusafirisha mizigo yetu. Namwomba Waziri wa Fedha, tuna reli nyingine ile inayopita Makambako, kwenye Jimbo langu pale ya Mgololo, watuwekee *station* pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na *station* ya reli ya TAZARA pale, tunajua wasafiri au wanaosafirisha mbao badala ya kutumia barabara ya lami ambayo tunajua barabara inaharibika kila siku, basi mbao zitasafirishwa kwa njia ya treni, hapo watakuwa wametusaidia sana. Kuna kituo kidogo sana, treni pale inasimama hata dakika tano haifiki, inakuwa ni shida sana pale, namwomba Waziri alifikirie suala hili pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine amegusia sana kwamba, ataimarisha bandari, ni kweli tukitumia bandari zetu za Tanzania tutakuwa tumefika mahali pazuri sana. Tunayo bandari ya Dar es Salaam, tuna bandari ya Tanga, tuna bandari ya Mtwara na sasa hivi kuna bandari moja tunajadili Bandari ya Bagamoyo, tuna Bandari ile ya kule Mbamba Bay. Bandari zote hizi zikiimarishwa vizuri uchumi wa Tanzania utakuwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameongelea vizuri sana kwenye elimu, nimempenda sana. Ametenga karibu trilioni 4.7. Tukiimarisha elimu, Watanzania tukipata elimu nzuri, watoto wetu wakisoma vizuri Vyuo Vikuu tutapata wataalam wazuri sana. Ukipata wasomi wazuri hata vitu vya kugombana gombana vidogo hivi wengine wanatoka toka, wanakimbia kimbiba wakielimika itakuwa haipo. Hii elimu sasa hapa naona mwaka huu Waziri wetu wa Fedha ameamua, maana kutenga trilioni 4.7 haijawahi kutokea. Kwa hiyo, ameliangalia vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema hatuna wataalam wa gesi. Nashauri gesi itatutoa, gesi ni kitu kizuri sana katika uchumi wa nchi, tukipata wataalam wa gesi wakatengeneza vizuri, nchi yoyote duniani yenye gesi na mafuta uchumi unakua haraka sana tuki-*control* vizuri, lakini tukishindwa ku-*control* gesi na mafuta, basi uchumi hauwezi kukua. Kama tunataka tufikie malengo lazima tuhakikishe gesi na mafuta tume-*control* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji kwenye viwanda wengine wamesema sasa hivi wanashindwa kutumia gesi kwa sababu ni gharama kubwa. Nadhani Waziri wa Viwanda atatusaidia, kuna viwanda vingine havitumii gesi lakini ukitaka upate *production* kubwa, utumie *cost* ndogo lazima utumie gesi. Sasa wengine wanasema gesi ni gharama, wanakimbilia kutumia umeme, suala la gesi hii nataka nisisitize sana, Tanzania lazima tujikite vizuri kwenye gesi. Gesi na mafuta ndiyo neema pekee, ndiyo tutaondokana na umaskini. Ukisema unataka kuuvua umaskini, lazima tuhakikishe kwamba pato la Taifa limekua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri ameeleza vizuri, amesema kwenye *focus* hapa kwamba mwaka 2016 pato la Taifa litafikia 7.2, hii kuipata siyo mchezo! Mwaka jana tulikuwa na *point zero* sasa hivi unasema *point mbili*, hii mbili kuipata siyo mchezo, lakini tuki-*control* vitu ambavyo ni vya uzalishaji tunaweza tukafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema maisha ya kila mtu maana yake tunaangalia hata maisha ya vijijini. Maisha ya vijijini tunaangalia nini? Tunaangalia watu wana maji? miundombinu ya maji imejengwa? Vituo vya afya tumejenga? barabara zile ambazo hazipitiki zinapitika? Zahanati zimekwisha? Vituo vya Afya vinafanya kazi? Basi tukifanya vitu vya namna hii tutafikia mahali pazuri sana. Mpaka sasa hivi kwenye bajeti, wananchi sasa wana imani kubwa sana wanasema tutapata maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri umesema utafufua viwanja vya ndege. Sasa kuna sehemu nyingine hata viwanja vya ndege watu wanasema sisi hatupandi ndege tunataka barabara. Nadhani barabara zile ziwekwe kwa kiwango cha lami ambacho Serikali iliahidi, itakuwa imefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa sababu ni kitu kizuri sana. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga atafuatiwa na Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo kusimama hapa na kwa kweli nina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa sababu hiki ni kipindi changu cha tatu ndani ya Bunge, namshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na nimpungeze kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya na Baraza la Mawaziri. Watu wamekuwa wanafanya kazi vya kutosha, wanapiga kazi ambayo inasifika sana na kila mtu kwa kweli anaona utendaji wao, ingawa kuna wengine wamezidi zaidi, wengine viwango vyao ni vya juu sana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia kuhusu suala la makato ya kwenye kiinua mgongo. Hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha amegusa pabaya kwa Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, nafahamu kwamba una busara sana, kwa hiyo utafikiria tena upya ili angalau mambo yakae vizuri sina haja ya kueleza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza bajeti hii ni bajeti ambayo ina kila sababu ya kutuonesha na kutupa imani kwamba huko mbele tunakokwenda pako vizuri sana. Naisifu kwa sababu angalau imetuonesha na inatupa picha kwamba huko mbele yale ambayo tunayafikiria yameanza kidogo kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala zima la uchumi wa viwanda. Tunapozungumzia suala zima la uchumi wa viwanda, najiuliza, kwamba tunazungumza kuhusu suala la uchumi wa viwanda je, tuko tayari? Kwa sababu tunaweza tukakaa tukazungumza mambo mazuri sana na tukawa na mipango mizuri sana, tukapiga makofi hapa tukawa na sifa nyingi sana lakini tusipofunga mikanda na kusema kwamba hapa sasa tumeamua kufanya kazi vya kutosha, haya masuala yataishia kwenye makaratasi na utekelezaji wake utakuwa ni mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu lipo jambo moja ambalo sijapata picha sawasawa, suala hilo ni la *Inter-Ministerial Coordination*. Wizara hii na Serikali hii kwa ujumla kwenye suala hili la uchumi wa viwanda, Wizara ya Kilimo inashirikiana vipi na Wizara ya Elimu, Wizara ya Nishati, Wizara ya Maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu tunapozungumzia uchumi wa viwanda, huu ni uchumi na ni biashara ambayo ni mkakati wa muda wa kati na muda mrefu. Sisi wengine siyo wafanyabiashara wakubwa, lakini angalau tunajaribu jaribu kidogo. Kwa hiyo, ninapozungumzia hivi ni kwa sababu tukisema kwamba tunazungumzia viwanda lazima tujiulize, Wizara ya Elimu imejiandaa kwa kiwango gani? Wizara ya Maji licha ya kwamba Tanzania

ni Taifa ambalo ni la tatu duniani kwa wingi wa maji, imejiandaa kwa kiwango gani ili kuweza ku-*facilitate*? Kwa sababu kiwanda bila maji ni kitu ambacho hakiwezi kwenda. Wizara ya Kilimo imejiandaa? Wizara ya Nishati imejiandaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipokuwa makini tutajikuta kwamba watu wanakuja, wanasema sisi ni wawekezaji tunataka kuwekeza, mimi nataka kuja kuwekeza labda pengine kwa wananchi wangu wa Shinyanga kule, nataka nifungue kiwanda cha kitu fulani, lakini akikaa anaanza kwanza kujiuliza wakati anafanya *due-diligence*, hivi maji hapa nitayapataje? Anajiuliza hivi umeme bei yake na upo kwa kiwango gani? anajiuliza hivi kwa mfano, kama nikifanikiwa kama endapo nitawekeza kwenye kilimo, masoko yako wapi? Anajiuliza hivi, hapa nikifungua kiwanda *human resource* nitaitoa wapi? Kwa hiyo, haya ni maswali ambayo inatakiwa kama Serikali kwa ujumla wetu tujiulize kwa pamoja ili tuweze kuwa wote na kauli moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu sisi kama Watanzania, wapo Watanzania ambao tunafanya kazi vizuri sana, lakini wapo watu ambao wamezoea *business as usual*. Wao kazi yao mtu anaingia ofisini, tunaona hata kwenye ofisi na taasisi za Serikali, mtu anaingia asubuhi saa mbili anatoka saa tisa, uvivu na ile kukaa tu kwa kujiona kwamba mimi sina tatizo lolote yaani mtu anakaa tu ile *laissez-faire* imekuwa ni tatizo letu. Kwa hiyo, hatuna budi sisi kama Viongozi na Wanasiasa tuseme kwamba tumejiandaa vipi kwenye hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tu mdogo nitolee, *National Housing* ni Shirika letu la Umma, lakini siyo wawekezaji, *National Housing*, wanajenga nyumba za Serikali wanaziuza, Wabunge tumekuwa mara nyingi sana tunapiga kelele kwamba nyumba hizi bei yake ni kubwa sana, lakini ukikaa na *National Housing* wanakwambia kwamba tunapokaa wakati tunaanza hii *project* ya kuanza kujenga nyumba sehemu, tunajikuta kwamba maji mimi mwenyewe *National Housing* ndiyo nivute, umeme mimi mwenyewe ndiyo nikae nifanye hizo jitihada, kwa hiyo unajikuta ile pesa ambayo unaiweka pale ni kubwa sana kiasi ambacho baadaye inabidi irudi kwa mlaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu suala zima la mifumo yetu pia. Mifumo yetu na *system* yetu ya nchi ya kuchukulia mambo, lazima tubadilishe pia sheria zetu za kazi kabla ya kuanza kukaribisha hawa wawekezaji. Sheria ya Kazi iliyopo sasa hivi inatakiwa iwe *fair* kwa mwajiri pamoja na mwajiriwa. Hivi sasa unakuta Sheria ya Kazi ime-base zaidi kwa yule mwajiriwa kiasi kwamba anajiona kama Mungu mtu, sasa nini kinachotokea?



Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea sasa ni kwamba, watu wanafanya kazi, mtu anajua kwamba kwa mfano, mimi kama labda nafanya kazi kwenye shirika lolote labda pengine *tigo*, *airtel* na kadhalika, anaweza mwingine aka-misbehave, mwingine anafikia kiwango hata cha kuiba lakini haya mashirika na haya makampuni, hiki naomba Serikali kwa kweli tujitahidi sana, tuwe makini sana, tukae tujiulize na ikiwezekana tuunde timu ya kuangalia hawa wawekezaji tu tulionao hapa, sasa hivi kabla ya kuwakaribisha hawa wengine kwenye uchumi wa viwanda, wana matatizo gani? Maana kinachotokea sasa hivi, mtu anaiba *airtel* au anaiba *tigo* kwa mfano au anaiba sehemu nyingine yoyote lakini kinachotokea ni kwamba lile shirika au hiyo ofisi wanamchukua yule mtu wanamwambia tu naomba *u-resign*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga muda wako umekwisha.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Moshi Kakoso ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama jioni ya leo ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na ripoti ya Kamati ya Bajeti maana mimi ni sehemu ya taarifa ile, hivyo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yote kwa ujumla. Baada ya pongezi hizo naomba nitoe michango kidogo kwa sababu naamini mengi yameandikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kuipongeza kwa moyo wa dhati kabisa TRA kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, hii *achievements* ambayo imeonekana ni ushirikiano miongoni mwao na wanaweza kufanya vizuri zaidi, naomba tuwatie moyo. Sisi Wabunge tuwe ni sehemu ya kuhimiza ulipaji wa kodi, bila kulipa kodi nchi hii haiwezi kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachia mbali Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kwa maana ya *Commissioner General*, Wakuu wa Idara karibu wote ni Makaimu. Sasa haiwezekani, watu ambao wanafanya kazi nzuri na mpaka wanavuka malengo waendeleo kukaimu hili halifai. Naiomba Serikali kwa



kupitia Bodi husika hebu hawa watu ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu kama Makaimu muwa-*confirm* na kama hawatoshi, muwaondoe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la pili ambalo naomba kuchangia na hili limejitokeza bayana kwenye taarifa yetu, ni namna ya ushirikishwaji wa Bunge kwa kupitia Kamati ya Bajeti pale ambapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anakwenda kukutana na Mawaziri wenzake Arusha. Jambo hili halijaanza katika mwaka huu wa fedha, lilianza mwaka wa fedha 2015/2016 na ukisoma *report* yetu hatukuridhika na kile ambacho kilijitokeza na Waziri mwenye dhamana wa kipindi hicho, aliahidi kwamba halitajitokeza, lakini safari hii limejitokeza tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, wenzetu tunavyokutana nao kwa maana ya Mawaziri wa Fedha wa nchi nyingine, wanakwenda wakiwa wamejiandaa, wamehusisha Mabunge ya kwao kwamba baadhi ya mambo wanakwenda nayo wakisema haya ni ya kufa na kupona. Wanakwenda kuyatetea, wanajenga hoja na wanahakikisha kwamba yanapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, kuna msururu wa vitu vingi sana ambavyo vimepitishwa. Imekuja orodha ya nondo nyingi, unasema haya yametoka wapi? Alishauriana na akina nani? inachekesha mahali fulani unakuta kwamba, wanasema tuondoe kodi ili tuweze kulinda viwanda vya kutengeneza viberiti kwa sababu hatuna misitu ya kutosha!

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna viwanda, kiwanda chetu kilichokuwepo cha Moshi kimekufa, leo tunasema kwamba hatuna miti ya kutosha kwa ajili ya kukidhi viwanda vyetu, hivyo viwanda ni viwanda vipi? Ni kwa manufaa ya nani? Kwa faida ya nani? Naamini, mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati ya Bajeti kwamba jambo hili litazamwe lisijirudie, hakika halitajirudia, maana Mheshimiwa Waziri ni msikivu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu yangu nyingine ni kuhusiana na suala zima la mradi wa maji na hasa maji vijijini pamoja na suala zima la ujenzi wa zahanati na vituo vya afya. Tumependekeza kwamba iongezeke tozo ya sh. 50/= ili jumla iwe sh. 100/= kwenye tozo za mafuta kwa maana ya *petrol* na *diesel*. Hii itatuwezesha kutupatia kiasi cha shilingi bilioni 250 na tumependekeza kwamba mgawanyo wa pesa hizi bilioni 220 iende kutatua tatizo la maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Mbunge hata mmoja ambaye anaweza akaniambia kwamba kwenye Wilaya yake hawana tatizo la maji, hayupo! Kwa hiyo, ni vizuri tukatoka jasho jingi kulikoni tukasubiri kuja kuvuja damu nyingi. Naomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla mlisikilize. Pia

tumependekeza kwamba bilioni 30 iende kusaidia kumaliza ujenzi wa zahanati. Ni nani asiyejua kwamba ukirudi kwenye vijiji vyetu, wananchi wameitikia kwa moyo wa dhati wakajenga Zahanati zikafika usawa wa lenta, leo ukienda unamwambia mwananchi ashiriki kwenye shughuli nyingine ya maendeleo wakati maboma anayatazama hapati huduma ya afya, hawatuelewi. Kwa hiyo naomba hii shilingi bilioni 30 iende kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, karibia mwisho, nimesikia Serikali wana mapendekezo kwamba safari hii wanaenda kufanya *adjustment* kwa *inflation rate* ya *five per cent*, ni jambo jema! Lakini jambo hili haliwezi likienda *in a blanket form*, lazima kuwe na *exceptions*, ukiongeza kwenye bia haina tatizo kwa sababu wauzaji wa bia wameongeza bei tangu mwezi Februari, bia zimeongezeka kutoka sh. 2,300/= mpaka 2,500/=. Kwa hiyo hiki ambacho mnafanya *adjustment* is ok! Wala haitaathiri chochote, kwa sababu walishaanza ku-enjoy!

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo langu nalipata kwenye suala zima la vinywaji baridi na hasa soda na juisi. Hivi leo hii tunasema kwamba tunaweka *excise duty* ya asilimia tano kwenye soda na wakati huo Serikali hiyo inasema kwamba tunataka Mtanzania mnyonge ambaye ndiyo mnywa soda, leo hii ndiyo tunaenda kumwwekea *five percent*! Ukitazama kipindi hiki ndiyo kipindi ambacho wenzetu waliojaaliwa kufunga wanafunga, anataka wakati anapata futari yake apate na juisi, apate na soda. Ndiyo kipindi kweli Serikali mnataka mkaongeze hiyo? Bei ya soda haijapanda kwa ujumla kama miaka mitano, leo hii mnataka itoke sh. 500/=: iwe sh. 600/=: halikubaliki hili! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vyanzo vingi, *let's think outside the box*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba ajiandae. Mheshimiwa Kakoso hayupo! Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau na Mheshimiwa Stephen Ngonyani ajiandae.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti. Kwanza kabisa naomba nimpungeze Waziri na Naibu Waziri na timu yake kwa kuandaa hotuba nzuri ya bajeti yetu ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisoma bajeti hii, naiona katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, bajeti hii inajaribu kutuambia kwamba lazima watu wawajibike. Watu walioomba fedha kwenye Taasisi, Wizara, lazima wawajibike! Hata hivyo, nikiiangalia inajaribu kutuonesha kwamba nidhamu ya matumizi kwa walichopangiwa ni kitu muhimu sana. Pia inanionesha kwamba fedha zilizopangwa zinabadili mwelekeo kwa yale tuliyoyazoea na hatimaye kuwaza mambo mapya. Jambo la mwisho naiona kama inaenda kulenga maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nimesoma kitabu chake cha Hali ya Uchumi ukurasa wa 10 pale, kuna kitu amekisema kizuri sana pale. Hali ya umaskini; ametaja mikoa yeye mwenyewe kwamba kuna mikoa ambayo kipato chake ni kidogo. Mikoa mitano yenye umaskini mkubwa wa kipato ni Kigoma, asilimia 48.9, Geita asilimia 43.7, Kagera asilimia 39.3, Singida asilimia 38.2, Mwanza asilimia 35.3. Sasa nataka nimuulize; je, anafurahia kuitaja tu humu au ana mikakati gani aliyoipangia mikoa hii? Hii Mikoa ambayo anafurahia kuiandika kwenye vitabu vyake, kwenye bajeti ili aweze kuikomboa amepanga kitu gani? Hiyo ndiyo, ningependa atuambie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu naangalia Mkoa wangu wa Kigoma, Mheshimiwa Waziri ameutaja kwamba ni maskini. Jimbo langu lina mgogoro na Serikali yake, vibanda 120 katika Kijiji cha Mnanila walijenga kwa kupewa ramani na Halmashauri yao, lakini TANROADS wakaja wakavunja na mpaka sasa wanawadai, kila kibanda milioni nane, jumla yake ni shilingi milioni 960, wamewafanya maskini, hawataki kuwalipa, lakini kuwaandika kwenye vitabu kwamba ni maskini wanapenda! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wakulima 435, Waziri wa Kilimo yupo hapa Mwigulu Nchemba nimemwona, wamelima kahawa yao wameuza, wamepeleka kwenye vyama vyao vya ushirika ambavyo wamewapa leseni mpaka sasa wakulima hao tangu msimu uliopita fedha zao hawajalipwa. Bado anapenda awaandike kwamba hao watu wa Obama au watu wa Kigoma ni maskini na watu wanalima hawawapi hela zao! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma katika mipango ya REA, Kigoma ni kati ya mikoa ambayo mpaka sasa hivi *performance* yake ni ndogo sana, ni Serikali yake hiyo anayoandika kitabu kwamba Kigoma wako nyuma na huku hawataki kuwapelekea fedha. Hivyo hivyo ukienda kwenye *data* za maji, ukienda

kwenye pembejeo, Mkoa wa Kigoma tunapata pembejeo kidogo na zinakuja zimepitwa na wakati, lakini wanapenda watuandike kwamba sisi ni maskini! Kwa hiyo, hayo mambo mengine tunaomba mikakati ya kuokoa mikoa hii sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo hizi fedha milioni 50 ambazo mmesema, najua na nina uhakika, Mkoa wa Kigoma haujapangiwa kuanza na hizi fedha. Mnapeleka kule ambapo ni matajiri. Je, kama mnaonea hii mikoa kwa nini tusianze na hizi fedha zikaenda kwenye mikoa hiyo waliyoitaja? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili sikupendezwa nalo ni kuhusu madhehebu ya dini kwamba wanapoagiza vitu vyao walipie kodi kwanza halafu ndiyo waje wa *claim*! Tujue kwamba *nature* ya madhehebu yetu mengine yana shule, mengine yana hospitali na hawana fedha, kwa hiyo, ningeomba hilo mliangalie ili tusije kuwa na matatizo na madhehebu yetu ya dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *pay as you earn*, katika kitabu page 60, Rais alikubali kwamba *pay as you earn* itakuwa *digit* kutoka 11 kwenda tisa lakini ukiangalia ile *schedule* watumishi wa Serikali wanaonufaika na hiyo asilimia tisa ni wachache sana kwa sababu inatakiwa uwe chini ya 170,000. Kwa hiyo, watumishi kule wanafurahia kwamba Serikali imepunguza lakini *digit* za pale juu ni kuanzia asilimia 20, asilimia 25 mpaka asilimia 30, kwa hiyo kile kilio cha watumishi wengi hata Walimu wanaokuwa wanafurahia hakitaweza kuwafaidisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine tumeandika kwenye hotuba yetu ya Kamati ya Bajeti, nami nilikuwa sehemu ya Kamati, sina mengi ya kusema nilitaka nimkumbushe Waziri kuhusu hiyo mikoa maskini anayoisema ana mikakati nayo ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafauatiwa na Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba hizi mbili alizozileta Waziri wa Fedha na Mipango, Hali ya Uchumi na Bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na salama, leo tumekutana hapa kujadili mambo yanayohusu mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Dkt. Phillip Mpango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kutuletea bajeti ambayo nimeita ni bajeti ya kihistoria. Haijapata kutokea katika historia ya nchi yetu Bajeti ya Maendeleo ikawa asilimia 40 ya bajeti yote ya Taifa. Kwa kweli pongezi nyingi sana zimwendee Mtukufu Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa dhamira hii ya dhati ya kuwaondoa wananchi wa Tanzania katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata faraja kubwa sana, nilikuwa najaribu kufanya tathmini ndogo hapa, nikagundua miundombinu peke yake imetengewa asilimia 25.4, elimu asilimia 22 na bajeti ya afya ni asilimia 9.2. Hapa kwenye bajeti ya Wizara ya Afya, Abuja *Declaration* inatutaka tutege bajeti ya asilimia 15. Wanasema Rome haikujengwa siku moja, kidogo kidogo ndani ya bajeti mbili, tatu zijazo tunamwomba sana Dkt. Mpango Azimio hili la Abuja la asilimia 15 katika bajeti ya Wizara ya Afya lifikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchangia bajeti. Ushiriki wa sekta binafsi na sekta ya umma katika miradi ya pamoja kimekuwa ni kilio cha siku nyingi sana, tumelizungumza sana hili na ninayo furaha na nahisi faraja kubwa sana, kupitia kwenye bajeti hii nimeuona ushiriki huu wa sekta binafsi na sekta ya umma kwa maana ya PPP, tatizo langu ni dogo tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha basi atuletee na mchanganuo, kwa sababu tumeona tu humu miradi, mimi naiona kama ni *blanket* imewekwa humu, miradi kama ya barabara ile ya Chalinze – Dar es Salaam express way, mradi wa Reli ya Kati, miradi hii ya umeme ya *phase III* kule Kinyerezi ipo tu kwa ujumla ujumla!

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeomba sana hebu watupatie *break down* na *frame work*, *timeline* kwamba miradi hii tunafanya labda tutaanza na mradi wa reli ya kati *standard gauge*, labda tarehe fulani mpaka itakapofikia mwaka wa fedha miaka miwili, mitatu, mbele mradi huu utakuwa umekwisha; labda mradi wa bandari ya Bagamoyo utaanza tarehe fulani mwaka wa fedha fulani na utakwisha hivi, ili tupate kwa ujumla wake haya mambo yanakwendaje; lakini kutujazia tu miradi ya jumla bila ya kutupa *timeline* inatusumbua sana, kwa sababu tunajenga matumaini, lakini ndani yake hatujui miradi hii itakuja lini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye suala la utalii. Nilizungumza hapa kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ilipoleta bajeti yake na nashukuru sana Mheshimiwa Waziri namwona pale na namwomba Mheshimiwa Waziri anitegee sikio. Takwimu zinatumbua kwa miaka miwili kati ya mwaka wa fedha uliopita na mwingine wa nyuma yake, utalii wetu umeshuka kwa karibu watalii laki moja,

sasa sitaki kujielekeza kwenye sababu gani zimepelekea watalii kupungua. Nataka nijielekeze kwenye namna ambavyo tunaweza tukatangaza utalii wetu ili tupate watalii wengi na kuhakikisha kwamba tunapata mapato katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza utalii mara nyingi tunajikita kwenye vitu viwili tu, Mlima Kilimanjaro na Mbuga, wakati Tanzania na Naibu Waziri wakati anajibu swali hapa juzi alisema wazi kwamba Tanzania ni ya pili duniani kwa vivutio vya kitalii, sasa hivi vivutio vingine vitatangazwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Kisiwa cha Mafia na nilizungumza hapa wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwamba kule Mafia tuna samaki anaitwa 'Papa Potwe', huyu samaki ni samaki wa ajabu, anatabia kama za *dolphin*, ni samaki rafiki, watalii wanapenda sana kuja kuogelea naye. Je, ni wangapi wanajua habari za samaki huyu 'Papa Potwe'?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunaomba sana mtengeneze *package* ya vivutio vyote ili muweze kwenda kuviuza huko nje, kwa sababu Halmashauri hatuna uwezo wa kumtangaza 'Papa Potwe'! Ni lazima tusaidiwe na nguvu ya Serikali. Kwa hiyo naomba sana tutanue wigo katika utalii wetu katika kuutangaza na kuhakikisha kwamba tunapata mapato mengi ili kuendeleza nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango, hili nililizungumza kwako kama mara moja au mara mbili hivi, masikitiko yangu makubwa kuona kwamba Kisiwa cha Mafia hakikuingizwa katika zile *flagship project* kwa ajili ya Mpango wa Pili wa Maendeleo, kwa maksudi kabisa! Mimi nilikuwa naiona Mafia kama ndiyo Zanzibar mpya! Tuifungue kiutalii Mafia ili watalii waje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale tuna matatizo mengi na tunahitaji *investment* ndogo sana kuifungua Mafia. Barabara inayotoka Kilindoni mpaka Rasimkumbi kilometa 55 ikitengenezwa hiyo ikitiwa lami pamoja na bandari yetu na ndugu yangu Ngonyani pale ananisikia, kuhusu bandari ya Nyamisati, Mamlaka ya Bandari imetenga nafahamu kwamba bilioni 2.5 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ile, ikikamilishwa sambamba na bandari ya Kilindoni na kuongezwa kwa *runway*, *airport* ya Mafia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dau muda wako tayari.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama ajiandae.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kupitia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo ameionesha kwa muda mfupi ambao ameingia madarakani. Nataka tuwaambie kwamba hatutawaangusha, tutawaunga mkono kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa mambo ambayo yameongelewa juzi pamoja na Waziri, ameongelea sana kwamba ataimarisha Bandari na Viwanja vya Ndege na ataimarisha Reli. Nimeshangaa sana katika mambo ya kuimarisha reli yeye anaizungumzia tu reli ya kutoka Dar es Salaam mpaka nyumbani kwake Kigoma, hajawahi kuitaja reli ya Tanga – Moshi - Arusha mpaka Musoma. Hapa pana tatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati uliopita nilizungumzia sana suala la reli, nikazungumzia sana kama tunataka kuimarisha biashara ni lazima muiangalie reli ya Tanga. Reli ya Tanga kutoka Tanga kupitia Moshi kwenda Arusha mpaka Musoma ingesaidia sana katika uchumi wa nchi yetu. Nashangaa rafiki yangu ambaye ni Dkt. wangu Mpango, ameangalia sana reli inayokwenda nyumbani kwake ameisahahu ile ya Tanga. Naomba atakapojumuisha aiangalie hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ni suala la Mkaguzi Mkuu. Kiwango cha pesa ambacho amementengea, Serikali hapa hamuwezi kwenda kila mahali kukagua na mkapata wale mafisadi, lazima Mkaguzi Mkuu wa Serikali awakagulie, awaambie huyu ndiye fisadi, anatakiwa kupelekwa Mahakamani, leo mnapowapunguzia pesa watakwenda kukagua hiyo miradi na nini? Naomba Serikali iliangelie sana suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamepunguza bei ya mafuta ya petroli kwamba bei ya mafuta ya petroli imeachwa kama ilivyo, naomba Serikali ipandishe kwa sababu bei ya petroli haimsaidii Mtanzania, maana kupunguza bei ya mafuta maana yake ni kwamba wasafiri wapunguziwe gharama, lakini toka wamepunguza bei ya petroli hakuna Mtanzania yeyote ambaye anapanda nauli kwenye gari kwa kupunguziwa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa waiongeze, tujue kabisa kwamba kwa sababu hatufaidiki lolote Watanzania wa hali ya chini. Kwa hiyo, kwa sababu ni kitu muhimu na wameona kwamba ni vizuri, basi tunaomba wapandishe petroli, watupunguzie sukari. Sukari hawajaiongelea hapa, lakini sukari ni kitu muhimu



sana kwa Watanzania. Naomba hiyo Mheshimiwa rafiki yangu Waziri wa Mipango, Mpango yeye ni rafiki yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni muhimu sana na barabara; wamezungumzia masuala ya barabara kuna mikoa wameshaanza kuionesha kwamba ni mikoa matajiri sana, lakini mbona wanashindwa kuwaambia hii mikoa maskini kama mikoa ambayo wamenyima hata kuwatengenezea Bandari, mtawapa kiwango kiasi gani kwa sababu tuna bandari ya Tanga pale, tuna Bandari ya Mtwara pale, tuna Bandari ya Bagamoyo, katika Mpango walisema hizi Bandari wataziongeza lakini hatuoni chochote kinachoendelea eti Tanga kwa sababu kunajengwa bomba la mafuta kutoka Uganda ndiyo isahaulike? Haikubaliki!

Hili bomba la mafuta linakuja kwa ajili ya nchi mbili! Haliji kwa ajili ya Tanga! Kama Tanga linakuja ni kama bandari nyingine. Naomba hapa iongezewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Mbadala, tunazungumzia suala hili kwa masikitiko makubwa. Kwa niaba ya Kambi Mbadala, wenzetu wa Kambi ya Upinzani walisema kwamba *sitting* za Wabunge zifutwe, nasi tunasema hata *per diem* pia zifutwe kama tunataka kuisaidia Serikali, si Waheshimiwa Wabunge wote tulikuja kwa ajili ya kuwatetea wanyonge? Kama tumekuja kwa ajili ya kuwatetea wanyonge, wenzetu wamesema *sitting* mwondoe, sisi Kambi Mbadala tunasema hivi, hata ile *per diem* inayotegemewa na hawa, kama kweli tumekuja kuwasaidia watu, zote ziondolewe ziende kwa maendeleo ya wananchi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uti wa mgongo sana, lakini kwangu kulitakiwa kujengwe bwawa la maji toka miaka ya nyuma sana. Bwawa hili lilikuwa linagharimu shilingi bilioni 13, lakini fedha zile ziliondoka zikaenda Kilimanjaro. Sasa hii bwawa ambalo lilikuwa lijengwe katika Jimbo langu; mmesema safari hii ni wakati wa kilimo, naomba hili bwawa liendeleo kujengwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni viwanda. Katika Tanzania, mikoa ambayo ilikuwa inaongoza kwa kuwa na viwanda vingi ni mikoa mitatu au minne. Ni Mkoa wa Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Arusha. Hebu niambieni leo, tunazungumzia viwanda. Rafiki yangu Waziri wa Viwanda, *best* wangu hapa ana hakika kabisa kwamba atafanya; hela za kuanzia hivyo viwanda zitapatikana wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, Serikali yangu sikivu, nampenda sana Mheshimiwa Dkt. Pombe Magufuli na Mawaziri mlioko hapa, mnafanya kazi kubwa sana kwa kujituma na hata leo tutamwomba dua Naibu Spika ili

aendeleo kukaa mpaka Bunge la mwaka 2020 kwenye jukwaa lile pale. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema haya kwa sababu tuna uchungu. Sisi tunaotoka kule Majimbo tunapokuja hapa, tunaonekana kama Waswahili. Mnaposema kwamba maendeleo yanakwenda vijijini, mtuambie maendeleo haya ni ya namna gani, siyo kusoma vitabu. Leo hii hakuna dawa mahospitalini, hakuna elimu ya kutosha, Walimu wanadai haki zao hawapewi, Madaktari hospitalini hawaongezewi posho; leo tunasema kwamba tunataka kufanya mambo, hebu tumalize haya madeni tunayodaiwa na watu ambao tunawatumia muda mwingi mpaka wakati wa uchaguzi hawa ndiyo tunaowatumia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunawatumia watu mpaka wakati wa uchaguzi tunawapenda, leo hii madeni yao hatuwalipi, eti tunategemea tu kukaa; inakuwa siyo nzuri. Naomba kabisa Mheshimiwa tuanze na madeni ya ndani. Tukishamaliza madeni ya ndani tutakuwa tumefanya kazi za msingi sana kwa wananchi, Watanzania ambao wanaipenda sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ukimwona mtu anaipinga Serikali ya Chama cha Mapinduzi, basi ujue ni fisadi. Ukimwona mtu yeyote leo anakuja kulalamika kwa bajeti yenu, ni fisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Mahakama naomba muianzishe mapema, kwa sababu tumechoka kuonekana Wabunge... (Makofi)

## TAARIFA

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, naomba uzime *microphone* yako. Mheshimiwa Keissy, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji, kutumia neno “Kambi Mbadala”, kusema kweli ifutwe kwenye *Hansard*, ni makosa ya hali ya juu. Anazungumza maneno; hapa tuko Bungeni, ni chombo cha sheria kabisa hiki. Bunge lina hadhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuingiza maneno ya dhihaka kwenye Bunge lako Tukufu, ni kosa la hali ya juu. Tuzungumze maneno yaliyotuleta hapa, lakini kuleta mizaha kwenye Bunge ni makosa ya hali ya juu. Nampa taarifa mzungumzaji, afute kauli ya kusema ni Kambi Rasmi ya Upinzani pale ni makosa. Wapinzani wako nje, yeye sio kambi mbadala pale. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. STEVEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei, mimi sio Kambi ya Upinzani. Mimi ni mmoja kati ya Wabunge wa CCM ambao tumekuja hapa kuweka chachu ya michango yetu kufuatana na hawa wenzetu waliokimbia eneo hili. Kwa hiyo, mimi bado ni Mbunge wa CCM, hiyo taarifa yake siisikii. Ninaposema Kambi Mbadala ni kambi ambayo imekamilika kwa ajili ya kujenga hoja za msingi ya kuisaidia Serikali yetu. Sisi sio Upinzani, kwa hiyo taarifa yake siikubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya, nimeipenda sana bajeti hii, naiunga mkono kwa asilimia mia moja, siungi mkono taarifa yake huyo. (Kicheko/Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani ajiandae.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa nami nichangie katika bajeti kuu. Nianze kwa kusema kwamba kauli mbiu ya bajeti hii naikubali ambayo imelenga kuongeza uzalishaji viwandani na kupanua fursa kwa ajira. Niseme tu kwamba nasi kama Jimbo la Kigamboni tumeshajipanga vizuri, tayari tumeshapima ekari 1,000 na tumetoa viwanja vipatavyo 461 vya viwanda ambavyo viko tayari kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niseme tu kwamba bajeti hii mwelekeo wake ni mzuri, kutoka asilimia 26 mpaka asilimia 40 ya fedha za ndani kutengwa katika kuelekea katika bajeti ya maendeleo, ni jambo jema. Jambo jema lingine ni kupunguza utegemezi kwa wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna changamoto ambazo nami naziona. Pamoja na juhudi ambazo zinaendelea za kuongeza ukusanyaji wa kodi za ndani, bado tuna changamoto ya wigo wa kukusanya kodi, kwa maana ya *tax base*, hilo bado ni tatizo kubwa sana. Bado naona tunaendelea kuvikamua vyanzo vile vile ambavyo tumekuwa tunavitumia siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kwamba sasa hivi inabidi tuangalie na vyanzo vingine. Sekta ya Kilimo, Uvuvi pamoja na Utalii vinaweza vikachangia kwa kiasi kikubwa. Tuweke pesa ili tupate pesa. Kwa hiyo, nataka kuishauri Serikali ijaribu sasa kuangalia vyanzo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kushauri ni kuhusiana na matumizi makubwa ndani ya Serikali. Tunazona juhudi ambazo mnazifanya katika kupunguza matumizi ya Serikali. Asilimia 49.5 ya mapato ya ndani yote yanaenda kwenye mishahara. Hii ni gharama kubwa sana. Ni lazima

sasa mwangalie upya ndani ya Serikali, kuangalia reforms za kuboresha ufanisi lakini na kupunguza gharama ambazo zinaingia katika masuala ya mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuangalie tena maeneo mengine ambayo tunaweza tukapunguza matumizi makubwa. Katika eneo la ununuzi wa magari, matumizi ya magari ya Serikali bado ni mbovu. Tunayanunua magari kwa gharama kubwa. Ni muda muafaka sasa kuweka sera nzuri ya ununuzi, matumizi na matengenezo ya magari ya Serikali; yanatumia gharama kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni ushirikishwaji wa sekta binafsi. Tuna Sheria nzuri ya PPP na sera nzuri sana ya PPP; lakini ukiangalia katika hotuba hii ya bajeti kwa kiasi kikubwa sana, miradi yote mikubwa tunategemea sana Serikali kwenda kukopa fedha kwa ajili ya kuendesha hiyo miradi. Kwa nini tusi-engage sekta binafsi tuka-freeup some resources kwa ajili ya huduma nyingine za jamii kama afya, elimu na maji? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali ijaribu kuangalia hii, miradi mingine kuna watu wana fedha zao, tuwashirikishe ili hizo fedha nyingine tuweze kuziokoa kwa ajili ya mambo mengine katika huduma za jamii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilikuwa nataka kuchangia ni concern. Sisi kama Bunge jukumu letu ni kupitisha bajeti ya Serikali. Nilipokuwa nasoma hotuba ya Kamati ya Bajeti, imenishtusha kidogo kuona kwamba Serikali inatumia fedha kupita kile kiwango ambacho kimeidhinishwa na Bunge, hilo ni kosa. Tuanze sasa kujenga msingi wa Serikali kuheshimu maazimio na zile idhini ambazo zimepitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupeleka fedha asilimia 140, 120, 150 zaidi ya zile zilizopitishwa na Bunge bila kuleta maombi hayo Bungeni ni kuvunja sheria na kuvunja Katiba. Kwa hiyo, lazima sasa tufike mahali turudi kwenye ile misingi ya matumizi ya fedha ya Serikali na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali izingatiwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulichangia ni hususan ushirikishwaji wa Kamati ya Bajeti. Kamati ya Bajeti inafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Serikali ione kuwa, wanapofanya kazi na Kamati ya Bajeti, wanafanya kazi na Bunge. Ni muhimu sana wakawashirikisha. Bajeti itakuwa nyepesi kama Kamati ya Bajeti itakuwa imeridhia kwa niaba yetu sisi. Sasa Serikali inapokuwa inaleta bajeti na vitu vingine havijapitishwa katika Kamati ya Bajeti mnaifanya kazi ya kujadili na kupitisha bajeti inakuwa ngumu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, Bunge linaweza likawa rafiki pale mnapokuwa mnatoa ushirikiano kwa Bunge, lakini kazi inaweza ikawa ngumu pale mnapokuwa hamuwashirikishi Wabunge kikamilifu. Sasa nawaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, msiwaone Kamati ya Bajeti kwamba wale ni maadui, wale ni marafiki zenu na wako pale kwa niaba yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema, nami nataka kugusa suala la kiinua mgongo kwa Waheshimiwa Wabunge na nataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha naye ajaribu kunisaidia, nini hasa lengo la kuiweka hoja hii katika bajeti yake? Kwa sababu Bunge letu hili ndiyo limeanza 2015 litakwisha 2020; unapoliweka hili suala la kukata kodi katika kiinua mgongo, lengo lake ni nini? Ama ilikuwa kama hivyo alivyokuwa anasema Mheshimiwa Kangi Lugola, kuwa-beep Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme, huwezi ukaleta usawa katika kupofua wenzako. Kama kuna watu vipofu nawe ukawapofua wengine ili wote tuwe sawa, nadhani hiyo siyo mantiki sahihi. Suala kubwa la msingi hapa, kama tunaongelea masuala ya kiinua mgongo, *lets cut across board. We should not single out a single group*. Kwa hiyo, hili nataka niliseme kwa Mheshimiwa Waziri ili liveze kueleweka. Maana yake unapokuwa na *single out a single group*, inaleta mashaka kuhusu dhamira ya lengo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mheshimiwa Sophia Mathayo Simba ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi. Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa uwasilishi wake mzuri. Pamoja na kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Waziri nina mambo mawili, matatu ya kuishauri hii Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, unajua habari ya viwanda Tanzania siyo habari ngeni. Tumekuwa na viwanda miaka ya 80 kuelekea miaka ya 90 na viwanda vingi vimekufa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, sehemu pekee au mkakati pekee ambao ameuweka ambao umeonekana wa namna ya kulinda viwanda vya ndani ni kuongeza kodi kwenye bidhaa zinazotoka nje, zile bidhaa ambazo tunaweza kuzizalisha ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu huo ni mkakati mzuri, lakini mkakati huu pekee hautatosha kulinda viwanda vya mafuta ya kula, hautatosha kulinda viwanda vya sukari nchini, hautatosha kulinda viwanda vya nguo nchini. kwa sababu kikwazo cha viwanda vya Tanzania siyo tu ushindani wa bei za bidhaa zinazolingia, bali pia mikataba ambayo tunaingia na nchi marafiki ambao tunafanya nao biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote vile, mikataba ile bado inatubana. Pengine hata kuweka hizo kodi kwenye hizo bidhaa huenda tukagomewa na wadau marafiki tunaofanya nao biashara kwa sababu na wao wanataka kulinda viwanda vyao. Kwa hiyo, naishauri Wizara ya Fedha ifanye kazi ya kina. Mwezi wa Pili nilitoa ushauri huu na sasa narudia tena kwa sababu mpaka sasa sijaona *assessment* ya kutosha ya ku-assess kwa nini tulifeli miaka ya 1980 na 1990 na kwa nini tunadhani tutafaulu katika kipindi hiki? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ni suala zima la maji. Sera ya Taifa inatutaka Watanzania wote popote walipo waweze kupata maji katika umbali usiozidi mita 400. Ukiiangalia sera hii na mpango mkakati uliowekwa na Wizara ya Fedha, havifanani kabisa. Kukata sh. 50/= kwenye mafuta ya *petrol* na *diesel* pekee, havitoshi. Kamati ya Bajeti imeshauri tuweke angalau sh. 100/= na baadhi ya Wabunge wameshauri tuweke angalau sh. 100/=. Nami naomba tuweke angalau sh. 100/= ili tuweze kusogea mbele kwa haraka zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Madaba ni moja katika Majimbo ambayo yana tabu sana ya maji. Hivi ninavyoongea, Kijiji cha Lilondo na Maweso toka miradi imeanza mwaka 2015, haijakamilika na Wakandarasi bado wanahangaika kulipwa. Naishukuru Wizara ya Maji, tunawasiliana kwa jambo hili, lakini huu ni ushahidi kwamba kuna matatizo ya kutosha kwenye hili eneo, tulitengee bajeti ya kutosha kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni ombi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango avae viatu vya Walimu wa Sekondari na Shule za Msingi ambao katika uhai wao wote wanalitumikia Taifa hili, mishahara yao inakatwa kodi na wanapomaliza kipindi cha utumishi wanalipwa kiinua mgongo na kinakatwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri avae viatu vya watumishi wengine wa Serikali na Sekta ya Umma ambao mishahara yao ni ya chini, wanakatwa kodi, wanafanya kazi, lakini wanapomaliza utumishi wao, bado kiinua mgongo kinakatwa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lililopita lilienda hatua mbele, likaiomba Serikali iondoe kodi kwenye hivi viinua mgongo, yaani kwenye mafao ya

wafanyakazi. Nilitegemea Wizara ya Fedha ije na mkakati huo sasa wa kuondoa hizo kodi kwenye mafao ya wafanyakazi na kupendekeza njia mbadala ya kupata fedha kwa ajili ya kuendeshea Serikali, kwa sababu hawa wafanyakazi wameendelea kukatwa kodi wakati wote. Kilichonishangaza, tunazidi kurudi nyuma. Tulishapiga hatua mbili mbele, tunarudi hatua nne nyuma, tunaanza sasa kufikiria kukata kodi kwenye mafao ya Wabunge. Tunakwenda wapi? Tutafika lini tunakotaka kwenda kuwatengenezea Watanzania maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri avae viatu vya Wabunge wanaotoka katika Majimbo yenye changamoto kama Jimbo la Madaba. Mbunge wa Madaba akishapata posho humu Bungeni, anakwenda kununua solar kuweka kwenye Vituo vya Afya. Anakwenda kuchangia maji Matetereka ili wananchi wapate maji kwa sababu Serikali bado haijaweza kufikia wananchi hao.... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhagama, muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Nasikitika sana ninapoambiwa kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mathayo Simba na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kupata fursa ya kuchangia katika hoja iliyokuwepo sasa hivi Mezani ya Bajeti ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hapa taarifa yake nzuri. Vile vile naishukuru sana taarifa ya Kamati ya Bajeti, imeshauri mambo mengi ya msingi, Namwomba Mheshimiwa Waziri aiangalie kwa jicho la aina yake. Nina mambo kadhaa ambayo napenda niishauri Serikali kuweza kuyaangalia na ikiwezekana kuyafanyia marekebisha. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nataka kuzungumza juu ya suala zima la tozo ya bidhaa za mbogamboga za kilimo na hasa kwa wafanyabiashara wale ambao wanatoka Bara kwenda Zanzibar na wale ambao wanatoka Zanzibar kuja Tanzania Bara. Mheshimiwa Waziri hili linarudisha tena kidonda cha kero za Muungano; isitoshe, suala hili halijaangaliwa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar hivi sasa ina zaidi ya mahoteli 450 ya utalii. Asilimia 70 ya vyakula ambavyo ni mboga mboga na matunda vinatoka Tanzania Bara. Mazao haya ni *very perishable*, yaani hayana uwezo wa kustahimili kwa muda mrefu. Leo ukichukua nyanya Ilula, ukifika Dar es Salaam, umemaliza siku moja au siku moja na nusu; robo ya ile bidhaa tayari imeshaharibika. Unangoja meli uyasafirishe kufika Zanzibar, nusu yake nyingine tayari imeshaharibika; lakini bado unatoa pale uyapeleke Kiwengwa au Nungwi ambako ndiko kwenye ulaji wa yale matunda. Mfanyabiashara yule atakwenda mara mbili mara tatu, biashara ile imemshinda. Hapa hatujengi. Tunawavuruga hawa wafanyabiashara na mwisho wake badala ya kwenda mara tatu, mara nne, biashara hii imemalizika. Hakuna biashara itakayokwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utafiti tulioufanya mwaka 2014 kwa mwezi mmoja, biashara ya mboga mboga na matunda ni zaidi ya tani 160,000 kwa mwezi mmoja zinasafirishwa kutoka Bara kwenda Zanzibar. Biashara hizo zinaingiza zaidi ya shilingi bilioni 2.6, fedha zinazunguka kila siku kutoka Bara kuja Unguja; yaani eneo hili tunalivuruga. Lazima tuwe makini na tupate maelezo yaliyo sahihi kuhusiana na mazao haya kutozwa tozo hizo ambazo zimependekezwa na Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka kuzungumza suala zima la makato au tozo za Waheshimiwa Wabunge. Ni eneo ambalo kwa kweli limemgusa kila Mbunge aliyekuwemo ndani ya Bunge hili. Siyo hivyo tu, hasa wale Wabunge ambao wanatoka katika Majimbo waliyogombea; hali ni ngumu Mheshimiwa. Sms zaidi ya 300 kwa siku, kati ya hizo sms 200 zote zinaomba hela. Leo Mbunge huyu unakwenda kusema unamkata kile kiinua mgongo chake unategemea nini? Atarudi vipi hapa? Ni wazi kabisa huo ni mkakati wa kuwadhibiti kwamba hapa wasirudi mwaka 2020 au 2021. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo tu athari yake haitokani na hapo, athari hiyo itatokana vilevile na ile miradi ambayo ilonekana kwamba Mbunge huyu angeweza kusaidia kuleta maendeleo katika maeneo yake. Kwa mtazamo ninaouona, katika watu wenye hali ngumu hivi sasa ni Waheshimiwa Wabunge. Waonewe huruma! Waangaliwe kwa jicho ambalo litaweza kuwafanya Wabunge hawa, hasa wengi wa CCM, warudi katika miaka mitano ijayo. Vinginevyo, wanakwenda na maji kama eneo hili halikufanyiwa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumza vile vile suala zima la zile shilingi milioni 50. Naomba nishauri kwamba fedha hizi tusingalie kuzipeleka kwenye SACCOS, ziangaliwe kuboresha mazingira ya vijiji ambavyo vinapelekewa hii fedha, kwa sababu, kuna mahitaji mengi ya msingi; hospitali hazijamalizika, zahanati, shule zimekaa magofu na zilizomalizika hazina vitendea kazi, hazina madawati, hazina vitu mbalimbali; maji hamna na barabara ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha ni muhimu sana, lakini ziangalie kujenga maendeleo ya vile vijiji, viwe bora zaidi na watu wanahitaji kuishi maisha bora zaidi kuliko hali ilivyo sasa hivi. Kila mmoja anatamani fedha ile iende katika eneo lake kwa ajili ya kuboresha vijiji vilivyokuwa na hali mbaya katika maeneo husika. Naomba kasma ikatwe kwa ajili ya kuangalia vikundi vya akinamama na hizo SACCOS, lakini zaidi fedha hizi zielekezwe kuangalia miradi ya maendeleo katika kila kijiji ili kuboresha mazingira yaliyokuweco kule na kuwafanya watu wawe na maisha bora zaidi kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania bado tuna fursa nyingi ambazo Serikali kama itaweza kusimamia vizuri, tunaweza kutengeneza maeneo mengine ya mapato kuliko vyanzo ambavyo sasa hivi vimeainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Fursa iliyokuweco katika *corridor* ya Mtwara na hasa kwenye yale maeneo ya uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehani, kengele ya pili imegonga. *(Makofi)*

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mathayo Simba, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah ajiandae.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mchana huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kuweza kuwa mmojawapo wa kuchangia bajeti hii ya mwanzo kabisa, bajeti ambayo inakwenda kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 mpaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyofanya kazi nzuri katika kutekeleza hii Ilani, lakini katika kutekeleza yale aliyosema mabadiliko ya kweli. Ni kweli, Mheshimiwa Rais tunaona katika bajeti hii ni vipi mabadiliko ya kweli yanaweza yakapatikana. Hongera sana Mheshimiwa wetu, tunakuomba kwa Mwenyezi Mungu uendelee kuwa na nguvu ya kutusimamia na hivyo kuleta maisha bora kwa Watanzania wengi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nachukua nafasi hii pia, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa jinsi unavyoendesha Bunge lako kwa busara, kwa umakini na kwa jinsi unavyohakikisha unaleta nidhamu ndani ya Bunge hili, ukitumia weledi wako mkubwa wa kutafsiri Kanuni za Bunge tulizojiwekea wenyewe. Hongera sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti ni nzuri, lakini inahitaji sana Watanzania tubadilike, tunahitaji *discipline* ya hali ya juu katika ukusanyaji na katika utumiaji wa fedha hizo. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge, tupo pamoja na Rais wetu, tunakubalina naye kwamba tutabana matumizi kama tulivyoanza na pia tutahakikisha huko Majimboni kwetu kila mtu anafanya kazi. Kabla sijaendelea naomba niunge mkono hoja mia kwa mia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwapongeze sana Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa kazi nzuri waliyofanya. Nawapongeza sana wadau wangu akinamama nadhani wanne au watano, wamefanya kazi kwa umahiri mkubwa sana. Pia nawapongeza na akinababa ambao walikuwano, lakini walionesha umahiri wao kwa vile wamesheheni weledi katika taaluma zao na wanazielewa vizuri, kwa hiyo, nawapongeza sana. Kwangu mimi nikiwa Mwenyekiti wao, *I am proud of them*, wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kazi hiyo, moja ambalo limenifanya niwapongeze ni pale walipogundua lile tatizo kubwa ambalo wameliona na wamepeleka mapendekezo, ingawa sijui kama yamechukuliwa katika ukurasa wa 11. Moja ya pendekezo lao ni lile walilosema, ziongezwe shilingi bilioni 30 kwenye bajeti ili kumaliza zile Zahanati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo zahanati ambazo wananchi wamejitolea kujenga. Nilipokuwa nikitembea mikoani wakati wa kampeni kilio kikubwa walichonacho akinamama, walikuwa wanasema, unaona boma lile, ndiyo Zahanati yetu, haijakwisha. Hivyo basi, kama hatukuwasaidia hawa katika hizi zahanati, kwanza tunawavunja moyo wa kujitolea, lakini kubwa zaidi akinamama wanaendelea kufa kutokana na kukosa huduma za afya. Baya zaidi, vipo pia Vituo vya Afya ambavyo vimejengwa vizuri, lakini havina vyumba vya upasuaji. (Makofi)

(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mbona saa inaenda upesi! (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini fedha hizi zingesaidia sana katika kutengeneza hizo *theater* ili tupunguze vifo vya akinamama. Pia, waliozungumzia kuongeza tozo ile ya senti 50 kuwa sh. 100/= kwa ajili ya Mfuko wa Maji. Nawaunga mkono mia kwa mia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda wenyewe siyo rafiki, lakini napenda niwapongeze sana kwa jinsi walivyotenga pesa ya kutosha kwenye miradi ya maji. Nashukuru sana kama pia wangetenga pesa ya kutosha kwenye miradi ya mazingira. Kazi yote tunayoifanya kwenye maji haitakuwa na maana kama mazingira yetu yanaendelea kama yalivyo. Tunahitaji kuwe na Mfuko wa Mazingira uweze kupanda miti mingi sana. Kwa hiyo, hilo naomba liishie hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Mheshimiwa Waziri afafanue, kuna uwoga ndani ya jamii kuhusu huu ushuru wa simu pamoja na benki; hizi ada. Wananchi na sisi wenyewe tuna wasiwasi; mzigo usije ukarudi kwa wananchi. Hali siyo nzuri. Wananchi hawana hali nzuri ya kifedha, pesa imepotea; sasa tusiwaongezee tena matatizo katika masuala ya simu. Hata mkisema watakaolipa ni wale wenye Makampuni ya Simu, lakini mwisho wa siku hawa ni wafanyabiashara, watatafuta ujanja zitarudi kwetu tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu shilingi milioni 50. Mimi na wenzangu ambao wako humu tulikuwemo katika kutengeneza ile Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nataka nitanabahisha, tuelewe. Tuliposema vijiji 50 tulikuwa na maana ya Vijiji, Mitaa na Shehia. Kwa hiyo, kwa sababu kila mtu anazungumzia vijiji, wale kule mitaani wanaweza kudhania hawamo. Wamo! Hata hivyo, nawapongeza sana kwa utaratibu mliouchukua wa kufanya kwanza *pilot project* ya mikoa 10. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi shilingi milioni 50 tulisema zitakuwa *revolving fund* katika kile kijiji, hazitoki. Kwa hiyo, leo wanapata hawa, kesho wale, ni za kijiji, hazi-revolve kutoka nje. Kwa hiyo, hilo likumbukwe, nia yetu ilikuwa hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *gratuity* kwa Waheshimiwa Wabunge kutozwa kodi siyo sahihi. Zile sababu zilizosababisha kusamehewa, bado zipo mpaka leo. Warudi kwenye makabrasha yao wasome, zile sababu zimekwisha? Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti. Kwanza kabisa, naomba niipongeze bajeti yetu, bajeti nzuri, naomba niiunge mkono kabla sijaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niipongeze Serikali yangu sikivu kwa kututengenezea barabara ambayo ilikuwa inasumbua sana wananchi wa Mpanda; Mpanda – Tabora kwenye Daraja la Ipole. Lile daraja sasa hivi limekwisha. Nomba tu Serikali yangu basi itoe kauli hilo daraja liweze kufunguliwa ili wananchi wa Mpanda sasa waweze kupata maisha mazuri, waweze kufanya biashara zao na kufanya shughuli zao kwa amani kwa sababu daraja lile la Ipole lilikuwa ni kikwazo, walikuwa hawawezi kusafiri, walikuwa wanazunguka mwendo mrefu. Naomba Kauli ya Serikali kwa ajili ya daraja hilo, kwa kuwa limekwisha ili tuweze kupata manufaa ndani ya maisha ya wananchi wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchangia bajeti hii kwa upande wa akinamama. Kwa kuwa mimi ni Mbunge wa akinamama, nianze na akinamama. Asilimia tano ya akinamama mara nyingi tuncitenga lakini akinamama hawaipati kutokana na Halmashauri zetu kwamba hazina uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukiangalia, makusanyo mengi yameingia Serikali Kuu, ina maana TRA ndiyo watakusanya. Ina maana Halmashauri watakuwa hawana kipato cha kuwapa akinamama pamoja na vijana zile asilimia tano. Sasa sijui Serikali itafanyaje kwa sababu akinamama wengi sasa hivi wameshapata mwamko, ni wajasiriamali. Nanyi wenyewe mnaona sasa hivi hata mkienda vijijini mnakuta akinamama wengi ni wajasiriamali kutokana na juhudi nzuri za Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Sasa tunaomba hii asilimia tano iliyowekwa na hivi vigezo ambavyo viliwekwa, hela nyingi zimechukuliwa Halmashauri, akinamama hawa wajasiriamali watapataje mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sasa hivi kupata hiyo asilimia tano kwenye Halmashauri zetu ni shida. Sasa naomba Serikali yangu sikivu kwa bajeti hii ione ni jinsi gani ya kuweza kutenga au kutafuta ili hawa akinamama waweze kupata asilimia tano ili waweze kufaidika na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye upande wa maji. Hakuna kitu kigumu na shida katika maeneo yetu kama maji. Nikiangalia, Wilaya yangu ya Mpanda kuna vyanzo ambavyo Serikali ilifanya jitihada kubwa, lakini unakuta miradi ile haiishi na ile bajeti inayopangwa haiendi kwa wakati ile miradi ikaisha.

Sasa sijui bajeti hii ambayo imekuja mbele yetu, itaweza kukamilisha miradi ile ya maji na wananchi waweze kupata kwa urahisi na wepesi zaidi. Hususan Wilaya ya Mpanda, kuna mradi wa *Ikorongo One*; bajeti ya mwaka 2015 mkatupangia kuwa mtatupatia shilingi bilioni nne, lakini zile pesa hazikuweza kupatikana. Matokeo Wilaya ya Mpanda Mjini, Manispaa, maeneo mengi maji ni shida. Yaani maji yale yakipatikana leo, kesho hawapati; au wanaweza wakakaa siku tatu ndiyo wanapata maji. Maeneo mengine kama Makanyagio, Ilembo, hakuna maji kabisa, ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi, hii bajeti ya safari hii, miradi ambayo inaelekezwa, iweze kukamilika ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. Nafikiri na Waziri alivyotusomea bajeti yake, alisema sasa ni kipindi cha akinamama kufurahi; anawatua ndoo. Sasa naomba basi akinamama hususan wa Mpanda Vijijini, kuna vijiji havina maji kabisa wala havina miradi kabisa. Akinamama wanapata shida sana. Naomba bajeti hii iweze kutimiza yale malengo waliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi ni mikubwa mno. Ukiangalia kama Wilaya yangu ya Mpanda, Kata ya Ilembo ni shida. Naiomba Serikali sasa kupitia bajeti hii, migogoro hii ya ardhi iweze kwisha. Tunaomba bajeti hii ambayo leo tunaisema hapa ifanye kazi kama mlivyoileta mbele yetu, kwa sababu, migogoro ya ardhi haiishi. Kwa nini haiishi? Mimi nashangaa kila siku, kwa nini haiishi? Lazima sasa bajeti hii ambayo tunaichangia hapa, tunaomba migogoro ya ardhi kupitia bajeti hii, iishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijijini mwetu wanavijiji wanavaa mitumba na ndiyo nguo rahisi walizozioea, ndiyo maana ukienda sasa hivi vijijini unawakuta akinamama wengi ni wasafi kutokana na mitumba. Leo sisi bado viwanda vya kutengeneza malighafi ya nguo havijafika, lakini leo tumeipandishia mitumba ushuru mkubwa, ina maana wale wananchi wa vijijini washindwe kuvaa kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuhusu mitumba iangalie upya, watoe ushuru wa mitumba kwa sababu wananchi wetu ndiyo mavazi yao wanayayategemea kuliko kitu kingine chochote.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lupembe, kengele imeshagonga...



**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kwanza niwapongeze tu walioandaa bajeti hii, lakini pia nielekeze zaidi mchango wangu kwenye suala zima la afya. Afya ni jambo la msingi sana kuzingatiwa katika uwekezaji wowote ule unaotakikana kama tulivyosema kwamba tunataka kutengeneza Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Tanzania ya viwanda ambayo tunataka kuitengeneza bila kujali ama kuweka kipaumbele kwenye afya za watu wake ambao wengi ndio wazalishaji, wengi ndio wanaofanya kilimo cha mkono, ama ni wakulima wadogo wadogo ambao wako vijijini; hawa watu tusipowapelekea zahanati za kutosha, tusipopeleka Vituo vya Afya vya kutosha, tusipowapelekea watumishi wa kutosha wa kada za afya, hawa watu wanawezaje kusaidia uzalishaji na hatimaye viwanda vyetu vikafanya kazi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona upungufu kidogo katika bajeti yetu hii kwamba ingawa Serikali imeweka kipaumbele kwenye Sekta ya Kilimo na kuainisha kwamba mazao ya kilimo yatakuwa moja ya malighafi kwenye viwanda hivyo, bado vipaumbele vinaenda kwenye kujenga reli, barabara, Viwanja vya Ndege na kadhalika; lakini kwenye vyanzo vya kilimo ambavyo ndivyo vitakuwa malighafi, kusababisha uzalishaji ukue hakujawekewa mkazo huku; na asilimia 80 ya wanawake walioko kijijini ndio wakulima, lakini bajeti hii haioneshi ni jinsi gani afya ya mwanamke huyu imezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi upande wa Mkoa wa Manyara na Wilaya zake zote, hatuna watumishi wa kutosha katika kada ya afya na hatuna vituo vya kutosha. Kwa mfano, katika Kata ya Eshikesh, mama mjamzito anatembea kilometa 40 kwenda kwenye Zahanati ya Yaeda Chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya hii ya Mbulu Vijijini haina Hospitali ya Wilaya wala gari la wagonjwa. Akinamama hawa wanapata shida kusema ule ukweli; siyo Mbulu tu, tuna maeneo kama Simanjiro, mahali ambapo gari la wagonjwa ni moja, hawana Hospitali ya Wilaya, wanatumia Hospitali ya KKKT. Mama akishindwa kujifungua, anatakiwa apatiwe operation lakini anatakiwa alipe shilingi 400,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi yule mama wa Kimasai anayetembea na punda, anayepoteza muda wote kwenye maji, ni saa ngapi ametafuta shilingi 400,000 za kuweza kumsaidia yeye kwenda kujifungua? Nafikiri tungehakikisha



kwamba kipaumbele kinawekwa kwanza kwenye afya, watu wetu wakiwa na afya njema watazalisha kwa tija. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nizungumzie hili suala la asilimia tano ya akinamama na vijana. Tulijinadi sana kwenye kampeni zetu kupitia asilimia tano kwa akinamama na vijana. Sasa inaonekana sehemu kubwa ya *own source* inakusanywa na Serikali Kuu. Changamoto ipo kubwa; mara nyingi, hata leo Mheshimiwa Umbulla ameuliza hapa, akinamama ama Wabunge wa Viti Maalum hawaingii kwenye Kamati ya Mipango na Fedha ya Halmashauri zetu, ndiyo maana hizi fedha zimekuwa *misused* wakati mwingi. Hakuna mtu wa kuzisimamia; tunazona tu kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwahakikishia akinamama ambao ndio wamekipa Chama chetu kura nyingi ya kwamba tunakwenda kudai asilimia hizi. Je, tunarudije kwao? Tunaomba hizi fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya akinamama, kwa mwaka huu haidhuru, basi kwa mara ya kwanza zifike katika ukamilifu wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna shilingi milioni 50 kila Mtaa na kila Shehia na kila Kijiji. Nako tulijinadi kwa sababu ni ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tu kwamba pamoja na Mikoa 10 inayotaka kutengwa hapa ya *pilot run*, nashauri ili wananchi wetu mioyo yao isikunje ngumi, kwa nini isitumike mikoa yote, halafu haidhuru vichukuliwe vijiji hata kama ni vitano kwa kila mkoa? Maana changamoto na mazingira hayafanani. Haidhuru na sisi tupate cha kusema tukirudi kwa wananchi wetu. Hawa kumi tu, tuseme Mkoa wa Manyara, haufanani na Dar es Salaam; Mkoa wa Manyara haufanani na Kilimanjaro; changamoto zinatofautiana. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sijajua kwamba labda hawa walioweka hivyo kwamba wanachukua mikoa kumi wamezingatia nini. Ila nashauri tu, kama inawezekana, mikoa yote ichukuliwe na vijiji haidhuru vitano vitano kila Mkoa ili tuone kwamba tunawezaje kuokoa maisha ya wananchi wetu kupitia mikopo hii ya shilingi milioni 50 kupitia SACCOS.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mgongano wa maslahi. Pale mwongozo unapoelekeza kuwa mapato yote ya mamlaka ya Serikali za Mitaa yawasilishwe Serikali kuu, changamoto kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kwamba fedha hizi huwa zinachelewa sana kuteremka chini huko kwenye Halmashauri zetu. Sasa itakuwaje ikiwa fedha hizi zinakusanywa na Serikali Kuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma kiambatanisho cha masuala ya afya; elimu ya watoto wetu wa kike ni tatizo. Imeelezwa sana, kwamba tunaomba kodi ziondolewe kwenye vifaa vyote vinavyosaidia akinamama pamoja na mabinti mashuleni. Kwenye *towel* zao kodi iondolewe. Binti anakosa shule siku saba katika mwezi. Mwisho wa siku inaonekana watoto wa kike ni vilaza; kumbe ni kwa sababu hawa-*attend* shule inavyotakiwa kama wanavya-*attend* watoto wa kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili litazamwe upya, tuwasaidie watoto wetu wa kike. Utakuta miundombinu kwenye shule, watoto 400 vyoo viwili au watoto 600 vyoo vitatu, watoto wa kike wanapataje kujisitiri? Je, bajeti hii inamwaliaje mtoto wa kike? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kushea hii keki sawasawa, naomba tuwekeze zaidi kwa akinamama ambao ni waaminifu hata wanavyochukua mikopo kwenye mabenki, wamekuwa wakirejesha kwa uaminifu mkubwa. Kwa hiyo, naomba sana akinamama watazamwe kwa jicho la pekee ili waweze kusaidia pato hili la Taifa hasa kupitia kilimo na ujasiriamali. Hakuna asiyejua kwamba akinamama ndiyo wanaokimbia kimbia asubuhi mpaka jioni kutafuta riziki za familia zao, kupitia biashara ndogo ndogo. Akinamama hao watazamwe kwa jicho la pili ili waweze kusaidia katika kukua kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna upungufu mkubwa wa urari baina ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo. Matumizi ya kawaida ni karibu mara tatu ya yale ya maendeleo. Kwa hiyo, nashauri tu kwamba, bajeti hii iangalie ni jinsi gani inaweza ikawekeza zaidi kwenye bajeti ya maendeleo, japo imepandishwa mpaka asilimia 40, lakini kama inawezekana, iendelee kusogea hata ifike mahali iwe asilimia 50 kwa 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba nisisuburi kengele inayofuata, niseme tu kwamba yangu ni hayo. Zaidi sana, nawalilia akinamama waweze kusaidiwa na bajeti hii pamoja na watoto wa kike ili waweze kupata elimu sawasawa pamoja na watoto wa kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga hoja mkono. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida Bakar.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hoja hii ya bajeti yetu kuu. Naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kupeleka pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri. Mimi namwita Mheshimiwa Waziri wa Mipango;

huyu jina lake Mpango, kwa hiyo ana mipango mingi. Mheshimiwa Naibu Waziri, dada yangu au mdogo wangu, huyu ana jina gumu sana huyu! Ashatu, sijui jina la Kichina hili au la wapi, sielewi lakini Ashatu ni jina zuri sana, nafikiri la kihindi. Napenda kumpongeza kwa ushirikiano mzuri wa kazi. Wanashirikiana, wanafanya kazi na inaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda moja kwa moja kwenye hoja. Suala la maji limezungumzwa sana na kweli Serikali yetu inajitahidi sana katika kusaidia huduma za maji mijini na vijijini; lakini tukiangalia sana vijijini maji yanayotegemewa sana ni ya visima. Sasa maji yaliyoko vijijini hasa ya visima, visima vingi vinakuwa havitoi maji. Tunaomba sana, watu hawa wa vijijini hususan wanawake, sisi wanawake ambao tunahangaika sana, tunatoka usiku wa manane kwenda kutafuta maji masafa marefu na inafikia wengine hata kuachwa na waume zao kutokana na matatizo haya ya maji. Hebu tuwaondolee matatizo haya ya maji wanawake hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi katika kutekeleza ilani yake ya 2015 hadi 2020 inatekeleza vizuri sana kujenga zahanati vijijini na mijini, lakini ukiangalia zahanati nyingi hazina vifaa. Akinamama wengi ambao wanakwenda kujifungua wanaambiwa wabebe ndoo, kanga, nyuzi, mikasi na viwembe. Huu ni udhalilishaji wa wanawake. Naomba sana Serikali ilione hilo na ilipe kipaumbele mambo ya zahanati na vifaa, siyo iwe zahanati tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, zile zahanati ambazo zimejengwa na ambazo hazijamalizwa, zimalizike, siyo kutenga tena bajeti mpya ya kujenga zahanati nyingine ambapo zile za zamani zilizokuwa zimejengwa hazijamalizwa na vile vile vifaa hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunaishukuru Serikali yetu kutenga shilingi milioni 50 za vijijini, mitaa na kule Zanzibar tunaita shehia. Fedha hizi kwa kifupi ni nyingi sana. Serikali yetu imetenga fedha nyingi sana, lakini je, tujiulize, matumizi yake yatakwenda sawia? Sisi ni mashahidi kuona kwamba fedha za Mheshimiwa Jakaya Kikwete vilivyoteketea na fedha za TASAF zinavyoteketea. Je, hizi fedha shilingi milioni 50 za vijiji, shehia ya mitaa zitakwenda kutekeleza majukumu ya kuondolea wananchi umaskini zinatumiwa vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iangalie sana suala hili ili wanaohusika walisimamie vizuri tukiwemo na sisi Wabunge, maana na sisi tusijitoe, tumo katika utekelezaji wa majukumu ya shilingi milioni 50. Asilimia tano hizi za kwenda Halmashauri za vijana na wanawake ni siku nyingi tu, ni miaka mingi zinatengwa na zinaonekana katika makaratasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati ya PAC na zamani nilikuwa LAAC, tulikuwa tunazona, lakini fedha hizi hazitumiki vizuri kule. Fedha watu wanatumia vibaya, sijui wanazifanyia nini kusema ukweli. Ukitazama hesabu, haziendani na wanawake hawa na vijana huwa hawapatiwi fedha hizi. Naishukuru sana Serikali kutenga hilo lakini tunaomba sana Serikali yetu iwe simamizi sana ya fedha hizi za asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wameongelea watoto wetu wa kike. Watoto wetu wa kike ni watoto ambao wanataka hifadhi kubwa sana; hivi ni kwa nini hizi *pad* siziwe *free*? Hizi taulo za watoto wa kike! Mtoto wa kike siku zake zikifika anaomba dunia ipasuke aingie; mtoto mama yake maskini, baba yake maskini, fedha ya kununulia taulo hana. Mtoto anabakia haendi shule siku saba au siku nane. Hii hatuioni kama ni muafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana, tuko chini ya miguu yenu Serikali, mwondoe VAT ili watoto hawa wapate kusitirika. Watoto wetu wa kike wanapata shida sana; wakati mwingine wanafeli madarasani kutokana na tatizo hili. Tatizo hili katujalia Mwenyezi Mungu, hatukulitaka wenyewe; watoto wetu hawakulitaka wenyewe. Wanaume hawana hili. Kwa hiyo, tunaomba na Waheshimiwa Wabunge wanaume wakichangia hapa watetee hili ili watoto wetu waweze kuhifadhika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi/Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa muda uliobaki hatutaweza kuwa na mchangiaji mwingine, lakini nina matangazo kadhaa hapa na mambo mengine ni ya kukumbushana.

Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa *Youth Parliamentary Group*, Mheshimiwa Stephen Masele, anawatangazia na kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wote kushiriki, *Training on Policy Analysis* ambayo itafanyika kesho tarehe 11 Juni, saa 5.00 asubuhi ukumbi wa *African Dreams*. Semina hii imeandaliwa na IRI yaani *International Republican Institute*.

Tangazo lingine pia linatoka kwa Mheshimiwa Masele, anawatangazia na kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wote wanawake na vijana kwenye *Panel Discussion on Leadership and Legislative Decision Making* na *Panelists*, yaani watu watakaokuwa wanaongea ni Spika wa *East Africa Legislative Assembly*, Dkt. Daniel Kidega na Mama Anna Abdallah. Hii ambayo inawahusu wanawake na vijana, itafanyika siku ya Jumapili, saa tano asubuhi sehemu hiyo hiyo ya *African Dreams*; na watu wanaowaalika huko pia ni wale wale *International Republican Institute*. Kwa hiyo, kesho saa tano na kesho kutwa saa tano kwa wale wanaohusika.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo na kwa hiyo, shughuli za Serikali Bungeni anayekaimu ni Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho ni kukumbushana, Kanuni ya 66(3)(c) inazungumzia staha ndani ya Bunge na hii (c) inazungumza kutokupita kati ya Kiti cha Spika na Mbunge anayezungumza. Mnakumbushwa kutokupita kati ya Spika na mtu anayezungumza, kwa sababu anayezungumza anakuwa anaongea na Spika. Sasa ukisimama kati yake, kanuni inakataza kwa sababu unakuwa unamzuia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kanuni nyingine ambayo ni muhimu tukumbushane ni Kanuni ya 106(1) na (2). Kwa sababu hii inahusu mjadala tunaoendelea nao nadhani ni muhimu tuisome fasili ya (2) hasa, ama nisome zote mbili, zinasema:-

“(1) Mjadala kuhusu hotuba ya Bajeti ya Serikali, utaendelea kwa siku zisizozidi saba, ambapo dakika zisizozidi kumi zitatolewa kwa kila Mbunge anayetaka kuchangia hotuba hiyo.

(2) Katika hatua hii, majadiliano yatahusu mambo ya jumla kuhusiana na hali ya uchumi, na Mbunge yeyote hataruhusiwa kupendekeza mabadiliko katika makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali.

Ni kanuni hizi ambazo tunazo na tumetunga sisi wenyewe. Fasili ya (2) inatupa masharti kuhusu mjadala wetu humu ndani kuhusu bajeti ya Serikali. Sasa kwa kuwa hizi kanuni wote tunazo nakala zake nawashauri Waheshimiwa Wabunge tukaisome hiyo Kanuni ya 106(2) ili tuone namna ya kuelekeza mjadala yetu, tunataka kuzungumzia mambo gani. Kwa hiyo, nimeona tukumbushane hilo. Nawakumbusha tena Kanuni ya 106(2) tukaisome tunapoenda nyumbani ili mjadala yetu iweze kwenda vizuri kwa hizo siku zinazokuja.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 13 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*